Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 25 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kikao cha leo, ninalo tangazo la huzuni. Ninapenda kutangaza kwamba, Mheshimiwa mwenzetu, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, amefariki dunia jana usiku. *Regional Medical Officer* ameniambia kwamba, sababu ya kifo ni kiharusi *(stroke).* Kwa hiyo, mwenzetu hayupo tena duniani na kama kawaida yetu, nitaomba sasa wote tusimame kwa dakika moja kumwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema, peponi.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego aliyefariki dunia tarehe 24 Juni, 2004)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 119

**Barabara ya Busoka - Bulyanhulu**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza: -

Kwa kuwa barabara ya Busoka - Bulyanhulu yenye urefu wa kilomita 76 imekuwa haieleweki: -

(a) Je, Serikali kupitia Bunge hili inaweza kuitangaza barabara hiyo kuwa ya Kitaifa?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zinazofanya barabara hiyo isiwekwe kwenye mpango wa kuwekewa lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, hadhi ya barabara ya Busoka - Bulyanhulu yenye urefu wa kilometa 76 inaeleweka. Barabara hii ni ya Mkoa na ipo chini ya Wizara ya Ujenzi na kwa maana hiyo inapaswa kuhudumiwa na Wizara hiyo kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Waziri wa Ujenzi amekuwa akielezea hapa mara nyingi, barabara hiyo inaweza ikapandishwa hadhi hadi kufikia hadhi ya Kitaifa kutegemea na kukidhiwa kwa vigezo ambavyo Waziri amekuwa akivieleza. Kwa hiyo, baada ya kupata swali hili, tumekwishaiarifu Wizara ya Ujenzi ili iweze kutazama suala hilo sambamba na barabara nyingine.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara hiyo haijawekwa kwenye mpango wa kuwekewa lami kama zilivyo barabara nyingine nyingi zenye hadhi ya barabara za Mikoa. Lakini hii inatokana tu na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, lakini vinginevyo nia yake iko pale pale.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza.

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kufahamu kwanza kama yeye binafsi anafahamu kwamba kuna mkataba baina ya *TANROADS* ambaye ni Wakala wa Barabara wa Serikali na mmiliki wa mgodi ule ambaye ni *Kahama Mining Corporation?*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna malalamiko makubwa ya Wananchi dhidi ya matumizi ya barabara hii kwamba yanasababisha vumbi kubwa. Je, Serikali inafikiria nini cha zaidi katika kuondoa kero ya vumbi hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika maelezo yangu nimesema mara tu tulipopata hili swali kutoka kwako tuliliwasilisha rasmi kama tatizo kwenye Wizara ya Ujenzi kwa sababu ni barabara ambayo ni ya Mkoa na kwa utaratibu huo, wao ndiyo wanapaswa kwa kweli kushughulikia mambo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninapenda kuuliza kama ifuatavyo: Kwa kuwa barabara hii katika Kijiji cha Segese ina-*branch* na kuzaa barabara nyingine ambayo inafika mpaka Kijiji cha Nyan'holongo; Jimboni Nyang'wale, Wilaya ya Geita na kwa kuwa barabara hii iko chini ya Halmashauri na inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama; je, Serikali inaweza sasa kuipandisha iwe ya Mkoa kama ile ya Busisi Nyan'holongo ili ipate

matengenezo kwa sababu Wilaya ya Kahama imeshindwa kuihudumia barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea hiyo rai yake na kama nilivyosema katika maelezo ya awali, nalo nitaliwasilisha Wizara ya Ujenzi ili waone uwezekano wa kuipandisha hiyo barabara daraja.

Na. 120

**Upungufu wa Matibabu kwenye Vituo vya Afya na Zahanati**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza: -

Kwa kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa Matabibu kwenye Vituo vya Afya na Zahanati nchi. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuondoa upungufu huo nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la upungufu wa Watumishi wa Sekta mbalimbali ndani ya Serikali za Mitaa likiwemo la upungufu wa Maafisa Tabibu kwenye Vituo vya Afya na Zahanati. Ili kutatua tatizo hili la ajira, ofisi yangu mwaka 2001 iliziagiza Halmashauri zote nchini kuwasilisha mahitaji ya Ikama ya Watumishi kupitia kitengo kinachoshughulikia Ajira ya Watumishi wa Serikali za Mitaa kwa lengo la kurahisisha zoezi la uombaji wa vibali vya ajira ya Watumishi kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kila mwaka imeendelea kutoa vibali vya ajira kwa Halmashauri mbalimbali nchini ambazo zimeweza kuvitumia vibali hivyo kuajiri Watumishi wanaohitaji. Aidha, kwa upande wa ajira ya Maafisa Tabibu kwenye Vituo vya Afya na Zahanati, zoezi la ajira yao linaendelea kwa kuzingatia upatikanaji wa wataalam wnyewe lakini vile vile na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2004, mahitaji ya Maafisa Tabibu katika Vituo vya Afya yalikuwa Matabibu 18, lakini katika kipindi hicho aliajiriwa Tabibu mmoja tu. Pia, mahitaji ya Maafisa Tabibu katika zahanati yalikuwa 82, lakini wameweza kuajiriwa 8 tu. Takwimu za hapo juu zinaonyesha wazi kabisa kuwa, tatizo hili ni kubwa na hali hiyo hairidhishi. Zipo sababu nyingi zinazosababisha hali hii ikiwa ni pamoja na mazingira ya kazi yasiyoridhisha, maslahi madogo, uhaba wa wataalam, kulikotokana na kupanuka kwa Sekta binafsi na ufinyu wa Bajeti ya Serikali kuweza kuajiri wataalam wote wanaohitajika.

Kwa hiyo basi, naomba tu tumwombe Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wabunge wengine wote, kufahamu kwamba, Serikali inalijua tatizo hili na inafanya kila linalowezekana kujaribu kulitatua.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Naibu Waziri amesema kwamba, tatizo mojawapo ambalo tunalipata ni ukosefu wa Maafisa Tabibu hao nchini kwamba hawapatikani. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuweza kuwafunza Maafisa Tabibu ili tuweze kuwaajiri na kuweza kujaza nafasi hiyo, mpango ambao unafanana na ule wa Wizara ya Elimu na Utamaduni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wataalam wa Afya hasa Madaktari Tabibu idadi yao ni ndogo sana ndani ya nchi. Kwa hiyo, hatua zinazochukuliwa na Serikali kwanza ni kuhakikisha kwamba, kwa kuwa Sekta ya Afya ni moja ya Sekta ya kipaumbele, tunachokifanya ni kuongeza idadi ya Madaktari Tabibu, kuongeza kwa kuwapeleka vyuoni na kila wanapotoka badala ya kungojea waombe nafasi za kazi, wanapelekwa moja kwa moja kwenye maeneo yenye upungufu. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, ni lini mkakati wa kuvipatia Vituo vya Afya magari ya wagonjwa ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya cha Kibakwe utaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu Matabibu, siyo magari. Nadhani hilo ni jipya.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa ni kweli na ukweli usiokatalika hivi sasa Maafisa Tabibu wengi wako barabarani hawajaajiriwa; na kwa kuwa tangu nimeingia katika Bunge hili mwaka 1985 bado tuna *deficit budget*, lakini magonjwa hayajali *deficit budget;* je, Serikali kweli kabisa haiwaonei imani Wananchi kule vijijini wanaoshindwa kutibiwa na Madaktari wao wako barabarani hawaajiriwi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna upungufu wa Maafisa Tabibu kwenye Zahanati zetu na Vituo vya Afya na ni kweli vilevile Serikali inachukua hatua ya kuweza kuwapeleka kote ambako kuna upungufu na kama kuna Maafisa Tabibu ambao wamekosa kazi wanapaswa wapeleke majina yao au basi waombe nafasi hizo kwa sababu ziko wazi, kama wana sifa watapewa kazi hizo. *(Makofi)*

Na. 121

**Tatizo la Kukatika Umeme**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali iliamua kukodisha Menejimenti ya *Net Group Solution* ya Afrika Kusini kuendesha Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO);* na kwa kuwa hali ya upatikanaji wa umeme bado inasuasua mbali na makusanyo makubwa yanayopatikana: -

(a) Je, ni fedha kiasi gani zimetumika kuilipa menejimenti hiyo tangu ilipoanza mkataba hadi sasa ikiwa ni pamoja na mishahara, posho, nauli za likizo, matibabu, *bonus* na malipo mengine yaliyotajwa katika Mkataba huo?

(b) Kwa kuwa hali ya umeme bado haijaimarishwa hadi sasa; je, bado zipo sababu za kuendeleza Mkataba wa Kampuni hiyo ambao unaonekana kuwa manufaa yake ni madogo ikilinganishwa na gharama?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la wajina wangu, Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa; Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Wakati najibu swali Na. 70 la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni Masunga, katika Bunge lililopita juu ya *Net Group Solution,* nilitaja kazi walizopewa Kampuni hii na mafanikio ambayo Serikali imepata kutokana na kuwepo kwa Kampuni hii.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *Net Group Solution* una sehemu mbili za malipo, sehemu ya kwanza inaitwa *fixed retainer fees/management fees,* malipo yanayolipwa kutokana na kuwepo na wataalam wa Kampuni ile na sehemu ya pili ni malipo yanayotokana na mafanikio yanayotokana na kazi wanayoifanya wao, inaitwa *success fees.* Hizi *management fees* zinajumuisha vipengele alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya mishahara, posho, nauli za likizo, matibabu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, malipo haya yanatokana na tenda iliyoainisha mchanganuo wa mahitaji ya wataalam kitaaluma kulingana na saa za kazi kwa kila mtaalam. *TANESCO* hailipi malipo haya. Fedha zote zinatokana na msaada wa *SIDA.* Kwa miaka miwili takriban Dola 2.6 zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *success fees* au malipo yanayofanyika kutokana na mafanikio, hii imekuwa ikilipwa kulingana na kufikiwa malengo yaliyowekwa kwenye Mkataba. Baadhi ya malengo yanahusu kuongeza mapato, kupunguza upotevu wa umeme na kupunguza matumizi ya uendeshaji. Malipo haya yanatofautiana kutoka muhula mmoja hadi mwingine. Mwaka wa kwanza wa Mkataba ulioishia Mei, 2003, kiwango cha juu cha ada hiyo kilichofikiwa kilikuwa ni asilimia 6 ya faida iliyokusanywa. Kiwango hicho kilifikiwa kwa sababu mafanikio yalipimwa kulinganisha na mahesabu ya Shirika ya mwaka 2000, ambapo makusanyo wakati huo yalikuwa ni asilimia 67 tu. Jinsi marekebisho yalivyokuwa yakifanywa, ndivyo kiwango cha *success fees* pia kilivyokuwa kinapungua hadi kufikia asilimia 3.8 ya faida ilipofikia Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, ankara zote zilizokusanywa katika kipindi cha miaka miwili ni Shilingi bilioni 364, lakini faida ni Shilingi bilioni 168. Malipo ya *success fees* yamekuwa yakilipwa tu pale mshauri alipohakiki na kuridhika kuwa malengo yanafikiwa kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba. Mkataba pia una kinga kwa upande wa *TANESCO* kwamba, hawalipwi *Net Group* kwa mafanikio yasiyotokana na juhudi zao na pia hawaadhibiwi kwa matukio yoyote yaliyo nje ya uwezo wao kwa mfano ukame na hivyo kushindwa kuzalisha umeme kutokana na vyanzo vya maji kwa kiwango kinachotakiwa. Kwa miaka miwili ya Mkataba, kiasi cha Dola milioni 6.5 kitakuwa kimelipwa na *TANESCO* kama *success fees*. Mshauri Maalum wa Mkataba wa *Net Group* ni Kampuni ya *AF International* ya Sweden ambayo nayo kama nilivyosema awali, inalipwa ada yake kutoka *SIDA.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, hali ya upatikanaji umeme bado inakabiliwa na matatizo, Wafanyakazi wa *TANESCO* chini ya Uongozi wa *Net Group* wamefanya kazi kubwa. Kutokana na ufanisi mzuri wa *Net Group*, katika mazingira magumu ya ukame na uchakavu mkubwa wa mfumo wa umeme, bado *Net Group* inahitajika kuiboresha *TANESCO.* Hivi sasa Kampuni hiyo imeongezewa Mkataba wa muda mfupi wa miezi mitatu ili kukamilisha majadiliano kwa ajili ya Mkataba mpya.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa ni dhahiri kwamba Kampuni hii ya *Net Group Solution* ya kutoka *South Africa* haijafanya kazi yoyote tofauti na kazi iliyokuwa ikifanywa na Wazalendo wa Kitanzania hapo nyuma mbali na upendeleo ambao Serikali imetoa ikiwa ni pamoja na Serikali kulipa malipo yake ambayo yalikuwa hayalipwi huko nyuma wakati wa Menejimenti ya Kizalendo. Je, Serikali inadhani tuna sababu ya kuendelea kuwa na hii *Hired Management* ya *Net Group* kwa sababu bado matatizo haya ya umeme yako pale pale na huenda yakawa yameongezeka? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa fedha ambazo zimetajwa na Naibu Waziri ambazo zinaendelea kulipwa kwa Kampuni hii ni fedha nyingi, hivi pamoja na umaskini wetu tutakuwa tunalazimishwa kupewa misaada hata pale ambapo hatuko tayari kupokea misaada hiyo kwa faida ya maendeleo ya nchi hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, ninafahamu na ninaelewa sababu za kizalendo anazozungumza kwamba, pengine ingekuwa bora zaidi kuwa na Kampuni ya Watanzania au Watanzania wenyewe kuongoza Shirika hili. Ninaelewa na ningeshangaa kama Mheshimiwa Mbunge asingekuwa mzalendo. Kwa hiyo, ninafahamu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, kwanza hakuna upendeleo ambao Serikali inafanya na pili kama nilivyoeleza awali na kama nilivyojibu swali katika Bunge lililopita la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni

Masunga, Uongozi wa Kampuni hii na Wafanyakazi wa *TANESCO* kwa ujumla kwa kweli wamefanya kazi kubwa katika kuliboresha Shirika.

Mheshimiwa Spika, nilisema wakati najibu swali hilo na pengine labda nirejee maelezo mafupi niliyoyatoa wakati huo. Ni kwamba, katika kufanya kazi waliyopewa, Kampuni hii pamoja na mambo mengine wamefanya kazi ya kuboresha mapato kwa zaidi ya asilimia 30 iliyopangwa katika Mkataba na kwamba kuongezeka kwa mapato ya Serikali kumepatikana kwa asilimia 60 kutoka Shilingi bilioni 10 kwa mwezi hadi Shilingi bilioni 16 kwa mwezi, kupunguza gharama za uendeshaji kwa asilimia 27 kutoka Shilingi bilioni 14.7 mwaka 2002 hadi Shilingi bilioni 11.6 mwaka 2004, kufundisha upya menejimenti (Mameneja 220), kupunguza upotevu wa umeme katika njia kuu za usafirishaji, kuboresha na kukusanya ankara kutoka kwa wateja kwa asilimia 24 kutoka asilimia 75 mwaka 2002 hadi asilimia 93 mwaka 2004 na kufanya ukaguzi wa mita *(Metre Auditing)* na hivyo kuweza kuokoa karibu Shilingi bilioni tatu kwa mwezi kwa umeme unaoibiwa.

Mheshimiwa Spika, haya ni baadhi tu ya mafanikio ambayo yamepatikana katika kipindi hiki na maelezo mengi yamo katika jibu la maandishi ambalo nina hakika Mheshimiwa Mbunge atakapolipata ataridhika kwamba, kuna kazi kubwa imefanywa na Serikali haiwezi kuwa na upendeleo kwa Kampuni ya Kigeni, isipokuwa imechukua uamuzi wa kuchukua Kampuni ya nje kwa ajili ya uendeshaji wa *TANESCO* kwa sababu uendeshaji wa Mashirika ya Umeme ni taaluma adimu na hapa kwetu kwa hivi sasa bado hatujaweza kuwa na uwezo huo. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, ninafurahi kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri ametamka kwamba, hii *success fees* inatokana na faida na kwa sababu utundu unaweza kufanyika katika mahesabu na mimi sikumbuki kuona mahesabu yaliyowasilishwa hapa Bungeni kwa kipindi cha *Net Group*. Je, ni nani anatathmini na kudhibiti faida hii ili wasiikuze kimahesabu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda nimtoe wasiwasi ndugu yangu, Mheshimiwa Henry Shekiffu na Bunge lako Tukufu kwamba, katika ufanisi wa kazi na katika kufanya mahesabu hayo kwanza kuna vigezo. Kuna mlolongo wa vigezo ambavyo kwa sababu ya muda nitashindwa kuvitaja hapa, lakini niko tayari kumpa Mheshimiwa Mbunge, kwa taarifa zake. Kuna mlolongo wa vigezo vya kitaalam kabisa ambavyo vimepangwa.

Lakini pili, Shirika hili pamoja na kwamba ni Menejimenti ya *Net Group* ndiyo inaongoza *TANESCO,* lakini hao wako chini ya Bodi ya Wakurugenzi na Bodi ya Wakurugenzi wenyewe hupitia mahesabu haya wakati hadi wakati na wanasaidiana na Taasisi nyingine za Serikali ikiwemo *PSRC.*

Kama nilivyosema awali, ipo pia Kampuni ambayo inasimamia utendaji wa kazi *(Monitoring Consultant),* ambaye na yeye anatoa ripoti yake kwa Bodi, Bodi inapitia

ripoti hii mpaka iridhike kwamba, pamoja na yote pia na ile ripoti ya *monitoring consultant* ina ukweli na ndipo malipo yanafanywa. Kwa hiyo, hakuna uwezekano wa kufanya ujanja ujanja wa kiajabu ajabu na katika Bodi ile wapo watu maarufu na wenye uwezo mkubwa na ninakumbushwa hapa kwamba, Mwenyekiti ni Mtanzania. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 122

**Ujenzi wa Chuo cha Ufundi - Lindi**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO (k.n.y. MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ)** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga Chuo cha Ufundi Mkoani Lindi mara tu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Chuo cha Kigoma. Je, hadi sasa Serikali imeshafanya maandalizi gani ya awali ya ujenzi wa Chuo hicho kama vile utafutaji wa kiwanja na kadhalika?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo: -

Tayari maandalizi ya awali yameshafanywa na *VETA* ili kukiwezesha Chuo cha Ufundi Lindi kujengwa. Hatua ya kwanza ilikuwa kufanya uchunguzi Mkoani Lindi ili kujua kozi zinazotakiwa kufundishwa Mkoani humo. Tayari kozi hizo zimejulikana, ingawa ni nyingi tutaanza na nne tu. Chuo kinatarajiwa kujengwa kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza itakuwa na kozi nne tu, awamu ya pili itakuwa na kozi tatu na awamu ya mwisho kozi tatu.

Hatua ya pili ilikuwa ni kutafuta kiwanja, ambacho tayari kimepatikana eneo la Mitwero, ambacho kina ukubwa wa ekari 50 na sasa taratibu za kupata hati zinaendelea. Tunaomba Uongozi wa Mkoa utusaidie kupata upatikanaji wa hati ya kiwanja hiki mapema iwezekanavyo kwani kukosekana kwake kunaweza kukaathiri kasi ya ujenzi wa chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, hatua ya tatu ilikuwa ni kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka 2004. Katika hili, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira mpaka hapo tutakapowasilisha bajeti yetu Bungeni.

Ningependa kusisitiza kuwa, kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza mwaka huu wa 2004, lakini tarehe kamili ya kuanza na kumalizika itafahamika baada ya mshauri *(Consultant)* atakayepatikana kwa taratibu za Serikali *(Public Procurement Act),* kukamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, kwa jitihada zake za kufuatilia kwa karibu juu ya ujenzi wa Chuo hicho kwa maendeleo ya Wananchi wa Mkoa wa Lindi.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, ni lini hasa Waziri alipeleka maombi ya kuomba kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Chuo hicho, kwa kuwa Lindi hatuna shida ya viwanja na hivi sasa Mkuu wa Mkoa anahitaji wateja wa viwanja vilivyopo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, maombi yetu ya kupatiwa kwa hati ya kiwanja yana karibu mwaka na nusu, ni ndani ya miezi mitatu iliyopita ndiyo tumepata *offer,* lakini hatujapata hati na ili hatua zingine za ujenzi ziweze kuendelea, tunahitaji hati.

Na. 123

**Kufuta Kodi kwa Makampuni ya Simu za Mikononi**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza: -

Kwa kuwa kutokana na umuhimu wa Sera ya Utandawazi na ili kuwawezesha Watanzania kujiingiza katika ushindani huo, Serikali imefuta kodi zote zinazotozwa kwa Kampuni zinazoagiza vyombo vya tarakishi *(Computers):* -

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufuta kodi zote zinazotozwa kwa Kampuni za Mawasiliano ya Simu za Mkononi zikiwemo kodi za kuagiza vifaa vya kusafirishia mawimbi ili kuwaunganisha wateja wake na kadhalika na kuweza kueneza mawasiliano hayo katika Wilaya zote na hata vijijini?

(b) Je, kwa dhana hiyo iliyotumika kufuta kodi kwenye vyombo vya tarakishi, Serikali haioni umuhimu wa kufuta kodi kwa vyombo vya simu za mikononi *(Cellular Phone Handsets)* ili vipatikane kwa bei nafuu na kufanya mawasiliano kwa Wananchi kuwa mazuri na ya gharama nafuu zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, ningependa kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Sera ya Utandawazi ni muhimu na itawezesha Tanzania kujiingiza katika ushindani huo. Aidha, utandawazi unahusisha mambo mengi sana ikiwa ni pamoja na masuala ya mawasiliano kwa njia ya simu na yale ya mtandao *(internet),* ambayo yanafanyika kwa njia ya *computer.* Lakini pia ni ukweli

usiopingika kuwa, Serikali bado inahitaji sana mapato ya ndani badala ya kutegemea misaada ya Wahisani katika kuendeleza mipango ya kawaida na ile ya maendeleo.

Ni vyema kufahamu kuwa fedha za Wahisani zinatokana na kodi wanazolipa Wananchi wa nchi hizo, hivyo nchi hizo zinatushangaa kwa kusamehe kodi kwenye baadhi ya bidhaa ikiwa ni pamoja na kutokutoza kodi kwenye *computers.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kujibu swali la mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mawasiliano na namna ya kutoa vivutio katika Sekta hii muhimu, Serikali imeamua kutokutoza ushuru wa forodha bidhaa zote *(Capital Goods)* zinazoagizwa na Makampuni ya Simu za Mkononi kwa ajili ya uwekezaji hii ikiwa ni pamoja na vifaa vya kusafirishia na kupokea mawimbi *(Transmission and Reception Apparatus)* kwa ajili ya kueneza mawasiliano kwa wateja wao.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inauona umuhimu wa kuwapatia Wananchi simu za mikononi ambazo zitakuwa za gharama nafuu. Umuhimu huu unadhihirishwa na uamuzi wa Serikali wa kutokutoza ushuru wa forodha simu za mikononi. Hata hivyo, kwa kuzingatia ukweli kuwa tunahitaji kupanua vianzio vyetu vya mapato ya ndani, uagizaji au ununuzi wa simu za mikononi hauna msamaha wa *VAT.* Pia, matumizi ya simu hizo *(airtime)* yataendelea kulipiwa ushuru wa bidhaa *(Exercise Duty),* pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza kwamba, hivi karibuni Waziri wa Mambo ya Nje, alizindua aina ya simu ya mkononi inayoitwa *Thuraiya* ambayo inatumia *satellite,* lakini bei yake ni kama Shilingi milioni moja kwa seti. Sasa simu hii ingefaa sana kwa sehemu za vijijini kwa sababu inatumia teknolojia nzuri. Je, bei hii kubwa inatokana na kodi na kama ndiyo hivyo Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba simu hii inafika vijijini? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa bado bei ya mawasiliano ya simu za mkononi ni kubwa sana kutokana na makampuni haya binafsi yanayouza hizi simu kuwa na aina ya *(cartel)* au ukiritimba wa kulipa kodi na pia udhaifu wa Tume ya Mawasiliano. Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha matatizo haya, ili simu hizi ziweze kutumika popote mijini na vijijini na wananchi wa Tanzania waweze kunufaika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli *Thuraiya* ni bei kubwa, lakini utambue kwamba, teknolojia ya kutumia *satellite* ni *very expensive.* Kwa hiyo, lazima kwa hali yoyote ile, itakuwa na *fund* kubwa lakini *on the long run* unapotumia *Thuraiya* unatumia kwenye *satellite,* gharama yake ya kutuma ujumbe, ya kuwasiliana na nchi yoyote ukiangalia ni rahisi zaidi kuliko baadhi ya bei hizi ambazo *other GSM System* zinatumia. Ina *advantage* nyingine

*Thuraiya,* unanifanya nitangaze biashara ya watu, lakini ninazungumzia kiteknolojia, ina *advantage* nyingine *Thuraiya* ni kwamba, kama ulivyosema popote pale ulipo, kama uko baharini, kama umepotea, *still* unaweza kutumia *GPS System,* unapotumia *GPS System* unajijua hapa uko mahali gani, *longitude, latitude, minutes* na hata *location* na ukipeleka *SOS* hata ndege inakuja moja kwa moja pale pale ulipo na kukufikia.

Kwa hiyo, unajue kwamba, bei yake kuwa kubwa ni kwa sababu unatumia mtandao mkubwa zaidi. Lakini *initial cost* tu ambayo ni kubwa, lakini *on the long run* unapotumia kwa mawasiliano inakuwa ni *cheaper* kuliko hizo nyingine.

Juu ya swali la pili kuwa wame-*form cartels* na kwa sababu mmoja yuko mbali na kwamba Tume ya Mawasiliano ifanye kazi yake, mimi naamini Tume ya Mawasiliano inafanya kazi yake. Lakini naamini *exclusivity* ya *TTCL* ikishaondoka tu tatizo hili ninadhani litapungua. *(Makofi)*

Na. 124

**Uanzishwaji wa Vyombo vya Benki Kata**

**MHE. JOB J. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa anafunga hoja ya Bajeti ya Wizara yake tarehe 7 Agosti, 2001 hapa Bungeni alitoa ahadi ya Wizara yake kutoa *Regulatory Framework* ya uanzishwaji wa vyombo vya Benki Kata ambavyo vitawasaidia sana wananchi vijijini:-

(a) Je, ahadi hiyo imetekelezwa vipi?

(b) Je, Benki Kata huandikishwa rasmi katika chombo gani cha Kiserikali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Benki Kata ni vyombo vidogo vya wananchi wa Kata moja ambao huchangishana mafungu ya fedha kama mtaji wa kuweka na kukopa kwa maendeleo ya wanachama. Benki Kata inaweza kuandikishwa chini ya Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003 kama *SACCOS* au *SACCAS,* yaani Ushirika au Umoja au kama Kampuni ndogo chini ya Sheria ya Makampuni au kama *NGO* chini ya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya kutoa *regulator framework* ya uanzishwaji wa Vyombo Kata, mnamo Februari, 2003, Bunge lako Tukufu, lilipitisha marekebisho ya sheria mbalimbali za asasi za fedha *(Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2003),* ambayo yalipelekea kutambuliwa kwa Benki Kata katika Sheria za Fedha *(Financial Laws)*. Hivi sasa rasimu ya kanuni zitakazotumika kusimamia asasi za *Micro Finance* vikiwemo vya vya ushirika vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* na Benki Kata, *SACCAS* iko tayari na inatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha wa 2004/2005 baada ya wadau wote kuiridhia.

(b) Mheshimiwa Spika, Benki Kata zinaweza kuandikishwa na Wizara ya Mambo ya Ndani chini ya Sheria ya *Societies Ordinance* ya mwaka 1954. Aidha, zinaweza kuandikishwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika chini ya Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003 kama *Pre-SACCOS* na *SACCAS* yaani Ushirika au Umoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri mwenyewe wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, amekuwa akisisitizia sana umuhimu wa kuanzisha vyombo hivi vya fedha katika Kata vinavyoitwa Benki Kata na sisi Wilaya ya Kongwa tayari tunazo kumi ikiwa ni pamoja na Benki Kata ya Kibaigwa inayoitwa *Kifi SACCOS,* ambayo sasa hivi inajenga jengo la ghorofa. Sasa naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Je, Wizara hii ya Fedha iko tayari sasa kutenga kiasi fulani cha fedha kama mitaji kuzisaidia Benki Kata hizi kuweza kukua zaidi badala ya kutegemea wanachama peke yake?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kupitishia sehemu fulani ya fedha za pembejeo na mikopo ya wananchi ya kukarabati matrekta yao katika Benki Kata kama hii ya Kibaigwa ambayo inafanya vizuri sana katika eneo hili la Mkoa wa Dodoma, ili waipate kwa karibu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Waziri wa Fedha, amesisitiza juu ya uundaji wa Benki Kata, lakini kama inavyosema sheria, bila shaka wenye umoja wenyewe wawe ndiyo kianzio kama walivyofanya wenye *SACCOS* katika sehemu nyingine mbalimbali kama ile ya Mwanga ambayo Mheshimiwa Mbunge wa Mwanga, alishiriki vya kutosha na kuhakikisha kwamba, inafikia kiwango kile ambacho kinahitajika kwamba, iwe *SACCOS.* Kwa hiyo, hatutakuwa na upendeleo kwa *SACCOS* fulani, utaratibu utakuwa ni hivyo hivyo kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Pili, juu ya kuteua pembejeo, kama ilivyoelezwa katika bajeti wakati Waziri wa Fedha, anatoa bajeti yetu ya mwaka huu, tumesema chombo hiki ambacho kinatakiwa kutoa mikopo kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo, kitakuwa inapeleka hizi fedha kwa hizi *SACCOS* na *SACCAS* na benki nyingine ili kuhakikisha wale wakulima wadogo wadogo hawaendi moja kwa moja katika Mfuko ule, ila kile chombo ambacho kimeundwa kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wameitikia wito kwa kiasi kikubwa sana wa kuanzisha benki hizi ndogo ndogo, Benki Kata na *SACCOS* na hasa wale wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, ambao mpaka sasa wana benki hizo katika kila Wilaya, lakini tatizo kubwa limekuwa ni kutokupatikana kwa mikopo na mitaji kwa urahisi. Je, Naibu Waziri yuko tayari sasa kutunga sheria itayovishirikisha vyombo vyote vya fedha kuhakikisha kwamba, havifanyi upendeleo na kuwasaidia wananchi hao kuwapa mitaji kwa urahisi bila masharti magumu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, imechukua muda kutengeneza hizi kanuni ambazo zitawezesha hizi Benki Kata kufanya kazi zake kwa ufanisi ili kuhakikisha kwamba, yale yote ambayo ni matarajio ya wananchi yanapatikana. Kwa hiyo, hilo lipo na hayo yataangaliwa. Nimesema baada ya wadau kupelekewa zile *regulations* na kuridhia, kwa hiyo, bila shaka wanaohusika wote watahusishwa katika jambo hili.

Na. 125

**Barabara ya Kidodi - Mahenge**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** alijibu:-

Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa Mikoa ya Tanzania yenye ardhi yenye rutuba na mvua za uhakika kwa mwaka mzima na kwa kuwa hali kadhalika wananchi wake wanajishughulisha sana na shughuli za kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kamambe wa kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kidodi - Ifakara na kutoka Ifakara - Ulanga - Mahenge yenye urefu wa takriban km. 150?

(b) Kama Serikali itakubaliana nami kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, je, haioni kwamba iko haja ya kuunganisha Wilaya hizo mbili kwa kujenga daraja kwenye kivuko cha Ifakara kwenda Ulanga?

(c) Kama Serikali haina mpango wa karibuni wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, je, haioni kwamba inawarudisha wananchi hao kwenye dimbwi la umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, ningependa kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Barabara ya Kidodi - Ifakara - Mahenge ni sehemu ya barabara kuu itokayo Mikumi - Ifakara hadi Mahenge ambayo ina urefu wa kilometa 178.14. Barabara hiyo

ina jumla ya kilometa 37.83 za lami, ambapo kilometa 35.23 zipo kati ya Mikumi na Ruaha na kilometa 2.6 zipo katika Mlima Ndololo. Kilometa 140.31 zilizosalia ni za changarawe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa, barabara zote muhimu kiuchumi na kijamii zinajengwa katika kiwango cha lami, tatizo ni ukosefu wa fedha. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la *SDC,* imepanga kufanya matengenezo katika sehemu mbalimbali korofi za barabara hii zenye urefu wa kilometa 58 kuanzia Ruaha hadi Kikwawila. Kilometa 12 katika sehemu hiyo zitajengwa kwa kiwango cha lami na sehemu iliyobaki itatengenezwa kwa kiwango cha changarawe.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa wananchi wangependa kuona daraja linajengwa katika Mto Kilombero. Pamoja na Serikali kutambua hilo na kutamani sana kufanya hilo, bado kikwazo kikubwa ni uwezo wa kifedha wa kutimiza hilo. Aidha, kwa sasa Serikali imeweka kivuko cha uhakika katika mto huo.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya ukosefu wa fedha, Serikali haiwezi kujenga barabara yote kwa lami sasa hivi. Aidha, kama nilivyoeleza katika jibu langu katika sehemu (a) ya swali hili, Serikali inaendelea kufanya matengenezo ya barabara hiyo, ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa mwaka mzima na kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Ulanga wanapata mahitaji yao muhimu kwa kupitia barabara hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu kama ifuatavyo: Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo inalima mpunga ule unaopendwa sana Tanzania, unaitwa tule na bwana na vile vile ili kumpa moyo au nguvu zaidi Mkuu wa Mkoa mchapa kazi aliyekuwepo hivi sasa Mkoani Morogoro; na kwa kuwa Naibu Waziri amezungumza kwamba Serikali haina fedha; je, kwa nini Serikali kwa sasa haitumii Mifuko ya Hifadhi za Jamii ili baadaye utaratibu wa kujenga, kukodisha na hatimaye kukabidhi Serikalini haufanywi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba wananchi wa Mkoa wa Morogoro wanalima mpunga unaoitwa tule na bwana, bado siyo sababu muhimu ya kujenga daraja wakati Serikali haiwezi kujenga daraja. Si vizuri kuwaongopea kwa ahadi kwamba tutajenga daraja hili, isipokuwa kama yupo mtu ambaye yuko tayari, kama iko kampuni tayari kujenga daraja hilo kwa *BOT,* aje Wizarani tutazungumza naye. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Wizara ya Ujenzi imeweka lami aina *alter seal* katika Mlima wa Ndololo kwa umbali wa kilometa 2.5. Je, Wizara haioni kwamba ni muhimu kuweka lami hii ya *alter seal* kwenye Mlima wote wa Ndololo kule Mahenge? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Ujenzi imeweka *alter seal* kwenye Mlima wa Ndololo na hapa kabla sijaendelea, kwa kweli ipo haja ya kumpongeza Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, kwa kufuatilia sana juu ya Mlima wa Ndololo kama vile ni nyumba ya kuishi. Lakini naomba Mheshimiwa Kasapira avumilie, angojee aone hotuba yetu ya bajeti inasema nini? *(Makofi)*

Na. 126

**Barabara ya Usagara - Lusahunga**

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikwisha waahidi wananchi kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Usagara - Sengerema - Geita - Biharamulo - Lusahunga:-

(a) Je, mpango huo umefikia wapi?

(b) Kwa nini mpango huo usijumuishe kipande cha barabara ya Kamanga - Katunguru - Sengerema?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ya kuzijenga barabara zote kuu kwa kiwango cha lami iko pale pale na utekelezaji wake unaendelea kwa awamu mbalimbali sehemu nyingi nchini ikiwemo ya barabara ya Usagara - Geita - Biharamulo - Lusahunga. Ujenzi wa barabara ya Usagara - Sengerema - Geita - Biharamulo - Lusahunga umepangwa kutekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Usagara - Sengerema - Geita - Kyamiyorwa/Biharamulo km. 386 tayari imekwishafanyiwa upembuzi yakinifu kupitia kwa Mhandisi Mshauri wa Kampuni ya *BKS* kutoka Afrika Kusini. Ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 na utatekelezwa kwa utaratibu wa usanifu na ujenzi *(Design and Build)*. Mgharamiaji wa kazi zote ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na *(Makofi)*

(ii) Barabara kati ya Biharamulo - Lusahunga ni sehemu ya mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kagoma hadi Lusahunga km. 154. Zabuni za ujenzi zimerudishwa tarehe 15 Juni, 2004 wakati tuko hapa na mradi huu umepangwa kuanza

kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, kwa fedha toka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).*

(b) Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara ya Kamanga - Katunguru - Sengerema hakikujumuishwa katika mpango huo kwa sababu kipaumbele cha kuweka lami kipo katika barabara kuu zinazounda kanda kuu *(Trunk Roads),* ndiyo kipaumbele cha kwanza kuweka lami katika Tanzania.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa mpango wake, lakini napenda niulize kwamba hii barabara ya Usagala - Sengerema - Geita - Biharamulo mpaka Lusahunga imekuwa vile vile katika mfumo wa mpango wa barabara ya mzunguko wa nchi tatu za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaani Tanzania, Uganda na Kenya, kwa kile kinachoitwa barabara ya kuzunguka Ziwa Victoria. Je, mpaka sasa kuna fedha kiasi gani ambazo zinaweza kuwa zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa sehemu hiyo, pamoja na barabara ya kuzunguka hilo Ziwa Victoria kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa kipande cha Kamanga - Katunguru - Sengerema ni kipande muhimu sana katika mfumo wa usafirishaji katika Kanda ya Ziwa kwa watu na bidhaa. Je, kwa nini Serikali isitafute mpango wa kujenga, kuendesha na kukabidhi *(Build, Operate and Transfer)* kwa wafanyabiashara wakubwa kama *Claus Gaggle* ambao huwa wananufaika na mfumo huo na wameonyesha katika kipindi kilichopita kwamba wangependa kupewa nafasi hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge iko ndani ya mtandao wa barabara zilizo chini ya *East African Community (Lake Circuit)* na ndiyo maana katika jibu letu la msingi tumeeleza hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba, barabara hizi zinatengenezwa kwa kiwango cha lami. Barabara hizi kama zilivyotajwa ni kutoka Usagala - Sengerema - Geita - Biharamulo na nyingine ni kutoka Lusahunga - Biharamulo pamoja na km. 1.5 za Mji wa Bihamulo, Muleba hadi Kagoma.

Hii inaunganisha na barabara ya kutoka Kagoma hadi Mtukula ambayo kwa sasa hivi iko kwenye hatua za mwisho za kukamilika katika kutengenezwa kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na kuunganishwa na ile barabara ya Kyamyilwa. Kwa hiyo, *Lake Circuit* iko kwenye mpango wa kutengenezwa kwa kiwango cha lami na kwa barabara ya kutoka Kagoma - Biharamulo hadi Lusahunga tumepata fedha jumla ya shilingi bilioni 73 kutoka *African Develoment Bank*. Kwenye ile barabara nyingine ya kuja mpaka Usagala tunatumia fedha zetu za Serikali na katika Bajeti ya mwaka huu, zimetengwa karibu shilingi bilioni 8 ambapo itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Kwenye sehemu ya barabara ya kutoka Sengerema, Katungulu hadi Kamanga katika swali lake la msingi ni kwamba, barabara hii ni ya mkoa siyo barabara kuu.

Kipaumbele tunaweka katika barabara kuu. Kuna barabara kuu nyingi hapa nchini ambazo hazijaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami, ikiwa ni pamoja na Arusha, Dodoma hadi Iringa. Kwa hiyo, hatuwezi tukaanza kutengeneza barabara za lami za Mkoa wakati barabara kuu hazijaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Lakini hii barabara tutaendelea kuitengeneza kwa kiwango cha changarawe. Katika bajeti ya mwaka huu, tumeitengea fedha kwa ajili ya kutengeneza kwa kiwango cha changarawe kwa kutumia fedha za *road fund. (Makofi)*

Kuhusu suala la *BOT,* kama wapo wawekezaji wanaotaka kujenga barabara ya kutoka Sengerema hadi Kamanga kwa kiwango cha lami kwa *BOT,* wanakaribishwa hata leo tutawapa Mkataba na kama wapo tayari waje. *(Makofi)*

Na. 127

**Mvua Iliyonyesha Mkoani Singida**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD (k.n.y. MHE. SALOME J. MBATIA)** aliuliza:-

Kwa kuwa miezi kadhaa iliyopita ilinyesha mvua ya mawe huko Mkoani Singida na ikaleta uharibifu mkubwa wa mali za wananchi:-

(a) Je, ni nini maelezo ya kitaalam ya sababu ya kunyesha mvua ya mawe/barafu?

(b) Je, jina la mvua ya namna hiyo ni nini hasa mawe, barafu au nini?

(c) Kwa kuwa si mara nyingi mvua hizo kunyesha, je, watalaam wanaweza kubashiri huwa zinanyesha kila baada ya tukio gani/muda gani?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, ninapenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mvua ya mawe ni mvua inayotokana na kuganda kwa matone ya mvua yanapopandishwa juu ndani ya mawingu marefu sana kufikia sehemu zenye baridi sana za nyuzi joto 45 *centigrade* chini ya sifuri. Mawingu hayo yanayopanda juu sana kwa kitaalam huitwa *cumulonimbus,* hali hii husababishwa na msukumo wa upepo ndani ya mawingu unaosukuma matone/barafu kwenda juu. Matone haya yaliyoganda mawe hupandishwa juu na kushuka na hivyo kuendelea kuwa makubwa. Mawe haya huweza kukua kufikia ukubwa wa mpira wa *tennis.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mvua ya mawe huweza kutokea sehemu yoyote na hasa sehemu zenye miinuko na sehemu ambazo huwa na msukumo wa upepo uelekeao juu. Sehemu zote hizi sharti ziwe na hewa yenye unyevunyevu mwingi.

(b) Mvua hii ambayo huambatana na barafu huitwa mvua ya mawe *(hailstorm).*

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa mvua za mawe hazinyeshi mara ka mara, Mamlaka ya Hali ya Hewa, inao mabingwa wa kutabiri matukio mbalimbali ya hali ya hewa. Wataalamu hawa wanaweza kutabiri matukio kama haya kama wakiwa na vifaa muhimu vinavyohitajika katika kuchunguza na kufuatilia kwa karibu mwendo wa hali ya hewa katika maeneo husika.

Kwa kutumia vifaa viitwavyo *radar,* mawingu yenye ngurumo na maji yaliyoganda barafu huweza kutambuliwa. Kifaa hicho vile vile huweza kukadiria kiasi cha mvua katika mawingu hayo. *Radar* hii ni tofauti na ile ya kuongozea ndege. Mamlaka ilikuwa na vifaa hivi enzi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyovunjika mwaka 1977. Imekuwa vigumu kununua vifaa vingine sasa kutokana na ughali wa vifaa hivyo. *Radar* moja hugharimu zaidi ya dola milioni moja za Marekani ambazo ni zaidi ya shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Msimamizi Mkuu wa sekta ya hali ya hewa, ninamalizia jibu langu kwa kutoa utabiri wa hali ya hewa kwa Mikoa ya Kanda ya Kati yaani Mikoani ya Dodoma na Singida. Leo usiku kunatarajiwa kuwa na hali ya mawingu kiasi pamoja na baridi, kiwango cha chini cha joto kinatarajiwa kuwa nyuzi joto 13 *centigrade*, kesho mchana kunatarajiwa kuwa na hali ya mawingu kiasi na vipindi vya jua. Pepo katika ukanda wa kati zitavuma kutoka mashariki kwa kiasi cha kilometa 30 kwa saa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud una maneno? *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Hapana. *(Kicheko)*

Na. 128

**Kuimarisha Reli Kati ya Manyoni na Singida**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* wamefanya kazi nzuri ya kuanzisha huduma ya usafiri wa Reli kati ya Dodoma na Singida kupitia Manyoni na kwa kuwa ili kuboresha na kuimarisha reli kati ya Manyoni na Singida inahitaji kushindiliwa kokoto na kujengwa magenge na kuwekewa mawasiliano ya simu. Je, kazi hizo zitaanza kushughulikiwa lini?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuimarisha reli kati ya Singida na Manyoni itaendelea kufanyika kwa kutumia uwezo wa Shirika la Reli Tanzania na fedha za Bajeti ya Serikali chini ya Wizara yangu. Katika kipindi cha kuanzia Mei, 2003 hadi kufikia Mei, 2004, Shirika limebadilisha reli za uzito wa *pound* 50 kwa yadi na kuweka za uzito wa *pound* 56 kwa yadi, umbali wa kilomita moja na nusu. Hali kadhalika mataruma yamebadilishwa na kokoto imemwagwa umbali wa kilomita mbili kwenye sehemu korofi likiwemo eneo la Choda. Katika kuimarisha tuta, kilomita 34.25 zimeimarishwa, sambamba na kupigilia reli, usafirishaji wa mifereji ya maji, ulimaji na ufyekaji wa majani na vichaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu njia za mawasiliano Stesheni za Manyoni, Ikungi, Puma na Singida, kuna mawasiliano ya Redio ambayo yanatosheleza uendeshaji wa shughuli za treni. Shirika pia limejenga sehemu za kusubiri abiria wanaposubiri usafiri *(Waiting Shelters),* Puma, Ikungi na Singida Mjini. Kwa upande wa ujenzi wa magenge tayari magenge mawili, Genge Na. 1 na Genge Na. 2 kati ya 11 yanayohitajika yamejengwa na kukamilika. Ujenzi wa Genge Na. 2 umeanza na tayari asilimia 80 ya ujenzi imekamilika. Magenge mengine yatajengwa kufuatana na hali ya fedha.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 mpaka 14 Julai, 2001, nilisafiri kwa kiberenge na kujionea mwenyewe hali ya reli ya Manyoni, Isuna, Ikungi, Puma na Singida. Katika safari hiyo nilifuatana na Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Jumanne Nguli, Mheshimiwa Samuel Nyalandu na Mheshimiwa Leonard Shango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa safari hizi za ukaguzi wa reli, wenzangu wamenipa heshima kubwa ya kunipa cheo kinachoitwa *Pigilia Grade Three,* yaani Genge *Man* Namba Tatu, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wananchi wa Singida wanamwamini sana Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na kwa kuwa tuliposafiri pamoja kwenda Singida, aliahidi kwamba, ngejitahidi zile kazi nzito nzito zikamilike wakati yeye akiwa bado ni Waziri. Je, atajitahidi kukamilisha hizi kazi mapema iwezekanavyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, dhamira ni kukamilisha kazi ambazo tumekuwa tumetarajia kuzifanya kabla ya mwaka 2005, fedha zilizopo ni kwamba, mmenipatia katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, shilingi milioni 100 kwa mwaka kwa reli ya Manyoni - Singida na reli ya Kaliua -

Mpanda. Kwa hiyo, ni kiasi kidogo lakini tunaweza kufanya yale tunayoweza kuyafanya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Tangazo la kikao cha Kamati ni Kamati moja tu ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 25 Juni, 2004 kuanzia saa 5.00 asubuhi watakuwa na mkutano Chumba Na. 227 ghorofa ya pili.

Kesho Jumamosi hatukupata aliyekuwa tayari kutoa semina kwa Wabunge wote, lakini tulimpata mmoja anaitwa *Basic Needs*, wapo chini ya Wizara ya Afya, wanashughulikia kitu kinachoitwa Afya ya Akili na wana Mradi Maalum unaotekelezwa katika Mkoa wa Mtwara, unaoitwa Mradi wa Afya ya Akili *(Mental Health and Development Project).* Wao wako tayari kutoa semina kwa Wajumbe wa Kamati tatu zifuatazo: Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Huduma za Jamii, Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mtwara, ambako mradi unatekelezwa. Kamati inayohusika moja kwa moja na Wizara ya Afya ni Kamati ya Huduma za Jamii, lakini Mwenyekiti wake ameniambia anaondoka kwenda kwenye shughuli nyingine, kwa hiyo, Mwenyekiti wa Semina kesho atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mwisho, wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niongee machache tu kuhusu Wizara yetu ya TAMISEMI. Kwanza kabisa, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake.

Kwa hiyo, hotuba hii imetoa sehemu kubwa ya dukuduku za Wabunge katika maeneo mengi ambayo ameyazungumza. Pamoja na nia nzuri ya Wizara kufanya mambo yake na shughuli zake lakini kazi nyingi za Wizara hiyo zinatoka katika Wizara nyingine hasa ukifikia ngazi ya *DC* au *DED.* Halmashauri zilizopewa shughuli zote kutoka kila Wizara zinaishia kwenye ngazi ile ya *DED* na *DED* husaidiwa zaidi na Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji na hao ndio tuna shida nao kubwa kwa vile hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ningependa kujua kama hiyo Kada ipo *officially* kwenye kompyuta ya Hazina? Maana Walimu tunawaweka kwenye kompyuta na wao wanakwenda mpaka vijijini. Lakini hawa Watendaji inaelekea wakati kabla ya kufuta zile kodi walikuwa wamepewa tu kama *contractors* au wakandarasi wa kukusanya kodi.

Kila wanavyokusanya na ndivyo *percent* zao za mshahara zinatolewa hapo. Wasipokusanya hawapewi. Kwa hiyo, kule pia wanazidai Halmashauri mbalimbali hawa Watendaji.

Mheshimiwa Spika, halafu baada ya kuchukuliwa na Serikali Kuu mwaka 2003, wanasema wangeanza Januari, 2004. Sasa kipindi kile cha Julai, mpaka Januari bado kinadaiwa na Januari mpaka sasa wengi bado wanapata matatizo ya kupata mishahara yao. Nadhani ningeomba Wizara i-*regularize salaries* za hawa watu wawe nao kwenye kompyuta na tujue wameajiriwa na Serikali. Sasa hivi hawana uhakika kama wameajiriwa na Serikali au na *DED* peke yake kwa mtindo ule wa ukandarasi.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la umaskini au ufukara wa Halmashauri mbalimbali, tuseme Halmashauri karibu robo hazina mapato kabisa. Hawana njia ya kupata mapato, Songea ikiwa mojawapo. Halmshauri yangu ya Songea sisi kazi yetu hasa ni kulima mahindi na kuuza. Sasa katika kulima na kuuza mahindi hakuna *channels* ambazo ziko *proper, the only channel* inayojulikana kabisa ni ile ya *SGR.* Lakini *SGR* hawalipi kodi maana wao wanasema hawafanyi biashara. Kwa hiyo, wakulima wa Songea wanalisha nchi, wanapata fedha, lakini Halmashauri yao haiwezi kupata fedha kwa sababu wanachouza kinauzwa barabarani na mitaani na Serikali ilishatoa vizuizi vya njiani vya kukusanya hayo mapato. Sasa vile vizuizi vimetolewa na kodi hiyo sasa imefutwa, kwa hiyo, hatuna. Nidhani kuwa wangetufanyia *HIPC* ya ndani, watutengenezee utaratibu wa kutupa ruzuku kubwa kuliko vile inavyokuwa kwa Halmashauri kama za Dar es Salaam zenye mapato ya shilingi ya bilioni 60 au bilioni 50. Sisi hata kufika shilingi milioni 50 ni kazi kubwa sana. Nilidhani kuwa zipo Halmashauri kama hizo mbili, nadhani nne, tano, hivi zingepewa umuhimu wa pekee wa kupewa upendeleo katika ruzuku.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nataka kuzungumzia ni mfumo wa ujenzi na utunzaji wa barabara. Tunayo *TANROAD*. Sasa *TANROAD* nao wana *structure* yao, wana Bodi yao, pamoja na *Managing Director* wao na hivyo wanakwenda mpaka Mkoani, sasa Mkoani wamechukua tu wale waliokuwa *Regional Engineers,* sasa wamekuwa *Regional Managers* wa barabara. Sisi tumebaki hatuna *Regional Engineer as such*, angalau tumebaki na wale wanaoitwa watunza nyumba wa Idara ya Nyumba na Idara nyingine ya *Engineering.* Lakini *TANROADS* ndiyo yenye uwezo. Sasa uhusiano wa *TANROAD* na ile inayoitwa *Regional Road Board* ni *very weak.* Hiyo *Regional Road Board* kazi yake ni kusikiliza zaidi maelezo na nini wamefanya na habari zao wanazofanya hazieleweki, hawasemi kwa undani kabisa kuwa wao wanafanya kazi kwa ajili ya Wizara yao na sijui kama inapitia *TANROAD Headquarters* au kazi za Wizara zinaenda moja kwa moja *TANROADS* Mkoani, hakuna uhakika huo. Kwa hiyo, wanapata fedha za *Road Fund* halafu wanapata fedha za Mashirika ya Kimataifa, kwa mfano, *Africa Development Fund* za *World Bank* za miradi mbalimbali kama kwetu kule tulipata za *European Union.* Sasa hatujui hizo zikienda *TANROAD* zinapitia *TANROAD Headquarters,* zinakuwa *co-ordinated* moja kwa moja toka kule mpaka chini au zinakwenda moja moja toka Wizarani mpaka kwa *Regional Engineer* au Mheshimiwa Rais. Hiyo hatujui.

Mheshimiwa Spika, hiyo hatujui, halafu ukifanya uhusiano wa *TANROAD* na *District Engineer* ndiyo *even more confusing,* ina matatizo ya kuelewana na kusaidiana. Tunasema huyo akiona barabara haifai anasema hii ya *District Engineer* na *District Engineer* ndiyo kama alivyo *DED,* hana uwezo, yeye ndiyo kabisa hapati kitu na tunakuwa tunaongea habari ya *theory* kuliko *practical* za kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninaitaka kuzungumzia ni kuhusu hizo *NGOs* hasa za nje, ni kuwa zimepewa *blank check* ya kuchagua Mikoa na Wilaya na mahali wanapotaka kufanya kazi na wanavyotaka kufanya kazi. Sasa hiyo inaleta *distort* kabisa katika utaratibu wa maendeleo wa nchi nzima. Utakuta Mkoa au Wilaya fulani zina *NGOs* zaidi ya tano, halafu pia inapewa tena pesa toka Mfuko wetu wa Taifa. Sasa utakuta zile zinakwenda na Mikoa mingine haina *NGO* kabisa. Ukiwauliza wanasema wao wana ruhusa ya kuchagua wapi wanakwenda.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kuwa labda tuweke vigezo maalum kwa ajili ya hizi *NGOs* na hasa vigezo vipendelee Mikoa ile ambayo iko chini kabisa kwa mapato ili waweze kupata na wao unafuu wa kutengeneza hizo njia zao za mapato. Lakini sasa tukiwaachia wao wachague watachagua sehemu zile ambazo wanasema *more assessable* kama Kilimanjaro, kuna barabara, kuna reli, kuna *international airport,* basi wengi watapenda kwenda kule kwanza kabla hawajaenda Rukwa, utakwenda wakati *from Dar es Salaam to Rukwa is thousand kilometers,* wengi wanasema hapana.

Mheshimiwa Spika, sisi ilitupata hiyo upande wa Songea ambako tulikuwa na *SNV,* mwisho wakasema kuwa wanashindwa ku-*co-ordinate* kati ya zile za katikati na za Arusha na za Songea, mbali sana huko Songea. Kwa hiyo, wameondoka. Mbali ndiyo ilikuwa zaidi watupe sisi zaidi kuliko wale waliokuwa karibu kwa kuwa wale wako mbele zaidi. Lakini ndiyo hili ninasema kuwa labda *NGOs* hizi zitengewe vigezo kuwa kama mtakuja Tanzania tafadhali tuna vigezo kadhaa, mnaweza mkaingia, chagueni pale au hapa na *preference* itakuwa kadri ya shughuli wanazokuja kuzufanya, kama ni zaidi shida za mjini basi waende mjini. Kama ni Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na kadhalika. Kwa hiyo, hayo nadhani yalikuwa ya kwangu machache, zilikuwa hasa pongezi tu.

Ninatoa pongezi kwa Wizara, Waziri wenyewe, Naibu Waziri na Watendani wote wa Wizara ya TAMISEMI na kila la kheri kwa mwaka huu unaoanza 1 Julai, 2004. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini kabla sijazungumza kutokana na msiba tuliopata, ninaomba nitoe rambi rambi zangu kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Babati Mashariki, kwa Wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa kufiwa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego. Kwa kweli kati ya Wabunge ambao walikuwa wapole humu ndani na wanaozungumza kwa utaratibu, yeye ni mmoja wapo. Tunaomba wenzetu wa Mbeya wawe na subira, wawe wavumilivu katika kipindi hiki ambacho kwa kweli ni majonzi makubwa na Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitumie nafasi hii nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba aliyoiandaa pamoja na wenzake wote na nitumie nafasi hii kusema machache yatakayohusiana zaidi na jimbo langu la Babati Mashariki. Katika eneo hilo nitazungumzia zaidi barabara na mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Mji wa Babati. Mji wa Babati ndiyo Makao Makuu ya Mkoa Mpya wa Manyara. Mji wa Babati sasa ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Babati. Kutokana na hali hii ya Babati kuwa Makao Makuu ya Mkoa pamoja na Halmashauri ya Mji, tumekuwa na ongezeko kubwa sana la watu, ongezeko kubwa la magari, ongezeko kubwa la biashara na huduma zingine ambazo sasa zinahitajika kwa kiwango kikubwa ikiwa ni pamoja na huduma za afya na huduma za maji. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile na kwa vigezo vyovyote, Babati inahitaji kuwa na miundombinu mipya kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa Babati tunaiangalia kama mtoto aliyezaliwa na TAMISEMI. Sasa mtoto huyu ambaye amezaliwa na TAMISEMI ni lazima baba yake awe na majukumu na majukumu ya baba kwa mtoto ni kuhakikisha mtoto anapata chakula cha kutosha na kizuri, anapata mavazi, matibabu na vile vile anapata ulinzi na mahali pa kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wajibu wa TAMISEMI kuhakikisha kwamba, Babati inakuwa na kwa kawaida mtoto akizaliwa hata majirani hupongeza, hupeleka zawadi, huwapa moyo wale ambao wamepata mtoto. Kwa hiyo, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao mlitupongeza wakati tulipopata Makao Makuu ya Mkoa na Halmashauri ya Mji wa Babati. Tunawashukuru sana kwa kutupa moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme sasa mahitaji ya mtoto huyu, nianze na mji wenyewe wa Babati na hasa barabara. Mji wa Babati ulikuwa Kijiji sasa una hadhi ya Halmashauri ya Mji. Kwa hiyo, tunahitaji barabara zinazofanana na hadhi ya mji. Kwa sasa hivi barabara zilizopo kwa kweli ni za vumbi, kwenye mitaa ni makorongo matupu. Hakuna mifereji ya maji, hatuna soko zuri na maeneo mengi ya biashara. Kwa ajili hiyo, tunahitaji kwa kweli kuangaliwa kwa namna ya pekee kutoka kwenye ngazi ya kijiji. Kutoka kijiji mpaka kuwa Makao Makuu ya Mkoa na Halmashauri ya Mji, kwa kweli ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheheshimiwa Spika, katika hali hiyo, jana nilimfuata Waziri wa Ujenzi, nikamwambia tatizo hili la barabara ndani ya Mji wa Babati, akaniambia barabara za mji wa Babati yupo mwenyewe na mwenyewe ni Waziri wa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi nikamwambia wewe na Waziri wa TAMISEMI ndiyo tunawapa fedha za barabara, sasa niambie mwenzako umempa kiasi gani na wewe umechukua ngapi? Akasema mimi bado. Akaniambia basi utakuta kwenye bajeti yako. Lakini mwenzangu yeye amepewa shilingi bilioni 22. Sasa kama ninasema uongo basi

Waziri wa Ujenzi ni shahidi, maana nilimwuliza na aliniambia kabisa. Sasa shilingi bilioni 22 basi atumegee hata shilingi bilioni moja, maana Babati ni mtoto. Tunahitaji barabara za mji walau hata Waheshimiwa Wabunge mkipita pale wakati mnaelekea kwenye Makao Makuu ya Afrika Mashariki, mpite mahali ambapo panaonekana pana hadhi ya mji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri katika shilingi bilioni 22 ambazo umepewa basi utusaidie walau hata shilingi bilioni moja na nina hakika kwamba, sisi katika ngazi ya Mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, aliandika barua ambayo sisi tunaikiri, akiomba fedha karibu shilingi milioni 700 na nadhani yupo kama hajafika hapa sijui, lakini nadhani atakuwepo leo, kwa hiyo, nadhani ananisikia na ninashukuru kama yupo. Kwa hiyo, barua hii ambayo umeandikiwa nataka nikuhakikishie kwamba, umeandikiwa kwa niaba yetu sisi Wananchi wa Babati na hasa Wabunge tunaotoka huko. Kwa hiyo, tunaomba sana jambo hilo liwekewe msisitizo mkubwa kabisa, la barabara za Mji wa Babati. Nafahamu wewe mara nyingi umefika pale Babati lakini hatujawahi kukutembeza kwa miguu, ungetoka katikati ya mji ukafika kule Mkuu wa Mkoa anakoishi, nadhani ungefahamu. Lakini wakati ujao karibu sana Babati, utembee kwa miguu kidogo ujionee wewe mwenywe hali halisi na kwa sababu umeshakuja mara nyingi hutakuwa mgeni sana. Kwa kweli kwa nyakati za kiangazi Mji wa Babati una vumbi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaotoka upande wa Magharibi wakienda Mashariki inabidi watembee kinyumenyume kwa sababu ya vumbi kubwa. Kwa hiyo, ni hali ambayo kwa kweli si nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani hilo niliachie hapo, ili wananchi wetu waweze kuondokana na umaskini basi hali ya Mji wa Babati ikiwa nzuri nina hakika kwamba, wenzetu wanaozunguka mji wataweza kuwa katika hali ya biashara na kwa kweli wanaweza wakapunguza umaskini na kukua kwa biashara. Miundombinu hakuna.

Mheshimiwa Spika, niende vile vile kwenye barabara za Mkoa ambazo zipo kwenye jimbo langu. Tunayo barabara ya Mbuyu wa Wajerumani, hii inahudumiwa kimkoa, nashukuru na ninaipongeza Wizara ya Ujenzi. Nimeona kuna shilingi milioni 50 zimewekwa pale walau zitasaidia na hasa zisaidie sasa katika maeneo ya madaraja na kuweka tuta kati ya maeneo ya kutoka Mbuyu wa Wajerumani na Maghala katika sehemu za Kou na kuinua lile tuta na kwenye Mlima Magara, baadaye nadhani itabidi iwekwe lami nyepesi hasa ile *sand seal* kwa sababu ni kati ya milima ambayo kwa kweli ni mikali kidogo.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni suala la barabara kati ya Makao Makuu ya Mkoa Babati na Wilaya ya Simanjiro na Kiteto. Barabara ambayo inaanzia eneo linaloitwa Singe inapitia Galapo inakwenda Olekosleimet Wilaya ya Simanjiro na Mji wa Kibaya Wilaya ya Kiteto. Barabara hii ni ya ahadi ya Rais wakati anaunda huu Mkoa na kwa sababu ni ahadi ya Rais na ameahidi kabisa kwamba, barabara hii itatengenezwa wakati akiwepo. Basi na barabara hii itakuwa kubwa kwa vyovyote vile itakuwa kwenye

ngazi ya *trunk road,* ambayo ina kilomita si chini ya 250. Gharama za ujenzi inavyoonekana baada ya Mhandisi kufanya tathmini yake inafikia shilingi bilioni 9. Hii ndiyo gharama ya kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara, pamoja na Wilaya zake. Barabara inahitaji shilingi bilioni 9. Sasa katika bajeti ya mwaka 2003, kidogo yale maeneo ambayo sasa hivi yalikuwa yanaendelea kuhudumiwa na Halmashauri za Wilaya kwa sasa yametengwa shilingi milioni 330 na kwenye bajeti hii kama 300, jumla ni shilingi milioni 630. Lakini barabara ni shilingi bilioni 9. Sasa milioni 630 kwa mwaka itakuwa ni tatizo kubwa sana. Tutachukua zaidi ya miaka 10 kujenga barabara hii.

Ninaomba barabara hii iwekwe katika Mpango Maalum kama barabara zingine. Kwa leo asubuhi namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, amejibu kwamba barabara ya Usagara mpaka Lusahunga zimetengwa fedha za ndani karibu shilingi biloini 8. Naomba basi ndugu yangu tumia huo ujuzi tusaidie na sisi ya kwetu ni shilingi bilioni 9. Tusaidie, tuikamilishe na ijengwe walau kwa awamu tatu. Mwaka huu zikitolewa shilingi bilioni tatu, mwaka unaofuata shilingi bilioni tatu na mwaka wa mwisho shilingi bilioni tatu, basi Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na Wilaya zake utaunganishwa vizuri. Barabara hii ni lazima iwekwe kwenye Mradi Maalum.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo hatutafika mbali kwa hela ndogo kama hii shilingi milioni 630. Sasa hivi fedha hizi ndogo zinatengeneza eneo dogo tu la kilometa 17 kati ya Singe au Babati na Galato. Kwa hiyo, ni fedha kidogo sana. Kwa hiyo, tunaomba kabisa iwekwe kwenye mpango wa Mradi Maalum na hasa kwa sababu hii ni ahadi ya Rais kwa kweli ingependeza zaidi iwekwe kule.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni barabara za lami. Tuna barabara ambayo iliahidiwa na Wizara, Barabara ya Otasil kilometa tatu walau kusafisha uso wa mji ule wa Babati na kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Nashukuru Waziri wa Ujenzi, baada ya mazungumzo tuliongea jana, akanihakikishia kwamba, kilomita hizi tatu sasa zitatengenezwa. Kwa hiyo, tunakushukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni barabara kutoka Minjingu hadi Babati kwenda Singida. Nimeona kwenye bajeti zimetengwa shilingi bilioni mbili. Mwaka 2003 ilikuwa shilingi milioni mbili za upembuzi yakinifu. Lakini safari hii nimeona shilingi biloni mbili. Sasa pengine wakati wa hoja yako tutapenda kufahamu hizi shilingi bilioni mbili zitafanya nini na kwa sababu tunataka kujenga barabara ya lami kutoka Minjingu - Babati - Singida na hii barabara ni muhimu sana kwa sababu ina magari mengi sana, inahitaji matengenezo ya kila baada ya miezi mitatu, kwa kweli ni jambo ambalo ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea ni suala la ugawaji wa vijiji. Kuna vijiji ambavyo ni vikubwa na hii ni ahadi ya Serikali vile vile ni hitaji la kisheria kwamba, kila kijiji kinapaswa kuwa na vitongoji vitano. Sasa vijiji vingine ni vikubwa na vichache kati ya vile vikubwa kwenye jimbo langu ni hivi vifuatavyo: Minjingu, Mwada, Kisangaji, Magala, Samasi, Tashi, Kirundugu, Sigino, Lalapo, Endakiso na Mayoka. Vile vile Mji wa Magugu ambao sasa una wakazi zaidi ya

12,000 nadhani sasa unapaswa kupata hadhi ya kuwa Mji Mdogo na tukitaka kuendeleza miji yetu ni vizuri tukaanza kuhakikisha kwamba, miji inapanda hadhi inapofikia idadi inayotakiwa na zile sifa zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka kabisa la mwisho nizungumzie waliojenga kwenye barabara au hifadhi ya barabara. Babati ilikuwa *minor settlement* kabla ya mwaka 1996. Kwa hiyo, sheria zilizokuwa zinatumika kwa *corridor* ya barabara ilikuwa ni mita 25 kwa sheria zilizokuwepo baada ya kutangaza kuwa *planning area.* Lakini baadaye ilipoonekana kwamba, kuna haja ya kupitisha barabara kubwa hapo katikati ndipo ndipo Mkurugenzi na Kamishna wa Ardhi walipokubali kwamba, basi ramani iliyokuwepo sasa ibadilishwe. Basi ni vizuri kama ramani hii ilishabadilishwa, imeshakubalika, wale walioko kwenye yale maeneo ambao sasa wanaathirika na hizi mita 45 basi ni vema walipwe na ipo mifano katika maeneo mengine ambayo watu wamelipwa kwa sababu Sheria ingekuwa inatumika zilikuwa ni za *minor settlement.* Kwa hiyo, ni vizuri suala hili likashughulikiwa na Halmashauri pamoja na Wizara ya Ardhi na Wizara ya Ujenzi. Hakuna haja ya kusononesha wananchi wakati wana haki zao. Ni vyema walipwe kama wana haki basi ile barabara ijengwe na wote tunaihitaji kweli barabara.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kutoa pongezi kwa Chama cha Walimu Tanzania, kwa kusimamia kidete kutetea haki za Walimu. Naomba niwashukuru vile vile na kuwapongeza Wabunge kwa kutambua na kujali madai na maslahi ya Walimu. Lakini kubwa zaidi nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kabla hujaanza ngoja niwataarifu kwamba, Waheshimiwa Wabunge wanne waliokuwa wamejiorodhesha kuchangia siku ya leo wameondoa majina yao. Kwa hiyo, nimebaki na hawa wafuatao, baada ya Mheshimiwa Aggrey Mwanri atafuata Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Chiristopher Wegga, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Edward Ndeka na mwisho Mheshimiwa Isaac Cheyo. Kwa hiyo, wajiandae.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sisi Wananchi wa Jimbo la Siha, tumepokea kwa masikitiko makubwa sana taarifa za kuondokewa na ndugu yetu mpendwa, Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego. Leo asubuhi tu kwenye *corridor* za Bunge wenzangu waliniambia kwamba, tumeondokewa na ndugu yetu huyu mpendwa.

Kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Siha, ninachukua nafasi hii kuipa pole familia yake, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Ndugu Yete Mwalyego mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuomba msamaha, hii sauti kama unavyojua itapanda tu na juzi *TBL* walinipa zawadi kwa sauti na mchango wangu hapa Bungeni. Naomba niombe msamaha sauti hii kuipunguza inakuwa ngumu na huwa inapanda kidogo kidogo hivyo hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nichukue nafasi hii kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba yake ya mwisho hapa Bungeni alipokuwa ana-*wind up,* ilinifurahisha hasa hasa alipotatua lile tatizo la Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeomba nizungumze kwenye Wizara yake lakini sikupata nafasi lakini naomba nichukue nafasi hii wakati tunapoijadili hii Ofisi ya Rais (TAMISEMI), nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba ile ilikuwa ni *scientific,* nafikiri imetupeleka mahali pazuri, naiunga mkono na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, kwa hotuba nzuri aliyoitoa. Siku hizi nikiwatumia hawa jamaa ninapata tabu, ninataka nimtumie Abraham Lincolin ndio inaonekana ni *contemporary,* unakwenda vizuri. Abraham Lincolin aliwahi kubadili Wakuu wake wa Jeshi mara saba, anambadili huyu, anamweka huyu anamwondoa, anamweka huyu anamwondoa, mwisho kabisa alikuja kuishia na bwana mmoja anaitwa Grant ndiye alikuja kuwa Mkuu wake wa Majeshi ambaye alifanya kazi nzuri sana. Huyu Grant alikuwa na matatizo yake, ana hasira, ana hamaki, anachukuiana na watu, anakunywa pombe wakati mwingine analewa, Waziri wetu huyu siyo mlevi wala hana hamaki. Abraham Lincolin akaulizwa kwa nini unamchukua huyu Grant ambaye ana matatizo yote haya? Akasema: "Kila tunapokwenda kwenye vita tunashinda, Grant akiongoza vita tunashinda, mimi kwa msingi huo namchukua Grant". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hapa ndani yamesemwa maneno mengi sana kuhusu Waziri wetu huyu, ana Wizara kubwa, Wizara ambayo ndio inayofanya kazi ya kufunga magoli. Ukisema MMEM kule mbele mimi ninaiona TAMISEMI ndiyo itakayofanya kazi ya kwenda kufunga goli. Ukisema afya kule mbele naiona TAMISEMI ndio itakayokwenda kufunga bao. Ukisema kilimo, *extension services,* huyu ndiye atakayekwenda kufunga bao. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, *and it is my judgment as a Member of Parliament* kusema kwamba, kazi anayofanya Brigadia ni kazi nzuri, ameonyesha utumishi wa kutukuka. Wakati mwingine ukitaka kuwa *objective* jiweke kwenye nafasi yake halafu jiulize ingekuwa ni mimi nimekaa pale ningefanyaje? Sikuona tatizo lolote, kazi yake ni nzuri. Mafanikio makubwa tuliyoyapata katika eneo la MMEM, tunasahau hilo, ni kweli kabisa Wizara ya Elimu imefanya kazi nzuri lakini wafungaji bao ni TAMISEMI. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri na ninaunga mkono kazi inayofanyika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marehemu Mao Tse Tung aliwahi kusema maneno yafuatayo: "Tatua tatizo la msingi kwanza halafu hayo mengine yote yanaondoka, *resolve the primary contradiction first the secondary one will go automatically."* Tatizo la

msingi katika nchi yetu ya Tanzania ni umaskini. Hii kelele yote unayoisikia humu ndani, vita yote unayoisikia humu ndani, *its particularly because* nchi yetu ni maskini. Uki-*resolve* tatizo la umaskini unaweza usiwe na bajeti ukaingia humu kwa sababu una hela ukagawa tu, unazo! Bajeti ni *realization* ya kwamba, *resources* zako ni kidogo kwa hiyo unahitaji ku-*budget* ili uweze kuzitumia vizuri ili kila mtu aweze kupata. Uki-*resolve* hiyo *problem* huna tabu. Wenzetu mabepari wanakwenda wakiwa na pesa hawana matatizo sisi tunafanya nini katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, hela yako unapata kutokana na kilimo na unaambiwa kwamba 55% ndiyo yako 45% unategemea kutoka nje, unafanyaje katika hilo? Nchi hii ni ya kilimo unapata hela kutoka kwenye kilimo, madini, utalii, unachukua hiyo unaipeleka kwenye matumizi, unatumia yote imekwisha, *development* ni ziada. Kama umekula zote zimekwisha umesomesha watoto, umekwenda hospitali, mmevaa nguo, mmelipa Majeshi, mmelipa mishahara zimekwisha, hakuna *development* mpaka utengeneze ziada ndipo unapoweza kuwa na maendeleo. Hapa kwetu tunakula, tunamaliza, habari imekwisha! Sasa ukimaliza hapo huyu mtoto wa Mungu utamparamia tu, wewe ni mtu wa ajabu na nini, mimi nafikiri tu-*address* hiyo, hela inayotokana na maeneo hayo sehemu kubwa ya hela hiyo irudi kwenye *production unit* pale chini. Marx alisema: *"Always the economic base determine the superstructure".* Unayosema hapa yatakataliwa hapa chini kwa sababu huna uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, nilishtushwa sana na ile *statement* iliyosema kwamba, nina miwani hapa naomba niisome, nitasema eneo moja tu halafu nitakaa, ukurasa wa tatu unasema: "Hivyo katika mwaka huu wa fedha, Serikali haikusudii kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Hali ya uchumi itakapoimarika Serikali itaendelea kugawa maeneo mapya ya utawala, yale ambayo kwa kugawanywa yanaleta manufaa kiuchumi, kisiasa na kijamii."

Mheshimiwa Spika, najua ni sehemu ya hiyo ninayoisema lakini naomba nieleze, *decentralization* ilikuwa inamaanisha unapeleka madaraka na huduma muhimu karibu na wananchi. Imeelezwa hapa, wenzetu wamezungumza, tumeeleza kwamba, kuna haja ya kuangalia mazingira ya nchi yetu na kuhakikisha kwamba, tunapata maeneo mapya ya kiutawala. Ni kweli kabisa *resources* zetu ni ndogo na juzi Rais alipokuja hapa tuliambiwa kuna Wilaya mpya zimeanzishwa na tukaahidiwa kwamba, huko mbele ya safari Wilaya nyingine zitakuwa zinaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Serikali kuhusu vigezo ambavyo vinatumika katika kuangalia suala zima la kuanzisha Wilaya mpya za kijamii, za kisiasa na za kiuchumi, ni sahihi kabisa. Pia nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo kwamba, suala la *population* nalo ni muhimu lakini kwa nchi kubwa kama Tanzania huwezi kuishia kwenye suala la *population* tu, utaangalia mazingira ya eneo lenyewe kihistoria, hali ya maisha ya wananchi, uchumi wao ukoje, utaangalia utamaduni wao, huwezi kuishia kwenye *population* tu, *population* ni moja ya kigezo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza hapa tunao wenzetu wa Zanzibar ni nchi ile, ile nchi ukisoma historia yake na taratibu nzima, *culture* na mambo

yalivyokwenda toka walivyotawaliwa huwezi kusema kwa vile wako 800,000 hatuwezi kuwatambua kama nchi. Ile ni nchi na tukisikia mtu anasema ile siyo nchi, tutamshangaa! Ungesema unakwenda kwa kigezo cha *population* tu, ungesema hivi, hii wala hai-*qualify* kuwa Mkoa wala kuwa Wilaya lakini kwa sababu ya historia yake na namna tulivyokwenda unatambua hilo. Burundi, Rwanda zile ni nchi ndogo tu nazo hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais alikuja katika Jimbo la Siha, tukamweleza nchi yangu ya Siha ni nchi ya wakulima na wafugaji, sisi tuko hapa katikati. Sisi hapa ni Wamasai, Mheshimiwa Edward Lowassa anafahamu, Mheshimiwa Lekule Laizer anafahamu, Mheshimiwa Benedict Losurutia anafahamu, mimi ni kiongozi wa Wamasai, eneo ambalo liko nyuma kimaendeleo, eneo ambalo halina *dispensary,* eneo ambalo halina shule, eneo ambalo halina barabara wala majosho. Tukamlilia Rais akaja katika Jimbo letu la Siha, Rais, tunakuomba, baba hapa upende usipende mzee wetu cha kutusaidia hapa ni kupata Wilaya nyingine mpya. Mimi nakaa na Mheshimiwa Lekule Laizer hapa, lakini hii Kilimanjaro, Kilimanjaro niko mbali, mimi niko Olmoluk, nikutajie vijiji vyangu Olmolil, Olkolil, Donyomoruak haya ni majina ya Kimasai mkiniacha hapo katikati hivi nirudi nyumbani nikawaambie wananchi wa Siha Serikali imeniambia hatugawi tena, niwaambie nini wazee wangu, mnanitakia mema mimi? Hebu naomba mnisaidie, Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili nimelisema sasa mnatakaje, nilie hapa Bungeni?

**MBUNGE FULANI:** Aaah, usilie.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Nisilie siyo, basi afadhali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tukamwomba, ukisema tu unajua wale ni wachache sana wamekaa pale, nenda kaangalie hali ya maisha ya wananchi wale, hatuko Arumeru, hatuko Mondulu, huku Hai huku pembeni, mimi natoka Kamangwa nakwenda mpaka kule Bomang'ombe tunakwenda na Mheshimiwa Lekule Laizer, tunafuata hiyo barabara moja. Chonde chonde wazee wangu, Serikali nawaombeni, tuliomba jambo hili, mkituambia hapa kwamba eti hatuzungumzi hilo, mimi hapa ndio basi. Ninawaambieni, Waziri Mkuu, jambo hili baba unalifahamu mzee wangu unalijua wacha niliseme hapa hebu nisaidie mzee wangu wale wananchi wa Siha waweze kwenda Benki, unakwenda pale ni wachungaji wanatembea mpaka sasa hivi mnaanzisha Daftari la Wapiga Kura sijui mtakwenda kuwapatia wapi? Watu wanasema Kilimanjaro, natoka Kilimanjaro mimi, Mheshimiwa Edward Lowassa Olmoluk ni Kilimanjaro? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, najua huu ni utaratibu wa nchi wa kutuchanganya namna hiyo, mzuri tu niko kwenye Mkoa wa Kilimanjaro kwa kiutawala. Ombi langu Rais alikuja katika Jimbo langu la Siha akasema litafanyiwa kazi, tumelipitisha kwenye Halmashauri, *Regional Consultative Committee,* tumelileta kwenye Taifa na tumeambiwa taratibu zote zimefuatwa na kumbukumbu zote muhimu zimefika hapa, msifike mahali wazee wangu mkasema hili haliko tena, unajua ninyi sijui wachache, sijui nini, hapana. Soma Liwale, soma Ngorongoro, chukua takwimu zao, chukua Hanang, wote hao nenda kawaangalie, utakuta wala ilikuwa sio suala la *population.* Kwa niaba ya wananchi wa

Jimbo la Siha, naomba nifanye *registration* tena upya na kuikumbushia Serikali ombi lao la kupata Wilaya ya Siha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, nakushukuru. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mungu ibariki nchi ya Siha, Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mheshimiwa Christopher Wegga jiandae. *(Kicheko)*

**MHE. ABDULLA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Tumepata pigo kubwa la kuondokewa na ndugu yetu, mwenzetu, rafiki yetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini na mimi nimepoteza kwa hakika rafiki yangu mkubwa sana, *classmate* wangu, tumetoka mbali sana. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii, tumwombee marehemu huyu awekwe mahali pema peponi na familia ya wafiwa na wapiga kura wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Mbeya nzima wapate subira, waweze kuhimili machungu haya ya kifo hiki cha ndugu yetu, Marehemu Yete Mwalyego, *amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimesikiliza alivyomalizia hotuba yake, nimepata faraja kubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu usingefanya kama ulivyofanya juzi, yangesemwa mengi sana, pale umemaliza kazi, nakupongeza sana na nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa yote anayofanya, anavyoiendesha Serikali hii tuliyomkabidhi na hasa hasa kwa hatua yake ya kutembelea Jimbo langu la Tandahimba mwezi wa Septemba, 2003. Tulikuwa na mengi na mimi nimeshafuta hata swali maana limeshapata majibu. Niliuliza swali hapa na tumekubaliana tunalifuta maana majibu yake tuliyapata kupitia kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namshukuru alikuja maana matatizo sugu tuliyokuwa nayo sisi kwa miaka mingi alifika mahali wakati wa mkutano wake akasema msinieleze tena maana huko kote nilikozunguka nilipata tatizo hili la maji akasema sasa hatua ninayochukua ninamtuma Waziri wangu wa Maji aje kutazama jambo hili na alipatie ufumbuzi. Waziri wa Maji, alipokuja hakufanya mkutano wa hadhara hata mmoja, kazi tupu, kila akisikia tatizo hapo hapo, akisikia tatizo hapo hapo. Niliwahi kumwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, kuna watoto wamezaliwa wakasoma mpaka *Form I* wanaona mabomba hayatoki maji na hawajui kama mabomba yale yanatakiwa kutoa maji kwa sababu toka wamezaliwa, wanasoma *primary* mpaka *secondary* hawajui hapa panatakiwa kutoka maji, wanashangaa ni kitu gani. Alichofanya Waziri wa Maji wamekuja kulimaliza tatizo hilo moja kwa moja. Sitaki kueleza yote ambayo yanaendelea kwenye Serikali yake, kutufikisha hapa tunapofikiria kwamba, tutafika kulimaliza tatizo hilo, lakini nakushukuru sana, sisemi zaidi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumza habari ya mpango na bajeti ya Wizara hii ya TAMISEMI. TAMISEMI, sisi tunapozungumza tunataka kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000 ya Chama cha Mapinduzi tunazungumzia TAMISEMI maana hii iko kule ambako tuko sisi wananchi tunaopiga kura. Kama tunazungumza habari ya Utawala

Bora basi *reflection* yake inatakiwa itoke kwenye *performance* ya Wizara hii katika maeneo haya ambayo sisi tunatoka.

Mheshimiwa Spika, sitaki kuchukua muda mrefu nataka niseme hivi, hili limekwishasemwa na wengine lakini si vibaya nami nikasema kwa kusisitiza. Ukisema kuboresha MMEM tumeiona na ilikuwa inapitia TAMISEMI. Nimezungumza habari ya maji, nimemshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa sasa hivi ni kwamba, itapita TAMISEMI tu. Tunazungumza habari ya uboreshaji wa vijiji, barabara, *Road Fund* iko inayofanya kazi ni TAMISEMI. Sasa nasema kule kioo chetu ni TAMISEMI na kielelezo kikubwa cha *performance* ya Serikali hii ni *performance* ya Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi najua si aghalabu Serikali kugeuka jiwe lakini nataka niseme Mheshimiwa Waziri alipokuwa anazungumza hapa Bungeni kwamba, sasa tunaachana na utaratibu wa kuwataka Madiwani wawe katika utaratibu mzima wa tenda katika Halmashauri, mimi ni mmoja kati ya watu ambao nilishangilia na nikapongeza sana. Nilishangilia na kupongeza kwa sababu nilikuwa naamini dhana yenyewe ni sahihi. Lakini uzoefu unaojionyesha sasa na nadhani ni kwa sababu Wabunge tu hatuuelewi vizuri, inawezekana jambo hili liko kila mahali. Inawezekana tulitaka kuitekeleza dhana ile kabla hatujaandaa viwango vya uadilifu kwa watendaji wetu. Kwa sababu ili uweze kuitekeleza vizuri hii, umfanye Diwani kazi yake iwe kuhoji tu basi unatakiwa uwe na watu waadilifu katika kutekeleza majukumu yale. Inaonekana kama upande mmoja tulikwenda haraka upande mwingine tukasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejifunza kuzungumza au kutoa kauli ndani ya Bunge kwa ushahidi lakini sitaki kutoa ushahidi huu. Ninachotaka kusema ni kwamba, uzoefu wangu kule kwetu toka tulipoanza utaratibu huu wa kwamba, Madiwani wasiwe tena katika vile vikao vya tenda, tuna matatizo makubwa na matatizo haya ndiyo yanayonifanya mimi kushauri ikiwezekana tugeuke jiwe turudi kwenye utaratibu ule ule wa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inajitokeza kwenye Halmashauri hizi kwamba, nikiwa mimi *chairman* wa tenda na mdogo wangu yupo pembeni, basi tenda ile nitapewa mimi kwa jina langu, kwa jina la kampuni yangu au kwa jina la kampuni ya ndugu yangu, jambo hili liko sana.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi inapofika Watendaji wa Halmashauri wanakaa katika kikao wanasema leo tunataka ku-*award tender* halafu wakatoa tenda kwa *Lutavi and Company, Lutavi and Company* yuko Mbeya, lakini tenda inatolewa leo na *Lutavi and Company Manager* wake anafika pale kesho. Kesho ile *Lutavi and Company* anasema basi tutasaini Mkataba, unasainiwa siku ile ile, siku ile ile *Lutavi and Company* baada ya kusaini Mkataba anasema basi naomba nipate angalau *advance* nianze kazi. Siku ile ile *advance application* yake itakuwa *processed, voucher* itaandikwa na cheque na ikiwezekana na pesa ikatoka siku hiyo hiyo. Sasa nasema utaratibu wa namna hii hauwezekani kama sio kwenye mazingira ya rushwa. Viwango vya ufanisi ambavyo tulitegemea sisi kuendeshea nchi yetu ingekuwa ufanisi huu uko kwenye viwango vya

namna hii ninavyovieleza mimi hapa, basi maendeleo kwenye Wilaya zetu ingekuwa sio jambo la sisi kukaa hapa tukalilalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema tatizo lipo lakini kwa mfano huu ninaouzungumzia, mbaya zaidi ni kwamba, kama tulikuwa tunategemea wako wengine wanataka kuwa-*awarded* ile tenda na wamekosa huyu aliyepewa tenda anapewa na *advance*, anapewa pesa za Halmashauri akafanyie kazi ile, kwa nini asingojewe mpaka a-*perform* kwanza halafu alipewa kwa *phases?*| Tunasema hapa iko harufu kubwa ya rushwa, haiwezekani. Ninachosema ni kwamba, mtu anayefanya maamuzi ya namna hii hayupo pamoja nasi.

Mheshimiwa Spika, sipendezwi na namna baadhi ya Watendaji kwenye Halmashauri zetu wanavyoendesha Halmashauri, inakuwa kama Halmashauri zile wamekabidhiwa kama sehemu ya urithi wao, wanaendesha kama mali ya kurithi, haiwezikani kuachia jambo hili kuendelea. Halmashauri hizi zina wenyewe, wao wanaletwa kwa ajili ya utaalam tu ambao wanao, basi watusaidie kuendesha Halmashauri zetu katika namna ambayo itatunufaisha sisi lakini kwa utaratibu huu tunaona fedha ya Halmashauri inaondoka, kuna wizi mkubwa unafanyika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimejifunza kwamba, ndani ya Bunge lako Tukufu lazima uzungumze ukiwa na uhakika na unalosema na ikiwezekana uwe na ushahidi. Ninachozungumza ni kwamba, hata ushahidi upo, kuna baadhi ya Wabunge walikwenda kule wakahoji wakakuta jambo hili. Tena wanauliza aah, mambo ya Halmashauri sasa yanatoka nje? Hivi sisi tunakaa hapa tunazungumza habari ya kutoa fedha hapa tupeleke kwenye Halmashauri sasa inaonekana jambo lililopo kwenye Halmashauri likijulikana kwa Wabunge basi limetoka nje kumbe baina ya Halmashauri na Bunge hili ndani wapi? Hapa ndani ya Bunge hili Mbunge akifahamu iwe imetoka nje, sasa ndani wapi baina ya Bunge na Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi inayofanywa na Halmashauri na Wizara hii ni nzuri, mimi ndugu zangu hawa, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, tunafanya nao kazi vizuri. Nashukuru kila nilipokwenda kulalamika walinisikiliza na kwa hakika pale nilipofikia mpaka nafikia kuhoji kwamba, hivi hawa walikuwa wapi hawajaletwa kwetu kule? Nawashukuru sana, kazi hii wanaifanya vizuri lakini hawa wengine wataharibu sura nzuri ya utendaji wao wa kazi ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Ofisi za Wabunge. Mimi kwa bahati mbaya ni miongoni mwa wale wengi ambao hawana ofisi za kufanyia kazi na hili Mheshimiwa Waziri analifahamu. Tumepigana kutazama namna ninavyoweza kupata mahali pa kufanyia kazi bado haijawa sawasawa lakini sisi tunaamini kama ikipatikana Ofisi ya *DC*, Wilaya yetu ni mpya haina ofisi ya *DC* labda Mbunge angejibanza pale. Nataka niulize jambo moja kuhusiana na ujenzi wa Ofisi ya *DC* Tandahimba. Mwaka 2003 kwenye *Vote* ya 80, kifungu cha 6255 tulipata shilingi milioni 73 na mwaka huu nashukuru Serikali inatupangia shilingi milioni 110. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, hivi leo bado siku tano tu bajeti ya mwaka 2003 ikamilike, hizi shilingi milioni 73 ziko wapi, zimepelekwa kwa nani na kazi hii inafanyika wapi?

Maana ninasikia kama fedha haikutumika basi fedha hizo hurejeshwa Serikalini, mimi siwezi kujua kama fedha hii ilikuja na kama ilikuja, ilikuja kwa nani na ilikuwa inafanya kazi gani mpaka inapofika kesho kutwa zitarudi au zimekwishatumika? *Value for money* urahisi wake ni kwenda kuangalia kazi ambayo imefanyika Tandahimba pengine karibu tutahamia kama kweli ofisi ile ipo. Lakini ninachosema hapa ni muhimu tukafahamu fedha hizi ziko wapi, amepewa nani na zimefanya kazi gani maana sasa tunategemea kupata nyingine. Sasa kama tunapata hizi shilingi 110 milioni zingine zikienda kwa utaratibu huu basi sisi tunaweza kumaliza mpaka 2005 na fedha hizi zinatengwa zinakwenda, sijui kama zinarudi ikiwa sisi hatuna ofisi. Ninacholilia hapa ni kupata Ofisi ya *DC* Tandahimba ili nami nipate mahali pa kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hapa amezungumzia ajira ya hawa Watendaji wa Mitaa, hawa wanaendelea, kama ikifika miaka mitatu hawajajiendeleza *out*, sasa kule kwetu kazi hii itakuwa kubwa kweli. Maana kwa vigezo vile vilivyowekwa wale Watendaji walioko sasa hivi sidhani kama wenye vigezo hivi wanafika watatu na tunao wengi. Sasa tukisema wote wale *out,* sijui tutafanyaje. Nadhani utaratibu wa namna wa kufanya ili kuhakikisha wanajaza nafasi zile kama hali hiyo ikitokea kwamba watu hawa wameshindwa kujiendeleza katika miaka mitatu tuliyokuwa nayo, upo ndani ya Wizara

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwa bajeti hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI). Nakushukuru sana na naunga mkono hoja moja kwa moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, uniruhusu nami nitoe pole kwa kifo cha Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambacho kimetupata asubuhi hii hapa Bungeni. Namwomba Mwenyezi Mungu, aipokee roho yake na ailaze mahali pema peponi na awape faraja wafiwa wote hata sisi tulioko hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mimi leo sisemi sana nitashauri tu. Kwanza, tukubaliane Wizara hii sisi ndio tumeipa mzigo, Bunge hili ndio limeipa mzigo. Nimesikiliza sana michango ya Wabunge lakini tukubaliane kwamba, Wizara hii sisi tumeipa mzigo kwa tulivyopanga fedha zikitoka Hazina zote zinakwenda TAMISEMI, nguvu za wananchi tukizichangisha kujenga matofali anayesimamia TAMISEMI, *timing* yake pale kama ni gari haliwaki, hilo gari utavuta wewe mpaka utakapofika kilomita 100 haliwezi kuwaka.

Mheshimiwa Spika, nashauri TAMISEMI ingekubali yapi iyabebe na yapi ibaki nayo. Kwa mfano, tuzungumzie tu Utumishi, Wizara ya Fedha, Ujenzi na Kilimo, wote hawa lazima wanafikia pale TAMISEMI, ndiko watakaporipoti. Utumishi ikiajiri watu itawapeleka TAMISEMI, Kilimo ikiajiri watu itawapeleka TAMESEMI, Elimu ikiajiri watu itawapeleka TAMISEMI, Afya ikiajiri watu inawapeleka TAMISEMI, mmemuandaaje huyu mtu mmoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo hapa ni mwandalizi, Makatibu Wakuu wa Wizara hizo wote wanakwenda kumtulia mzigo huu Katibu Mkuu mmoja. Sasa hili tulishasema kwamba, ilishasemwa kwamba, ukigeuka nyuma utakuwa jiwe, lakini kama utakuwa jiwe halafu linapiga mtu geuka uwe jiwe lakini mambo yafanikiwe. Kama ni kugeuka nyuma sisi hatutakuwa jiwe tutatengeneza mambo, basi tugeuke. Sasa maana yake nini hapo, ni kwamba kama tunaacha Katibu Mkuu anayeshughulikia Wizara muhimu kama tano, sita, zenye mipango yote hii niliyoisema basi tumpe wataalam wazuri huyu TAMISEMI. Sasa hivi pale juu Mkoani, Mkuu wa Mkoa anashauri, Mkuu wa Wilaya anashauri, Mkurugenzi ndiye mwenye mambo yote, sasa pale ndiyo kazi inaanza, timu aliyopewa Mkurugenzi, Wahandisi, Wataalam wakitoka pale anakwenda tena na Watendaji wa Vijiji. Sasa hawa kwa fedha tunazopitisha ndiyo wenye hela, hizi zote tulizopitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana sehemu kama Wizara ya Afya watu waajiriwe. Kwanza, ile kazi ni ya kitaalam, waajiriwe wa Wizara ya Afya kama inavyofanya Wizara ya Elimu. Tupunguze mzigo. Tutamlaumu bure Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa sababu tumempa mzigo, halafu mwisho tunamlaumu hatujiulizi tumempa mzigo wa namna gani. Wizara ya Afya iajiri yenyewe na isimamie yenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi nina zahanati moja ilifunguliwa mwaka 1998 na Mkuu wa Mkoa wakati ule Dr. Gama. Toka imefunguliwa mpaka leo Wizara ya Afya imeshindwa kuajiri. Haiwezi kuajiri kwa sababu mapendekezo yatatoka TAMISEMI, yakitoka TAMISEMI yatakwenda Utumishi ndiyo kwenye haki huko, sasa hapo tutafika? Tumekubaliana hapa kwamba tukitaka kuondoa umaskini lazima tutumie raslimali zetu kuibuka kiuchumi. Mheshimiwa Waziri wa Mipango alisema, tunaibuka kiuchumi, ukitaka kuibuka kiuchumi ni kilimo. Sasa hivi nendeni kwenye Halmashauri zenu wataalam wa kilimo mnao? Wataalam wote wazuri wa kilimo walikuwa Mikoani, pale mkasema tunavunja tufanye Sekretarieti ya Wilaya, ninyi hapa Mkoani mnapewa *notice*, afadhali mngewashusha wale basi waende Wilayani kwa mshahara ule ule wa Mkoani, wale watu wapo.

Mheshimiwa Spika, kama tatizo lililopatikana juzi, hilo ndilo litaleta matatizo kweli kweli. Juzi imepigwa dawa ya pamba, mimi nilikuwa napiga kelele humu pamba Kilosa, Wizara ya Kilimo ilisema limeni pamba, tumelima pamba, sasa watalam waliopo kule wameshindwa kupiga dawa ya pamba. Wamechukua dawa ambayo inapigwa mdudu anatazama hivi, mimi nikamwomba Waziri hapa twende tukaangalie, Jumamosi nilikwenda peke yangu Waziri hataki kwenda na mimi, sasa tutafanya nini! Nimekwenda kuangalia ile pamba, nikawauliza wananchi mnasemaje? Wakasema ni hasara kubwa tu, jana nilikuwa nazungumza na Mkuu wa Mkoa nani atalipa hii fidia ya pamba iliyokufa katika hekta 11,000? Pamba ndefu kupita Mkuu wa Mkoa lakini haina hata maua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa hilo jambo jamani kweli nalo tuseme tuilaumu TAMISEMI. Hii ni mipango mibaya kwa sababu hata Afisa Kilimo ukitaka kumpata

pale lazima uende TAMISEMI. Huwezi kuzungumza tena na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, atakwambia huyu mtu nimeshakuletea lakini sasa hivi ukitaka kumpata mfuatilie Mkurugenzi, Mkurugenzi hana mafuta. Sasa hivi hili tatizo hatuwezi kulibadili, tunakazana tu kumlaumu Waziri wa TAMISEMI. Yaani mtu anakwambia nyoka huyo unasema sijamwona mpaka akugonge. Tutaumia kweli kwa utaratibu huu. Tulichodai pale tulisema madaraka yaende kwa wananchi, hilo ndilo tulilodai, haya mambo mengine tukumbuke, Wabunge hapa tumesema sasa tupeni madaraka ndiyo mfumo wenyewe ulivyo kwamba sasa wapeni maendeleo wapange wenyewe kuanzia kwenye Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya na ndiyo maana ya TAMISEMI. Sasa shida hatuna wataalam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naamini mtoa hoja amenielewa niombe sana namna gani tutafuatilia tatizo la pamba la Kilosa ili wote kwa pamoja tuone ni nani awajibike. Sasa hili siyo la Waziri peke yake, mimi nazungumzia pamba na kule nako niseme nimefanya nini. Kule nimewahamasisha wananchi wamelima na wamepanda. Hiyo ndiyo *Full Council* nzima. Sasa hapa tunaposema pamba imepigwa dawa ambayo haiuwi wadudu, nimekwenda Dar es Salaam, nikawauliza watu wa *Pamba House* mbona dawa mliyotupa kule iliwahi kuonekana kule Shinyanga kwenye miaka ya 1998 na *expired* hii? Wakasema hapana watu wako hawajui kuchanganya, inaua vibaya. Nikasema si kweli twendeni kwenye mashamba mengine. Mashamba eneo la Mamlaka ya Pamba ambayo tumeyaandaa kwa ajili ya mbegu yamepigwa dawa nzuri inaitwa *Kick Star,* kitu kama hicho, mimi siyo mtaalam wa madawa ya pamba. Sasa tatizo wananchi wanauliza kwamba kwa nini mashamba ya wakubwa mazuri, mashamba ya wananchi tumeshindwa kuhudumia. Mheshimiwa Naibu Waziri nisaidie kushirikiana na Wizara ya Kilimo ili tuondoe umaskini huu tunaosema.

Mheshimiwa Spika, suala la sifa za Kilosa nilisema sana mwaka 2003, mwaka 2000 nilisema sana tatizo tulilopelekewa kukitwa kwenye ngema ya msingi hata hatuwezi kujikwamua na wale wataalam wa Ki-Irish. Katibu Mkuu unalifahamu hili, Wa-Irish hawa kila wanapofanya ubadhirifu wa pesa walisema Kilosa inafanya ubadhirifu wa pesa, sasa sifa tuliyonayo mpaka leo Katibu Mkuu tunaomba utuondolee mzigo huu kwamba kwa kweli Kilosa hakuna ubadhirifu wa pesa, Wa-Irish wale walikuwa ni wabadhirifu kweli kweli. Walichofanya sasa wamekwenda kwa wafadhili wengine wakasema msiende Kilosa wale ni wabadhirifu wa pesa. Sasa sisi Mikoa yote na Wilaya zote za Tanzania zinapata wafadhili, sisi Wa-Irish wale wamekwenda kutia kitumbua mchanga, msiende Kilosa kuna wezi. Lakini wezi wale tuliwapa Serikali, Wizara ya TAMISEMI, tuliwaambia wezi wenu hawa hapa, fanyeni kazi. Sasa hilo nalo lilikuwa jukumu la wananchi? Sasa Kilosa inahukumiwa kwa nini?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie tatizo lililotukuta jana kaka yangu hapa, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, alilisema sana sana. Mimi nimalizie kwani pale aliposema panatosha, sijui kama kuna mtu hakumsikia vizuri. Inatosha kabisa sasa na sisi tufikirieni kutupa Wilaya na hili nilikuwa namwangalia sana Mheshimiwa Waziri, pale alikuwa amenukuu mambo mengi sana kuhusu mchango wa Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo. Lakini la msingi tupeni hata Kata. Tumeomba Kata na Vijiji na sisi kuna tatizo tunaliona kwamba pengine Vijiji mnapunguza, mnaamini kwamba tutalipa nini. Dhana ya kuongeza Vijiji ni kuhimiza tu maendeleo na kuwapa

watu mamlaka katika kusogeza madaraka Vijijini na huduma Vijijini. Sasa hili la mshahara lisije kuanza kukata Vijiji tunavyotegemea. Tunategemea kwamba Vijiji mlivyoainisha humu na Kijiji cha Kidodi, Kata ya Ruaha imo, Mshohoro imo na bahati nzuri juzi nilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri nikamnong'oneza haya mambo, usiandike ulishaandika kule ndani, wewe endelea na yale yale tu uliyoandikia ofisini, nami nitakuja tena. Hatuwezi kugombana humu ndani, sisi wenyewe tuliyapanga haya.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara nimeshapita pale ofisini, nikasema mipango hii ya daraja la Zogo tumepanga Mkoani na Mheshimiwa Mashishanga hivi yuko hapo juu lakini na yeye anazungumzia habari ya jana ile kuongeza Walimu kwa sekondari nilizotaja jana, yuko pale na Waziri humu ndani hayumo, wanazungumza habari ile ya Walimu wa Zombo, Kidodi na Sekondari yaUlaya. Kwa hiyo, mambo mazuri kama haya tuliyoyafanya tunasema tunakarabati tu mambo siyo kwamba tunapiga kelele. Tulipokosea tunarudi nyuma kusahihishana na sisi tunasema mpaka sasa tusingekuwa tunasifiwa hivi kama Wizara ya TAMISEMI ingefanya vibaya. Yale mazuri tunasifu, yapo mazuri mengi tu ila ni kwamba mzigo ni mzito mno. Yale mazuri lazima tukusifu kwa sababu huwezi kusema tumejenga sekondari, barabara zinatengenezwa, Vijijini kunapitika, Utawala Bora Vijijini umeingia, wanakijiji wanajua haki yao, ni kazi ya TAMISEMI. Lakini wataalam wengi wamezungumzia kwamba ni tatizo.

Sasa Mheshimiwa Spika, kwa sababu mzazi naye ana tatizo, saa nyingine ukimwambia bwana Mkurugenzi huyu hafai mzazi anamkumbatia, haya ndiyo yatamponza sasa. Sasa angekuwa anatuuliza kwa nini hafai. Tunampelekea matatizo, yeye atume timu yake ikayachambue. Mimi mengine siwezi kusema, tulitaka kidogo kupambana na Katibu Mkuu wa TAMISEMI, nikanyamaza nikasema ukigombana na mkubwa kama huyu hivi utapataje misaada. Lakini mwaka 2003 ilikuwa tugombane na Katibu Mkuu wa TAMISEMI. Imeandikwa barua ndefu ya kwenda TAMISEMI na mimi naandika ndefu napeleka TAMISEMI, Katibu anapelekewa na mimi nampelekea Katibu. Baadaye nikakaa chini, nikajiuliza, nikaona hapana mimi niongee naye kwa mdomo. Tukamaliza maneno. Tatizo ni wataalam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, leo tumefiwa usemaji ule wa kawaida huwezi kuupata, tuna majonzi kweli kweli humu ndani. Nimalizie tu na ofisi zetu za Wabunge. Nilikuwa naongea hapa jana kwamba tuna mchapa kazi hodari Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Mzee Stephen Mashishanga. Mheshimiwa huyu tumemalizana matatizo yetu, tunauliza huyu aliyepeleka taarifa kwamba ofisi za Wabunge walioko Majimboni kwa mfano mimi Jimbo la Mikumi ijengwe Wilayani ni nani? TAMISEMI ipo sahihi hapa, imeambiwa ofisi ya Mheshimiwa Christopher Wegga itakuwa Mikumi, naunga hoja mkono ofisi iwe Mikumi. *(Makofi)*

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa niaba ya wakazi wa Arumeru Mashariki na kwa masikitiko makubwa, natoa rambirambi za pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kuondokewa na Mbunge wao mpendwa. Mungu ailaze roho yake Mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kuandaa hotuba hii ambayo ni nzuri na naomba nichangie kwenye maeneo manne ambayo ni kero kubwa katika Jimbo langu la Arumeru Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa katika Jimbo langu kwenye Mlima Meru kuna eneo ambalo linapandwa miti kwa ajili ya biashara ya kuvuna mbao. Eneo la Seela kuna mahali nimeona kwamba kutakuwepo na mradi wa kujenga barabara na anayefadhili ile barabara ni *The African Development Bank (ADB)* na ile barabara inapita msituni haipiti kwenye Vijiji vya wananchi. Bahati kwa upande wangu inapitia karibu na Kijiji changu, taratibu zinazotumika pale ni kwamba kila wakivuna wananchi ndiyo wanakwenda wanalimia ile miti inayopandwa, wanapanda mazao ya muda mfupi kwa taratibu za kisheria na taratibu za Wizara. Wanavuna kwa mfano, viazi, mahindi, maharage na mazao mengine. Wanayachukua kwa kichwa kwa sababu ya hali mbaya ya barabara wanapeleka kwenye soko la Tengeru lililo kilomita sita mpaka saba. Hiyo barabara haipiti kwenye hilo eneo na ingepita kwenye hilo eneo ingeweza kufika kwenye hilo eneo panapovunwa hiyo miti. Ombi langu kwa hii Wizara ni kwamba, hiyo barabara ipite penye watu badala ya kwenda kupita kwenye msitu ambako hakuna mtu hata mmoja anayeishi huko, ipite kwenye maeneo ya wakazi wanaozunguka hilo eneo la msitu. Naomba ipite kwenye Kijiji cha Seela iende kwenye huo msitu na pia ihudumie wananchi ambao ndiyo wanaoishi jirani na huo msitu wa Seela. Hilo ndilo ombi letu rasmi, tunaomba tafadhali tupewe kipaumbele kwenye hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu daraja la Mto Nduruma kwenye Kijiji cha Loita Nkwamala kilichoko kwenye Kata ya Nkwanrua. Daraja la Loita Nkwamala mwaka wa 1992, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anna Abdallah, alikuja kutembelea sehemu hizo akatoa yeye mwenyewe fedha za kujenga hilo daraja, fedha zikatumika, mkandarasi akatafutwa, kazi ikafanyika kwa kiasi cha kupandisha msingi na mifuko karibu mia moja ya sementi ikawekwa kwenye Ofisi ya Chama. Huo ni mwaka wa 1992, daraja halikujengwa, mkandarasi hakuonekana na hiyo mifuko ya sementi mpaka leo imeozea pale na haina kazi tena. Hilo suala tumelipeleka kwenye mamlaka zinazohusika mpaka leo hilo daraja halijajengwa.

Mheshimiwa Spika, hili nadhani kama kuna kero hii ni mojawapo na ambayo kwa kweli wananchi wamekata tamaa na wanadhani labda huenda hakuna mtu anayewajali. Fedha zilitolewa kwa kujenga hilo daraja lakini haifahamiki zilikwenda wapi na masuala tunayoambiwa ni kwamba, hazifahamiki zilipo. Tunaambiwa kwamba litajengwa lakini hatuoni likijengwa. Tunaomba Wizara husika ihakikishe kwamba, mwaka huu hauishi kabla hilo daraja la Loita Nkwamala kujengwa kwenye huo Mto Nduruma.

Mheshimiwa Spika, la tatu linalofanana nalo na ambalo pia Mheshimiwa Anna Abdallah, alihusika linahusu daraja la Mto Kikuletwa kwenye eneo la Karangai linalounganisha Kata ya Kikwe na Valeska, Kata ya Kikwe pia kwa upande wa Makiba. Siku moja Mjerumani mmoja Mmisionari alikuwa anapita pale Mto Kikuletwa, ni mto ambao ulikuwa na maji mengi sana, akamwona mama mmoja ambaye alikuwa na mimba,

alikuwa anavuka, maji yakamfika karibu na shingo, karibu yamchukue. Akaona uchungu, yeye mwenyewe akajitolea kwamba nileteeni mchoro wa daraja hili, mimi nitasaidia kutoa fedha na kuhamasisha wengine watusaidie kuchangia kujenga hilo daraja. Mheshimiwa Anna Abdallah yeye mwenyewe alitoa mchango kuongezea mchango ambao tayari wananchi walikuwa wameshachanga kwa kiasi kikubwa mno kuhakikisha kwamba hilo daraja linajengwa. Huo ni mwaka wa 1992, mpaka leo bado mchoro tunaambiwa kwamba ulichorwa ulikwenda sijui wapi, tumeutafuta, mimi mwenyewe nimekwenda mpaka kwenye ofisi husika tunaambiwa tu kwamba hatujauona, hatujauona, mpaka hivi leo nimeomba ofisi fulani fulani zitusaidie, bahati mbaya hatuna ujuzi sana, tunapozungumza hapa kwamba hatuna utaalam katika Halmashauri zetu ni kweli hatuna na hilo ni eneo mojawapo ambalo hatuna huo utaalam.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la kwanza kwa Wizara hii ni kwamba, tupewe huo mchoro. Pili, tusimamiwe kuhakikisha kwamba hilo daraja la Karangai linajengwa mwaka huu. Ni ombi letu la tatu. Naomba mno kwa niaba ya wenzangu wa Arumeru Mashariki, kuokoa maisha ya watu ambao wanachukuliwa na huo Mto wa Kikuletwa hasa wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu barabara ambayo ilikuwepo na ambayo inatuunganisha Jimbo langu la Arumeru Mashariki na Jimbo la Mheshimiwa Aggrey Mwanri kupitia Ngabobo, Kata ya Ngarenanyuki, ina kilomita karibu sita mpaka kumi na tano kwenda Sanya Juu. Hiyo barabara ilikuwepo wakati tukiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bahati mbaya baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki nayo hiyo barabara ikawa haipitiki tena. Wananchi wa upande huu wa Ngarenanyuki, Ngabobo, Ilkirimun na sehemu zingine hawana tena mawasiliano na wenzao wa upande wa Siha. Kwanza tunawashukuru watu wa Siha kwamba wanatusaidia, tunashukuru kwa kweli uongozi wote wa Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ushirikiano ambao upo, wanatusaidia katika mambo mengi tu lakini tunaomba hiyo barabara ifufuliwe ili iweze kurahisisha mawasiliano kati ya hizi Kata mbili na Kata ya tatu ya Leguruki, hiyo ni barabara muhimu ilikuwepo, ni kuifufua tu, watu wanapita sasa hivi lakini haipitiki, watu wanapita kwa punda.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo tunataka ipate ufafanuzi ni barabara ya kutoka Oldonyo Sambu kupitia Ngarenanyuki kwenda mpaka *Usa River.* Hiyo barabara ni barabara ya Mkoa lakini tunakuwa na matatizo hasa kipande kile ambacho kinaanzia Ngarenanyuki kwenda mpaka Oldonyo Sambu. Kinakuwa kama vile hakina mwenyewe, hatufahamu hicho kipande cha kutoka Ngarenanyuki kwenda mpaka Oldonyo Sambu ni cha Mkoa au Wilaya, maana yake pia nayo ni sehemu ambayo haikuwa inatumika baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunaomba huo ufafanuzi tuupate na hiyo barabara nina matumaini kwamba, huenda ikawa kwenye mpango lakini tunataka tuthibitishiwe kwamba kweli ipo kwenye mpango na kufunguliwa na itafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwamba kutakuwepo na *World Bank Study* ya ku-*establish road network.* Inanikumbusha wakati fulani Waziri wa Fedha alisema kwamba, kwa maeneo yetu kama tukiweza kutengeneza *roads master*

*plan*, yeye yuko tayari kutufikiria. Lakini kama nilivyozungumza ni kwamba sehemu nyingi hatuna huu utaalam. Ombi langu katika Wizara ni kwamba na si eneo hilo tu ni maeneo mengi kwa kweli ujuzi hatuna katika sehemu nyingi katika Halmashauri zetu, kwa hiyo, tunaomba *training* katika *specialized areas* katika *planning*, ujenzi na katika mtandao. Kwa kweli tunahitaji kupewa nguvu.

Mheshimiwa Spika, langu la mwisho ni kuhusu shule ambazo ni za *English Medium* na kuna mpango ambao nina imani unahusisha Wizara ya Elimu. Kuna shule ambazo ni za *English Medium*, wanapofika darasa la saba, wanafanya ule mtihani kama watakavyofanya hivi karibuni. Wale wanaofaulu sana wanapelekwa katika *special schools,* kwa mfano, shule ya Mzumbe, Ilboru na shule za aina hiyo. Unakuta kwamba shule moja au mbili ndizo tu peke yake zinachukuliwa, wanafunzi wanakwenda kwenye hizo *special schools* na mara kwa mara wanakuwa ni wale ambao wamepitia kwenye shule za aina hiyo ambao wao wanapata *special instruction.*

Mheshimiwa Spika, mimi naona hiyo inatupunja katika kutupa fursa sawa. Hiyo ina maana kwamba, nachukulia mimi mwananchi wa kawaida, ambaye siwezi kumpeleka mtoto wangu kwenye shule ambayo inatoa *special education* kwa gharama kubwa lakini atafaulu kama wengine. Lakini siwezi kumpeleka shule kwa mfano kama ya Ilboru kwa sababu eti ni *special school.*

Kwa hiyo, mimi nanyimwa ile *opportunity* kwa sababu ya kipato changu kidogo sikuweza kumpeleka kwenye shule inayotoa *special education.* Mimi naona mpango huo ufikiriwe jinsi ya kuhakikisha kwamba kila mtu anapata fursa sawa za kupata *equal access to all forms of education including special education.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kwenye Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, naomba nitoe rambirambi zetu kwa wananchi wa Mbeya Vijijini kwa kumpoteza mwakilishi wao. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, napenda kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Maafisa katika Wizara hii kwa kuandaa hotuba yenye kina na yenye maudhui yanayolingana na aina ya Wizara ilivyo kwamba ni Wizara mtambuka ambayo majukumu yake yanakwenda katika Wizara ambazo siyo mtambuka, Wizara za sekta. Kwa hiyo tunapoijadili hotuba ya Wizara nadhani ni vema tukazingatia ukweli huo kwamba ni Wizara mtambuka na kwa jinsi walivyoiandaa hotuba yao napenda niwapongeze kabisa kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia vipengele mbalimbali katika hotuba hii, nitavitaja vipengele kumi ambavyo ndani yake nitachambua vichache nikihusisha na matatizo

yaliyo katika Jimbo langu la Kigoma Kusini. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imezungumzia sera na mkakati wa maendeleo Vijijini ikiwa na mlengo wa kuratibu sera za Wizara zile zote ambazo siyo mtambuka. Kwa kweli hii sera na mkakati wa namna hiyo ni muafaka kabisa na utasaidia sana katika kuainisha sera zilizo katika Wizara hizo zingine.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo wamelizungumzia ni mpango wa fursa na vikwazo. Mpango huu ni wa kueneza mfumo wa upangaji wa mipango shirikishi kwa sababu tumekwishaamua kama Taifa kwamba, sasa mipango yetu ianzie katika ngazi za vijiji. Kwa kweli Wizara hii ikiendeleza mafunzo katika eneo hilo itafanya upangaji wa mipango katika ngazi za vijiji uweze kuwa na mafanikio, kwa sababu tunataka hili suala la ushirikishi liweze kuimarika na mipango yetu itaweze kupangika vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilifurahishwa nilipoona timu ya Maafisa Mipango wakienda katika maeneo mbalimbali katika vijiji na Tarafa ya Nguruka na katika maeneo ya namna hiyo, kwa hiyo, hili ni lengo nzuri ambalo Wizara hii imelifanya. Eneo lingine ni mafunzo kwa Viongozi na Watendaji. Hapa ni kueneza mbinu stadi na udhibiti wa fedha katika Halmashauri na katika vijiji. Hili ni jukumu nzuri sana na ambalo tunalihitaji Nimefurahishwa pia na uenezaji wa demokrasia na utawala ili kuimarisha demokrasia shirikishi na hii inaviwezesha vijiji kuweza pia kutekeleza majukumu yao. Kwa sababu Serikali zetu za vijiji ziko katika kuundwa, ziko katika kuimarishwa na Wizara kuliona hilo na ikaandaa programu ya namna hiyo iko katika mstari mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa pia na usajili wa vijiji na hasa lengo walilonalo kwamba, inatakiwa liwe limekamilika jukumu hilo ifikiapo Agosti, 2004, hii ni hatua nzuri na kwa sababu kumekuwepo na migongano kati ya mipaka ya vijiji, kati ya kijiji na kijiji au vitongoji kuomba viwe vijiji kamili. Sasa majibu yaliyokuwa yanatolewa yalikuwa ni kwamba, bado upangaji unaendelea na yatatolewa. Sasa kwa sababu ametupa muda, Agosti ni miezi miwili kuanzia sasa, nadhani wamefanya vizuri itatusaidia katika kuimarisha na kuondoa migogoro ambayo imekuwa ikipatikana.

Mheshimiwa Spika, ajira ya Maafisa Watendaji, hili nimelifurahia hasa kwa kuweka fungu la fedha ambapo kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, fungu limetengwa kulipa mishahara yao. Sasa nirejee katika hilo kwa kurejea kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ambapo kumekuwa na malalamiko ya Watendaji kwa malimbikizo ambayo mengine yanafikia mpaka miaka minne. Sasa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyotoa maelekezo kwa upande wa Walimu ni jambo nzuri sana alilolifanya, katika eneo hili la Watendaji malimbikizo yale ambayo yapo yalipwe ili yasiingiliane na hili fungu ambalo limeandaliwa kwa mwaka huu wa fedha tunaojadili bajeti yake. Hilo likifanyika tutaweza kurudisha ari ya Watendaji katika Halmashauri zetu . Halmashauri ya Kigoma ikiwa miongoni mwa Halmashauri zilizoathirika katika hili na habari nilizopata za hivi karibuni ni kwamba, Mkurugenzi ameendelea kujaribu kuwalipa. Sasa nataka haya malimbikizo yasiingiliane na hili fungu ambalo limeandaliwa kwa mwaka huu wa fedha tunaokaribia kuuanza na ili hilo litekelezeke vizuri, ningemwomba kabisa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, atoe maelekezo ya kusisitiza hilo kama vile alivyofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Eneo lingine ambalo ni zuri kabisa ni mpango wa usafirishaji na uchukuzi vijijini. Kwa mpango huu tunalenga Taifa nzima na hapa kilichosisitizwa katika mpango huu ni uimarishaji wa njia za wapita kwa miguu vijijini. Matumizi ya mikokoteni na wanyamakazi ili waweze kupita katika maeneo mbalimbali. Lakini pia imeonyeshwa kwamba suala la vivuko na madaraja lihudumiwe. Sasa katika Jimbo langu la Kigoma Kusini kuna barabara ya mwambao wa Ziwa kutoka Mto Malagarasi, Kijiji cha Ilangara hadi Kalya yapata kilomita 150. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri, alipopata fursa ya kutembelea huko mwaka 2003, aliona hali ilivyo kwamba safari ya kule ni boti lakini bila boti maana yake hakuna usafiri na uchukuzi katika eneo hilo. Lakini ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba, wananchi katika ukanda ule wamehamasika baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kigoma, kujitosa kabisa akaingia katika eneo hilo akishirikiana na wananchi kutafuta njia na akaweza kufanya hivyo hadi kufika Kijiji cha Kalya, wananchi walipoliona gari walifurahi mno kwa sababu ni kitu ambacho walikuwa hawajakiona kwa muda na wengine tangu wamezaliwa.

Sasa baada ya hilo wananchi walihamasika sana wakaanza kukata miti, kuondoa mawe na hatimaye hata Mkuu wa Mkoa akaenda na yeye kwa gari. Sasa mwaka 2003 niliuliza swali nikasema katika kuhudumia Vituo vya Afya Wizara, imeonyesha kwamba vitapewa magari vituo vya afya na mimi nikauliza je, Kituo cha Afya cha Buhigu, nililiuliza kwa maandishi kwa sababu sikupata fursa ya kuchangia. Nilijibiwa kwamba, gari litanunuliwa lakini tuwahimize wananchi watengeneza barabara. Sasa barabara wananchi wamehamasika ukanda mzima kuanzia Vijiji vya Kalya, Buhigu, Sigunga, Igalula, Malangarasi na Sunuka vyote hiyo hamasa iko tayari, lakini kikwazo ni pale Mto Malangarasi pale kuna kivuko kidogo na kivuko kikuu kuu. Nimewahi kumwandikia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa sababu nilielezwa kwamba anayehusika na vivuko ni Waziri wa Ujenzi lakini inaposhindikana inaonekana kwamba ni Waziri wa TAMISEMI, kwa hiyo, mimi wito wangu ningeomba Waheshimiwa Mawaziri hawa wakae pamoja kututatulia tatizo la kivuko kwenye Mto Malangarasi eneo la Ilangara.

Mheshimiwa Spika, mwezi uliopita (Mei, 2004), Waheshimiwa Wabunge kadhaa walikuwa Kigoma kwenye maadhimisho ya Mwaka wa Familia Duniani, nilibahatika kwenda nao pale walishangaa walivyoona kivuko kilivyo kidogo na hatari sana. Sasa ningetahadharisha tusije tukasubiri mambo ya Kilombero yatukute kule. Bahati nzuri mwaka 2003, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, alinusurika kutumbukia pale na gari lake. Sasa ninadhani ni bahati kwamba aliweza kunusurika katika hilo. Sasa ni vizuri kivuko kile kikabadilishwa kwa sababu kwanza ni kidogo na hata kukikarabati hakiwezi kufanya kazi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niende katika suala la alama kwenye barabara. Kijiji cha Mulela, kijiji cha Karenge na Kazuramimba hivi ni vijiji ambavyo vilianzishwa wakati wa wito wa kwenda vijijini mwaka 1974 na lilikuwa ni pori tupu kwa hiyo, siyo kwamba kulikuwa na barabara wakati huo. Sasa wananchi walipewa maeneo wakajenga nyumba, sasa wote hao wamewekewa alama za "X" kwamba ni

makazi yaliyokuwepo. Sasa nimeandikiwa barua na nitamwomba Mheshimiwa Waziri tulijadili hili. Kwa sababu wameniandikia barua wakisema sasa sisi tunahusikaje katika kukosea kwa sababu sisi vijiji vile ni vipya kabisa tulipelekwa katika pori na kwa hiyo tulikuwa tunaelekezwa wewe jenga hapa na wewe jenga hapa. Sasa msururu wa barua nilizoandikiwa nadhani itakuwa ni vizuri kulitafakari hilo tuangalie kwamba wanakuwa katika fungu gani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, nimefurahishwa na bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii kwa sababu imepanda kwa asilimia 38 na ni bahati nzuri pamoja na kwamba fungu kubwa ni fedha za nje nao zimelipwa zote kwa asilimia 100. Sasa hii nadhani ni kwa sababu wako kwenye Ofisi ya Rais, sasa watumie fursa hiyo kutekeleza mambo ya kimaendeleo kwa sababu naona fungu lao la maendeleo linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nirudie tena kuwapongeza Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ninasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niwape pole tu watu wa Mbeya Vijijini, kwa kumpoteza mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Kabla sijasema chochote nataka kusema tu kwamba, siku moja nilikuwa nasikiliza Waheshimiwa Wabunge wakichangia hoja. Mbunge mmoja akatangaza Jimbo langu liko wazi sasa huko ni kufahamu utaratibu au kutofahamu. Mimi ninajua kwamba, wewe ndiyo unajua nani na wakati gani wa kutangaza Jimbo liko wazi na yule aliyesema hayo ni kwa sababu tu alishajaribu miaka mingi kunitoa ikashindikana mpaka mwenyewe amekimbia. Sasa kama amekimbia kwenye Mji mpya ni sawasawa na mama aliyekimbilia kwa mume mwingine, amkumbatie yule amshike vizuri asiwe na ndoto za kuanza kumuota mume wa zamani la sivyo atafukuzwa na huko.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri, kwanza nimpe hongera sana kwa sababu Wizara hii ni Wizara ambayo amekubali kuibeba pamoja na malimbikizo ya matatizo yote ambayo inayo kwa miaka mingi, ya shule, ya elimu, ya afya, ya barabara na kadhalika. Hata jana Waheshimiwa Wabunge, walipokuwa wanachangia mtu mmoja akasema hameni huko mje huku, lakini alipogeuka kuangalia waliokuwa wanasema ni wale tu ambao kweli hawana Majimbo, aidha, ni wa kuteuliwa, lakini wale ambao wana Majimbo matatizo haya yanafanana kote, nikageuka nyuma kumwangalia Mheshimiwa Estherina Kilasi na Jimbo lake la Mbarali nikaona amekaa kimya, nikamwangalia Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni Masunga, naye nikamwona amekaa kimya kwa sababu kule Magu Shule ya Sekondari ina Walimu wawili sasa ni shule gani hiyo?

Yule Mbunge wa Mbarali shule yake iko kilomita 200 kutoka Mbarali Mjini na ina Walimu wawili wakati wa mvua hawawezi hata wakafika Mbarali kwenda kupokea mishahara yao wako jela huko miezi sita wakitaka kuvuka watumie boti. Sasa haya ni matatizo yako katika nchi nzima na Mheshimiwa Waziri umeyabeba.

Mheshimiwa Spika, sasa lazima Mheshimiwa Waziri, avumilie pale Waheshimiwa Wabunge wanapokulimbikizia matatizo yote kama wewe ndiyo unaweza kuyatatua. Lakini mimi nafikiria kwamba, unaweza kuyatatua kama unaweza kuweka *priorities,* lipi kwanza uanze nalo na lipi uweze kuliweka kwa ajili ya kipindi kinachofuata kwa kufuatana na fedha yako unayopata. Hii Wizara nimeangalia katika kitabu cha maendeleo fedha za ndani ni shilingi milioni 270, fedha za nje shilingi bilioni 1.4. Zile fedha za ndani na zenyewe zinategemea ni wakati gani Waziri wa Fedha atoe, leo tunapitisha bajeti lakini mpaka uje uzipate hizo fedha zitakuwa zimepita *two quarters* sasa kama zimepita *two quarters* kuja ku-*implement* hizo progamu zako matatizo yatabaki pale pale na Waheshimiwa Wabunge wataendelea kukulaumu. Hata wale *donors* na wenyewe ni hivyo hivyo kwa wakati wao ndiyo wanaweza kumpa hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna matatizo ambayo ni ya siku nyingi. Nimpe hongera Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu nimekaa ndani ya hili Bunge leo mwaka wa tisa, juzi alitoa *authoritative statement* inaonyesha kwamba kweli ni Waziri Mkuu anasema na anaagiza. Akaagiza Walimu wote walipwe fedha zao zote za malimbikizo lakini kuna kada moja pale akaisahau ya Manesi na Waganga na wenyewe wanadai fedha nyingi tu, katika *formula* ile ile ya Walimu. *(Makofi)*

Wilaya yangu ya Bariadi pamoja na kwamba kwa mara ya kwanza tangu Halmashauri ianzishwe wamepata *Clean Certificate of findings* lakini bado wamewekewa, wana *two queries* ambazo hazina majibu, nayo ni kwamba, wanadai fedha za Waganga na Manesi za malimbikizo yao shilingi milioni 20 na bado kuna tatizo la kutupiana mpira, wakienda kudai wanaambiwa nenda *Treasury*, wakifika *Treasury* wanasema hili ni tatizo la Wizara ya TAMISEMI. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba, sasa umefika wakati Wizara yako Mheshimiwa Waziri na *Treasury* mkubaliane kuwalipa hawa watumishi fedha zao Manesi na Waganga wamefanya kazi zao na wanatakiwa walipwe.

Mheshimiwa Spika, hii Wizara inabeba watoto wa kambo wanaitwa Walimu na hao Walimu kuna matatizo mengine hayatokani kabisa na Wizara ya TAMISEMI, lakini yanatokana na tatizo la *DEDs*, wanafanya makusudi kabisa kuhakikisha kwamba, wanakwamisha hata mpango mzima wa MMEM, nilimsikia jana Mheshimiwa Mbunge wa Simanjiro, mimi ni shahidi kwake nimeenda Simanjiro, fedha za MMEM badala ya kupelekwa kwenye *Account Number Five,* fedha za MMEM zinapelekwa kwenye *OC* na fedha ile wametumia kwa matumizi mengine tofauti kabisa. Kamati za shule wakapewa *rubber cheques* na *rubber chueque* ambayo ingetoka kwenye *Account Number Five* ikatoka kwenye *account* nyingine kabisa ya barabara. Sasa ukianza kuangalia hii ni moja tu, Wilaya ya Simanjiro lakini kuna Halmashauri nyingine ziko hivi hivi.

Fedha ya MMEM inatakiwa iende kwenye *Account Number Five* kwa ajili ya madawati, tulipokuwa tunatembelea Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Kinondoni tulienda katika shule moja inaitwa Tuliani badala ya ile fedha kupelekwa kwenye shule ili Kamati ya shule ichukue tender na itengeneze madawati wanasema sisi hatufahamu anayejua ni *DED* au Afisa Elimu, Afisa Elimu tukamwuliza naye hana habari zile fedha zinakwendaje. Kwa hiyo, natumaini hapa kunatakiwa agizo ambalo liko wazi la namna gani hizi fedha za MMEM ziweze kutumika kama ni kwenda kwenye *Account Number Five* ziende kwenye *Account Number Five* na zile Kamati za Shule ziweze kuchukua *tender* na kuweza kutengeneza madawati na kujenga madarasa.

MMEM imepokelewa kwa furaha sana na wananchi kwa sababu wananchi wamepewa mradi ule kwamba wao katika vijiji vyao waone shule kama ni mali yao na wao ndiyo waanze kutengeneza boma la darasa likifika kwenye rinta Serikali ichukue na kuweza kuezeka, kuweka milango, madirisha na watoto waweze kukaa kwenye madawati mle ndani. Kwa hiyo, wananchi kujua kwamba, hii Serikali na hii fedha ni ya mkopo wakaamua ku-*supplement* nguvu zao, wakapangiana kwa *Administration* zao wenyewe kwamba, kijiji kama kina vitongoji saba, vitongoji vitatu vitajenga madarasa na vitongoji vinne vitajenga nyumba za walimu. Hiyo ndiyo maana imetupelekea sisi katika Wilaya ya Bariadi katika kipindi cha miaka kama tisa sasa mpaka kufikia kujenga madarasa 1,365 kutoka madarasa 241 kwa mwaka. Hii imetusaidia kwamba, walipoona vile wananchi wakaamua kujenga maboma ya nyumba za Walimu kwa kufuatana na mpango ambao wao wenyewe wamejipangia. Lakini kukaanza kutokea, walipoitwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, hawakutumia kama shilingi milioni 900 hivi. Mkurugenzi wangu asubuhi nilimwuliza, hebu niambie kumetokea nini mpaka leo una maboma katika shule mbalimbali ambayo bado nyumba za Walimu hazijakamilika, akasema walipoitwa yeye ali-*raise* swali akasema hela ndogo mliyonipa nimejenga madarasa kadhaa na nyumba za Walimu, wakamwambia ulipata wapi mamlaka hayo. Kwa hiyo, tangu alipotoka pale akaamua kutokuendelea na ule mradi wa kujenga nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa watu wa Bariadi kwamba sasa tuna maboma 500 ya nyumba za Walimu, ambayo bado hayajakamilika sasa muwaruhusu hao watu aidha, *in writing* ama muwaambie kwamba, kama Waziri wa Elimu na Utamaduni jana nilimwuliza akasema wapeleke *request* kwenye Wizara ili waweze kupewa fedha ili waweze kumalizia zile nyumba za Walimu. Mkimalizia nyumba za Walimu 500 hizo tutakuwa na jumla ya nyumba za Walimu kama 1,091 hivi na bado tutakuwa na upungufu mdogo wa Walimu wetu ambao wanahitaji nyumba. Kwa hiyo, kwa hili tunaomba kama ni ombi rasmi kwa ajili ya Walimu wa Bariadi, ili pia tuwape moyo wale wanavijiji, nyumba ambazo walikuwa wamejipangia kuzijenga kwa ajili ya Walimu kwamba Serikali nayo inawapa moyo na ina wajali zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hili la kutekwa nyara kwa Halmashauri na Serikali Kuu. Serikali Kuu ilikuwa imetoa mamlaka kwa Halmashauri kuweza kujiendesha zenyewe lakini haziwezi kujiendesha kama hazina fedha za kutosha. Sasa Serikali ikaona jinsi ya kuwakamata hawa ni kuweza kuwanyang'anya s*ources of revenue.* Tukawafutia zile kodi mimi sisemi kwamba warudishe kodi ya kichwa kwa

sababu kodi ya kichwa ilikuwa ni tatizo, kodi ya ng'ombe ilikuwa ni tatizo na kero nyingine.

Lakini ile ahadi ya Serikali basi itimizwe kwamba, ile *difference* ambayo ilikuwepo kati ya pato lao halisi waliyokuwa wanakusanya basi hizo fedha wapewe mara moja iweze kuingia kwenye *accounts* zao ili waweze kupanga shughuli zao kama ambavyo walikuwa wanaweza kuzifanya wakati walikuwa wanakusanya fedha kutokana na *other sources* zao, bila kufanya hivyo hapo ndiyo tumewamyima nafasi Madiwani hawana kazi. Kwa sababu hata ile kazi ndogo ya kujua mali yao ikoje na yenyewe wamenyang'anywa, walikuwa wanatakiwa kuwa kwenye Baraza la *Tender* wote wametolewa, kwa hiyo, hakuna muangalizi. Waheshimiwa Wabunge jana walikueleza ni namna gani Halmashauri sasa zinaonekana hata wale wenye mali hawajui mali zao zinaweza zikasimamiwa namna gani kwa sababu wamekuwa *side lined.*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la Madiwani kwa nini hawalipwi mishahara, mbona nyie Waheshimiwa Wabunge mnalipwa mishahara, si miaka mitano nao pia ni miaka mitano? Halafu ukiangalia Madiwani wenyewe wako kama 3,000 hivi nchi nzima lakini *VEOs* wako *in terms of thousands* kama mmeweza ku-*afford* kuwalipa *VEOs* na *WEOs,* mshahara wa kila mwezi kwa nini hawa wachache msiweze kuwalipa. Diwani ana kazi ngumu kweli asubuhi saa moja ni sawasawa na kwa Waheshimiwa Wabunge. Saa moja asubuhi tayari kuna watu wana shida zao badala ya yeye kwenda kulima ama kusimamia duka lake, anasikiliza shida za watu. Kwa hiyo, ku-*supplement* hiyo ingekuwa ni jambo la busara kwa Serikali hii kuweza kuwafikiria Madiwani, kuwalipa mishahara. *VEOs* na *WEOs* na Wenyeviti kama *economic power* inakupa nguvu ya kuweza kutawala. Sasa Mwenyekiti ndiyo mwenye mamlaka na Halmashauri yote inakuja kwake, *VEO* ni Katibu wake tu na yeye analipwa mshahara, wewe Mwenyekiti hupati chochote haileti maana yoyote ile. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba, hapa wakati umefika kwa Wenyeviti wa Vijiji na wao waweze kulipwa mshahara sawasawa na *VEOs* pia na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishie hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, napongeza uamuzi wa Serikali wa kulipa Watendaji wa Vijiji na Kata mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tangu Serikali ilipotangaza kulipa Watendaji wa Vijiji na Kata, Watendaji hao bado hawajalipwa mishahara yao. Naomba sana Wizara ifanye kila linalowezekana kuwalipa hao Watendaji haki zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitakayochangia, naunga mkono hoja hii bila shida yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda nichangie maeneo mawili zaidi ambayo ni muhimu sana. Eneo la daraja la Munguri (Kondoa) na barabara ya Mnenia - Masange - Kisese - Kikore - Madege kilometa 57.

Mheshimiwa Spika, daraja na Munguri (Kondoa) lilikatika mwaka 1997/1998 wakati wa mvua za *El-Nino.* Mwaka 1999/2000 tulipata mhisani, yaani *SNV* kwa ubia na Halmashauri, daraja lilianza kujengwa upya kwa thamani ya shilingi 435,000,000/=. Lakini kabla halijakamilika, mvua kubwa zilinyesha na kulivunja tena. Ili kujenga upya tena zilitakiwa fedha shilingi 340,000,000/= tena ili kazi ianze. *SNV* imetuchangia kwa mara nyingine shilingi 120,000,000/= na zilizobaki shilingi 220,000,000/= zichangiwe na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ili kazi ianze, Halmashauri iliweka mkataba na Hazina mkopo wa shilingi milioni 40 na kukatwa katika ruzuku yao ya kila *quarter.* Kwa kuwa Wizara inajua shida na kero hiyo, TAMISEMI imepanga kusaidia Halmashauri hii ya Kondoa kwenye daraja hilo linaloendelea kujengwa kwa deni kiasi gani cha fedha?

Mheshimiwa Spika, bila msaada wa Wizara hii, fedha zote za ruzuku zitaishia kukatwa madeni na Hazina. Naomba Serikali ichangie kwani ni wajibu wake kuona daraja linakamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Mnenia - Masange - Kisese - Kikore - Madege kilometa 57, kwa kuwa Wizara ya TAMISEMI inaelewa sana malalamiko ya Wananchi wa maeneo hayo ya kuwa kisiwani mara mvua zinyeshapo, Wizara, Mkoa na Wilaya ikishirikiana kufanya usanifu yakinifu na kubaini kuwa zinatakiwa fedha kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 900 ili barabara ipitike wakati wote. Halmashauri inatoa kila mwaka kwa ajili ya matengenezo madogo madogo yenye thamani ya fedha shilingi milioni 5 mpaka 8 hivi kiasi ambacho hakitoshi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhangaika niliwahi kumwandikia Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa zaidi ya mara tatu mambo mawili kwamba Barabara hii ni ndefu sana inatoka Mkoa wa Dodoma - Arusha (wakati ule) saa ni Manyara na Wizara itoe fungu kubwa maalum ili kutatua au kupunguza shida za wananchi wa eneo hilo.

Pia Barabara hii inategemewa na Kata zifuatazo, Kolo yenye Vijiji vinne, Mnenia yenye Vijiji vinne, Pahi yenye Vijiji nane, Bumbuta yeye Vijiji 6, Masange yeye Vijiji 5, Kisese yenye Vijiji vitano na Kikore yenye Vijiji 5, jumla vijiji 37.

Pia, ni maeneo ya kiuchumi hususan *scheme* za umwagiliaji maji mashamba. Mazao ya *scheme* hizo hubaki huko kwa kukosa usafirishaji (barabara). *Scheme* hizo ni Madege, Kikore, Humi, Makurumuzi, Madisa, Sauna, Dissa na Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichangie fedha kwa kiasi kikubwa ili barabara hiyo ijengwe madaraja, makalvati na madrifti ambayo ndiyo kikwazo zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa ina mtandao mkubwa sana wa barabara za Halmashauri kuliko Halmashauri nyingine Mkoani Dodoma, lakini Halmashauri ya Kondoa ndiyo inayogaiwa fedha za Mfuko wa Barabara chache zaidi kuliko Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe wakati wa majumuisho.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawashukuru Wabunge wa Majimbo wa Mkoa wa Morogoro wametengewa ofisi, lakini sisi Wabunge watatu wa Viti Maalum tutatengewa lini? Kuna umuhimu wa kufanya hivyo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara, imejitahidi kutoa takwimu katika maeneo mengi, lakini bado kuna mapengo. Tatizo hili lipo kwani hata Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto huwa inapata usumbufu kupata taarifa za mikopo ya wanawake kutoka katika baadhi ya Halmashauri. Tukae ili tupate *consensus.*

Mheshimiwa Spika, kuna *breakdown* ya *flow* za taarifa kutaka ngazi za Wilaya hadi Taifa mfano Manispaa ya Morogoro, ni kuwa duniani kule taarifa zote zipo, lakini katika jedwali la mikopo hatuna. Halmashauri nyingi hazijatimiza agizo la Waziri Mkuu la kutenga asilimia 10 ya fedha kwa Mifuko ya Wanawake na Vijana. Kuna haja ya Waziri kufuatilia agizo hilo kwa nguvu zote. Sisi haturuhusiwi kutengua agizo la Waziri Mkuu. Takwimu sahihi inaleta sura sahihi ya mipango yote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa TAMISEMI mia kwa mia. Namponageza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote, Mungu awabariki.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa hotuba nzuri, naomba suala la Ofisi za Wabunge wa Geita liangaliwe. Waziri ameandika kuwa kulikuwa na makubaliano ya Wabunge wote, si kweli. Hatujakubaliana na pesa hizo sijawahi kupokea hata senti tano au moja.

Kwanza sina ofisi, Waziri apate taarifa kuhusu suala hili, vinginevyo sielewi hiki nini anachokieleza kuhusu Ofisi ya Jimbo la Busanda. Halafu kiasi kilichotolewa ni kidogo mno kulingana na ofisi zingine ni kwa nini? Tuko Wabunge watatu na Majimbo yako mbali?

Mheshimiwa Spika, pili, Waziri ameeleza kuhusu upanuzi wa elimu, lakini matatizo na madai ya walimu hakuyagusa. Ni Wizara gani inayohusika na Walimu wa Shule za Msingi kama siyo hii? Au ahadi ya Waziri Mkuu haitatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za barabara, tunasikitika sana kuhusu pesa hiyo. Wilaya ya Geita ni kwa nini haipati mgao kulingana na mahitaji japo kidogo? Barabara za Mikoa ni safi, ila barabara za Halmashauri ni mbovu sana katika Wilaya ya

Geita. Sisi hatuelewi huo mfumo walioutaja ukurasa wa 55 wa hotuba ya Waziri mbona hauonekani?

Mheshimiwa Spika, hakuna barabara yoyote ya Halmashauri inayoonyesha mafanikio katika Wilaya ya Geita. Tunaomba Waziri amuite Mhandisi wa Wilaya ya Geita aje atuambie na atuonyeshe mafanikio hayo yako wapi. Hizo barabara zinatengenezwa ndani ya kompyuta? Kweli hali ya barabara za Halmashauri zinatisha kwa uchakavu na ubovu na kutokarabatiwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba masuala ya walimu yarudi Wizara ya Elimu na Utamaduni. Pia, masuala ya Wabunge (Ofisi za Wabunge) yarudishwe Ofisi ya Spika. Vile vile, masuala ya barabara yarudishwe Wizara ya Ujenzi. Haya masuala kwenu ni tatizo. Tukubali kwamba Wizara hii ni kubwa masuala mengine Wizara haiyawezi, vinginevyo Waziri Mkuu ataendelea kuongezewa hoja za kujibu. Barabara ni kero, hoja za walimu ni kero, Ofisi za Wabunge ni kero zaidi. Ahsante na samahani kwa mimi kuwa wazi.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Katibu Mkuu, Ndugu Mmari pamoja na wataalam wao kwa kuandaa hotuba nzuri kuhusu mipango na utekelezaji wa majukumu mengi na makubwa ambayo Serikali imeyaweka chini ya mamlaka yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kukumbushia mambo machache ambayo nina hakika Mheshimiwa Waziri atayakamilisha kwa ufanisi kama ambavyo amekuwa akifanya kwa Wilaya mpya ya Kilindi na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri atembelee Wilaya mpya ya Kilindi mapema kadri nafasi itakapopatikana katika ratiba ya ziara zake itakavyoruhusu ili wananchi wa Kilindi wapate nafasi ya kumpongeza na kuishukuru Serikali kupitia kwake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo TAMISEMI imekuwa ikifanya Wilayani Kilindi.

Mheshimiwa Spika, nakumbushia pia msukumo wa fedha za kusaidia ukarabati wa barabara itokayo Lwande hadi Vyadigwa ambayo hata Mheshimiwa Naibu Waziri alitambua inahitaji shilingi milioni 100 alipotembelea barabara hiyo miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Kilindi wanaomba Mkurugenzi wa Maendeleo haraka kwa ajili ya Halmashauri itakayoundwa baadaye mwakani ili asimamie maandalizi ya Halmashauri yetu mapema. Uzoefu ambao Wilaya ya Kilindi tunao ni kuwa Uongozi wa Halmashauri ya sasa ya Ushirika na Handeni imekuwa inakwamisha utekelezaji wa maagizo na maelekezo mengi yatokayo TAMISEMI yanayohusu uendelezaji wa Wilaya mpya ya Kilindi. Uteuzi wa mapema wa Mkurugenzi wetu utatuwezesha kuweka misingi mizuri ya Halmashauri yetu mwakani. Aidha, uteuzi huu utawezesha usimamizi wa Uchaguzi Mkuu mwishoni mwa mwaka huu uwe wa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri aongeze uzito wa kutuombea *TTCL* watuwekee simu pale Makao Makuu ya Wilaya yaliyoko Songe. Simu ni muhimu kwetu na itarahisisha mawasiliano na Serikali na Taasisi za Maendeleo nchini na duniani. Mazungumzo na ahadi za *Celtel* yanaendelea ila uzito wa Waziri utasaidia.

Mheshimiwa Spika, tunaomba TAMISEMI itoe upendeleo maalum kwa Wilaya mpya kama Kilindi wakati wa kuingiza miradi na programu mpya za maendeleo hata kwa majaribio mbalimbali yanayofanywa kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, itakuwa vyema kukawa na utaratibu wa kuwahamisha Watendaji Wakuu wa Halmashauri katika kipindi maalum maana wakikaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu huharibiwa na Viongozi na Wananchi wenye ubinafsi wanaotaka urahisi wa kufanikisha maslahi yao binafsi.

Mwisho, natamka naunga mkono hotuba hii ili Waziri apate fedha za kutekeleza majukumu kwa manufaa ya Wananchi.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, Ofisi za Wabunge wa Majimbo ya Vijijini naomba wapewe fedha ili ujenzi uanze mara moja. Inakuwa ni kero kwenye Jimbo la Igalula kutokuwa na ofisi. Mbunge anadandia ofisi za aidha, Mtendaji wa Kata au wa Tarafa ambazo pia siyo za kudumu.

Mheshimiwa Spika, Wananchi hawaelewi nikiwaeleza kuwa ofisi yao iko Igalula kisheria, hawanielewi. Juhudi za kupewa shilingi 2,000,000/= na Wilaya bila michoro au ufundi wa namna ya kuanza kujenga haitatui tatizo. Ni *agenda* kubwa, naomba ofisi hii ianze kujengwa, Wananchi wako tayari kuchangia nguvu zao ili wapate ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa Vijiji hasa, wanakuwa kero kwa Wananchi. Taratibu zinazofanyika katika kuwalinda Watendaji wakorofi ni adha kwa Wananchi. Kuna kuwalinda wala rushwa, dhulumati, wakorofi, wabadhirifu, waonezi kwa Wananchi walio wanyonge. Katika ajira hii mpya ya Watendaji hao wa Vijiji wachujwe vizuri. Viongozi wachache, Watendaji katika Ofisi za Wakurugenzi wanawalinda Watendaji wa Vijiji walio wabovu, huenda kwa faida yao. Watendaji wa Vijiji pamoja na wote ndani ya Halmashauri watazamwe kwa ukaribu ili kukemea hali ya kuwalinda Watendaji wabovu wa maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, Wananchi sehemu zingine hawana raha wakiona Watendaji wao hasa wale dhulumati wa mali ya wanyonge. Tupate Watendaji wazuri wenye nia ya kuwahudumia Wananchi badala ya kuwa ni njia ya kujineemesha. Serikali iendelee kuwachambua Watendaji wabaya wote ili wasiajiriwe tena kwa ajili ya manufaa ya Viongozi wachache wa Halmashauri. Simamieni hili kwa ukaribu ili Wananchi waendelee kuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuwapa pole Wizara hii ambayo ni pana mno inajichanganya kwa kuwa na majukumu mengi, kitu ambacho hata Watendaji Wakuu wanashindwa kuelewa wafanye nini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuarifu kuwa Wizara hii imeshindwa kabisa kutatua matatizo ya Walimu. Hata kwenye Hotuba ya Bajeti inaonyesha mafanikio tu badala ya matatizo yanayowakumba walimu mpaka Waziri Mkuu aingilie kati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara, Wizara hii haifuatilii kabisa kwa kuwa Watendaji wake wote wako Wizara ya Ujenzi. Kwa mantiki hiyo, barabara nyingi Wilayani Geita hasa zinazosimamiwa na Halmashauri zina hali mbaya sana ukichukulia barabara ya Kasamwa - Mkoba, Lubanga, Mkolani hadi Busekeseke, Wilayani Sengerema haipitiki ingawa katika Hotuba ya Wizara, Geita ipo kati ya Wilaya 12 za mradi ambao haujaonyesha mafanikio kama hotuba inavyosema.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wabunge hazitoshi kwa Wilaya ya Geita kwa kuwa kuna Majimbo matatu ya Geita, Busanda na Nyang'wale tumepata shilingi 1,120,900/= wakati Magu ina Majimbo mawili na imepata shilingi 4,900,000/= . Huo si uungwana. Inaonyesha kuwa hakuna ufuatiliaji kabisa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tangu tuanzishe Mabaraza ya Kata hakuna kinachoendelea katika zoezi hilo. Kuna watu walioahidiwa ajira hizi kwa muda mrefu, wamekaa bila matumaini hivyo kusababisha wengine kushindwa kufanya shughuli nyingine za uzalishaji kwa mategemeo kuwa wameshapata ajira.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inatia kichefuchefu hasa ukiangalia walio chini kimadaraka, wanafanya kazi vizuri sana ukilinganisha na wakubwa wao. Kwa mantiki hii, vijana wazuri wanaoweza kufanyakazi wanakatishwa tamaa. Kwa kuwa inaonyesha kuna sera ya kutokujali maamuzi ya wengi na kujiamulia wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama kweli kuna haki inatendeka katika Wizara hii, Wananchi wa Geita wanaomba wapewe kiasi cha shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma yao 850 waliyojenga kwa nguvu zao wenyewe ili kukabiliana na kupunguza umaskini. Hali hii ya kujitolea haijatokea hapa Tanzania. Tuwaunge mkono Wananchi hawa wasije wakakata tamaa na kutusuta. Majengo haya ni maboma ya madarasa 620 na maboma ya nyumba za walimu 230. Mheshimiwa Waziri atoe uamuzi wa haki bila upendeleo.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekubali kuwaajiri Watendaji wa Vijiji na kwa kuwa kutokana na sifa zilizotolewa kutopatikana, Serikali ilisitisha zoezi la ajira mpya na kuagiza kuwa wale walioko waendelee kwa kipindi cha miaka 3 ambako wanatakiwa kujiendeleza

(a) Je, Serikali ina habari kuwa Watendaji wa Vijiji ambao ni *engine* ya kusukuma mbele maendeleo na hivyo kuwa kiungo muhimu katika vita dhidi ya umaskini hawajalipwa mishahara yao kama ilivyoelezwa na Serikali. Sasa watalipwa nini?

(b) Taratibu za ajira hizo haziko wazi na mahali pengine kama Karatu mchujo haukufanyika, mathalan waliokuwa wakituhumiwa kwa matumizi mabaya ya fedha na hata ubadhilifu huo kuthibitishwa na *CAG* wamerudishwa kazini jambo ambalo linaharibu dhana nzima ya Serikali Kuu kukubali kuwaajiri na kuwalipa mishahara.

Pili, kwa kuwa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu walisimamishwa kwa tuhuma zinazoelekea kuwa za kisiasa tangu mwaka 2001 na taratibu za kawaida za kinidhamu zinaelekea hazikufuatwa na watumishi hao hadi leo wanakaa tu nyumbani na kulipwa nusu mshahara, hasa ndugu Dominick Mushi aliyekuwa Afisa Biashara wa Wilaya na ndugu Longoiroi, Mwalimu wa Shule ya Msingi NT - Kata ya Baray, ni lini hatma yao sasa itajulikana kuliko kuwaacha miaka minne bila hatma yao kujulikana?

Mheshimiwa Spika, mashauri yao yalikuwa TUMITAA (Bwana Mushi) na Bwana Longoiroi sina hakika swala lake liko ngazi gani japo mara ya mwisho alikuwa *TSC,* Karatu. Je, ni kwa nini Serikali inaruhusu mambo ya namna hii ambayo kimsingi yanachafua jina la Serikali na rekodi ya Utawala Bora?

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita niliwasilisha maombi ya fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya mradi wa matengenezo ya barabara ya *Nachingwea Hospital*- Mwenge - Mitumbati - Ntila - Chiganga - Namkula hadi Namikango (sehemu ya Chiganga - Namikongo inaitwa *Kambarage Road.* Barabara hiyo inatumiwa na Tarafa ya Nambambo, Ruponda na Lionja kati ya Tarafa sita. Sijapata majibu hadi leo, naomba barabara hiyo ipewe mgao.

Pili, mapendekezo ya kuanzisha Tarafa ya Mnero yamefikia wapi? Je, maombi toka Wilaya yangu ya kutaka Vijiji vipya viandikishwe yamefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, tatu, taarifa ya Watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, tazama ukurasa wa 3, *item* ya matatizo. Je, Waziri alipewa taarifa aliyopewa *Prime Minister?* Naomba majibu ya kila *item* iliyotajwa kwenye ripoti hiyo aliyopewa *Prime Minister.*

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maeneo machache kwenye hotuba hii na kabla ya kuchangia naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha zana za utawala bora Serikali inajitahidi kuimarisha huduma za jamii na miundombinu. Pamoja na jitihada hizi za Serikali, bado kuna tatizo moja la eneo la utawala na uwakilishi. Yapo maeneo mengi ambayo ni makubwa mno kiasi kwamba watendaji na wawakilishi wanashindwa kusimamia

ipasavyo. Kwa mfano, Wilaya ya Bukombe yenye wakazi 3,992 ina Jimbo moja na Kata 14 tu. Baadhi ya Kata hizi ni nyingi, zina Vijiji zaidi ya vinane. Mfano, Kata ya Ushirombo ina Vijiji 20, Kata ya Uyovu Vijiji 12 na vingine vingi. Wilaya ya Bukombe hakuna Kata yenye Vijiji chini ya saba. Hivyo, Watendaji na Viongozi wanapata kazi kubwa namna ya kusimamia maeneo haya mapana.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Serikali ni kwamba, tunaomba zoezi la kuzigawa Kata na Majimbo katika Wilaya ya Bukombe ipewe kipaumbele kwani ina eneo kubwa na wakazi wengi hivyo utawala wake unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, mwisho niiombe Serikali itakapoanzisha mpango wa MMES iangalie uwezekano wa Bukombe kuijengea Sekondari. Wilaya ya Bukombe ina Sekondari tatu wakati ina Shule za Msingi 139, hivyo wanafunzi wanaofanya vizuri na kufaulu wanakosa nafasi ya kuendelea na masomo ya Sekondari kwa vile hakuna nafasi kwenye Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja wa TAMISEMI kwa asilimia mia moja.

**MHE. BALOZI DR. PIUS Y. NG'WANDU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani kwa kunipatia nafasi hii kuchangia kwa maandishi hoja ya Waziri wa TAMISEMI. Nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri yeye mipango mizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusema haya, mambo yafuatayo yanaweza kuboresha utekelezaji wa hoja ya Waziri.

Kwanza, kuwepo na mashindano ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo na Utawala Bora kati ya Halmashauri za Mijini na za Vijijini. Halmashauri zipangwe hadhi zake kutokana na maendeleo ya watu wake. Kuwe na *grade* za Halmashauri na kuwe na motisha kwa kupiga hatua mbele kupitia Bajeti na ruzuku pamoja na kupewa uwezo wa kuajiri na kutoa maamuzi.

Pili, ukaguzi wa mara kwa mara wa Halmashauri zote ili kuzipandisha au kuzishusha daraja. Idara ya Ukaguzi na Udhibiti iimarishwe hadi kufikia ngazi za Mikoa na Wilaya.

Mwishowe, ningependa barabara za Mikoa zinazounganisha Mikoa na Wilaya zake ziimarishwe. Ninayo fikra juu ya barabara ya Kolandoto hadi Somanda katika Mkoa wa Shinyanga. Barabara hii ilijengwa kwa hali ya uhandisi ya juu ya changarawe na Kampuni ya *Stirling Astaldi* mwaka 1968, lakini hadi sasa haijafanyiwa matengenezo makubwa *(periodical maintenance)* na sasa imekufa kabisa. Hebu Waziri kama bado katika barabara hii iko chini yako, ishughulikie. Zaidi ya nusu ya zao la pamba katika *Lake Zone* linabebwa na barabara hii *(Ginneries* - Luguru, Sola, Malampaka, Mhunze na Buzogore).

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Kwanza nakupongeza sana kwa hotuba nzuri. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, maboresho ya Serikali za Mitaa. Kwa kuwa wafadhili huchangia fedha na Serikali yetu nayo huchangia fedha kwa ajili ya maboresho ya Serikali za Mitaa, je, ni fedha kiasi gani za maboresho ya Serikali za Mitaa zimepelekwa katika Halmashauri 38 za mwanzo kwa ajili ya maboresho ya Serikali za Mitaa tangu mwaka 2000 maboresho yalipoanza?

Je, mpango huu wa maboresho utaendelea hadi lini ili Halmashauri zote ziweze kufikiwa na mpango huo mzuri ambao sote tunaunga mkono kwa kazi nzuri inayofanyika na Serikali.

Pili ni kuhusu ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa busara wa kuajiri Watendaji hao muhimu katika kusimamia maendeleo ya nchi yetu huko Vijijini na kukubali kuwalipa mishahara. Naipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna vitongoji ambavyo ni vikubwa na pia Kata zingine ni kubwa katika Wilaya ya Mpwapwa na tayari Halmashauri ya Wilaya imekwishapeleka mapendekezo hayo Wizarani. Je, kabla ya Uchaguzi wa Vitongoji na Vijiji kufanyika mwezi Novemba, 2004 Vitongoji hivyo Serikali itakuwa tayari kuvipa hadhi ya kuwa Vijiji kamili na mgao na Kata Serikali inasema nini kuhusu mgao wa Kata na Tarafa ambazo ni kubwa? Naunga mkono hoja hii kwa 100%.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kuniruhusu kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2004/2005 japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI kwa hotuba yake nzuri na ya kina kabisa inayoipa Wizara dira ya utendaji kazi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Napendekeza mara tu baada ya Hotuba hizi za Mheshimiwa Waziri TAMISEMI, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na kadhalika zitengenezwe Kanuni/Maagizo na kupelekwa kwa Halmashauri zote nchini kwa utekelezaji. Zikichelewa kwa siku 30 utekelezaji wake na Halmashauri kuzindua *by-laws* inakuwa ni maagizo ya Bunge ambayo hayatekelezeki.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2003/2004 ikiondoa kabisa ushuru wa bidhaa kwenye masoko/magulio ila wanunuao na wauzao kwa wingi *(in bulks)* watozwe ushuru. Halmashauri ya Moshi ilikataa katakata agizo hilo. Ushuru sasa unatozwa wa kila kitu hata kwa bibi kizee anayeuza ugoro kwa kijiko cha chai, vifungu vya nyanya, vitunguu, karoti, maandazi, vitumbua, mchicha, kabeji, magadi, mahindi debe, maharage kikapu, mitumba yote inayotandazwa asubuhi na kuanua jioni. Ushuru ni kati ya shilingi 100/= hadi 500/= hata kama hujauza.

Mheshimiwa Spika, kama kuna fedha hizo watoza ushuru wakifuatana na mgambo huzoa fungu moja au dengrizi moja au shati moja na kupeleka Ofisi ya Kata ili

ukakomboe baada ya soko kumalizika. Kila siku ya soko wanaokwenda kujitafutia riziki sokoni wanalia machozi ya maji mpaka macho yanavimba. Hawana pa kukimbilia .

Mheshimiwa Spika, sasa leseni za pato chini ya shilingi milioni 20 zitadaiwa tu wapende wasipende. Unyama unaofanywa na Halmashauri ya Moshi hauna kifani, kisingizio ni kwamba eti Serikali haipeleki fedha za kutosha kuendesha Halmashauri

Waalimu, *nurses* na wafanyakazi wanakatwa fedha za *NPF, NSSF,* lakini hazipelekwi huko, zinabaki Halmashauri. Ni kilio, ni mhangaiko tupu.

Mheshimiwa Spika, mwisho Waziri rudisha imani ya Serikali kwa wananchi. Naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Katika mipango ya maendeleo ya Manispaa inayotolewa kwenye Manispaa nchini mwaka 2003 tuliahidiwa kutengenezewa barabara 3 za lami na nikaambiwa Manispaa tutapewa shilingi milioni 250 kutengeneza kilometa 1.8 za lami. Fedha hizo hazikutolewa! Sababu zipi za msingi?

Katika taarifa za mwaka 2003 nilielezwa kuwa miradi ya kuboresha barabara na mitaro ya Manispaa kama ilivyo katika Manispaa zingine nchini ingefanyika kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 lakini sikuona miradi hii kwa Manispaa ya Shinyanga.

Katika kujibu hoja za Wabunge wakati wa Bajeti ya 2003/2004 TAMISEMI walidai Manispaa ya Shinyanga itakuwa na mradi wa barabara na mitaro Mjini

Naomba kupewa maelezo wakati wa kuhitimisha sababu zipi za misingi kazi hii haimo kwenye Bajeti ya 2004/2005. Sina matatizo mengine kuhusiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Natanguliza shukrani zangu kwa msaada wako wa haraka.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Hotuba ya Bajeti Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni mhimili wa maendeleo ya wananchi kwa ujumla na hasa wale wanaoishi Vijijini. Lengo la kuwa na Wizara hii ni kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo yao wenyewe. Lakini kinachofanyika sio kilichokusudiwa, badala yake Watendaji wengi hasa Wakurugenzi wanafanya mambo yao kama vile wao wapo juu ya sheria na kwa kweli wapo juu ya sheria kwa sababu Waheshimiwa Madiwani hawana uwezo wa kuwadhibiti sio tu kwa sababu ya viwango

vya chini vya Elimu ya Madiwani bali pia kutegemea fadhila kutoka kwa Watendaji. Mkurugenzi Mtendaji ndiye anawalipa Waheshimiwa Madiwani posho zao za mwezi. Hii inatosha kuwafanya Madiwani kuonekana kuwa wameajiriwa na Mkurugenzi Mtendaji na hii ndivyo ilivyo.

Nashauri posho ya Madiwani iongezwe kuwa kima cha chini cha mshahara na fedha hizo zitokane na Serikali Kuu kwa kupitia kwa Afisa Tawala wa Wilaya. Utaratibu huu utawafanya Madiwani kuwa na uhuru na uwajibikaji katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa hotuba ya Bajeti ya mwaka 2003/2004, Bunge lilishauri kuwa utaratibu wa manunuzi *(procurement proceedings)* kwenye Halmashauri ubadilishwe na badala yake pawepo na Bodi ya Zabuni ya Wilaya ambayo ni huru na utendaji wake uwe wa wazi zaidi. Lakini Wizara imefanya mambo ambayo yamepanua mianya ya rushwa katika Halmashauri, hali sasa ni mbaya sana. Waheshimiwa Madiwani wanalalamika, kwa nini wameondolewa kwenye tenda na kuwapo watumishi, ambao ndio ni watekelezaji.

Mfumo wa sasa umehalalisha rushwa, yapo malalamiko makubwa na ya kweli . Nashauri pawepo na Bodi ya Zabuni huru ambayo itaendesha shughuli zake kwa uadilifu na uwazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nilimwandikia Mheshimiwa Waziri, *in confidence* malalamiko ambayo wananchi wa Jimbo la Mbinga Mashariki, walinituma kuhusu baadhi ya Watendaji ambao utendaji wao unasababisha kero zaidi kuliko kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo yao. Baadhi ya kero hizo zilikuwa ni kama zifuatazo:-

(i) Halmashauri ilinunua Jenereta ya kuzalisha umeme kutokana na mkopo wa shilingi 43,000,000/=. Manunuzi hayakufuata taratibu za *tender,* Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu alihoji kukiukwa kwa taratibu. Lakini jenereta hiyo ni mbovu, wananchi wanalipa deni pamoja na riba, wakati umeme haupatikani. Mkurugenzi alipaswa achukuliwe hatua za kinidhamu, lakini kutokana na jeuri yake ya fedha ameweza kuwahadaa Waheshimiwa Madiwani. Hii ni kero kubwa na wananchi wamechoshwa na uongozi huo. Mimi kama mwakilishi wao nakusudia kulirudisha suala hili kwenye Kamati ya Bunge inayoshughulikia mahesabu ya Serikali za Mitaa.

(ii) Mkurugenzi huyu Mtendaji hakuwa na elimu au ujuzi katika masuala ya uendeshaji na usimamizi. Yeye aliajiriwa kama Mhasibu wa Wilaya lakini kwa kutumia vigezo vya ajabu alipandishwa cheo na kuwa Mkurugenzi Mtendaji katika Wilaya hiyo hiyo. Nilipohoji kuhusu uwezo wake, aliweza kuwarubuni Madiwani wakati wa Bunge tupo kwenye vikao vya Bunge kuchukua fedha shilingi 4,000,000/= ambazo zingesomesha wanafunzi 100 kwenye Sekondari ya Kutwa. Wakati anasoma, alitangazwa mfanyakazi bora na kukabidhiwa shilingi 1,000,000/= huko Dar es Salaam. Aliporudi Mbinga, magari, magreda na makatapila pamoja na pikipiki zilikwenda kumlaki. Sijawahi kuona hata Rais wa nchi anapokelewa na magreda, matrekta na

makatapila.  Haya ni matumizi mabaya, wananchi wanaona, waliniandikia na kutaka maelezo.  Mheshimwa Waziri anajua lakini hataki kuwasikiliza Wabunge.  Kwa hili nitahitaji maelezo kama huo ndio Utawala Bora

(iii) Mheshimiwa Spika, wakati nachangia hotuba ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 nilitaka kupata ufafanuzi kuhusu tafsiri sahihi ya ushuru wa mazao wa asilimia 5% *(crop cess 5% at source).* Upo utata mkubwa kati ya Mkurugenzi Mtendaji na wakulima wa Kahawa wanaouza Kahawa yao kupitia Vyama vya Ushirika.  Wanunuzi binafsi wanalipa ushuru wa 5% kwa bei ya shambani.  Vyama vya Ushirika ambavyo hupata mikopo kutoka Benki, hununua Kahawa kutoka kwa wakulima, Kahawa hiyo hupelekwa kwenye Kiwanda cha Kukoboa na hatimaye kusafirishwa kwenda kwenye mnada *(Auction)* Moshi.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wetu ameingia Mkataba na Bodi ya Kahawa ili ushuru wa Halmashauri ukatwe kwa bei ya mnadani tena kwa fedha za kigeni.  Makato haya ukilinganisha na makato halali ni 10%.  Malipo haya hufanyika moja kwa moja Moshi, badala ya kukatwa kwenye Vyama vya Ushirika husika.  Makato haya ni makubwa ambayo yanawafanya wakulima wa Kahawa, kupata fedha kidogo na hivyo kushindwa kuhudumia mashamba yao. Hili nalo nahitaji ufafanuzi pamoja na kuwahakikishia wakulima wa Kahawa kwamba fedha zao zilizokatwa zaidi wanarejeshewa vinginevyo, Mkurugenzi huyu atafikishwa Mahakamani.  Matokeo ya hatua hiyo yatakuwa ni mabaya sana.

(iv) Mheshimiwa Spika, yakp masuala mengi yanayohusu Mkurugenzi Mtendaji wa Mbinga kama nilivyokuwa nimemwandikia Mheshimiwa Waziri kwa nia njema, lakini nadhani Waziri ametingwa na majukumu mengi, kwa hiyo, sitamlaumu, lakini angalau angenijibu.

Nitaunga mkono hoja kama nitatoshelezwa kwa maelezo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza kwamba naunga mkono Bajeti ya TAMISEMI.  Nakumbuka kwamba mwaka 2003 nilipochangia kwenye Wizara hii nilisema Wizara zingine waige utendaji wa Wizara hii. Wizara hii ni kubwa na pana.  Pamoja na kuchukua majukumu ya Wizara zingine kama Afya, Elimu, Ujenzi hii ni Wizara nzito sana.  Kiongozi atakayelaumu ni kwamba hajui uzito wa Wizara hii.

Napenda kuelezea matatizo ya wananchi wa Jimbo langu la Longido, Kijiografia jimbo la Longido lipo mbali na Makao Makuu ya Wilaya jambo ambalo wananchi wanapata shida ya huduma.  Mkoa ukapendekeza Wilaya hiyo igawanywe taarifa ya kikao cha *RCC* italetwa kwako naomba muipitishe

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la huduma, Longido ina vituo vya afya viwili, gari inayohudumia zahanati ni bovu sana.  Kila mara iko Wilayani kwa matengenezo.  Ni ajabu kwamba bado wagonjwa wanabebwa kwa punda, naomba

tupatiwe gari la kuhudumia wananchi kutoka *West Kilimanjaro* mpaka *Lake Natron* bila gari ni ngumu.

Pili, barabara ya kutoka *West Kilimanjaro* kwenda Longido ni muhimu sana kwani kwa sasa mpaka upitie Ngarenairobi - Sanya Juu - Arusha ndiyo aende Longido au Monduli. Naomba fedha za kujenga barabara ya Olmolok - Longido.

Tatu, Mheshimiwa Waziri kama nilivyokueleza ukubwa wa Kata ya Ketumbeine ambayo ni kubwa sana. Kutoka Makao Makuu ya Kata kwenda Kijiji kingine ni kilometa 60. Naomba igawanye.

Kutokana na maelezo ya matatizo niliyoyataja nategemea Wizara itatusaidia Mheshimwa Waziri kwa kuwa maeneo yetu ni magumu. Wewe mwenyewe umepita wakati ulipokwenda kuzindua zahanati huko kwenye Kata ya Ketumbeine. Naomba muwape kipaumbele na nategemea maombi yangu yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti ya Waziri wa TAMISEMI.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza juhudi za Wizara kuendeleza Elimu, Afya, Maji, Barabara na Maendeleo mengine kwenye Halmashauri yetu ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kupongeza kwa hotuba nzuri na ningependa kutoa malalamiko yangu kuhusu mgao wa fedha kwa ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu katika Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, tumekuja Wizarani na kuongea na Mheshimiwa Waziri Hassan Ngwilizi, kuhusu makosa ya makadirio ya idadi ya upungufu wa madarasa. Mwanzo wa mpango huu Wilaya ya Njombe ilitoa makadirio kuwa kuna upungufu wa madarasa 250. Hivyo mgao wa fungu hili ni kwa madarasa 50 tu kwa mwaka yaani 1/5 ya madarasa haya ni 171. Sasa tunapewa idadi ya madarasa 50 tu yaani chini ya 1/3 ya mahitaji halisi. Tumekuja mara nyingi kueleza tatizo letu, lakini hakuna ufanisi wowote wa ombi hili.

Matokeo ya hali hii wananchi wanateseka kabisa. Majengo mengi ya Shule za Msingi hadi mwisho wa mradi huu yatabaki magofu. Kwa kweli tunasikitika kwa hali ya kuwatesa wananchi wakati sehemu nyingine nchini wanapewa shilingi milioni 3. 1 kwa darasa, Njombe siyo hivyo. Baada ya kufuta kodi ya Maendeleo, madarasa hayo yamekwama kabisa kwani tulikuwa tunatumia fedha hizo kumaliza ujenzi, baada ya Wizara kutoona tatizo letu.

Mheshimiwa Spika, tegemeo letu ilikuwa baada ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mradi ule tathmini ingekuwa imefanywa ili kuona kasoro zipo wapi! Mradi unakaribia kwisha pamoja na kasoro zake zote hizi tokea mwanzo wa mradi huu. Nadhani kweli huu siyo utaratibu kabisa wa mipango au miradi tunavyofahamu sisi wote. Hatujachelewa, tunaomba msaada wa Wizara hii, Halmashauri ya Njombe isaidiwe

kuliona tatizo hili na kupatiwa ufumbuzi ili nguvu za wananchi ziungwe mkono na Serikali yao. Rais anapenda watu wanaojituma kwa nguvu zao. Basi Serikali ione hili na tusaidiwe kama *special case.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii nikitegemea msaada wenu katika tatizo hili.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa hotuba yake nzuri na inayoonyesha matumaini makubwa kwa Serikali za Mitaa. Katika Wizara tulizonazo katika Serikali yetu, Wizara hii ni Wizara sikivu, ni Wizara iliyo na watendaji wachapakazi na hodari.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kusimamia Wizara hii vizuri. Timu ya watendaji inayoongozwa na Katibu Mkuu ambaye ni *serious,* ni timu ya watu wanaojituma. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii ya pekee kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa kutembelea jimbo langu. Alifika Malolo kujionea mwenyewe jinsi barabara ya kwenda Malolo ilivyo mbaya. Matokeo ya ziara ile ni kwa Wizara kutoa pesa shilingi milioni 45 za kuendeleza utengenezaji wa barabara ya Malolo.

Kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Ipera hasa wa Malolo ningependa kuishukuru Wizara kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya barabara ya Malolo. Kwa kuwa makadirio ya kitaalam yalikuwa ni shilingi milioni 120 kwa barabara hiyo, awamu ya kwanza Wizara ilitoa shilingi milioni 42 na sasa imetoa shilingi milioni 45. Naomba ikamilishe makadirio hayo kwa kutoa kiasi kilichobaki. Barabara hii ni muhimu kwa sababu ndiyo inayounganisha Mkoa wa Morogoro na wa Dodoma.

Naomba pia kukumbusha ahadi ya Naibu Waziri ya kuunda Kata ya Malolo kwa kuzingatia hali ya kijiografia ya Malolo.

Ningependa nizungumzie kidogo juu ya ajira ya Watendaji wa Vijiji na Kata. Wizara ilitoa sifa na viwango vya nafasi hizi na kwa bahati mbaya Wilaya nyingi hazikuweza kuwapata watu wenye sifa hizo ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Mpwapwa. Naipongeza Wizara kwa kutoa muda wa miaka mitatu kuwapata watu wenye sifa hizo. Sifa zinazotakiwa ni Elimu ya Sekondari Kidato cha IV na Kidato cha VI.

Hata hivyo, Waziri atakubaliana nami kuwa mpango wa MMES ndiyo utakaokuwa ufumbuzi wa tatizo la kuwapata vijana wenye sifa hizo. Mpango wa MMES unaanza mwaka 2004 na matokeo hayataonekana mara moja. Nina wasiwasi kama baada ya miaka mitatu tayari tutakuwa na watu wenye sifa hizo kule Vijijini. Nashauri zoezi hili lifanywe kwa awamu kulingana na upatikanaji wa watu wenye sifa.

Mheshimiwa Waziri anategemea kuwa baada ya miaka mitatu, Watendaji watakuwa wamekwisha kujiendeleza. Lakini ukweli na hali halisi ya vijijini tunaifahamu. Vijiji vingi havina kabisa Shule za Sekondari ambako Watendaji hawa wangeweza kujisomea, kujiendeleza wakati Watendaji wakiwa kazini kunahitaji kuwepo kwa mazingira ya kuwawezesha Watendaji hawa kujiendeleza, hasa ukizingatia kwamba Watendaji hawa wataendelea na kazi zao za utendaji za kila siku.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuwapata Watendaji wenye sifa ni jambo zuri na naliunga mkono. Tatizo ni namna ya kufikia lengo hilo, namna ya kuwapata Watendaji wa Vijiji katika Vijiji ambako kumpata kijana aliyemaliza Elimu ya Sekondari ni nadra sana.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nimetumwa na wapiga kura kwamba wana mpango wa kubadili Kituo cha Afya Nanguruwe kuwa Hospitali ya Wilaya hivyo jiandaeni kupokea maombi hayo ili maamuzi yasichelewe.

Pia mmetupa namba za Vijiji mwaka 2001 za Vijiji vitatu vya Kiwenguro, Niyumba na Mmvata bado hati tu na Serikali zipo hadi leo. Mwaka 2003 tumepewa namba za Vijiji 27 bado hati tu na namba zipo huko vijijini

Mheshimiwa Spika, tumeleta maombi ya mji mdogo wa Nanyamba bado hadi leo. Tunaomba tufikiriwe haraka mnachukua muda mrefu kutekeleza jambo fulani.

Kama umepewa milioni kadhaa mshahara wa ma-*VEO* kwa *rate* ya shilingi 90,000/= unashindwa nini kufanya shilingi 75,000/= uka *save* nyingine na kuongeza Vijiji ni kero si suala la kisiasa, shughuli za kiuchumi Wilayani zinakwama kwa migogoro ya Kijiji mama na kitongoji husika.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, walengwa wake wote na Serikali yetu Kuu kwa ujumla kwa hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri, hotuba ambayo inaungana na hotuba tatu ambazo zimetangulia kuwasilishwa hapa Bungeni ya Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii nitachangia maeneo machache, lakini kwanza nataka niungane na wale wenzangu ambao wanasema kuwa kwa kweli Wizara hii ni kubwa sana kiasi kuwa imechanganyika na maeneo mengine ambayo hayana ulazima wa hivyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuifanyia mabadiliko sana Wizara hii kwa faida na maendeleo ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Wizara hii iondolewe kutoka Ofisi ya Rais iwe kama Wizara nyingine zinazojitegemea. Pili, suala la Walimu ni vyema kubakia katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kama ilivyo sekta yenyewe. Tatu, suala la barabara za Halmashauri libakie Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ingebakia na majukumu ya kusimamia maendeleo ya wananchi, Vijiji, Wilaya na Mikoa kwa kuimarisha demokrasia na Utawala Bora kwa umma wa Watanzania na maeneo yao wanayoishi ikiwa ni pamoja na kusimamia umoja, haki na demokrasia kwa umma na wala sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna wananchi wengi hawaelewi haki zao za Kikatiba pamoja na kutojua sheria za nchi na kadhalika jambo ambalo linapelekea kuwaingiza vijana wengi kujiona wamo katika matatizo mbalimbali na wengine kufungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna wananchi wengi watoto, vijana na watu wazima wa kike na kiume wanasota Magerezani wengine wakiwa ni wafungwa na wengine ni mahabusu, wakiwa wamekaa huko wakisubiri hukumu za kesi zao. Wapo ambao wanasubiri kuhukumiwa lakini kutokana na tatizo la Mahakimu nchini wanakaa mahabusu kwa miaka mingi bila ya kupelekwa Mahakamani. Lipo tatizo la kuwepo Hakimu mmoja ambaye anahudumia Wilaya zaidi ya nne jambo ambalo linaleta usumbufu kwa mahabusu anayengojea hukumu yake, akiwa amekaa ndani kwa miaka mingi ni vizuri Serikali ikiliangalia hili, vinginevyo watu hawa ambao wengi wao wanatoka Vijijini/Wilayani wataendelea kukosa haki yao na kutokuona faida ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, pia kuna wasi wasi kuwa wapo wafungwa au mahabusu Magerezani kwa makosa ya kulipa kodi na uzururaji. Kwa hiyo, kama wapo basi naiomba Serikali kuwapatia msamaha hasa tukiangalia kuwa hivi sasa Serikali imefuta kodi mbalimbali hapa nchini.

Pia suala la watoto wengi wadogo kuwepo Magereani naomba Serikali kuliangalia sana na kulipatia ufumbuzi wa kudumu kuondoa tatizo hili. Vile vile kuna kodi ambazo tayari Serikali imezifuta, nawaomba Watendaji wa Vijiji/Halmashauri na kadhalika kuwaeleza wananchi kodi hizo zilizofutwa na kutowatoza tena kodi hizo kama Serikali ilivyozifuta.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono Bajeti hii kwa 100%.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza pongezi na shukrani. Nampongeza sana Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wafanyakazi wote Wizarani hapo.

Pili, *Road Toll,* naomba sana baada ya Bajeti yako kupita naomba kila mara unapotolewa mgao wa fedha za barabara Wabunge tupewe taarifa ya mgao huo ili tufuatilie fedha hiyo. Barabara ya Wilaya Jimboni ambayo haijachongwa tangu ukoloni, Ngerengere - Kidunda, Kwaba hadi Usungura. Watanzania bado hawajapata uelewa wa fedha hii. Naomba Tume ifuatilie fedha ya *Road Funds,* nchini zinarudishwa Wizarani au zinaliwa na Kitengo cha Wizara yako wakishirikiana na Wahandisi.

Tatu ni kuhusu Madiwani, posho zao ziongezwe, Madiwani ni kiungo muhimu na hali za Madiwani ni mbaya sana. Naomba tuwasaidie sana Madiwani na kuhusu mgao wa Kata za Morogoro Vijijini tangu mwaka 1997 tulipeleka maombi ya Kata mpya kama ifuatavyo:-

| Kata ya sasa | | Kata Mpya |
|---|---|---|
| 1. Ngerengere | - | Ngerengere na Matuli |
| 2. Mikese | - | Mikese na Kinonko |
| 3. Kidugalo | - | Kidugalo na Selegete |

Mheshimiwa Spika, hadi sasa bado hatujapata majibu.

Mehsimiwa Spika, kuhusu barabara, barabara mbovu Jimboni kwangu ni Ubena-Ngerengere hadi Kidunda, Msomvizi hadi Lubungo, Kibwaya hadi Mfumbwe, Madamu hadi Luhololе, Mkuyuni Kivuma hadi Kubuko, Kibungo hadi Mwarazi, Kwaba hadi Usungura, Daraja la Mto Ruvu kwenda Tununguo hadi Mbalangwe na Barabara Likenge hadi Selegete B.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake na kazi nzuri Wizara yake iliyofanya. Nampongeza Naibu Waziri kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Ujenzi wa Wodi ya Wazazi Hospitali ya Ludewa. Mwaka 2003 wakati wa Bajeti nilitoa kilio cha Wanawake wa Ludewa kuhusu ukosefu wa wodi ya wazazi. Wanawake Ludewa wanatumia sehemu ya Kliniki. Sina uhakika kama Mheshimiwa Waziri amelipa kipaumbele tatizo hili.

Pili, mwanzoni mwa mwaka 2004 Wizara ilipokea kilio cha wananchi wa Makete kuhusu ukosefu wa watumishi kutokana na vifo vingi vinavyotokana na ugonjwa wa UKIMWI. Naomba Wizara iliangalie kwa undani jinsi ya kusaidia Wilaya hii kwa haraka kupata watumishi. Watumishi hawa walipwe motisha ikiwa ni Posho ya Mazingira magumu. Wizara ifanye jitihada za makusudi kusaidia Wilaya ya Makete. Hakuna watumishi wa fani ngazi za Kata. Maafisa Maendeleo ya Jamii ni wachache sana. Kilio hiki kinahitaji ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la kutiliwa umuhimu wa vituo vya kulelea watoto wadogo *(daycare centres)* jamii ihamasishwe ili kila Kijiji kuwa na kituo cha kulelea watoto wadogo ili kuwapunguzia akinamama kazi na pia kuwafanya watoto waende shule badala ya kubaki nyumbani kulea wadogo zao.

Kuhusu Ofisi ya Mbunge Viti Maalum, Ofisi yangu haijakarabatiwa kama taarifa inavyodaiwa wala *furniture* hazijanunuliwa na sina Ofisi nyingine ila nimeonyeshwa chumba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Habari zilizoandikwa hapo siyo sahihi.

Kuhusu ubinafsishaji wa *Community Centres* uangaliwe upya kwani umeleta kero kubwa kwa akinamama. Sasa hakuna mahali ambapo jamii pamoja na Wanawake

wanaweza kukutana na kujadili masuala mbalimbali. *Community Centres* hizi zilitumika pia kwa kama vituo vya kulelea watoto wadogo. Vijiji vingi watoto wametoka katika *Centre* hii na sasa wanahudumiwa katika chumba kidogo cha Ofisi ya Mtendaji kwani *Community Centre* kukodishwa na jamii haina uwezo wa kulipia. Suala hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Naibu wake Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, pia Katibu Mkuu Bwana Mmari, Naibu Katibu Mkuu Bwana Foka na wasaidizi wao wote kwa kuandaa hoja yao ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2004/2005 ambayo ni nzuri na naiunga mkono asilimia kwa mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda niweke kumbukumbu sawa kwa kuishukuru Wizara hii kwa ushirikiano wa hali ya juu sana hasa kupitia kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa jinsi alivyotusaidia sisi wananchi wa Kinondoni hasa wale ndugu zangu wa Mabondeni Kigogo, Mzimuni, Magomeni na Mwananyamala. Kesi zote zilizokuwa ziko Mahakamani zilisitishwa huku tukitafuta kwa pamoja suluhu sahihi kwa wakazi wa Mabondeni. Kwa niaba ya wapigakura wangu wote wa Mabondeni katika Jimbo la Kinondoni tunashukuru sana kwa usikivu wa Wizara. Naomba tuendelee hivyo hivyo kuelimishana na kutatua matatizo yetu kidugu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Serikali kwa uharaka unaostahili na kwa kuogopa maafa yasitokee, itafute ufumbuzi wa kuzuia mmonyoko ya barabara inayounganisha Tawi la Mapera na Tawi la Kigogo Kati kwenye Kata ya Kigogo. Hili ni suala la haraka sana na naomba mkiwa tayari basi mimi, Diwani na Wenyeviti wa Mitaa hiyo wahusishwe pamoja na viongozi Kata ya Kigogo, Mto Msimbazi kutoka SUKITA unahama hama sana udhibitiwe, kama haudhibitiwi utaleta maafa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa wananchi wa Kata ya Kigogo na wale wanaotoka Kata ya Mburahati wanakosa njia ya kupita eneo la JABA kwa sababu mwananchi mmoja ambaye hajaendeleza eneo hilo amefunga hiyo njia. Uongozi wa Manispaa na Wilaya imejitahidi lakini suluhu haijapatikane. Sasa naomba Serikali iingilie kati na kulimaliza hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule ya Msingi ya Kigogo wakati wa mvua haiingiliki na wanafunzi wala Walimu. Naomba sana utafiti wa ujengaji wa *underground drainage* ufanywe ili kuondoa adha hiyo ya maji.

Sisi wote tunajua ukubwa wa janga la UKIMWI hivyo basi naomba utaratibu wa kuridhisha ufanywe ili kwa mfano vikundi mbalimbali vya vijana wanaotaka kuhamasisha wenzao wasiwekewe urasimu usio wa lazima, vinginevyo vijana wetu watavunjika mioyo na kuzagaa vijiweni ovyo.

Mheshimiwa Spika, *TACAIDS* wanaelekeza vijana waende Manispaa, Manispaa inasema haina fedha. Sasa unamsaidia nani kama sio hawa vijana wetu? Naelewa lazima vikundi viwe *scruitinised*, lakini basi Manispaa zifanye hima ku-*scrutinise* hivyo vikundi na kuvielekeza vifanye nini? Vinginevyo fedha hizo na hamasa dhidi ya UKIMWI vitabaki Benki na kwenye mafaili huku vijana wetu wakiangamia.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna Majimbo ya Uchaguzi 7. Kati ya hayo ni Majimbo matano yenye Vijiji na kadhalika kwa maana ya maeneo ambayo yana nafasi ya kupanuka na kuwa na kilimo. Majimbo mawili yaani Ilala na Kinondoni hayana pa kupumulia ni *totally urban*, kwa maana hiyo unapozungumzia kujenga zahanati mpya kujenga Shule ya Msingi, Shule ya Sekondari kwenye *open space* kwa maana ya burudani hakuna nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapozungumzia kupanua elimu kwa mfano, *1,500 Secondary Schools in 2004/2005* majimbo haya mawili yataambulia *zero,* kujenga zahanati mpya, Majimbo haya mawili Ilala na Kinondoni hayatafaidika kwa sababu hakuna nafasi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa kuzingatia hali halisi hiyo, basi ifanye utafiti na ku *buy-off* ama *squatter areas* zilizopo au hata nyumba za watu na wao wapewe viwanja sehemu zingine *plus* fidia, ili hayo maeneo sasa yawe *ear-marked for schools, both primary and secondary* pamoja na Zahanati na o*pen spaces* za burudani kwa Jimbo la Kinondoni, hili ni ombi rasmi. Tafadhali Serikali tusaidieni.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kinondoni ina wakazi milioni 1.08 na inahudumiwa na hiyo Hospitali ya Mwananyamala. Hospitali ilikuwa na *X-ray* ambayo iliharibika na hivi majuzi wamepewa *X-ray machine* ambayo ni ndogo sana *(only 20 X-rays per day).* Naomba Serikali itupatie mashine kubwa ya *X-ray* hata *second generation* kutoka Uholanzi na kadhalika ambayo inaweza kuhudumia angalau wagonjwa 100 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu wa usimamiaji wa *Road Toll Fund* urekebishwe hivi. Kwamba kila *Quarter remittance* iende kwenye Jimbo kwa mzunguko. Hii itakuwa na *impact* kubwa katika kutatua matatizo ya barabara, madaraja, makalvati na mifereji ya Majimbo yetu na yatasimamiwa vizuri na Mbunge pamoja na Madiwani wake, kuliko hivi sasa kuna uwezekano wa kupendelea jimbo moja na kadhalika. Lakini kijimbo *impact* inakuwa *visible* au *apparent.*

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano wa 15 wa Bunge la mwezi Aprili, nilielekezwa na *Muhimbili Orthopaedic Institute (MOI)* kufanyiwa *Physiotherapy.* Nilishangaa kuona kuwa *qualified Physiotheraphist* mmoja tu, hii ni Hospitali ya Mkoa. Naomba sana tena sana Serikali ifanye kila linalowezekana iajiri angalau *Physiotherapist* watatu au wanne ni *Orthopaedic* watatu au wanne. Hawa ni wauguzi au wahudumu wa muhimu sana. Kabla mtu hajapelekwa *MOI* Dar es Salaam basi apate unafuu wa wahudumu hawa. Naomba Serikali iliangalie hili kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Serikali ichukue jukumu la kuhakikisha kwamba taa za barabarani za Jiji la Dar es Salaam zinawekwa. Jiji na Manispaa zake tatu hawana uwezo kifedha wa kuweka hizo taa. Taa hizi ni mojawapo ya kitendea kazi kwa Jeshi la Polisi kwani vibaka na wahalifu wengi hawaendi kwenye maeneo yenye nuru au mwanga. Naiomba Serikali ifanye hii kazi kupitia Wizara za Ujenzi na TAMISEMI pamoja na *TANROADS* tafadhali kaeni pamoja mtekeleza ombi hili.

Mheshimiwa Spika, juzi kwenye mchango wangu wa Waziri Mkuu nimesema Tanzania tusiige muundo wa kiingereza kuhusu Madiwani. Madiwani wa Tanzania ni *full time employees,* hivyo tubadili mtazamo wetu juu ya hawa Madiwani tuwe wa Kitanzania. Diwani wa Tanzania anajituma na anafanya kazi kubwa sana. Anastahili kama Mbunge anunue gari kwa mfano, kama kitendea kazi kwa msamaha wa kodi. Naomba Serikali ilitazame hili na kulikubali. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka nagusia hili tatizo la mabwawa ya Msisiri huko Mwananyamala. Wananchi wamejitahidi sana kuyadhibiti haya mabwawa. Naomba kwa mara nyingine tena Serikali na sisi tukae tuzungumze tulitatue hili swali. Sasa hivi linatatulika vizuri. Tupeni baraka zetu tuondoe kero za wana-Msisiri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza Wahandisi kwenye Manispaa ya Kinondoni. Wahandisi waliopo sasa hawakidhi mahitaji ya utekelezaji wa kazi. Binafsi nimekaa kwa zaidi ya miezi 8 hadi 10 nikisubiri kazi za wananchi zifanyiwe kazi, lazima nibembeleze. Nadhani Wahandisi waliopo wana kazi nyingi sana. Tuongezeni Wahandisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi ngumu na nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono hoja yao nzuri, napenda kuomba na kushauri kuhusu Elimu ya Msingi. *Ceiling* ya *OC* kwa Idara ya Elimu mwaka 2003/2004 ilikuwa shilingi 171,439,400/=, mwaka 2004/2005 imeshuka dhadi shilingi 145,046,947/=. Upungufu huu utaathiri maendeleo mazuri ambayo Wilaya yetu imekuwa ikifanya kwa miaka miwili mfululizo kushika nafasi ya juu katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba. Mwaka 2002 tulishika nafasi ya pili Kitaifa na mwaka 2003 tulishika nafasi ya tatu Kitaifa. Aidha, tuna upungufu wa walimu 205 kwa shule za msingi. Tunaomba msaada.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri, tunaomba msaada wa magari makubwa kwani yale yaliyopo SM 1116 na SM 2604 yameharibika na gari SM 1116 tumefanikiwa kutengeneza, lakini tumeshindwa kulikomboa kwa sababu zinahitajika fedha nyingi. Magari hayo makubwa ni muhimu katika matengenezo ya barabara zetu, zinahitajika shilingi milioni 87.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya Tarafa, Kata na Vijiji. Nakumbushia ombi letu la zamani la kuwa na Tarafa nne badala ya mbili za sasa ambazo zimekaa kikabila. Utekelezaji wa ombi letu utaondoa hisia za ukabila na kurahisisha usimamizi wa kazi. Nakumbushia pia ombi letu la Kata mpya za Kalembo na Mlale. Maombi yalikwisha wasilishwa kwa taratibu za kawaida.

Mheshimiwa Spika, vile vile nakumbushia usajili wa Vijiji vyetu nane, vilianzishwa mwaka 1997, lakini hadi leo havina hati rasmi za kuandikishwa. Aidha, zipo sheria ndogo tulituma kwa ajili ya kibali na saini ya Mheshimiwa Waziri, hatujapata majibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji, Halmashauri yetu haikuwa na ajira rasmi na watumishi hao. Tuliomba kufanya ajira ya Watendaji hao waliohitimu Kidato cha IV na VI, lakini hatujapata jibu. Naomba ufafanuzi wa maelekezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii na nawatakia wenzetu wa TAMISEMI mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara kwa kukamilisha na kuiwakilisha hotuba nzuri hapa Bungeni. Hotuba imechambua kwa kina shughuli zote za Wizara na kwa hiyo, imetoa nafasi nzuri kwetu sisi Wabunge kuchangia hotuba ipasavyo. Kutokana na hali hii, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi kwa jumla. Kwa hito katika Jimbo langu, nina barabara tano na ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya Mbinga. Kwa muda mrefu hazijafanyiwa matengenezo, hivyo zinapitika kwa taabu sana. Barabara hizo kwa kuwa hazipati matengenezo hurudisha nyuma maendeleo ya wananchi. Barabara zenyewe ni Barabara ya Mbinga - Ngumbo, barabara ya Mambo - Mtuta, barabara ya Mapera - Lundo, barabara ya Liparamba - Mitomoni na mwisho ni barabara ya Mpepo hadi Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni barabara zinazotumiwa na wananchi wengi, zinapita maeneo yanayozalisha chakula na mazao ya biashara kwa wingi sana. Kwa hiyo, matengenezo ya barabara hizo ni muhimu mno kwa maendeleo ya wananchi. Mheshimiwa Waziri, naamini wewe ni msikivu na unatambua wazi wazi uzito wa jambo hili. Hivyo naomba sana fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo hapo juu. Ni matumaini yangu na naamini maombi yangu yatakubaliwa.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani mapema. Ahsante sana.

**MHE. DANIEL N. YONA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya fedha zilizotolewa mwaka 2003/2004 kwa ajili ya Ofisi za Wabunge, zinaonyesha Ofisi yetu ya Wabunge wawili wa Same Magharibi na Same Mashariki tulipewa shilingi 500,000/=. Mimi sina taarifa ya fedha hizo kutumika kwa *stationery* na mapazia. Mbunge mwenzangu pia ameniambia ametumia fedha zake kuboresha hiyo Ofisi ambayo ni yetu wawili. Je, hizo pesa zilitolewa kwa nani na kwa nini?

Mheshimiwa Spika, awashwaye ndiye anayejikuna, kwa hiyo, nashauri kila Mbunge apewe pesa hizo *cash.* Akitumia vibaya, aibu ni yake yeye mwenyewe na hatalaumu *DC, DAS* au *RAS.*

Mheshimiwa Spika, nashauri pia zitolewe pesa hizo kwa uwiano fulani. Kwa nini Ofisi ya Mbunge mmoja apate shilingi 2,000,000/= na mwingine jirani yake apewe shilingi 250,000/= tu. Naunga hoja mkono.

**MHE. PAULO N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ililetewa maombi ya Kata ya Bunambiyu - Tarafa ya Mondo, ibaki Wilaya ya Shinyanga Vijijini badala ya Wilaya ya Kishapu kutangazwa na Makao Makuu kuwa Mji wa Mhunze.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba umbali wa kutoka Bunambiyu hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu (Mhunze) ni mbali kwa kupata huduma wakazi wa Kata ya Bunambiyu. Hivyo naomba kama uwezekano upo, Kata hiyo iruhusiwe kubaki Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja ya TAMISEMI nimeuelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera na mkakati wa Maendeleo Vijijini. Kwa kuwa Wizara ya TAMISEMI imeliona hili, nawaunga mkono na kuwapongeza. Hii ni kwa sababu 80% ya Watanzania wanaishi vijijini wakitegemea kujiajiri katika kilimo, ufugaji na uvuvi na pia uchimbaji wa madini. Hata hivyo, wengi wa Watanzania hawa zaidi ya 75% wanaishi kwa kilimo na ufugaji. Ili lengo hili na mikakati ya maendeleo vijijini ifaulu, Waziri aeleze ni vipi atawawezesha Maafisa Kilimo kufanya kazi ya ugani vijijini, Afisa Mifugo na Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kada ya watumishi hawa muhimu katika mfumo na mikakati ya maendeleo vijijini, ambapo hivi sasa hawatembelei na kuhamasisha maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi za Wabunge, taarifa ya Mheshimiwa Waziri inasema kuwa Jimbo la Same Magharibi na Same Mashariki katika mwaka wa fedha, kila Jimbo litapewa shilingi 250,000/= na kubakia shilingi 50,000/=. Hii siyo kweli na taarifa hii ni kulidanganya Bunge. Fedha hiyo inasemekana ilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa *stationery* na mapazia, siyo kweli kabisa. Naomba kwa kwa sababu nimekuwa natumia fedha ya mshahara wangu kwa *stationery,* taarifa hii isahihishwe.

Pia naomba kigezo kilichotumika katika fedha za mgao katika kila Jimbo. Mkoa huo huo, Ofisi zingine zimepewa mgao wa shilingi 2,000,000/=, hii ni tofauti kubwa mno. Naomba maelezo hasa kwa msingi kuwa Ofisi zote wa Wabunge zinatakiwa ziwe na usawa *(uniformity).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, naipongeza sana Wizara ya TAMISEMI kwa kubuni na kuanzisha mfumo katika awamu ya kwanza ya Halmashauri 38 na sasa baada ya awamu hiyo ya kwanza kwisha, kuingia awamu ya pili ya Halmashauri 52.

Mheshimiwa Spika, maswali ni kwa nini majina ya Halmashauri zinazotengwa katika kila awamu hazitangazwi wazi na kujulikana kwetu Wabunge? Kuna usiri gani? Vigezo gani vinatumika? Halmashauri yangu ya Same iko katika awamu ipi? Kama haipo popote, ni kwa sababu gani ili tukajirekebishe? Naomba majibu na ufafanuzi kwa maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Barabara, hali ya barabara katika Halmashauri yangu ya Same ni mbaya sana hasa zile za milimani. Wananchi wengi wa Wilaya ya Same 75% wanaishi milimani ambapo usafiri wa barabara na mawasiliano ya simu ni mbovu na/au haupo kabisa. Mfano, Tarafa yote ya Mwembe-Mbaga, Gonja na Mambavunta. Mwaka 2003, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa alipotembelea Wilaya Same alifanya ziara eneo la vijijini katika Kata ya Suji iliyoko ukanda wa milimani. Alipongeza juhudi za wananchi za kuchimba barabara zao kwa mikono yao wenyewe kwa misaragambo na tamasha.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais aliahidi kutengeneza barabara hiyo aliyosafiri ya Makanya - Suji Malindi - Suji Gonjanza, itengenezwe kwa kiwango cha changarawe. Katika kufuatilia ahadi hiyo ya Rais Ikulu, nilijibiwa kuwa jukumu la kutekeleza ahadi hii, limetolewa kwa Wizara ya TAMISEMI. Tayari mwaka huo huo, Wizara ya TAMISEMI ilituma Wahandisi wake katika barabara hiyo na kuifanyia tathmini ili iingizwe katika Bajeti ya mwaka huu.

Swali langu ni kuwa je, barabara hii imetengewa fedha katika mwaka 2004/2005 ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais? Naomba majibu na ufafanuzi wa maelezo na maswali yangu kwa sababu kwa muda mrefu sasa wananchi wamekuwa wakiulizia juu ya ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, wakati huo huo kipindi chake kikiwa kinafikia ukingoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maliasili na Mazingira, Wilaya ya Same imeathirika sana katika uharibifu wa maliasili za msituni na mazingira ya matumizi mazuri ya ardhi na misitu. Halmashauri ya Same kwa maana ya uongozi, imeshindwa kusimamia utunzaji wa maliasili na mazingira. Karibu Wilaya hii itakuwa jangwa. Nimeifahamisha Ofisi ya Waziri wa TAMISEMI na Naibu wake, juu ya udhaifu wa uongozi wa Halmashauri ya Same na kwa miaka mitatu sasa hakuna majibu ya hatua zinazochukuliwa na Wizara ya TAMISEMI. Hivi karibuni viongozi wa Halmashauri

hiyo waliadhibiwa na Kamati ya Bunge ya *LAAC* kukatwa mshahara wao kwa kuwa na taarifa mbaya ya hesabu za Halmashauri ya Same.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamesikia upungufu huu ukitangazwa katika redio na magazeti, bado Wizara ya TAMISEMI haina hatua yoyote ya kuinusuru Halmashauri ya Same katika dimbwi kubwa la uongozi uliochoka na wa kubabaisha. Viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro wameliona hili na kulifikisha TAMISEMI, lakini bado hakuna majibu. Leo ni muhimu majibu yakapatikana ili kurejesha imani ya wananchi wa Same kwa Serikali yao ya CCM.

Mheshimiwa kuhusu Vituo vya Afya, wananchi wa Wilaya ya Same eneo la milimani katika Kata ya Chome na Vunta, wamejenga vituo viwili vya Afya ambavyo vilisajiliwa mapema mwaka 2003. Vituo hivyo ni Kituo cha Afya cha Shengena kilichopo Kata ya Chome na cha Vunta kilichoko Kata ya Vunta. Kwa sababu vituo hivi viko maeneo ya milimani ambapo usafiri ni wa shida, naomba kufahamu iwapo vimetengewa Bajeti ya gari la kubebea wagonjwa *(ambulance)* katika kila Kituo cha Afya. Nategemea kupata jibu la kero hii kubwa ya kupongeza juhudi za wananchi katika ujenzi wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza Waziri Mheshimiwa Hassan Ngwilizi na Naibu wake, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameifanya katika maendeleo ya nchi yetu kupitia Wizara yao ya TAMISEMI. Hakuna Mtanzania ambaye haishi katika Halmashauri *(Councils or Municipality).* Mmeshika roho zetu, tunastahili kuheshimu na kupongeza kazi yenu.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2003/2004. Nawatakia kazi nzuri zaidi katika mwaka 2004/2005 na naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba Wizara izingatie yafuatayo kuhusu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kasulu. Mji wa Kasulu ambao una wakazi zaidi ya 40,000 hivi leo na unainukia sana kibiashara, ulishatangazwa kati ya maeneo manane yatakayokuwa Mamlaka ya Mji Mdogo. Naiomba Wizara iharakishe kukamilisha taratibu za sheria ili hadhi hiyo iweze kuanza mapema iwezekanavyo na wananchi waanze kufurahia marupurupu ya kuwa Mji Mdogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya mishahara kwa Walimu Wilayani, kila mwisho au mwanzoni mwa mwezi Walimu wanalazimika kwenda Makao Makuu ya Wilaya kupokea mishahara yao kutegemeana na sehemu watokako, Walimu hao wanakosa kuwepo kwenye maeneo yao ya kazi kwa siku 2 au 3 kila mwezi na wanafunzi wanakosa vipindi kwa siku hizo hizo. Kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kuwapelekea mishahara hiyo walau hadi Makao Makuu ya Tarafa? Kuna maeneo ambayo Walimu wanalazimika kutembea kwa miguu au kwa baiskeli umbali wa kilometa

50. Serikali iwasaidie hawa kwa kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kama huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Huduma ya Afya, Serikali inajitahidi kuboresha huduma za afya kwa kujenga Zahanati karibuni kila kijiji. Lakini, kwa mfano katika Jimbo langu la Kasulu Mashariki, tunazo Zahanati saba ambazo hazina wafanyakazi wala vifaa. Naiomba Serikali ifanye inavyoweza kuelimisha vijana wengi ili Zahanati zipate Waganga na Wahudumu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ninawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, ninazo hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mufindi kwa miaka kadhaa sasa imekuwa ikitunga sheria ndogo ya *cess* ya zao la chai kuwa angalau ifike 2% ili mapato yake yasaidie maendeleo ya wananchi. Mara zote Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI imekuwa ikikataa kupitisha sheria hii wa maelezo kuwa ni zao nyeti. Tungependa ieleweke kuwa mazao yote yanayouzwa nje ni nyeti na kwa kweli tunaomba maelezo yanayoeleweka. Kwa sababu *cess* ambayo Halmashauri inapata kwa sasa ni shilingi 1.80 kwa chai iliyosindikwa *(made or block tea).* Hii ikiwa na maana kuwa shilingi 1.80 ukilinganisha na bei ya chai ya shilingi 1,250/= kwa kilo ni 0.12%, ambayo ni ya chini mno ikilinganishwa na iliyoidhinisha ya 5%.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwatoa Madiwani katika Bodi ya *Tender,* ni dhahiri kuwa kwa Serikali za Mitaa, uamuzi huu ni kuwanyang'anya wananchi madaraka. Hivi inakuwaje Ofisi ya Mkurugenzi itangaze kazi, ifungue *tender* na itoe kazi, imsimamie aliyepata kazi, imthamini, imlipe, bila Madiwani wenye Halmashauri yao kujua? Pamoja na kuwa sisi Mufindi tunaye Mkurugenzi mzuri, hii ni bahati yetu na tunamshukuru Mungu. Lakini Waheshimiwa Wabunge wana migogoro mingi juu ya Wakurugenzi na Watendaji wao kuhusu uadilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa dhati na kwa upendo kuwa uamuzi huu ni mbaya, badilisha. Kwa sababu si tu hauna *check and balance,* lakini unahamisha maamuzi makubwa toka kwa wananchi kwenda kwa Watendaji wa Serikali na pia uamuzi huu unafungua migogoro isiyoisha kati ya Watendaji na Madiwani. Lakini pia sina hakika kama *ALAT* Taifa ilihusika katika uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, pia ili Halmashauri iwe na wenyewe, ni vizuri maamuzi ya Bodi ya Ajira yathibitishwe na ya Fedha na Uongozi badala ya Bodi ya Ajira kuwa na uamuzi wa mwisho.

**MHE. HENRY D.SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo naomba yawekewe mkazo na Wizara hii ni pamoja na mabadiliko mbalimbali ya Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya yangu ya Lushoto, bado lipo tatizo la utendaji usioridhisha katika idara chache. Idara hizo ni Ardhi, Maji na Elimu.

Mheshimiwa Spika, bado upimaji wa viwanja ni duni sana, utekelezaji wa Miradi ya Maji, unakwenda pole pole sana. Idara ya Elimu bado upo uhaba mkubwa wa Walimu katika Jimbo langu hasa Tarafa ya Mlola. Naomba Wizara isimamie na kutoa msukumo na ikibidi watumishi wasio na uwezo waondolewe madarakani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kurejesha ajira ya Watendaji wa Vijiji. Katika hatua hiyo, Watendaji wapewe mafunzo. Chuo cha Mipango hapa Dodoma kitumike kikamilifu kuwafundisha Watendaji wa Kata na wa Vijiji, japo utaratibu wa kutayarisha mipango, udhibiti na usimamizi wa fedha za vijiji na miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tuhuma juu ya Watumishi wa Wizara Makao Makuu kwa kushirikiana na Watumishi wa Halmashauri kuhujumu miradi ya maendeleo Wilayani, ni budi zichunguzwe. Ni vizuri ushauri wa Wabunge unapotolewa dhidi ya watumishi husika, uchunguzi juu ya Watumishi wa Halmashauri mbalimbali ufanyike haraka na ukweli ukibainika, hatua za nidhamu zichukuliwe haraka. Kwa sasa inachukua muda mrefu sana malalamiko yanapotolewa na hatua kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naipongeza Wizara ya TAMISEMI na natoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa Tarafa ya Mlola kwa Wizara kutoa fedha shilingi 125,000,000/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya kutoka Ngwelo Mlola - Makanya hadi Milingano, Mashewa. Naomba ahadi ya kutolewa fedha nyingine za dharura mwaka huu itekelezwe.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kuhusu Serikali Kuu inazitumia fedha karibu 85% ya fedha zote kwa Halmashauri za Wilaya. Mahesabu ya TAMISEMI hufanywa na Kamati ya Bunge *(LAAC).* Kwa nini Mhakikimali wa Serikali hafanyi ukaguzi kwenye Halmashauri za Wilaya? Kwa nini Afisa Mhasibu anapoharibu katika Wilaya moja, anahamishwa bila adhabu kwenda Halmashauri nyingine?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuzipa Makao Makuu za Wilaya hadhi za Miji Midogo. Kwa kuwa Halmashauri ya Nzega ilishaleta mapendekezo hayo, je, hatua gani inayobaki kufanya Nzega iwe Mji Mdogo na baadaye Mji kamili? Zoezi litakamilika kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa?

Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha *ALAT* cha Arusha, Serikali iliahidi kufanya utaratibu wa kubadilisha sheria ili kuwapa maslahi mazuri Madiwani. Je, ni hatua gani imefikiwa kuboresha maslahi hayo?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwalipa mishahara Watendaji wa Vijiji, kwa nini hadi leo Watendaji hawajalipwa fedha zao hadi sasa ama inawezekana hiyo mishahara imeliwa?

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya vijiji vipatiwe hati na kujulikana mapema ili wajiandae vema kwa uchaguzi wa Serikali ya Mitaa. Pia baadhi ya Kata ni kubwa mno, nazo zinastahili kugawanywa.

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu gani wa kuvipatia Vituo vya Afya usafiri (magari) hasa vilivyo mbali na Hospitali za Wilaya? Mfano, ni Vituo vya Afya vya Puge na Bukene, vilivyo katika Wilaya ya Nzega?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema zenye ufanisi na endeleeni kusimamia Halmashauri zetu kwa karibu mno.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Bajeti ya Wizara na Mipango iliyoandaliwa ni mizuri sana. Imelenga mahitaji ya wananchi. Kwa hiyo, inaungwa mkono na wananchi wote wa Jimbo la Chilonwa.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa utekelezaji wa Mipango yote ya Maendeleo, ni mizuri na imetunufaisha sana. Wananchi wa Chilonwa wanaiunga mkono Serikali na kuipongeza Wizara ya TAMISEMI kwa yote waliyoyafanya. Tunaunga mkono jitihada zenu. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa kipekee kabisa, kwa niaba ya uongozi wa Wilaya ya Dodoma Vijijini, ningependa nilete ombi letu la kutufikiria kuigawa Wilaya yetu ya Dodoma Vijijini. Tumekwishawasilisha ombi hili rasmi sasa, lakini ombi letu lilikuwepo kwa muda mrefu. Wilaya yetu ina Tarafa 8 na ina Kata 48. Ni Wilaya pekee nchini yenye kata nyingi kiasi hicho. Tumewahi kuomba kuongeza idadi ya Kata zetu nyingine zenye vijiji kati ya sita na saba ili zigawanyike, lakini mara tumekataliwa kwa maelekezo kwamba iwapo Kata zitaongezwa, tutafikia kata 50 na zaidi. Kwa hiyo, tukawa tunashauriwa kufuatilia ombi letu la kugawa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ziko Kata mbili, ya Segela yenye vijiji saba, ambayo inazidi ukubwa hata baadhi ya Tarafa na Kata ya Fufu ambayo nayo ina ukubwa huo huo. Tumeomba mara tatu kwamba kata hizi zigawanywe, lakini Serikali ilisita kugawa kata hizi kwa kuona kuwa tutaendelea kuongeza kata bila kufikiria ukubwa wa Wilaya. Maana kama maombi hayo ya kugawa kata yangekubaliwa, yangefikisha wilaya yetu ya Dodoma kuwa na kata 50. Kwa hiyo, kwa kutokubali kutufikiria kugawa Wilaya maana yake Dodoma Vijijini itabakia na Kata 48 ambazo ni nyingi kuliko wilaya yoyote nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hizi kata nyingine zenye ukubwa unaolingana na Tarafa, nazo zitabakia hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ombi letu la kugawa Wilaya ya Dodoma Vijijini, tungeomba tuchukuliwe kama ni *special case* kwa kutufikiria kuigawa Wilaya yetu kama tulivyoomba kwenye hotuba ya Waziri, amesema kuwa mgawanyo wa Wilaya utaangaliwa kwa mazingira ya kipekee kisiasa, kiuchumi na kijamii, tunaafikiana na msingi huo. Lakini kwa sisi Dodoma Vijijini, tunaomba ombi letu litazamwe upya na tuna imani Dodoma Vijijini mnaijua na tungeomba ombi letu hili lifikiriwe.

Mheshimiwa Spika, hoja ni nzuri na Wanachilonwa wanaiunga mkono. Tunaomba ombi letu la kugawa Wilaya, lichukuliwe kama *special case.* Ahsante sana.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Waziri wa TAMISEMI, lakini naomba marekebisho katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Vitongoji, Vijiji, Kata na Tarafa ni nyingi katika Wilaya ya Bariadi, sasa vimepitwa na wakati. Baada ya sensa ya mwaka 2002, tumeona iko haja ya kuongeza Vitongoji, Vijiji, Kata, Tarafa na hata Wilaya zingine hususan Bariadi. Wilaya ya Bariadi ina watu zaidi ya 600,000, hata majimbo ya uchaguzi ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Serikali kufuta kodi nyingi, michango mingi na ushuru mwingi wa manyanyaso kwa raia maskini. Kama Halmashauri zina ukata, basi vitafutwe vyanzo vingine toka Serikali Kuu ili zipewe hizo Halmashauri. Lakini tatizo kubwa ni ufanisi wa kukusanya kodi. Halmashauri hizi zimejaa wizi na uzembe na ubadhirifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Madiwani kuondolewa katika Kamati ya *Tender* ya Halmashauri ni kurudisha nyuma maendeleo ya Halmashauri zetu. Kamati ya *Tender* sasa ni tatizo kubwa la rushwa na ucheleweshaji wa utekelezaji. *Tender* zinachelewa kutangazwa na kutolewa hadi wafadhili wa miradi hiyo wanatishia kuondoa hela zao, mfano ni Bariadi.

Mheshimiwa Spika, fedha za wafadhili za kujenga barabara ya Nyangokolwa - Matare, shilingi milioni 32 zimekaa Bariadi kwa Watendaji hawa tangu Machi, 2004 hadi leo bado hazijatumika. *Tender Board* ilikaa wakashindwa kuelewana kwa ajili ya rushwa. Wafadhili wanataka ripoti ya utekelezaji ambayo Watendaji hawana. Mpaka sasa *Tender* bado haijatangazwa tena.

Mheshimiwa Spika, sasa *Tender Board* hizi sifutwe zote na ziundwe upya, labda kwa kushirikisha wazee maarufu hasa wastaafu. Lakini ni muhimu sana Waheshimiwa Madiwani wakawakilishwa katika *Tender Board* hiyo. Hili suala halikwepeki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, napongeza mambo mengi mazuri yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na Wiszara ya TAMISEMI. Ni ukweli usiopingika kwamba Ilani ya CCM ya mwaka 2000 inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, napenda nishauri juu ya uwezeshwaji wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa katika suala zima la kujitungia sheria ndogo za maeneo husika. Katika suala hili, Wizara imezitekeleza Halmashauri bila msaada wowote wa maelekezo juu ya sera za nchi, hali halisi ya uchumi wa nchi na masuala mengine hasa yanayohusu mikataba baina ya wawekezaji wakubwa wa kigeni ambao wanaendesha shughuli katika maeneo ya Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano mmoja hai na ambao sisi katika Halmashauri ya Kahama, tayari tumeufikisha kwa Mheshimiwa Waziri kwa maandishi kuhusu sheria yetu ndogo ya ushuru wa huduma *(service levy)* ambayo inakanyagwa na mwekezaji ajulikanaye kama *Kahama Mining Corporation Ltd.*

Mheshimiwa Spika, mwekezaji huyu amekataa kutii sheria hii na hivyo kuinyima Halmashauri yetu mapato. Suala la *service levy* licha ya kulitungia sheria ndogo, lakini pia sheria ya fedha ya mwaka 2003 tuliyoipitisha hapa Bungeni inatambua *service levy.*

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi ni pale ambapo tangu Halmashauri yetu imefikisha malalamiko yetu Serikalini, Serikali haionyeshi kujali wala kutoa maelekezo kwa ugomaji huo. Kwa mtindo huo, nadhani TAMISEMI inazitelekeza *council* zake na hivyo kuziacha yatima. Inasikitisha.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile Wizara hii inasimamia mambo muhimu ya maendeleo ya nchi, ingeongezewa Naibu Waziri mwenye upeo kama Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda na Naibu Katibu Mkuu. Kazi za Wizara hii ni pana na zinagusa kila nyanja za maendeleo na shughuli za Halmashauri toka Utawala, Maji, Afya na kadhalika. Hivyo tunahitaji nguvu zaidi za uongozi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa viwango vya kuwepo kwa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali. Lakini nchi yetu ilivyo pana na yenye matatizo ya usafiri wa uhakika, Serikali ni lazima iwe *flexible.* Kwa mfano, Tarafa ya Pande, Wilaya ya Kilwa, ni eneo lenye umbali mkubwa, barabara mbovu, lakini wapo wananchi wanaoishi kule. Hata kama hawakidhi idadi ya kuwa na hospitali, basi Kituo cha Afya cha Pande kipewe vifaa vyote muhimu vya kusaidia wagonjwa.

Aidha, vifaa bila Waganga haisaidii, hivyo, nashauri Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo maeneo ya pembezoni na hazifikiki kwa urahisi, wapate Waganga Wasaidizi wenye stashahada *(Clinical Officers).* Hivi sasa unakuta sehemu nyingine kuna *Rural*

*Medical Aids* au *Nursing Auxiliaries.* Hali hii ni hatari kwa maisha ya wananchi. Kukarabati majengo ni muhimu, lakini bila kuwa na Waganga, majengo tupu hayasaidii na tunaweka maisha ya wananchi hatarini.

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Afya na Zahanati, zipatiwe umeme wa nguvu ya jua. Umeme huu ni muhimu kwa sababu ya hasa shida za dharura za usiku na wanaoathirika zaidi ni wanawake maana kuzaa gizani, nalo ni mushkeli wa aina yake. Aidha, siku hizi zipo pia taa za gesi ambazo zingeweza kusaidia sana kwenye vituo. Kwa vile upo mpango wa kubadili mafriji ya mafuta ya taa yawe ya gesi, basi nashauri Serikali iliangalie hili la taa za gesi. Bei za taa hizi hazizidi shilingi 40,000/=. Kweli Serikali itashindwa hilo? Halmashauri zikishauriwa, nina hakika wataweza kuangalia hili na kulifanyia kazi. Zahanati nyingine hata taa za kandili hakuna.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iache umangimeza. Lipo tatizo la Watendaji kutokujua hata maeneo yao kwa vile hawatembei hasa Watendaji Wakuu walio Wizarani, hawajui jiografia ya nchi. Kama hawatembei, itawawia vigumu kuelewa matatizo halisi ya nchi na kutoa uamuzi sahihi. Hivi sasa kuna Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi ambao wanahamahama kwa sababu ya matatizo yao. Lakini Serikali badala ya kuchukua hatua, wanapewa uhamisho wa mende, wengine wamezoea kudokoa. Hata iweje, hawawezi kupanga kitu au mpango bila yeye kujinufaisha. Wapo hawa ambao wanaendesha mifuko ya michango, kinyume cha taratibu na maagizo ya Serikali. Serikali iko wapi? Chukueni hatua haraka, tusichelewe. Watanzania siku hizi wana macho na wamepevuka, wanaelewa mengi.

Mheshimiwa Spika, nashauri hatua za haraka zichukuliwe badala ya kumhamisha mtu. Hivi hakuna Watanzania wengine wenye uwezo? Serikali ina macho kama chandarua hata zaidi. Isisinzie, bali iwe macho na kuchukua hatua bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo ambayo ni kuhusu elimu kwa Madiwani, miji na vijiji kuanzishwa na mipango, Wabunge wa Viti Maalum kutokuwa wajumbe wa Kamati ya fedha na mwisho ni kuhusu *Vote 1001 (6213) Rehabilitation of DC's Office and residence,* hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia naomba kuipongeza TAMISEMI kwa semina zinazotolewa kwa Madiwani. Semina hizi zimewaelewesha sana Madiwani kuhusu majukumu yao na jinsi ya kuendesha Halmashauri zao. Naomba hivi sasa angalau tifikirie kiwango cha elimu cha Madiwani.

Mheshimiwa Spika, vijiji na miji yetu mingi inaanza kama *shanty towns.* Naomba kuwe na sheria au sera ya kutaka kuanzishwe vijiji na miji vilivyopangwa. Ikiwezekana tuwe na *agency* ya kujenga nyumba na hizo nyumba zikapangishwe ili vijiji na miji viwe na mipango mizuri na *drainage* ya kitaalam.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Mheshimiwa Sophia Simba aliuliza Bungeni, ni kwa nini Wabunge wa Viti Maalum hawawi Wajumbe wa Kamati ya Fedha? Ikumbukwe kuna sensa imesema asilimia kubwa ni wanawake. Mwanamke asipokuwa na mwakilishi wake (Mbunge) ambaye anapata habari nyingi za mipango, sera na sheria Kitaifa, Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, aliahidi kulishughulikia suala hili kwa kuleta sheria ya mabadiliko *(amendment).* Je, ni lini Wizara italeta marekebisho?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anapofafanua hoja mbalimbali, afafanue hoja ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika*, Vote 71, Sub-Vote 1001,* Kifungu Na. 6213 katika Kitabu cha Maendeleo *(Rehabilitation Of DC's Office & Residence),* naomba ufafanuzi wa nyumba ya *DC* Mafia iliyotakiwa kufanyiwa ukarabati. Mhandishi wa Wilaya alikasimu ukarabati wa nyumba hiyo utakuwa milioni 15. Pesa zikatolewa na kupelekwa mkoani. Mkoani, Mhandisi wa Mkoa alisema kuwa ukarabati huu utagharimu milioni 30. Wizara iliongeza fedha. Mkandarasi alijenga paa la nyumba hiyo kwa kuweka vigae na mbao chache, kenchi ni ile ile ya zamani shilingi milioni 30 ikaisha. Mkoa ukaomba pesa zingine. Serikali ikatoa shilingi milioni 30.8. Pesa hizi zikatumika kupaka rangi ya nyumba na vyoo vitatu. Mpaka sasa nyumba haijamalizika. Je, kwa muda takriban miezi 9 sasa, *DC* anakaa wapi? Kama ni hotelini, nani analipa?

Mheshimiwa Spika, pia naomba Waziri akafanye uchunguzi kama pesa hizo zimetumiwa vizuri. Mimi kama Mbunge nina wasiwasi na matumizi ya pesa, hayafanani na matengenezo ya nyumba. Naomba Waziri alichukulie suala hili kwa uzito mkubwa na naomba alitolee maelezo. Nisingependa kuomba Kamati ya Bunge iende kuchunguza. Naomba taarifa itolewe Bungeni na kama kuna ubadhirifu, hatua zichukuliwe kwa Mhandisi wa Mkoa aliyepandisha gharama. Nasikia pesa zingine zinatoka Zimbabwe ili kumalizia nyumba hii.

**MHE. RAMADHANI H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Wataalam na Watumishi wengine wote kwa mchango kila mmoja wao katika kukamilisha kazi nzuri sana ya kuandaa na kukamilisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie Bajeti ya Wizara hii kwa kuanzia kuipongeza juu ya Sera na Mkakati wa Maendeleo Vijijini (kifungu cha 7). Ni dhahiri kabisa kwamba mafanikio makubwa ya maendeleo yetu nchini, msingi wake ni maendeleo yatakayopatikana katika ngazi ya vijiji. Napata faraja kubwa kufahamu kuwa Wizara itajenga uwezo wa Watendaji watakaohusika katika ngazi ya kijiji na kata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kifungu Na. 9, Mfuko wa Wanawake na Vijana. Pamoja na mapungufu kadhaa yanayoukabili mfuko huu katika ngazi za Halmashauri

zetu, nafurahi kutambua kuwa Wizara imeona umuhimu wa Halmashauri zetu zitaendelea kuchangia 10% ya mapato yao, ikiwa ni pamoja na kutumia sehemu inayotolewa na Serikali Kuu kama fidia ya mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya ofisi na nyumba za wakuu wa Wilaya (Kifungu Na. 12), naipongeza sana Wizara kwa zoezi la kufanya tathmini ya hali ya ofisi na nyumba za wakuu wa Wilaya nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hili napenda kuipongeza Wizara na Serikali kwa kutujengea Boma jipya Bagamoyo, naishukuru sana Serikali. Lakini naomba Mheshimiwa Waziri afahamu kuwa *DC* wa Bagamoyo, kimsingi ni kama hana nyumba kabisa ya kuishi. Kutokana na mapungufu yaliyoko Mkoani Kibaha juu ya mipango isiyoridhisha na matumizi yaliyo dhahiri mabaya, suala la ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, lipewe umuhimu wa kipekee na upendeleo maalum kabisa.

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya, mbaya, mbaya kupita kiasi. Hali haielezeki. Labda niombe tu Ofisi ya Mheshimiwa Waziri itafute uwezekano wa kufika Bagamoyo ili iweze kujionea yenyewe hali mbaya sana ninayojaribu kuieleza hapa. Mheshimiwa Waziri, kwa unyenyekevu mkubwa naweka ombi hili mbele yako na ninaamini kuwa kwa moyo wa huruma, utalikubali kwanza kabisa kuja kujionea wewe mwenyewe au msaidizi wako na la pili, ni kulifanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu demokrasia na Utawala Bora ngazi ya Kijiji (Kifungu Na. 22), naipongeza sana Wizara kwa kutambua na kuliweka bayana wazo au fikra za msingi kwamba ngazi ya kijiji ndiyo kitovu cha ujenzi wa utawala bora na demokrasia shirikishi, ni kweli na ni kweli kabisa. Nasubiri kwa matumaini makubwa namna tutakavyoitumia taarifa inayoitwa *Village Democracy Initiatives.* Ni vema tuhakikishe taarifa hii inaeleweka vizuri sana na wanavijiji wote na tuweke mikakati mahsusi ya utekelezaji mzuri na wa ufanisi mkubwa wa taarifa hii. Kipengele hiki cha demokrasia na utawala bora ngazi ya Kijiji, kinathibitishwa kwa vitendo kwa zoezi la Uchaguzi wa Viongozi katika ngazi ya Vitongoji na Vijiji (Kifungu 23/24).

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hesabu za Halmashauri (Kifungu 30), bado tatizo hili ni kubwa. Wakati tunao wajibu mkubwa sana wa kuzipongeza sana Halmashauri zetu chache zilizopata hati safi, tusiishie kaika kuzihimiza Halmashauri zile zenye mazoea ya kupata hati chafu, bali wakati umepita wa kuhimiza. Tunachohitaji sasa ni zaidi ya kuhimiza. Ni vizuri Wizara ione uwezekano wa kuwachukulia hatua kali zaidi Maafisa Wahasibu wote wanaoshindwa kufikia viwango vya ufanisi kazini. Hesabu za Halmashauri zetu zinaonyesha picha isiyopendeza kabisa ya ubadhirifu, ufujaji na hata wizi wa fedha za umma na kwa maana hiyo Halmashauri ndizo zinazotupa wakati mgumu katika hoja ya msingi ya kuwapatia maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, Afisa Uhasibu anayefuja na kuiba fedha za umma kwa kutumia Ofisi na wadhifa wake ni adui mkubwa wa umma. Maslahi ya umma yalindwe kwa kuwadhibiti na kuwachukulia hatua kali sana mapema sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Asasi na Miradi ya Maendeleo chini ya TAMISEMI (Kifungu 34/44), napenda kuipongeza Wizara kwa mengi na mazito iliyoyafanya katika kuzisimamia na kuzisaidia kwa hali na mali asasi husika.

Mheshimiwa Spika, shukrani mahsusi na za pekee naomba kuzitoa kwa Wizara kwa namna ilivyotusaidia na inavyoendelea kusaidia katika kukifanya Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo, kiweze kusimamia juu ya miguu yake na kiweze kufanya yale muhimu sana yanayotarajiwa kutoka chuo hiki. Maandalizi ya mambomengi sana muhimu kama mitaala na *scheme* nyingi za kusimamia fedha, utumishi na kadhalika, zimekamilika. Mafao ya Mkuu wa Chuo, yaliyokuwa duni sana, yameboreshwa kwa kiwango cha kuridhisha sana.

Kwa niaba ya Bodi ya Wadhamini ya Chuo hiki, nikiwa kama Mwenyekiti wake, naipongeza sana Wizara na ni matumaini yangu makubwa sana kwamba ushirikiano na misaada mingi na mikubwa ambayo Bodi ya Wadhamini na Chuo tumekuwa tukiipata kutoka Wizarani, iendelee. Naipongeza sana Wizara kwa dhati kabisa kwa yale waliyotufanyia sisi ndani ya Bodi na Chuo pamoja na watumishi waliopo pale chuoni.

Kuhusu programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa (Vifungu 47/49), Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi - MMEM (Vifungu 50/54), Mfuko wa pamoja wa Afya (Vifungu 55/59) na Mradi wa Ukarabati wa Vituo vya Huduma za Afya (Vifungu 60/64); naipongeza sana Serikali kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri sana na taarifa nzuri kabisa za utekelezaji mzuri wa mwaka 2003.2004 na kwa mwaka ujao 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa kuzisaidia Serikali ya Mitaa (Vifungu 65/69), naishukuru na kuipongeza kwa dhati Wizara yetu na nchi zote wahisani pamoja na vyombo vya fedha vya Kimataifa kwa namna vinavyojihusisha na suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Barabara (Vifungu 72/74), naishukuru Wizara kwa jinsi ilivyotusaidia Bagamoyo katika sakata la Bagamoyo kufungiwa mfuko huu kutokana na matumizi mabaya. Mfuko umefunguliwa, matengenezo ya barabara zetu zilizokuwa zimeharibika vibaya sana, sasa zimeanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itusaidie katika kuhimiza kutolewa fedha za mfuko huo ili kasi ya matengenezo ya barabara zetu iendelee vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maoni yangu pamoja na maombi. Nashukuru sana kwa maendeleo ya ujenzi wa barabara katika Jimbo langu la Kalenga kutokana na fedha zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2003/2004. Pamoja na hayo, nilikwisha zungumza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, juu ya maeneo *critical* ambayo ni muhimu tushughulikie kutengeneza barabara:-

(a) Eneo la kwanza ni barabara ya Kiwere, Mfyomi, Itagutwa mpaka barabara kuu ya Iringa - Dodoma. Eneo hili linalima sana Tumbaku.

(b) Eneo la pili ni barabara na Vidaraja kuunganisha Vijiji vya Kibena, Mfukulembe, Udumuka, Ilandutwa na Mgama. Eneo hili lina *potential* kubwa ya uwekezaji katika kilimo.

(c) Eneo la tatu ni barabara kutoka Makongati kupanda mlima mkali na kufikia tambarale zuri la Igangidung'u na Kihanga. Haya ni maeneo muhimu ya kilimo.

(d) Eneo la nne ni barabara kutoka Magunga mpaka Makombe. Kijiji hiki cha Makombe kiko mbali sana kutoka vijiji vingine. Eneo lote ni eneo lenye *potential* ya uwekezaji katika kilimo.

(e) Eneo la tano ni barabara kutoka Wasa mpaka Ikungwe. Kijiji cha Ikungwe kimetengwa na eneo lenye maji. Panahitajika tuta kubwa ili kuhakikisha kuwa barabara hiyo inakuwa ya kudumu.

(f) Eneo la sita ni barabara kutoka Wasa, Ihomasa mpaka Usangu Wilaya ya Mbarali. Tukiunganisha barabara hii, itawezekana wananchi wa Mbarali kuwa na *alternative* ya pili kufika Iringa kupitia Wasa, Kiponzelo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la afya, kuna vituo vitatu vya Afya vimejengwa toka mwaka 2001, lakini mpaka leo havijamalizika. Vituo hivyo ni vya Vijiji vya Udumuka, Kibena na Ifunda. Imefika hali ambayo wananchi hawaelewi kunatokea nini. Vituo hivi visipomalizwa kwa katika mwaka huu wa fedha, itailetea matatizo CCM katika Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2005, hiyo ni Kata ya Ifunda. Naomba tatizo hili litazamwe toka Makao Makuu ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nachukura fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watalaam wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii ambayo ina upeo mkubwa katika kuharakisha maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tutakuwa na chaguzi za Serikali za Mitaa na vitongoji mwezi Novemba, 2004, nashauri Serikali ikajenga mazingira mazuri ya kuufanya uchaguzi huu kuwa wa kweli, huru na wa haki na hili ni jambo rahisi iwapo Serikali itawashirikisha kikamilifu viongozi wa vyama vya siasa katika ngazi mbalimbali, katika kila hatua ya uchaguzi, kuanzia uandikishaji wa wapigakura, kuwahakiki wapiga kura walio halali, kupiga kura, kuhesabu kura na hatua ya matangazo kwa mshindi hili likifanikiwa, basi dhahiri ni hatua nzuri katika upanuzi wa wa demokrasia.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali na Wizara husika itapuuza mapendekezo haya na kuiachia  Tume ya Uchaguzi pekee, ni dhahiri kwamba Serikali bado haijawa tayari kuzifanya chaguzi hizi kuwa za haki, huru na badala yake Serikali ndiyo itakuwa imedhamiria kusababisha fujo, ambapo hatimaye na dosari kwa nchi kama hii inayojitangazia kama ni kisiwa cha amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, utulivu utakuwepo iwapo Serikali haitaonyesha hila, ujanja na fujo katika chaguzi hizi vinginevyo ni vurugu, lawama, vyama vya siasa vitadhibiti kura zao kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali katika kuelekea chaguzi hizi vyombo vyote vya dola vikapewa taaluma zaidi namna bora ya kutoa ushirikiano kwa raia na viongozi wa vyama vya siasa bila kuonyesha dalili za kuegemea upande wa chama tawala.

Mheshimiwa Spika, chaguzi za mwezi Mei, 2004, Bariadi na Moshi, hazikuwa shwari kutokana na Serikali, vyombo vya dola kuonyesha dalili za wazi kuegemea upande wa chama tawala, hila, mbinu na vitisho vilitumika kinyume na sheria na taratibu za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba dosari hizo zilizojitokeza katika chaguzi za mwezi Mei, 2004 zitakuwa ni za mwisho na hazitarudiwa tena. Nashauri Serikali kuwapatia ulinzi viongozi wa kitaifa wa vyama vya siasa katika kipindi cha uchaguzi ili kuweza kutembea mahali mbalimbali bila hofu. Kitendo cha kupigwa Katibu Mwenezi wa *TLP,* Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ni cha kihuni na ni cha udhalilishaji hivyo ni vyema kitendo kile kikawa ni fundisho kwetu katika kuhakikisha viongozi usalama wao. Naishauri Serikali kuvitumia vyombo vya habari katika utoaji wa elimu kwa wananchi kufahamu umuhimu wa chaguzi hizi kupitia redio *Television,* magazeti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. SUMRI A. S. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa shukrani kwa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa kuunga mkono Bajeti ya Wizara hii muhimu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kutoa salaam zangu na wananchi wa Jimbo langu la Mpanda Magharibi kwa kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mpendwa na baba yetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa maumivu aliyonayo na safari ndefu ya Uswiss kikazi na kimatibabu, mola amuongezee nguvu, afya nzuri na faraja ili apone upesi. Naamini Taifa letu linamhitaji sana kwa busara na hekima zake. Vijiji vyetu vyote vinazidi kumwombea.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda kuchangia katika Bajeti hii katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ni kuhusu barabara katika eneo lote la Tarafa ya Kabungu na pia katika eneo la Tarafa ya Mwese na Tarafa ya Karema. Vijiji vingi havifikiki wakati wa masika, licha ya kuwa vijiji hivyo ni wazalishaji wakuu wa mazao ya chakula na biashara. Tunaomba Wizara hii iweze kuweka dira ya barabara kwa kila jimbo katika kila mwaka ili wanavijiji wetu waweze kupata nafuu ya tatizo hilo, ili maeneo ya wazalishaji wetu wapate nguvu ya kuendeleza kilimo. Najua kazi hii ni ya Halmashauri husika, lakini mpango wa fedha unaanzia Wizarani.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu pembejeo za kilimo. Pembejeo ni tatizo ambalo linagusa kabisa watu wetu ndani ya Halmashauri ambayo ipo chini ya Wizara hii. Binafsi nashauri kuwa suala la mbolea na mikopo kwa wakulima lisimamiwe na Halmashauri ambayo ndiyo ina watu. Masharti ya Hatimiliki ni njia ndefu na hii itasaidia watu wachache tu waliojiandaa vizuri kihatimiliki. Pamoja na hayo hata riba kwa mikopo yenyewe ni juu zaidi hivyo inakuwa vigumu kwa wakulima wa kawaida kufikia *standard* ya kilimo cha kisasa na ambacho kitaleta kipato na kuwaondolea umaskini.

Kuhusu mkopo wa trekta wa milioni 30, unapaswa kulipwa ndani ya miaka mitatu. Riba ya mkopo huo ni milioni 12 sawa na kulipa milioni nne za riba kila mwaka, sijui mkihesabu milioni 7.5 za kulipia mkopo, mtapaswa kulipa milioni 11.5 kila mwaka. Je, kwa kilimo chetu kilivyo, Mtanzania wa kawaida, mkulima anaweza kunufaika vipi na mkopo huo? Tunaomba Wizara ifikirie jinsi ya kuwalinda watu wake ambao wengi wakiwa wakulima kutoka Halmashauri zetu ili waweze kupata mikopo hiyo bila riba kubwa kiasi hicho. Kwani kilimo chetu kinategemea sana hali ya mvua. Zaidi ya yote fedha zinazotumiwa ni kubwa mno. Kwa kweli nia ya kumwezesha mkulima kwa hali ilivyo haipo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuhusu zahanati, kuna zahanati katika Jimbo langu katika Kata ya Mishamo sehemu iitwayo Isenga hadi sasa bado haijapatiwa Mganga. Tangu mwaka 1999 ilikuwa tayari, mwaka jana katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 ilikuwa imesajiliwa na kuwa tayari na *kit* ya dawa. Tangu hapo hadi leo bado haijaanza kufanya kazi. Tunaiomba Wizara itoe msukumo ili tuweze kuanza kupata huduma kwa kupewa mganga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wakulima tunatoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile amesikia kilio chetu juu ya malipo ya malimbikizo yao. Lakini pia naomba Wizara hii ili ione pia fedha za nauli na malipo ya wakati wa likizo ya kila mwaka ya walimu kwa likizo zao. Waweze kuandaliwa haki zao kwani ofisi ya elimu inapaswa kujua ni walimu wangapi waendao likizo na nini haki zao. Hiyo nayo ni kero kubwa sana kwa walimu.

Mheshimiwa Spika, kama hoja ilivyo juu ya Madiwani, binafsi nazidi kuunga mkono hoja za Waheshimiwa Wabunge kuwa Madiwani wetu wana kazi sana. Wafikiriwe kupewa malipo yanayostahili na pia usafiri ili kuwapa moyo kwa kazi zao ngumu.

Mheshimiwa Spika, namalizia mchango wangu kwa kuwapongeza Waziri Brigedia *General* Mstaafu, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, pamoja na wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya na juhudi zao tunazithamini na kuziunga mkono kwani zipo katika Majimbo yetu na vijiji vyetu vyote matunda yanaonekana vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kuna mengi ya kuchangia kwenye Wizara hii, naomba mchango wangu nielekeze kwenye mambo mawili. Kwanza mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa na pili, ni kuhusu Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika Mfuko wa Akiba, hotuba ya Waziri inakiri kuwa mfuko huu kutekeleza na kufanikisha majukumu yake kwa mwaka 2003/2004 majukumu ya kukusanya michango na mapato mengine, kulipa mafao kwa wanachama wakopaji na watakaojiunga na mfuko baadaye, kuwekeza kwenye vitega uchumi kadhaa pamoja na kubuni mikakati endelevu yenye nia ya kuboresha mafao na maslahi mengine ya uzeeni kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, pia mapato au maingizo ya mfuko kwa mwaka 2003/2004 yalifikia shilingi za Tanzania bilioni 23.5. Michango ya wanachama yalifikia shilingi bilioni 12.3 ikiwa ni kiwango kilichozidi makisio kwa shilingi bilioni 0.1, uwekezaji kwenye vitega uchumi hususan dhamana za Serikali na amana za taasisi za kifedha ikiwemo na *Dar es Salaam Stock of Exchange (DSE),* takwimu zinaonyesha uwekezaji kwenye jukumu hili ya takribani shilingi bilioni 27.6 chini ya matarajio kwa shilingi bilioni 1.9 kwa mwaka 2003/2004 uwekezaji umefikia shilingi bilioni 52.6. Hivyo kuhitimisha azma ya sheria Na. 6 ya mwaka 2000 kwa kuweza kukusanya mapato zaidi kwa kuwezesha na taratibu mpya ya hazina ya makato moja kwa moja kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi kwenda kwenye mfuko.

Pia kuweza kuwekeza makato kwenye vitega uchumi, kwa mfuko kuwekeza takribani kiwango cha 94% ya lengo na hatimaye kufanikisha lengo la mwisho la kuwa na mikakati bunifu ya kuboresha mafao endelevu kwa kuwezesha kutoa vitambulisho kwa wanachama kuzuia *Gost Membership* na kuelekeza uchambuzi wa kuwezesha mfuko huu wa akiba kuwa na malipo ya pensheni.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi pamoja na mapungufu kama yapo hii ni ishara nzuri kwa Wizara hii ya utawala bora hasa kama ikiliangalia kwenye jicho la kuboresha mfuko huu kwa taratibu na nidhamu thabiti ya uhasibu na fedha. La kufurahisha zaidi ni kuwa uwezekezaji wa mfuko huu kufikia shilingi bilioni 53 bilioni, ni takriban 8% ya fungu zima la makadirio ya matumizi ya fedha kwa TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2004/2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba nielekeze fikra kwenye sheria Na. 9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa (Sheria ya Fedha ya *Minimum Compulsory*

*Reserve - MCR)* ambayo inawajibisha Halmashauri kuweka 10% ya mapato yake halisi ya mwaka uliopita. Basi kwa mtizamo huu pamoja na kuchungulia yaliyofanikishwa kwenye Mfuko wa Akiba. Mwelekeo ni kuwa Wizara hivi sasa inafanya vizuri takribani kwa 80% ya malengo. Wizara hii ni kubwa na ndiyo yenye kuhudumia wengi wa wananchi wa Taifa letu. Kama mlivyotanguliza kusema hapo awali haitakosa kuwa na matatizo mengi kwa sababu ndiye Wizara pekee yenye kushughulikia sekta zote na nyanja zote ya maisha na uhai wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu nina ushauri kwa Wizara hii hususani kwenye suala la Halmashauri kukopa kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ningeomba mimi niite Mfuko huu kama *SACCOS* za/ya Halmashauri zetu. TAMISEMI ni Serikali, kukopa kwake na kuwekeza ingawa ni sawia, kunaingiliana kidogo na azma ya Serikali kutojihusisha na biashara kwani mikopo hiyo kwa Halmashauri ni kwa ajili ya miradi ya kiuchumi na siyo kwa kutoa huduma kwa jamii kama jukumu la Serikali. Kwa sababu tayari tuna akiba ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa kwa uhakika na kwa kuwa unaelekea kuwa Mfuko wa Pensheni kama vile *NSSF* na *PPF,* kwani *MCR* za Halmashauri zisielekezwe kwenye Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa na ikibidi kukopa kutoka kwenye akiba hiyo Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi za Mitaa, badala ya taasisi zingine kama vile *CRDB* pamoja na *Dictum of using other peoples money is the best approach.*

Mheshimiwa Spika, la msingi hapa ni TAMISEMI kuhakikisha uchangiaji thabiti wa *MCR* kwenye mfuko tarajiwa wa pensheni ya Serikali ya Mitaa na pensheni hii kuendeleza uwekezaji zaidi wa mapato yake ikiwezekana ili iweze kupata pato lenye *competitive advantage interest rate in the market among the financial institutions* kwa maana nyingine TAMISEMI zitaweza kuendelea kupata ruzuku toka Serikalini, kukopa kwenye soko la fedha lenye riba nafuu pamoja na kupewa gawio kutoka kwenye Mfuko wa Pensheni ya Serikali za Mitaa kwa *MCR* zitakazowekezwa na pensheni ya Serikali za Mitaa kama vitega uchumi vyake kama vile pango za nyumba zijengwe kwenye Wilaya, dhamana Serikali Kuu na amana kwenye mabenki mengine. Vile vile kama zifanyavyo *NSSF* na *PPF.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja bila kipingamizi.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri wa TAMISEMI. Zaidi ya kuunga mkono hoja ya Waziri napenda kuchangia yafuatayo:-

(i) Mfuko wa Barabara, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga na Halmashauri ya Songe/Namtumbo tunashirikiana kutoboa barabara ya Wilaya ambayo ni kuunganisha barabara mbili za Mikoa miwili yaani barabara ya Mkoa wa Morogoro ya Lupilo hadi Kilosa kwa Mpepo na ile barabara ya Mkoa wa Ruvuma ya Songea hadi Kijiji cha Kitanda, kati ya Kitanda na Kilosa kwa Mpepo ni kilometa 20. Halmashauri hizi mbili hukutana kila baada ya miezi miwili. Kikao kijacho kitakuwa *CBE Campus* ya Dodoma tarehe 10 Julai, 2004. Huko nyuma Afisa mmoja wa TAMISEMI Wizarani amehudhuria

mkutano mmoja. Tunaomba aruhusiwe kuhudhuria kikao cha tarehe 10 Julai, 2004 saa 8 alasiri.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho viongozi wa *Selous Game Reserve* nilihudhuria na kuahidi kung'oa visiki na kuweka mambo mle ambapo barabara itapita yapo madaraja makubwa kama matatu hivi Mto Londo Ruvuma mpakani na Mto Mwatisi na Mto Urua Ulanga Wilayani Morogoro. Fedha za toka Mfuko wa Barabara za TAMISEMI tutazihitaji katika harakati ya kutoboa barabara hii. Aidha, utaalam pia unahitajika kikaoni. Tafadhari TAMIESEMI ichangie 2004 /2005. Barabara hii ina faida kubwa sana zifuatazo:-

(a) Inafupisha urefu wa barabara kati ya Songea - Kitanda - Kilosa kwa Mpepo - Ifikara hadi Mikumi kuelekea Dar es Saalam.

(b) Inarahisisha watalii kuvuka *Selous Game Reserve* wakitokea *Mikumi National Park* bila ulazima wa kuanza kupitia Njombe na Iringa.

(c) Inapitia sehemu yenye rutuba kubwa baina ya Kitanda ukielekea Kilosa kwa Mpepo. Hivyo ifafufua kilimo eneo hili.

(d) Inarahisisha wasafiri kufika Namtumbo kupitia Kitanda badala ya kupitia kwanza Songea Mjini.

Mhehsimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya Wakurugenzi wa Wilaya, napendekeza Chuo cha Hombolo kiendeshe kozi za *orientation* na *refresher courses* kwa *DEDs* angalau wajue wajibu wao wa Ukurugenzi. Wengi wao huwajui jinsi ya kutekeleza wajibu wao maana hawajawahi kufunzwa *formally* chuoni. *Local Government Reform* peke yake haitoshi. Kwanza wewe na *rudiments* za Menejimenti ya *councils.*

Tarafa, Kata ni kubwa Wilayani Namtumbo. Tarafa ya Undendeule ni kubwa mno. Ivunjwe na iwe na kata zifuatazo, Luegu, Mchomono na Namtumbo. Neno Undendeule lisitumike maana ni jina la Kikabila. Litafutiwe jina jngine mfano Tarafa ya Luegu. Kata Namabengo, Hanga na Kitanda ziwe na Tarafa yake. Iitwe Lumcha au Njuga , Kata na Tarafa zingine zibaki zilivyo zisivunjwe.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii kwa hotuba yao nzuri na kwa kutekeleza majukumu yao waliokabidhiwa na umma wa Tanzania. Hata hivyo naomba kuchangia katika hatua hii kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza utazamwe uwezekano wa kuboresha maslahi na marupurupu ya Waheshimiwa Madiwani ya kila mwezi au malipo ya Madiwani wanapomaliza kipindi chao cha uwakilishi. Wizara ya TAMISEMI au Serikali kwa ujumla iweke kitengo maalum cha kugharamia kuliko ilivyo hivi sasa Madiwani wanategemewa kulipwa na Halmashauri zao ambazo zinategemea Serikali Kuu kuendesha shughuli za Halmashauri hizo.

Pia yapo madeni sugu ya Halmashauri za Wilaya yanayotokana na malimbikizo ya *statutory deductions Resources* kwa mfano, makato ya wafanyakazi kwa ajili ya *pensions. LAPF* na kadhalika kwa kuwa madeni hayo hayalipiki na Halmashauri hizo. Je, Serikali haiwezi kusaidia kulipia madeni hayo ya Halmashauri za Wilaya kama ilivyofanya kwa madeni ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsisha.

Pia usajili wa vijiji na uanzishaji wa kata mpya umekuwa na vikwazo vingi, moja ya sababu za kukwamishwa kwa zoezi hili ni mtazamo wa gharama zinazoongezeka baada ya kusajiri kijiji au kata. Tunapendekeza gharama isiwe kigezo pekee cha kuruhusu au kutoruhusu vijiji na kata kuanzishwa bali matatizo ya uendeshaji, ufanisi na tija katika eneo hilo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara yako pia naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, haya mambo machache yafanyiwe kazi mapema iwezekanavyo. Wilaya ya Iramba tumeleta mapendekezo muda mrefu uliopita tukiomba Kitongoji cha Mdirika Kata ya Ilunda Tarafa ya Nduguti kisajiliwe na kupata hadhi ya kuwa kijiji kamili kwa sababu kimekidhi sifa zote za kuwa kijiji kamili, nakuomba sana wakati zoezi la kupandisha hadhi vitongoji kuwa vijiji Mdirika isisahaulike. Mheshimiwa Waziri pia tulileta mapendekezo ya kuomba Kijiji cha Munung'una ambacho kipo Kata ya Nkinto kihamie Kata ya Mwangeza kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji hiki kipo mbali sana na Kata ya Nkinto na huwezi kufika Makao Makuu ya Kata bila kupitia Kata ya Mwangeza.

Pia Kijiji cha Munung'una kipo katikati ya Kata ya Mwangeza kutoka Mwangaza kwenda Ikolo ambacho ni Kijiji cha Kata ya Mwengeza ni lazima ukatishe katikati ya Kijiji cha Munung'uza ndipo ufike huko. Wananchi wa Mwunguzwa huduma zote za kijamii kama vile shule, afya, maji na kadhalika, hupata toka kata ya Mwangeza kwa hiyo, ni vyema tatizo hili likipatiwa ufumbuzi viongozi wote wa kata zote mbili wamekubaliana juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri sana utekeleze maombi ambayo Mkurugenzi Mtendaji na sisi Wabunge Mheshimiwa Leonard Shango na Mheshimiwa Mgana Msindai, tulikuomba, Mweka Hazina, Afisa Mipango na Afisa Maliasili wahamishwe kutoka Iramba kwa sababu wamekaa muda mrefu Wilaya hii kitendo ambacho kimewafanya wamebutu kwenye utendaji wao wa kazi, wamezoeana sana na wananchi na pia uaminifu wao umepungua sana hivyo kumkwaza Mkurugenzi Mtendaji aliyeteuliwa hivi karibuni kwenye utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, pia namwomba Mheshimiwa Waziri sasa afanye tathmini ya Wilaya zote hapa nchini na kuhakikisha ya kwamba walimu wanapata haki zao na

mishahara yao ipelekwe karibu na maeneo wanayofanyia kazi ili wasiwe wanakatisha masomo kufuata mishahara hivyo kuathiri vijana wetu wa shule za msingi.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Brigedia *General* Mstaafu Hassan Ngwilizi, kwa hotuba yake nzuri na yenye kutujengea matumaini.

Mimi na wanachi wa jimbo langu la Siha tunatambua kuwa Wizara hii ni muhimu kwa uhai wa nchi yetu na kwamba ndiyo tunayoitegemea kama mfunga goli kwa Wizara nyingine zote. Mpango wa MMEM ambao umesifiwa sana nchini usingelifanikiwa kiasi chote hiki kama siyo Ofisi ya Rais TAMISEMI. Naipongeza sana Wizara hii na watendaji wake wote akiwemo Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Brigedia *General* Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda. Katibu Mkuu Bwana Deotrephes Mmari na Wakurugenzi wote walio chini yao kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nimeshtushwa sana na kauli ya Serikali kuwa haikusudii kuanzisha maeneo mapya ya utawala na kwamba hali ya uchumi itakaporuhusu ndipo zoezi hilo litafanyika kwa yale maeneo ambayo kwa kugawanywa yataleta manufaa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kauli hii ni ya kutisha kwa sababu mara kwa mara wananchi wa Jimbo la Siha wameifikisha kwa viongozi wa kitaifa akiwemo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Ombi la Jimbo la Siha kuwa Wilaya na akaahidi litafanyiwa kazi na kwamba tutaarifiwa kuhusu uamuzi wa Serikali kuhusu jambo hili. Mwaka 2001 Rais alifanya ziara katika Jimbo la Siha na kukutana na Wazee mashuhuri wa jimbo hilo wakiwemo pia viongozi wa Chama Tawala na kupokea ombi hilo rasmi. Rais aliwahutubia wananchi katika uwanja wa CCM Sanya Juu na kote alikopita wananchi wa Siha waliofurika katika uwanja huo hawakuacha kumwambia Rais tunaomba Wilaya kwa kifupi katika mkutano wa Chama na wazee na wadau muhimu uliofanyika katika Ukumbi wa Kanisa Katoliki, Rais aliahidi kuwa atalifanyia kazi ombi hilo na kuwa wananchi watapewa majibu kupitia taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, muda haukupita na kweli Halmashauri ya Wilaya ya Hai ikatakiwa kutoa kumbukumbu zote muhimu hii ikiwa ni pamoja na kikao kukaa cha *full council* ambacho kwa kauli moja kiliridhia ombi la Siha kuwa Wilaya. Wazo lilipitishwa kwa kauli moja. Vikao vya *council* ni vya wazi kama Bunge na Mahakama na kwa hiyo, wananchi wa Jimbo la Siha walifurika Bomang'ombe Makao Makuu ya Wilaya ya Hai na kushuhudia ombi lao likipitishwa na Baraza la Madiwani kwa kauli moja.

Ombi hili lilipelekwa katika kamati ya ushauri ya Mkoa *(Regional Consultative Committee)* na kupata baraka zote za kikao kuwa Siha ikubaliwe kuwa Wilaya. Ombi hili lilitetwa katika ngazi ya Kitaifa likiwa na kumbukumbu zote muhimu pamoja na zile za wataalamu kutoka *centre* yaani TAMISEMI zilizoangalia mipaka ya Wilaya mpya Makao Makuu ambayo yana majengo ya kisasa na yamewahi kutumika kama Makao

Makuu ya Wilaya ya Hai kabla ya kuhamishiwa Bomang'ombe, Kituo cha Polisi Sanya Juu, Posta, Mahakama, Maduka, Huduma za maji, umeme, simu na kadhalika. Haya yote yaliwafanya wananchi wa Jimbo la Siha wajenge matumaini mapya. Inatushangaza kusikia etu Serikali haikusudii kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Inasikitisha. Nitawaambia nini wananchi wa Jimbo langu la Siha baada ya hayo yote?

Mheshimiwa Spika, suala la vigezo, mimi nakubaliana na Serikali kuwa vigezo haviwezi kuwa ni suala la wingi wa watu tu. Ni kweli kwamba suala la *population* ni miongoni mwa vigezo vya kutizamwa lakini si kigezo pekee. Nakubaliana na Serikali kuwa vigezo vingine ni vya kisiasa, kiuchumi na vya kijamii. Tukisema tutumie vigezo vya idadi ya watu basi Zanzibar isinge-*quarify* kuwa nchi na Serikali yake kwani idadi ya watu wake haifikii hata theluthi moja ya idadi ya watu wa bara. Lakini kwa kuheshimu historia ya watu wa Zanzibar na masuala ya kisiasa tunaitambua kama nchi yenye Serikali yake na Rais wake, hili tunaliheshimu sana vinginevyo Zanzibar ingemezwa na Bara.

Tatizo la Siha ni la kisiasa, kiuchumi, kijamii na la kihistoria. Eneo la Siha lina 50% ya wakazi wake ambao ni jamii ya kimasai tunapakana na Arumeru na Monduli. Kiutawala tuko Kilimanjaro, lakini ukweli ni kwamba kijamii wananchi wa jimbo hili wako upande wa pili yaani Arusha. Vijiji vya Lekrimuni, Olmelili, Ndinyika, Dimologi, Donyomorok, Kandashi, Makiwarurivya Kimasai. Tatizo siyo tuko wapi bali tatizo ni hali duni ya maisha ambayo watu wote wa Siha wanaishi. Ni duni mno. Wengi wa wananchi wa jimbo hili ni wachungaji wala siyo wafugaji. Ni watu wa kuhamahama na kwa hiyo, hata huduma muhimu kama maji, zahanati, barabara, umeme majosho, shule za msingi na sekondari ni za kutisha. Wilaya ya Hai kwa mfano ina shule za sekondari 26. Siha katika hizo shule ina sekondari 4, mbili za kanisa na mbili za Serikali ambazo zimeanzishwa juzijuzi tu. Katika hizo 26, 22 zipo Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Spika, tuna vituo vya afya karibu 6 na Jimbo la Siha, halina hata kituo kimoja cha afya. Pale ilipo Hospitali ya Kibong'oto na ya Wilaya, kilichopo pale ni kliniki wala siyo zahanati, mtiririko huu upo hivyo hivyo hata katika huduma za maji, umeme, barabara, mifereji, posta, simu na kadhalika, ukiwa na *imbalances* za namna hii katika eneo moja la Wilaya unafanyaje?

Kibaya zaidi ni eneo la Jimbo la Siha ndilo linalozalisha mazao muhimu kama ngano, kahawa, shairi, mbao, mbogamboga njegere, ndizi, mahindi, mifugo kama ng'ombe mbuzi, kondoo na kadhalika mambo ambayo yanaliingizia Taifa hili na Halmashauri kipato kikubwa lakini hakijidhihirishi kwa wananchi wa kawaida kimapato na kihuduma. Kuna utajiri wa kunukia na umaskini wa kunuka. Unafanyaje katika mazingira ya namna hii? Huna jinsi kama kweli umedhamiria kuwasaidia wananchi wa Siha ni kuwakubalia wawe na chombo chao cha utawala. Kwa kufanya hivyo utakuwa unasukuma huduma muhimu karibu zaidi na wananchi. Hili huhitaji kuelezwa sana kulielewa, ni jambo la kawaida tu kuwa mgawanyo wa raslimali za nchi utakuwa wa usawa na wa haki zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Jimbo la Siha, lilianza kuwa na mwakilishi wake, Serikali ilipokubali liwe Jimbo la Uchaguzi, vinginevyo ilikuwa ni ndoto kumpata mwakilishi wa Hai kutoka Siha. Haikuwahi kutokea tangu tupate Uhuru. Jimbo hili lilikubaliwa kwa misingi ya kisiasa kuwa Jimbo la Uchaguzi. Lakini jimbo la uchaguzi ni *microphone* tu ya kupigia kelele sio *planning unit* ambayo inagawa raslimali. *Planning unit* yetu ni Wilaya ambayo ndiyo Jimbo la Siha linaomba sababu zile zile ambazo zilifanya wananchi wa Siha kujisikia wamekuwa *marginalized* na upande wa pili ndizo hizo hizo zinazotufanya tuiombe Ofisi ya Rais, TAMISEMI ione umuhimu wa kutukubalia kuwa Wilaya.

Tatizo lingine la Siha ni la ulinzi na usalama. Jimbo la Siha limekwenda mpaka mpakani mwa Tanzania na Kenya yaani Kamwanga. Tuna kituo kidogo cha Polisi cha Olmolog na kingine Ngarenairobi ambavyo vinatusaidia kupambana na ujambazi na uhalifu kwa ujumla. Lakini vituo hivi pamoja na kile cha Sanya Juu, vipo mbali mno na Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya na Ofisi ya *DC* kiasi ambacho mara nyingi wananchi wanavamiwa bila ya kupata msaada kutoka Makao Makuu ya Wilaya.

Mwaka 2002 tulivamiwa na majambazi Ngarenairobi na wananchi kwa kujihami wakachukua sheria mkononi na kuua majambazi watano. Kijiji cha Koboko kilivamiwa na majambazi na mwenye duka na mkewe walipigwa risasi bahati nzuri hawakufa, lakini ni kielelezo tosha kuwa hali ya ulinzi Siha bado ipo mashakani. Matukio ya wizi wa mifugo yametawala maeneo yote ya wafugaji na wachungaji na yale ya wakulima. Mifugo inavushwa kwenda nchi jirani na watu kutoka nje wanavuka mipaka na kuingia nchini na hivyo kuifanya hali ya amani na utulivu kutoweka. Jimbo la Siha linaamini kuwa sababu ya ulinzi na usalama ingeliweza kabisa kuwa miongoni mwa vigezo muhimu vya kutubulia kuwa Wilaya.

Mwisho, maendeleo ni *function* ya *land capital labour* na sasa *management.* Mambo haya yote yapo katika Jimbo la Siha. Siyo hivyo tu maendeleo siku zote ni kitu kinachohitaji msukumo na madai kutoka kwa watu wenyewe. Ni *demand driven* kama kweli wananchi wa Siha wanaamini kuwa wanaweza kuchukua changamoto hiyo na kujihudumia wenyewe litakuwa si jambo jema kuwakatalia ombi lao. Vinginevyo tutawakatisha tamaa. Si hivyo tu, kama nilivyoeleza juu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikwisha ahidi kulifanyia kazi ombi hili na kwa kweli kutowakubalia ombi lao kutapunguza imani kubwa walioyo nayo kwake jambo ambalo naamini halileti afya njema kwetu kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba nihudhurishe tena kwenye kikao hiki cha Bajeti na kwa kweli nikumbushie tena ombi la wananchi wa Jimbo la Siha kuomba kuwa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, anastahili sifa pamoja na Naibu Waziri wake.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni ulifanya mkutano wa viongozi wa vyama vyote vya siasa pamoja na CCM, sisi tulitia tamaa kubwa kwamba CCM imeanza kujirekebisha kikao kilifanyika mambo mengi yalikubaliwa kwa pamoja baina ya vyama vyote, baada ya makubaliano hayo viongozi wote walitia saini. Makubaliano hayo ni ya kufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuwa wa haki na kuaminiana.

Leo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mazungumzo hayo yalikuwa ni kutafuta mawazo ya wadau tu hayakuwa ya uamuzi. Maelezo hayo hayana kheri, ni maelezo yanayotayarisha vurugu katika uchaguzi. Makubaliano ambayo yalifanywa na vyama vyote pamoja na CCM yamekuwa hayafai kwa sababu hayataleta maslahi kwa CCM, kwa hiyo, CCM ikajifungia peke yake na kuyavunja makubaliano na wenzake ikisema kwamba Serikali ndiyo iliyovunja makubaliano wakati Serikali yenyewe yote ni ya CCM na Waziri ambaye anashughulikia chaguzi hizi ni Naibu Katibu Mkuu wake.

Mheshimiwa Spika, mawazo yangu ni kwamba amani katika nchi hii itoweke na amani katika nchi yetu itapotea kwa chaguzi na kumbe ndiyo maana mkaongeza fedha katika ulinzi ili mnunue silaha za kutosha za kuua raia. Ni hatari ilioje kutayarisha mazingira ya fujo, amani ya Tanzania ni ya bandia hivyo naomba isichezewa, ni kuchezea shilingi chooni.

Mheshimiwa Spika, kama vile ambavyo haiwezekani kuwa na Rais kutoka nje ya nchi yetu ni lazima awe raia mzaliwa ndiyo akubalike kuwa Rais, basi kwa mantiki hiyo hiyo ingefaa Mkuu wa Mkoa awe mzaliwa katika Mkoa wake. Rais akichagua Mkuu wa Mkoa kutoka ndani ya Mkoa basi utaratibu huo utaondoa malalamiko mengi, kila mmoja atasimamia maendeleo ya Mkoa wake kwa hali na mali, akifanya vibaya atawafanyia watu na jamaa zake mwenyewe, akifanya vizuri atanyanyua maendeleo ya Mkoa wake.

Mheshimiwa Waziri, utaratibu huu una manufaa kwa sababu mtu hufanya lake vizuri zaidi kuliko la mwenzake, Mkuu wa Mkoa akiiba ataleta kwao, akipata msaada atavutia kwao na utaratibu huu napendekeza iwe kwa Wakuu wa Mikoa tu, Wilaya na ngazi nyingine ziendelee zilivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jitihada yake ya kuondoa kero kwa walimu, walimu ni mtaji muhimu kwa Taifa, ndiyo wanaowatayarisha Watanzania wa kesho wasiwe wajinga kama msemo wa wahenga unasemao ukimuudhi mchinja mbuzi utakosa mchuzi. Naomba sana walimu wapewe malimbikizo yao, posho zao na wapewe mishahara kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza Wizara hii ipewe Manaibu Waziri wawili, mmoja ashughulikie Tawala za Mikoa na mwingine ashughulikie Serikali za Mitaa hapo ndipo ufanisi utapatikana kwa sababu Wizara hii ni kubwa mno, ina majukumu mazito karibu ya nchi nzima.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchangia sakata la Hospitali ya Temeke. Naipongeza Serikali kupitia TAMISEMI kwa hatua yake ya kuunda Tume ya kuchunguza utendaji kazi katika Hospitali ya Temeke

kufuatia uzembe uliopelekea mama mjamzito kuzalia chooni na hatimaye kupoteza maisha yake na ya mtoto. Tunaomba taarifa ya uchunguzi wake ifikishwe Bungeni haraka iwezekanavyo na hatua kali zichukuliwe dhidi ya wote watakaohusika na uzembe huo na Waziri atoe tamko kali sana juu ya matukio kama hayo ili yasiweze kutokea tena si katika Hospitali ya Temeke tu, bali katika hospitali zetu zote hapa.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara hii ya TAMISEMI ndio inayosimamia uchaguzi wa vitongoji na Serikali za Mitaa ambao unatarajiwa kufanyika baadae mwaka huu, ni vyema ikahakikisha kwamba uchaguzi huo unafanyika kwa kuzingatia sheria, haki na uadilifu wa hali ya juu ili tuweze kupata viongozi halali ambao wamechaguliwa na wananchi wenyewe. Namna yoyote ile ya kutumia dola, vitisho, manyanyaso na mabavu katika kukipatia chama fulani ushindi inaweza kuhatarisha amani na utulivu uliopo. Hivyo mnaohusika tunaomba muwe waangalifu sana.

Tatu, ajira kwa watendaji wa vijiji, kata na kadhalika, kwa kuwa tumo katika mfumo wa vyama vingi ni vyema uajiri nao ukashirikisha wananchi wa vyama vyote na hata wale wasiokuwa na vyama. Kwa ufupi ajira kwa watendaji zigaiwe kwa wananchi wote na kwa jinsia zote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Nne, Ofisi za Wabunge, Zanzibar. Tunaishauri Serikali kupitia TAMISEMI kuandaa utaratibu maalum ili kuhakikisha kuwa Ofisi za Wabunge zinajengwa chini ya usimamizi wa TAMISEMI ili kuondoa ucheleweshwaji ambao unaweza kusababishwa kwa shughuli hii kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Kiongozi kama ambavyo tuliambiwa hapo mwanzo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyotumia nafasi yake kama mtawala na kiongozi wa jeshi la miamvuli kuwaagiza watendaji kuwalipa walimu madai yao ambayo tayari yalishahakikiwa mara moja na pia kuwaagiza Wakuu wa Mikoa kuunda Tume kwa ajili ya kuchunguza madai ya walimu katika Halmashauri zao na pia yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kuunda tume ya kufuatilia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki mimi binafsi kimenifurahisha sana vile vile kwa saikolojia yangu kama mwalimu niliona hata Wabunge wote walifurahishwa na kauli hiyo iliyoonyesha ujasiri ukomavu na imani kubwa aliyokuwa nayo kwa walimu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo walioshiriki kuandaa Bajeti hii. Kwa ujumla Bajeti hii ni nzuri, nawatakia utekelezaji mwema na wenye mafanikio kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu napenda nitumie nafasi hii ya awali kuiunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. Naipongeza Serikali kwa

jinsi inavyowajali wanawake na vijana kwa kutoa agizo rasmi kwa kila Halmashauri kuhakikisha inatenga asilimia 10 kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa ajili ya kukopesha vikundi vya akina mama na vijana wanaojitahidi kuondokana na umaskini. Cha kusikitisha ni kwamba Halmashauri nyingi zimeshindwa kutekeleza agizo hili kwa kiasi kikubwa.

Kwa kuwa Serikali sasa hivi inatoa ruzuku kwa kila Halmashauri naishauri ianze kukata madeni hayo kwenye ruzuku zao moja kwa moja hazina ili akina mama na vijana waweze kupata haki zao za msingi, vile vile Wakurugenzi walioshindwa kwa makusudi kufanya hivyo wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iyatazame upya maslahi ya Madiwani kwani posho wanazopata kila mwezi hazitoshi kabisa kwa madai ya Halmashauri nyingi kuwa hazina pesa naomba malipo haya sasa yatolewe na Serikali ikiwa ni pamoja na kuboresha malipo ya kiinua mgongo cha Madiwani hao.

Naomba niikumbushe Serikali kutoa mafunzo kwa ajili ya Wakurugenzi ya utunzaji wa fedha na kutoa michanganuo ya miradi mbalimbali kwani wengi wao wanashindwa kufanya hivyo. Wengi wao wanashindwa kufanya hivyo. Ukizingatia wengi wao hawajatoka kwenye fani ya uhasibu. Kumbukumbu zangu zinanipa kwamba mafunzo ya mwisho kwa Wakurugenzi yalikuwa mwaka 1977 kwa hiyo, ni wazi watakuwa wamepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda niikumbushe Serikali kuwa kuna tofauti kubwa ya mishahara, marupurupu na kiiunua mgongo cha watumishi wa Serikali za Mitaa ukilinganisha na watumishi wa Serikali Kuu. Wakati kazi kubwa iko kwenye Halmashauri zetu waliko wananchi wengi. Naiomba Serikali izitazame upya sekretarieti za Mikoa ili ziwe na watumishi wenye sifa na uwezo wa kuzishauri Halmashauri zetu kwani maeneo mengine unakuta watumishi wa Halmashauri wanakuwa na uwezo mkubwa kuliko Mkuu wa Idara aliyeko Mkoani ambaye ndiyo mshauri wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na Madiwani Viti Maalum ili kuongeza uwakilishi wa wanawake katika Serikali zetu za mitaa, naiomba Serikali iondoe vikwazo vinavyowanyima haki Madiwani wa Viti Maalumu kugombea au kushika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya Halmashauri zao mfano kuwa Mwenyekiti wa Kamati, kuingia kwenye Kamati ya Maadili na Usalama ya Halmashauri, Kamati za kudhibiti ukimwi za Halmashauri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba tena Serikali iwakumbuke Wenyeviti wa Kata, vijiji na Mitaa kwa kuwapa posho, kwani wanasaidia sana Serikali hii, katika kusimamia, shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Napenda nitoe angalizo katika madai ya walimu ambayo hayajahakikiwa, inasemekana wapo Watendaji wa Halmashauri ambao wana roho mbaya ama chuki binafsi wamediriki kunyofoa risiti ambazo walimu huambatanisha kwenye barua zao za madai kama ushahidi.

Mheshimiwa Spika, naomba walimu wasisumbuliwe, walipwe madai yao kwa kutumia barua zilizomo kwenye mafaili yao la sivyo watasababisha udanganyifu na utapeli usiokuwa na sababu.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia tena naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi za dhati za wananchi wa Jimbo la Rorya, Wilaya ya Tarime Mkoa wa Mara kwako Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na wafanayakzi, wote wa Wizara hii.

Wizara ya TAMISEMI chini ya uongozi wako ukishirikiana na wafanyakazi wa Wizara na viongozi wa Mikoa na Wilaya imeweza kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2000 iliyotolewa na CCM kwa uadilifu ufanisi na ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Rorya, napenda kufikisha maombi maalum ya upendeleo kwako. Kwa miaka 20 wananchi wa Jimbo la Rorya wameteseka kuhusu miundombinu barabara. Barabara ya Mirare - Ryagoro - Rodi ni barabara inayounganisha kata saba za tarafa ya Girango. Tarafa ya Girango na Tarafa ya Ngaucho. Barabara hii sasa imejifunga kutokana na mvua kubwa zilizonyesha niliwahi kuleta ombi maalum kwako mwaka 2002/2003. Barabara hii isifanyiwe ukarabati itakuwa kero kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Rorya- Ryagoro - Rodi ni barabara inayounganisha kata saba za tarafa ya Girango. Tarafa ya Girango na Tarafa ya Ngaucho. Barabara hii sasa imejifunga kutokana na mvua kubwa zilizonyesha niliwahi kuleta ombi maalum kwako mwaka 2002/2003. Barabara hii isifanyiwe ukarabati itakuwa kero kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Rorya.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, ilihakikisha kwa barua iliyoletwa ofisini kwako kuhusu umuhimu wa barabara hii kutengewa fungu la kutosha kutoka mgawanyo wa fedha za *Road Toll,* Mheshimiwa Waziri nakuomba sana tena sana uniokoe hali ni mbaya.

Pili, barabara kutoka Kuruya hadi Kibuyi haipitiki, barabara hii pia inahitaji matengenezo ya dharura kwa kuwa ni kiungo muhimu kati ya barabara kuu kutoka Musoma hadi Nairobi. Kijiji cha Kibuyu ni maarufu kwa uvuvi wa samaki katika Ziwa Victoria. Wavuvi wengi wanalazimika kutumia mitumbwi isiyo salama na mara nyingi wavuvi wamepoteza maisha yao kutokana na dhoruba kubwa ziwani. Kutengenezwa kwa wananchi wa Kibuyi. Maombi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ililetwa Wizarani kuelezea umuhimu wa barabara hii. Naomba uniokoe naomba sana sana.

Tatu, barabara kutoka Randa Kirogo - Busanga imejifunga kwa miaka 30. Matengenezo ya barabara hii ilianza tangu mwaka 2002 na hadi sasa matengenezo yamefikia asilimia 40. Kukamilika kwa barabara hii itakuwa ukombozi wa wananchi wa Kata ya Kigunga na Kirogo ambao wengi wao ni wavuvi wa samaki katika ziwa Victoria. Nakuomba sana sana uniokoe. Hali ni ya kutisha. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilileta maelezo ofisini na mimi nilileta kwako ombi kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakutakia mafanikio mema.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitoe salaam za rambirambi kwa kifo cha ghafla cha Mheshimiwa Yete Mwaligo, Mbunge wa Mbeya Vijijini. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu uongozi katika ngazi za vijiji hadi Wilaya, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata na Makatibu Tarafa ni wahusika wakuu katika kuongoza shughuli za maendeleo katika ngazi za vijiji *grassroot level.* Pale ambapo wahusika hawa hawana ushirikiano mzuri na wananchi wanaowaongoza na pia viongozi wa Wilaya, shughuli za maendeleo ya wananchi hudorora na pia huzuka migogoro mingi hususan ya ardhi na mashamba. Matokeo yake ni kwamba badala ya wananchi kufanya kazi zao za kilimo kwa amani na utulivu, wanabaki kuandamana kwenda Mahakamani. Mfano mmojawapo katika jimbo langu ni Kata ya Ufana ambapo kuna migogoro mingi ya mashamba na ardhi ambapo pia kuna uonevu mkubwa. Je, Serikali itakubali kufuatilia suala la migogoro ya mashamba ardhi na suala zima la uwajibikaji katika Kata ya Ufana na Wilaya ya Babati kwa jumla ili wananchi waone kuwa Serikali yao inawasikiliza na kuwajali.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni barabara katika Halmashauri nyingi. tunalo tatizo la *capacity* kuwa ndogo katika idara ya ujenzi. Kwa hiyo, miradi mingi ya maendeleo kukwama ama kwa kutoandaliwa vizuri au uchache wa *staff.* Jimboni kwangu tumekwama kwa ujenzi wa daraja la Mto Bubu. Je, Wizara ya TAMISEMI itatusaidiaje katika mradi wetu huu ambao pia ni ahadi kutokana na swali nililowahi kuliuliza humu Bungeni?

**MHE. ADELASTELA MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wabunge, kutuatia jedwali linaloonyesha fedha zilizotumwa Mikoani kwa kazi za ukarabati Ofisi za Wabunge, mambo mawili nimeyaona ambayo hayakunifurahisha.

Kwanza, inakuwaje Majimbo mengine hawakuonyesha fedha zilizotolewa ni ngapi? Mfano ni Mkoa wa Tanga, isipokuwa Jimbo la Mkinga na Muheza Wilaya nyingine hazikuonyesha wamepata fedha kiasi gani ili kuhudumia Ofisi za Waheshimiwa Wabunge walio kwenye Majimbo hayo. Pamoja na kwamba wameonyesha mpango wa utekelezaji au ukarabati vipi tutaelewa kama kuna ubadhirifu wakati hela iliyotolewa haijulikani? Mgao wa fedha hizi kwa mwaka 2001/2002 yapo Majimbo yamepata 2002/2003, yapo majimbo yamepata 2003/2004 mbona sioni hata jimbo moja kupokea fedha hizo.

Kwa miaka miwili ya mwanzo ina maana kuna baadhi ya majimbo hayajapata hadi sasa? Nashauri taarifa hizi zitayarishwe kufuata vigezo vinavyofanana ili hata anayesoma aelewe wapi kumepungua nini, mfano yapo majimbo hakuonyesha uwepo wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum. Ina maana majimbo hayo hayapati mgawo wa Ofisi za Wabunge Viti Maalum wakati Wabunge hao wapo?

Jambo la pili ni mgao wa fedha kutolingana kwa ofisi zote. Mfano Mtera katika mwaka 2002/2003 imepata shilingi 3,000,000/= kiasi cha kuwezesha Mbunge wa Jimbo hili kuwa na *rotating hydrolic high back chair* na vifaa vingine vilivyoelezewa. Mwaka nadhani (maua haikuonyeshwa) huo huo Mbarali wamepewa shilingi 209,500/= kwa nini hali hii iwepo? Mimi sielewi hasa inakuwaje viwango kutofautiana kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, taarifa za fedha hizi haziridhishi kwa mfano taarifa ya Kibaha, Kisarawe na Mafia kwa ujumla tunaambiwa kazi hazijafanyika lakini fedha iliyotolewa imetumika je, nini kimefanya fedha itumike kama kazi zilizokusudiwa katika Ofisi ya Mbunge hazikutumika.

Mheshimiwa Spika, mwisho karibu ofisi zote za Wabunge ziko katika majengo ya Serikali mfano jengo la Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, majengo ya Halmashauri na kadhalika ili kuipunguzia Halmashauri husika gharama. Nasikitika Halmashauri ya Manspaa ya Tanga kubeba gharama ya Ofisi ya Mbunge wa Jimbo huko jengo la Bandari. Haiwezekani kwamba majengo yote yaliyopo tangu amekosa sehemu iliyo na gharama nafuu, ameamua kuchukua ofisi jengo linalomilikiwa na Mamlaka ya Bandari kwa nini gharama zisiwe zake? Kwa nini Manispaa kubeba mzigo huu?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi. Ahsante.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi kuchangia hotuba hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Nampongeza mtoa hoja Mheshimiwa Brigedia *General* Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa TAMISEMI, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Deotrephes Mmari. Nachukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Rais Benjami William Mkapa kwa maumivi aliyonayo na Mwenyezi Mungu ampe ahueni *inshallah* ili arudi kuendelea na shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nichangie kuhusu mikopo ya wafanyakazi wa Halmashauri, nia ya Serikali ambayo ni nzuri ya kuwapatia fursa wafanyakazi kukopa katika vyombo mbalimbali kulingana na viwango vyao vya mishahara vyombo kama *NMB.* Naipongeza sana lakini Mheshimwia Waziri naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kuna tatizo ambalo linajitokeza kwa wafanyakazi ambao mishahara yao hupitia Halmashauri za Wilaya wanapata taabu sana hadi kufikia sifa ya kupewa mikopo mfano toka *NMB* sababu zinazotolewa ambazo zinakera ni eti bado Halmashauri inafanya *reconcilliation* ya mahesabu yao toka TAMISEMI na hazina. Suala la kutokuwa na *report* safi kimahesabu si kosa la wafanyakazi wala hawahusiki, ni

watendaji. Hili linashangaza kwani inachukua muda mrefu na hasa urasimu wa kiutedaji ili kuwakwamisha ambapo kimsingi ni haki ya mfanyakazi kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 niliuliza swali Bungeni kuhusu mikopo holela inayowakopesha wafanyakazi. Nilitoa mfano wa Wilaya ya Handeni ambapo watu binafsi wanakopesha watumishi hasa wa elimu na afya na kuwatoza riba kubwa ya asilimia 50. Majina niliyataja, swali linakuja iweje wakopeshaji binafsi wanapatiwa fursa ya kuwapokesha wafanyakazi tena wengine ni watendaji wa Halmashauri kwa riba kubwa isiyolipika kwa urahisi na wanaruhusiwa na uongozi wa kurugenzi chini ya *DED* lakini mikopo ya *NMB* yenye riba ndogo na marejesho ya muda mrefu inashindikana kwa kisingizio cha mahesabu.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo idara nyingine ambazo mishahara yao haipitii Halmashauri kama mahakama, polisi, wameweza kupata mikopo. Je, Mheshimiwa Waziri huoni hapa kuna mizengwe? Tafadhali tunakuomba ulifuatilie suala hili kwani mikopo si tu inasaidia ni wafanyakazi hasa wa afya na elimu, ukombozi mkubwa ukizingatia wanaishi katika mazingira magumu na itapunguza malalamiko katika Wizara ya TAMISEMI. Nashauri pia endapo wataonekana watendaji hawa wanafanya hivi kwa makusudi ya kupotosha utawala bora basi wachukuliwe hatua ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za watendaji wa kata, naipongeza Serikali kwa kutoa kauli ya kuendelea na ajira kwa watendaji wa kata na kwamba wale waliokuwa wameshaajiriwa wasiondolewe na wamepewa muda wa miaka mitatu kujiendeleza. Hali halisi ya elimu kwa watendaji wengi ni elimu ya msingi. Sasa miaka mitatu wajiendeleze kufikia kiwango gani? Nani ataratibu jinsi ya kujiendeleza ukizingatia hali halisi ya sehemu wanazoishi na gharama. Waziri labda mimi sijalifahamu uzuri ni vema likaangaliwa na kutolewa maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu za posho za Madiwani, umuhimu wa Madiwani katika maendeleo ya wananchi Kiserikali na hata katika vyama vyao ni mkubwa sana. Wanajituma kwa hali na mali bila malipo kwa posho ndogo shilingi 30,000 na Halmashauri nyingine kiwango ni kidogo zaidi kulingana na mapato ya Halmashauri. Nauli wakienda vikaoni, posho wanakopwa na Halmashauri zao na madeni yanajilimbikiza mpaka inafikia Diwani anamaliza muda wake hajalipwa. Tunaomba posho iongezwe na Halmashauri zikemewe tabia ya kuwakopa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kujitahidi kutoa huduma bora kwa wananchi katika Halmashauri. Moja ya utawala bora ni pamoja na kuwa na watendaji walio makini na waadilifu. Matatizo mengi yanayojitokeza katika Halmashauri nyingi ni kukaa katika kituo kimoja watendaji bila kuhamishiwa hivyo kuzoeleka sana baina ya watumishi wanaofanya nao kazi na kuzifanya Halmashauri kama mali yao hivyo kuwapa kiburi. Haiwezekani kiongozi au mtumishi kukaa miaka 20 kituo kimoja. Ni lazima misingi ya utawala bora hayatakuwepo. Hivyo Mheshimiwa Waziri kwa vile malalamiko mengi yanakufikia ni vema basi swali hili ukalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za afya Kilindi, Mheshimiwa Waziri ni lini sasa Wilaya mpya ya Kilindi itakuwa na hospitali? Kumbukumbu zangu kabla ya Kilindi kuwa Wilaya kabla ya mwaka 2000 tuliomba ya Kituo cha Afya Songe kiwe hosptali. Hatimaye Kilindi imekuwa Wilaya na Kituo cha Afya Songe ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya bado kinaendelea kutoa huduma za Wilaya katika hali ngumu. Umbali wa kutoka Kilindi hadi hospitali ya Wilaya Handeni ni zaidi ya kilometa 150, barabara mbovu sana na hakuna magari matokeo vifo vingi hasa kwa akinamama wajawazito wanaopata *complications.*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini Kilindi tutaweza kupata hospitali au japo kupandisha hadhi ya *Health Centre* iweze kufanya *operation?* Ahsante  na nawatakia kila kheri.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Brigedia Jenerali Mstaafu, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza pia Naibu Waziri, ndugu yangu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa kazi yake nzuri anayoifanya ya kumsaidia Waziri kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kule Temeke tunalo tatizo katika Hospitali ya Manispaa ya Temeke. Tatizo hili limekuwa kubwa mpaka hivi sasa hatujalipatia ufumbuzi wake. Yapo malalamiko ya muda mrefu kuhusu rushwa kwamba wagonjwa hawatibiwi bila kuombwa chochote na hasa wodi ya wazazi nadhani Mheshimiwa Waziri, atakuwa amesikia malalamiko mbalimbali kutoka kwa wakazi wa Temeke.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Hassan Ngwilizi, kwa jitihada zake ameunda tume ili ichunguze tuhuma mbalimbali kwenye Hospitali hiyo. Sisi Manispaa pia tumeunda tume ya Madiwani ili wachunguze tuhuma zinazolalamikiwa ili tuzitafutie ufumbuzi.

Lakini tatizo kubwa ni uchache wa vyumba vya kulaza wagonjwa (wodi) hasa *Maternity Ward.* Hili ni tatizo la muda mrefu kwani hospitali hiyo ni ya muda mrefu wakati huo watu si wengi kwa kiasi hicho leo hii Wilaya ya Temeke ni ya pili kwa kuwa na watu wengi kufuatia taarifa ya sensa ya mwaka 2003. Pamoja na kwamba wakati wowote ujenzi wa ukarabati wa jengo la utawala utaanza, hivyo namuomba sana Mheshimiwa Waziri Hassan Ngwilizi, pamoja na kuunda tume basi aliangalie pia hili la kuongeza wodi ili kupunguza msongamano wa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, niliona niseme haya na naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia 100. Ahsante.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, katika matumizi ya Mikoa ipo Mikoa ambayo matumizi yake hayalingani na miradi yao kwa maana hiyo yapo matumizi mabaya ya pesa za Serikali au ubadhirifu. Katika Mkoa wa Pwani jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa lina nyufa kazi inayofanya kukabili hali hiyo ni kuchimba ili kurefusha msingi wa nyumba hiyo kwa kwenda chini *(Under Pinning)* maelezo yao kazi hiyo inafanywa chini ya ushauri za kitaalam wa Chuo cha Ardhi.

Kwa vile fedha nyingi zimeshatumika na bado zinahitajika nyingine nyingi zaidi na vyema ujenzi huu ambao tulielezwa kuwa ni *local method* ukafanyiwa tena utafiti kujua kama ujenzi huo hauliongezei ubovu jengo hilo, hasa na kwa kuzingatia kuwa hali hiyo inafanyika kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kazi za matengenezo ya nyumba ya mkuu wa Mkoa ambazo kazi zilizofanyika ni kuiezeka nyumba hiyo, kutengeneza chumba kimoja na kujenga mnara wa kuweka tanki la maji na kujenga uzio wenye urefu wa wastani wa mita 150. Kazi hiyo inadaiwa kutumia milioni 30, kima hiki kinatia mashaka makubwa kwa kulinganisha na kazi zilizofanyika. Ni vyema Serikali ikachunguza udhati wa matumizi haya kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo haistahili kukaa binadamu na hasa kwa kiongozi, nyumba hii ni mbovu, chafu, ndani haina kifaa chochote na haikutengewa fedha za matengenezo na mpaka sasa Mkuu wa Wilaya hajahamia nyumba hiyo kutokana na hali mbaya ya nyumba hiyo hivyo ni vyema Serikali ikabuni njia za kutatua tatizo hilo haraka iwezekanavyo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu.

Katika jimbo langu la Sumve na Jimbo la Kwimba tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kwa kuwahamasisha wananchi katika shughuli za wao kujiletea maendeleo hasa katika shughuli za ujenzi wa shule za msingi kupitia MMEM na ule mpango wa *TASAF*.

Naomba kupitia mchango wa maandishi kuwapongeza wananchi wote wa Wilaya ya Kwimba, watendaji *VEOs, WEOs* na Wataalam walioko chini ya *DED* kwa kusimamia vizuri shughuli za maendeleo kwani Wilaya ya Kwimba imekuwa kioo, shule ya watendaji wengine toka Wilaya mbalimbali kuja kujifunza jinsi gani tulivyofanikiwa kufanikiwa ujenzi we majengo bora ya madarasa ya kisasa, Kwimba ni mfano.

Pamoja na yote mazuri yaliyofanywa na watendaji wetu chini ya *DED* naomba kuleta ombi pamoja na mazuri yote kuiomba Wizara yako kutubadilishia Mkurugenzi kama tulivyokuomba mimi na Mheshimiwa Bujiku Sakila na tulipokuomba ulituahidi kuwa utafanya hivyo ilikuwa ni wakati wa kikao cha Bunge la mwezi Aprili, lakini hadi leo haijafanyika, inawezekana ni kutokana na taratibu za kiofisi. Tunajua wewe ni muungwana sana, hubabaishi, ukisema utekelezaji unafanyika. Hivyo tunasubiri utekelezaji. Nawasilisha.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na mimi nachukua fursa hii adhimu sana kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa maoni yangu kuhusu Bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa mkono wa pole kwa Waheshimiwa Wabunge, wote na wewe binafsi, pamoja na familia ya marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, kwa msiba mkubwa wa mwenzetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia leo tarehe 25 Juni, 2004. Hii ni safari ngumu, nzito na isiyoshaka. *Kulu nafsi dhakatul mauti.*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapa pole wale wote ambao wamefiwa na wazazi wao, watoto wao na wenzetu waolipatwa na maafa mengine.

Baada ya pole, sasa nianze kwa muhtasari kabisa kumpongeza Brigedia Mstaafu Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Naibu Waziri wa TAMISEMI na wasaidizi wao wote kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo inalenga kumsaidia mwananchi wa Tanzania huko vijijini anakoishi katika kuboreka kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi na wapigakura wa Jimbo la Kitope, wote tumeridhika na tunaendelea kuridhika na maelezo ya hotuba za Wizara hii hususan ya mwaka wa fedha 2004/2005. Hotuba hii imeonyesha umahiri wa Serikali hii ya Tanzania hasa huku Bara. Kwa maana hiyo basi, mimi natamka rasmi kuinga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ni ndefu kwa maandishi lakini kulingana na maelezo mazuri muhimu na ya uwazi yaliyomo, kwa kweli imeonyesha au imebainisha kwa kina kikubwa majukumu ya kiutendaji ambayo yanalenga kufanikisha sera kwa kujenga uwezo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kusimamia, kuratibu na kusimamia Halmashauri katika kutekeleza wajibu wake kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa bahati mbaya Wizara hii siyo ya Kimuungano, lakini mimi naridhika na mfumo wake kiutendaji kwani hata kule Zanzibar ni sehemu ya Tanzania sasa nadhani wakati sahihi umeshawadia wa Wizara hizi kufanya kazi kwa karibu zaidi na kwa maana hiyo Mawaziri wetu wawili na watendaji wao wafufue ule utaratibu wa asili wa kutembeleana, kujuana na kuzungumzia mambo yao.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa hakika huwa sifurahishwa na tabia ya Wakuu wa Mikoa wa nchi hii ya Tanzania yenye Serikali mbili kuwa hawatambuani kuanzia majina na hata mazingira yao wanayofanya kazi, hii si busara, hivyo ni masafa gani toka Zanzibar hadi Tanzania Bara? Sisi ndugu wa damu na Wakuu wa Mikoa ni mawakala wetu na ni budi sasa Serikali zetu zote mbili ziwe zinawatambulisha Wakuu wetu wa Mikoa kama ambavyo Mawaziri wetu wanavyotambuana.

Mheshimiwa Spika, sisi tuliwahi kuishi wakati nchi hizi zinaungana na kuzaliwa Tanzania, nadhani tunalo jukumu kubwa kwa watoto kujua kuwa kumbe Zanzibar na Bara ni ndugu na ni vyema basi tuanze kwa tabia ya viongozi wetu hawa kutembeleana. Mazingira yetu kati ya Zanzibar na Mikoa mingi ya Tanzania Bara, yatasaidia zaidi Zanzibar katika juhudi zake za kusoma mambo ya Bara kwa kuinua uchumi wake. Aidha,

kitendo cha kutambuana kitapanua mawazo zaidi ya ukweli uliopo tokea hapo asilia kuwa wote ni ndugu wamoja ambao tuna haki ya kuishi kwa pamoja na kila mmoja ana haki kuishi popote hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kurejea kauli yangu ya kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Shukrani.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii kubwa na nyeti kwani ndiyo pekee inayogusa kila Wizara katika utekelezaji wake. Kero nyingi utakazozitaja iwe barabara, elimu, afya, maji kwa kutaja chache ambazo zote zina Wizara zake, Wizara hii inazitekeleza kwa nafasi yake, hivyo naipongeza sana.

Sasa nikija kwenye Jimbo langu la Morogoro Mjini, tunayo Hospitali ya Mkoa ambayo ina kitengo cha wagonjwa wa akili. Kitengo hiki kiliimarika sana miaka ya 1980, kwa kuwa na majengo mazuri na imara yaliyokuwa yanashughulikia wagonjwa hawa wa akili. Majengo haya sasa ni magofu ambayo inasemekana kuwa yametelekezwa yakisubiri ukarabati mkubwa. Wagonjwa wa akili ambao wanaongezeka kila wakati sasa wamezagaa mitaani, wengine wakitembea wakiwa watupu kwa kukosa makazi yao hayo hospitalini hapo.

Ombi langu kwa Wizara hii ambayo ndiyo yenye dhamana ya kuendesha hospitali hii ya Mkoa, ni kutaka kufahamishwa ni lini ukarabati wa majengo haya ya wagonjwa wa akili utafanywa ili kuondoa adha ya kuwahudumia waathirika hawa pale Morogoro. Hii ni kero kubwa sana kwangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata jibu hilo mimi sina sababu yoyote ya kukataa kuunga mkono hoja hii. Natanguliza shukrani za wananchi wa Jimbo la Morogoro Mjini.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waziri, Mheshimiwa Brigedia *General* Mstaafu, Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kuandaa hotuba nzuri na yenye mwelekeo wa maendeleo kabisa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, mengi yaliyoongelewa na Mheshimiwa Waziri ni mazuri sana, sina budi na kwa niaba ya wananchi wa Mafia kuishukuru sana Serikali kupitia Wizara yako kwa yote yaliyofanyika katika Wilaya yetu ya Mafia. Pamoja na hayo katika Wilaya ya Mafia jambo kubwa linalotuathiri ni upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali kwa mfano watumishi wa Idara ya Afya, Elimu, Kilimo na kadhalika. Lakini kubwa kabisa ambalo linatuathiri na pengine hata Wilaya kukosa maendeleo ni kutokanana wakuu wa idara wenye fani husika na uzoefu mkubwa pia kwani idara nyingi zilizokuwepo Wilayani zinashikiliwa au kuongozwa na makaimu wakuu wa Idara (maafisa wa ngazi za chini za Idara hizo).

Mheshimiwa Spika, hilo ni tatizo kubwa kabisa mfano wa idara ambazo hazina wakuu wa idara wenye sifa ni Afisa Mipango Wilaya, Mhasibu Mkuu wa Wilaya, Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya, Afisa Ardhi wa Wilaya, Afisa Utamaduni wa Wilaya, Afisa Vijana wa Wilaya, Afisa Utumishi wa Wilaya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nina amini kwa mfano huo sidhani kuwa maendeleo yetu Wilayani yatakua kwa haraka. Hivyo tunaomba kwa heshima zote tupatiwe haraka iwezekanavyo wakuu hao wa Idara ili tukomboke na tusonge mbele kimaendeleo.

Kuhusu Ofisi ya Wabunge (Wilaya ya Mafia sijapokea hata shilingi moja toka tulivyoanza Bunge, Novemba, 2001 hadi hili leo. Wilaya haijapokea pesa hata thumni. Binafsi sina budi kushukuru sana Serikali kwa kufanya mengi kabisa ambayo yameweza kutekelezeka na kuonekana kwa macho na wananchi na anayeisema vibaya Serikali basi ana yake.

Mheshimiwa Spika, japokuwa bado yapo matatizo makubwa makubwa kama usafiri wa baharini kwa kuwa hatuna gati, usafiri wa anga kwa sababu uwanja wetu mbaya sana na usafiri wa ndani wa barabara na kwa kuwa Wizara husika bado huleta fedha ndogo ambazo wakandarasi hata wanapokuja kule Mafia basi wanababmbika tu barabara kama kampuni ya *TANHOPE,* wamekuja Mafia na vifaa vibovu, hawakuwa na watalaam na kusababisha kuchonga barabara bila kumwagia maji wala kushindilia kwa (Shindilia) zaidi ya matusi tu tuliyoyapata kwa wananchi kuwa viongozi tumezibwa mdomo na kampuni hiyo kwa kuwa kampuni hiyo *TANHOPE* ni ya kigogo mwenzetu ambaye ni Makamu Meya wa Manispaa ya Kinondoni. Wanauliza mbona hawakumpa barabara za Wilaya yake? Amekuja kutuborongea Wilaya yetu? Hapo kuna walakini!

Mheshimiwa Spika, naomba kuthibitisha taarifa iliyotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maendeleo. Mfano ni ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Mafia, hivi kweli milioni 60 au zaidi ziwe kwa kupanua na kuezeka paa la nyumba na kupigia rangi na kukarabati vyoo vitatu na kuweka *ceiling board* na kuweka vipapatu vya mbao visivyopendeza kwenye madirisha (siyo kuondoa madirisha)?

Nimesikia zimeombwa zingine shilingi milioni 15 kwa kuweka mfumo mpya wa umeme hivyo nyumba hii ya *DC* wa Mafia iliyogharimu zaidi ya milioni 75 hivyo hapo si dalili ya kuwa kuna kitu hapa kilichojificha kwa hao wahusika? Kama siyo wizi basi rushwa. Hata hiyo nyumba iliyotangazwa na kampuni ya *Celtel* ya milioni 60 ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba hao wachache wasitutukanishe na tena uchuguzi ufanyike ili tusichafuane na ikithibitika kama kuna ubadhilifu basi hatua za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, bado nazidi kuomba Wilaya ya Mafia, tufikiriwe na tupewe kipaumbele kwa kupatiwa vifaa vya ujenzi wa barabara, hili ndiyo sababu ya kuiweka Wilaya yetu katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naomba nirudie kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wote wa Wizara hiyo na bila ya kusahau naomba pia nitoe rambirambi zangu kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mafia na Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Yete Mwalyego, mahali pema Peponi. *Amin.*

Naomba ndugu wa Marehemu awape subira kutokana na kuondokewa na kipenzi chao huyo, pamoja na wananchi wa Mbeya Vijijini. Mwisho naseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya furaha ya kupata taarifa mpya mbili katika wilaya yangu ya Mbulu kwa mara ya kwanza katika muda wa zaidi ya miaka 15 sitasimama kujadili hotuba ya Bajeti ya Serikali za Mitaa.

Hata hivyo naomba maombi yetu ya muda mrefu yaliyoletwa Wizarani ili kugawa vijiji vikubwa vyenye kaya zaidi ya 1,000 yatekelezwa. Ombi la pekee ni kuhusu Ofisi ya Mbunge wa Mbulu, jengo la Ofisi ya Mbunge wa Mbulu linalotaka ukarabati matengenezo makubwa lilijengwa na Serikali mwaka 1962 kwa vile Mbunge wa wakati ule Mheshimiwa Sarwatt alikuwa Mbunge wa kujitegemea. Hii ni ofisi ya kwanza ya Mbunge kujengwa na Serikali kwa ajili ya historia ya jengo hilo naomba Serikali itenge fungu maalum.

Pia salaam kwa Katibu Mkuu TAMISEMI, kwa miaka 15 na zaidi mfululizo nimekuwa nachangia mawazo hotuba za Bajeti na Serikali za Mitaa. Mwaka huu najinyima kwa sababu ya furaha ya Tarafa mbili kubwa katika Wilaya ya Mbulu kugawanywa, hata hivyo nina maombi matatu yafuatayo:-

Kwanza, kuna makosa katika taarifa ya Ofisi ya Mbunge wa Mbulu. Ofisi inayosemwa kutaka matengenezo makubwa siyo mali ya hazina bali ni ofisi ya kwanza ya Mbunge wa Jimbo, kujengwa na Serikali baada ya uhuru kwa vile Mbunge wa Mbulu wakati ule Mheshimiwa Sarwatt alikuwa *independent.* Kwa ajili ya jengo hili kuwa na historia ya kipekee Serikali ingetenga fedha za kutosha za kuifanyia matengenezo.

Pili, Wilaya ya Mbulu tunaleta maombi ya kugawa vijiji vikubwa vyenye kaya zaidi ya 1,000. Tunaomba uandikishaji wa vijiji vipya uhakikishwe.

Tatu, hadi mwaka 2003 Mbulu na Meatu zilikuwa ni Wilaya zilizokuwa zikitekeleza kikamilifu miradi iliyokuwa ikifadhiliwa na Serikali ya Uholanzi. Tuna wasiwasi na hatma ya mradi huu *DRDP* katika utaratibu huo mpya wa kuzisaidia Halmashauri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia mapema kwamba, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamejiandikisha kuchangia leo wameondoa majina yao.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Isaac Cheyo, ndiye alikuwa msemaji wa mwisho. Kama kawaida yetu, tutawapa Waheshimiwa Mawaziri nafasi ya mchana huu kuandaa majibu yao kwa kushauriana na wataalam wao ili tutakaporudi saa 11.00 jioni ndiyo waitwe watoa hoja tukianza na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu msiba uliotupata jana usiku, kumekuwa na vikao vikiendelea katika Ofisi ya Katibu wa Bunge kufanya maandalizi ya mambo yote yanayohitajika na hali ambayo imefikiwa sasa ni kwamba mwili wa marehemu utaletwa kwenye Viwanja vya Bunge, hapo kwenye sebule ya Waheshimiwa Wabunge eneo la *pigeonholes,* jeneza lililo na mwili wa marehemu litaletwa hapo saa 8.30 mchana huu. Kwa hiyo, kuanzia hapo itakuwa ni nafasi ya Waheshimiwa Wabunge kutoa heshima za mwisho kwa mwenzetu aliyeaga dunia. Halafu baada ya kutoa heshima za mwisho tunakusudia shughuli hiyo imalizike saa 9.45 jioni ili mwili wa marehemu upelekwe kiwanja wa ndege. Ndege ya Serikali itakayochukua mwili huo wa marehemu itaondoka saa 10.00 jioni kutoka Uwanja wa Ndege wa Dodoma.

Kama ilivyo kawaida yetu, huwa tuna taratibu za kusindikiza mwili wa Mheshimiwa Mbunge anayefariki wakati sote tuko hapa. Kwa hiyo, imepangwa kama ifuatavyo kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mbeya, pamoja na Mkuu wa Mkoa huo ambaye yuko hapa wataingia kwenye ndege hiyo kusindikiza mwili wa marehemu.

Mheshimiwa Spika, Marehemu alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa hiyo, Spika kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, tutateua Wajumbe wawili wa Kamati hiyo kusindikiza mwili wa marehemu.

Marehemu alikuwa vile vile Mjumbe wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, Spika atashauriana na Uongozi wa Kamati hiyo, tuteue Wajumbe wa kusindikiza mwili wa marehemu na kama Kambi ya Upinzani nayo ingependa kuwakilishwa nitashauriana na Kiongozi wa Upinzani, tuteue watakaojumuika katika msafara huo.

Vile vile kama ilivyo kawaida yetu, huwa tunatoa rambirambi kwa utaratibu ambao tulishauweka siku nyingi wa shilingi 5,000/= kwa kila Mbunge, kwa hiyo, zimeshatayarishwa fedha shilingi 1, 465,000/= ambazo zitakwenda pamoja na Afisa wa Bunge aliyeteuliwa kwa madhumuni hayo kama rambirambi ya sisi Waheshimiwa Wabunge, zitakwenda kwa ndege inayoondoka saa 10.00 jioni. Kwa hiyo, la kuzingatia sasa hivi Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, tutaaga mwili wa marehemu kuanzia 8.30 mchana hapa katika Ukumbi wetu wa Bunge.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 05.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niweze kupata mwanya huu kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Bajeti ya TAMISEMI. Lakini naomba kabla sijaanza na mimi niseme kwamba naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine wote katika masikitiko kutokana na maafa yaliyompata Mheshimiwa Mwalyego. Tunatoa pole kwa familia yake na ndugu zake wote.

Lakini pili, nilitaka kusema kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alikwishatangulia kutoa pole pamoja na pongezi kwa viongozi mbalimbali na mimi nasema naungana naye katika yote aliyokuwa ameyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kusema nimekuwepo Bungeni humu sasa ni mwaka wa nne huu kwa maana ya Bajeti ya Serikali na kwa kweli nime-*enjoy* sana Bajeti zote zilizopita. Lakini safari hii nilimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba naona kwamba mwaka huu ni mgumu kweli kweli, hasa zile saa 6 za kwanza tulipoanza. Lakini nashukuru kuona kwamba baada ya hapo nimeona Wabunge kwa kweli wametusaidia angalau hata ku-*cool down* ile *temperature* tuliyokuwa tumeipata. Na mimi nafikiri hata rafiki yangu Mheshimiwa Kone kwa hili atatuelewa tutakapokuwa tumetoa maelezo ili kwa pamoja tuweze kusonga mbele katika kazi ngumu ambayo inatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kubwa, ni ngumu na ina mambo mengi sana. Inashughulika na watumishi wote na inashughulika na shughuli za maendeleo zote. Tunahangaika usiku na mchana katika kujaribu kusimamia eneo hili vizuri kwa kumsaidia Waziri wetu mimi pamoja na Katibu Mkuu na viongozi wengine. Maeneo mengi sana tumejaribu kutembelea. Mimi nadhani mpaka sasa tumekwishazungukia Mikoa 16 na katika kila Mkoa tumejitahidi kwenda karibu kila eneo katika kujaribu kuona tufanye nini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi rai yangu ya jumla tu kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba muendelee kutusaidia na naweza nikasema kabisa wala hatusononeki, wala hatusikii uchungu kuona mnatukosoa kwa sababu mnatusaidia kuweza kuelewa zaidi matatizo katika hii Wizara. *(Makofi)*

Na napenda kabisa niwahakikishie upande wangu na hata Waziri atayasema haya haya, tutashirikiana na ninyi kikamilifu kabisa kuhakikisha matatizo yote ambayo yapo ndani ya uwezo wetu tunayazingatia ili tuweze kuhakikisha tunasaidia Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niende katika michango yangu ingawa mambo ni mengi kweli kweli lakini tutajitahidi tuone kiasi ambacho tutaweza. Kwanza nilitaka nianze na suala hili la fedha la Serikali za Mitaa kupelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri zetu bila kupitia Hazina Ndogo. Waliochangia hili ni Mheshimiwa Kabourou, Mheshimiwa Janguo, Mheshimiwa

Lubeleje, Mheshimiwa Ndugai, Mheshimiwa Namkulala, Mheshimiwa Cheyo, Mheshimiwa Makundi, Mheshimiwa Shibiliti, wote wameligusa kwa namna moja au nyingine na sisi kama Ofisi tunasema suala hili kwa kweli tumelizingatia, tayari fedha zinapelekwa moja kwa moja kutoka Hazina kwenda kwenye Halmashauri husika katika mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo bado hatujalikamilisha ni lile la kupeleka fedha za mipango ya maendeleo na kwa kweli tunajitahidi tuweze kubanana vizuri ili utaratibu huu uweze kuzingatia eneo hili vile vile. Katika fedha hizi za Serikali za Mitaa liko suala vile vile la Halmashauri zote zipate fedha za maboresho.

Hili tunaweza tukawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa upande wa fedha hizo za maboresho ikiwa ni pamoja na fedha kutokana na mpango wa kuzisaidia Serikali za Mitaa *Local Government Support* Halmashauri zote kuanzia mwaka huu 2004 wa fedha tutahakikisha zinapatiwa fedha hizo ili ziweze kutekeleza mipango inayohusiana na maboresho. *(Makofi)*

Lakini lilikuwepo suala lingine zito tu kuhusiana na hizo fedha za mitaa ambazo ni ruzuku ya fidia, vyanzo vilivyofutwa kuwa hailingani kidogo ikilinganishwa na mapato yaliyokuwa yakikusanywa kutoka vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Mheshimiwa Mohamed Missanga pamoja na Mheshimiwa Mutungirehi walilieleza kwa kirefu lakini nafikiri Mheshimiwa Waziri atapata nafasi pengine ya kuweza kulieleza vizuri zaidi. Lakini naomba niseme tu kwamba zoezi hili lilifanyika kwa kina sana, tulitumia wataalam wetu, tumetumia wataalam wa nje ili waweze kutusaidia kuona ni namna gani tunaweza tukafikia *formula* ambayo inaelekea kukidhi haja ya fedha za Serikali za Mitaa na ilikuwa baada ya zoezi hilo ndipo mkaona tukaanza ku-*disburse* na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri asubuhi nadhani leo au jana ni kwamba kwa mwaka huo uliopita tuliweza kutoa kiasi cha shilingi 22.9 bilioni na mwaka huu tunatarajia kutoa bilioni 25 kwa ajili ya kwenda kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima tukubali kwamba Waheshimiwa Wabunge mlichokisema kingine ni kizuri tu kwamba kuna ucheleweshaji wa fedha hizi na kwa hiyo inafanya kidogo shughuli za Halmashauri zinakuwa na mgogoro. Tumelikubali na tutajitahidi kurekebisha hiyo kasoro ili tuone kama zinaweza zikafika kwa wakati ili ziweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye eneo hilo kwa sababu lilikuwa na michango mingi lilikuwa ni suala la Wataalam kwenye eneo la Uhasibu. Hili linajulikana na Ofisi yangu na kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tunalishughulikia. Ni matarajio yetu kwamba tutaweza kukidhi haja hiyo kubwa. Tayari yameshaanzisha mafunzo kwa ajili ya kupata Wataalam hawa ili kuweza kuimarisha eneo hili la Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utozaji wa ada na ushuru kinyume na taratibu, nadhani hili ni mapungufu kwa kweli ya utendaji na lazima tukubali kuwa ni mapungufu

tu katika utendaji. Marekebisho yaliyofanyika hapa Bungeni wakati Waziri wa Fedha alipowasilisha Bajeti yake mwaka jana ni mwongozo mzuri sana kuhusiana na nini kinatakiwa kitozwe na kipi hakitakiwi kitozwe. Lakini bado tunaona malalamiko yanajitokeza. Tumekubaliana Ofisini kwamba itabidi tulifanyie kazi ili tuweze kuona wapi kuna matatizo na wapi hakuna matatizo. Na kwa hili pengine niseme mambo mawili tu, moja ni la ushuru *i.e. cess* ya mazao *categorically* ilisemwa hapa kwamba mazao yatatozwa si zaidi ya asilimia 5 na hii asilimia 5 itatozwa *at the point* ya ununuzi kule shambani au pale kwenye kituo ambako jambo hili limefanyika. Lakini bado kuna watu wanakwenda wanatoza sehemu ambazo siyo sehemu zake. Kwa hiyo, tutajaribu kulikazia zaidi ili tuhakikishe kwamba halirudiwirudiwi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo suala ambalo Mheshimiwa Maghoba naye aliligusia ni la *Property Tax* kuhusiana na watu wale ambao nyumba zao hazikupimwa, si kupimwa hasa, lakini pengine ziko katika hali ambayo haifanani na nyumba zinazopaswa kutozwa ile *Property Tax.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Wabunge wote wanakumbuka, lilielezwa vizuri sana hapa wakati tumetengeneza ile Sheria. Nyumba zote ambazo tumesema ni nyumba, *well* tusiziite duni lakini ni nyumba ambazo zimetengenezwa kwa udongo haziko katika hali ile ya kusema ni kitu cha kudumu. Na nyingi hizi mtazikuta mijini na hasa kwenye *squatter areas.* Tulisema nyumba hizi zisiingizwe katika utaratibu huo. Lakini bado inaonekana baadhi ya maeneo bado wanaenda kuwabana watu hawa. Kwa hilo nalo tutajaribu kulitolea maelekezo zaidi ili tuwe na uhakika kwamba jambo hili linaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niende kwenye eneo la pili ambalo ni uhusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Parseko Kone amelizungumza kwa nguvu sana, Mheshimiwa Kabourou, vile vile Mheshimiwa Janguo, Mheshimiwa Kidunda na Mheshimiwa Ntimizi, walilizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maelekezo ya kutosha kabisa juu ya suala hili. Lakini tukubali kwamba binadamu wakati mwingine tunakuwa wagumu sana katika kujaribu kutekeleza mambo ambayo yanaleta mabadiliko. Kwa hiyo, tutaendelea kulikazia na kulitolea ufafanuzi zaidi. Lakini niseme kidogo kwa upande wa Wakuu wa Wilaya. Kulikuwepo hoja kwamba madaraka ya Wakuu wa Wilaya kuhusu Halmashauri pengine halikukaa vizuri. Tunaloweza kusema hapa ni kwamba Wakuu wa Wilaya kama ilivyo kwa Wakuu wa Mikoa, wote tumewataka watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Taratibu na Sheria za nchi. Hatutegemei kwamba mtu atakuwa nje ya utaratibu huo. Kwa hiyo, chochote kile atakachokifanya lazima kizingatie jambo hilo na Ofisi ya TAMISEMI haitasita kwa kweli kuchukua hatua ya kutoa maelekezo kadhaa endapo itaonekana kwamba kuna jambo limejitokeza ambalo ni nje ya jambo hilo. Utungaji wa Sheria ndogo hili nalo bado ni tatizo lakini tulikwisha kulielekeza kwamba ni vizuri sheria ndogo zikatungwa miezi sita kabla ya mwaka wa fedha kuanza ili tuweze kupata muda wa kuweza kuzishughulikia na kuingiza mawazo yote ya kibajeti katika taratibu hizo. Kwa hiyo, tunadhani hili ni suala la usimamizi tu tutaendelea kuwaasa na kuwahimiza watekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa TAMISEMI kuzisaidia Halmashauri. Waheshimiwa Wabunge ndiyo juhudi kubwa kwa sasa ambayo tunaifanya, tumeleta programu hii ambayo ni mpango wa uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa katika kujaribu kuonyesha nia yetu ya kuzisaidia Halmashauri. Sasa bahati mbaya jambo hili ni process kwa hiyo inaweza ikachukua muda kidogo. Lakini nadhani wote mmekwishaona juhudi zinazoendelea katika eneo hilo la mpango huo wa uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Waheshimiwa Wabunge wamesema mnapoleta masuala pale TAMISEMI kuna kuchelewa na kwa hiyo mkahimiza kwamba ni vizuri yawe yanatoka mapema. Tunakubali, lakini tulitaka vile vile upande wa Wabunge nao mkubali kwamba jambo hili kidogo linakuwa zito hasa inapokuwa ni suala linataka uchunguzi, inabidi tuchukue muda kidogo kuweza kuwa na uhakika kwamba hatua tutakayoichukua haimwonei mtu. Kwa hiyo katika hali hiyo inaweza kidogo tukaonekana tunachelewa lakini tunapenda kuahidi kabisa kwamba tutajitahidi kuongeza nguvu zaidi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utaratibu wa kuteua Watendaji Wakuu wa Halmashauri kwa maana ya Wakurugenzi. Tunaloweza kusema hapa WaheshimiwaWabunge ni kwamba kwa kweli uteuzi wa Wakurugenzi wale wanaotarajiwa au wale wanaoomba kuajiriwa, bado ni eneo ambalo sasa hivi tunasema liko *squarely* chini ya Halmashauri zenyewe. Lakini tunaelewa kabisa kwamba hapa na pale inabidi vile vile TAMISEMI iingilie kati kwa sababu ya kutaka kuhakikisha tu kwamba taratibu na sifa pengine zinazotakiwa zimezingatiwa na ndiyo maana mara zote unaona tunatangaza kwenye magazeti ili watu waweze kujitokeza ili kuwa na uhakika kwamba tumepata watu wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko eneo la tatu ambalo linahusu upungufu wa watumishi. Mheshimiwa Kabourou na Mheshimiwa Cheyo pamoja na Mheshimiwa Mussati na Mheshimwia Halinga, wote wamelisema hili kwa nguvu sana. Kwa kweli hapa tunachoweza kusema Waheshimiwa Wabunge tukubali kwamba hili ni tatizo la kitaifa na limeelezwa na linagusa karibu sekta zote. Tunachoweza kusema ni kwamba kazi yetu kama waratibu wa shughuli za Serikali za Mitaa tutaendelea kuzungumza na Idara Kuu ya Utumishi pamoja na sekta nyingine ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linakwenda linapungua kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wenyewe wa uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Kilichojitokeza zaidi hapa ni kwamba inaonekana ni kama vile unakwenda *slowly* na kwamba ni Halmashauri chache tu ndizo zimenufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu kwa sasa umeenea nchi nzima. Hakuna Wilaya hata moja ambayo haimo. Lakini kilichojitokeza tu hapa ni kwamba yako maeneo ndani ya programu hiyo ambayo hayawezi kuenea nchi nzima kwa mara moja na moja ya maeneo hayo ni mpango wa Kompyuta ambao unatumika katika Halmashauri na tumekwishauanza. Sasa kwa sababu mpango huu unakwenda mpaka mwaka 2011 ni

matarajio yetu kabisa kwamba tutakapofika huko wale watakaokuwepo basi mpango huo wa kompyuta utakuwa umeshafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini liliulizwa swali vile vile kwamba ni kiasi gani cha fedha kimetumika hadi sasa kwenye zile Halmashauri 38 za awamu ya kwanza. Ni kiasi cha shilingi bilioni 2.6 zimeshatumika hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa utoaji wa huduma jambo ambalo Mheshimiwa Ndugai na Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, pamoja na Mheshimiwa Shibiliti, lakini vile vile Mheshimiwa Sophia Simba na Mheshimiwa Watondoha, pamoja na Mheshimiwa Selelii, waliligusia vile vile. Tunaloweza kusema hapa ni kwamba tutajitahidi hasa kwa sasa baada ya Sera ya Maafa kuwa imetoka. Kwa hiyo, tutaizingatia sana katika kuboresha utoaji wa huduma hasa kwenye nyanja hizi za maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda niseme *more specifically* kuhusu mpango wa kuzisaidia Serikali za Mitaa, *Local Government Support Programme.* Tunaloweza kuwaelezeni hapa ni kwamba Halmashauri zote 114 zitafaidika na mpango huo hatukubagua. Ila labda linajitokeza tu ni kwamba ziko zilizoanza katika maeneo fulani fulani na ziko nyingine ambazo zitafuata baadaye. Kwa hiyo, kwa kuanzia tuna Halmashauri 89 ambazo zitapata fedha kutokana na mpango wa kuzisaidia moja kwa moja lakini vile vile kutokana na kitu tunaita programu ya eneo. Ni *components* za fedha ambazo moja ziko moja kwa moja nyingine zimezingatia kieneo kwa maana kwamba kuna wafadhili fulani fulani ambao wamekubali kusaidia katika eneo hilo katika baadhi ya Halmashauri. Kwa hiyo, Halmashauri 25 zitakuwemo katika mpango lakini hizi zitakuwa katika hatua tofauti ya kuwezeshwa kwanza kujengea *capacity* kidogo ili waweze kuingia katika utaratibu wa sasa tunaouzungumza. Mpango huu ni wa miaka mitano unaanza *Financial year* hii na utakwisha 2009. Kwa hiyo, tunaamini kabisa tutaweza kukidhi baadhi ya hisia zilizokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro kati ya Madiwani na Watendaji, ni kweli kabisa matatizo haya yapo, yapo kabisa kabisa. Iko migogoro hasa kati ya Madiwani na Watendaji. Lakini sababu zake ni nyingi. Lakini moja ambayo kiofisi tulibaini ni kutokuwepo kwa mafunzo ya aina yoyote ya kuweza kuwasaidia kujua majukumu yao na mipaka ya majukumu yao. Kitu ambacho tumekizingatia sana katika kipindi hiki cha miaka miwili, mitatu na nadhani ninyi wote ni mashahidi na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atalifafanua vizuri zaidi atakapokuwa anatoa maelezo yake. Na hatukuishia hapo, pale ambapo tuliona mapungufu yana uzito zaidi, hatukusita kuchukua hatua za kudhibiti hiyo *situation* ili isiweze kuendelea zaidi.

Mheheshimiwa Naibu Spika, madai ya Mkurugenzi kushindwa kusimamia MMEM. Hili limetolewa na Mheshimiwa Kone na ndiyo maana nilisema aah! Mimi nadhani baada ya maelezo haya na mengine yatakayofuata bila shaka Mheshimiwa Kone ataona kwamba tumejitahidi. Jambo moja zito alilolisema ni kwamba zilitoka hundi 11 ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya MMEM lakini zilipokwenda benki zika-*bounce*. Kwa hiyo, kidogo ilimkera na hakuona ni kwa nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme tu kwamba Mheshimiwa Kone mimi amekuwa *very close* kwangu tumeshirikiana vizuri sana na alipopata tatizo hilo hakusita kuleta zile hundi kwangu, alileta na mimi sikuchelewa nikatoa maagizo jambo hilo lifuatiliwe. Kwa hiyo, iliundwa Timu ambayo tumechukua *Zonal Reform Officer* mmoja na tukachukua Wakaguzi wa Ndani kutoka Manyara na Arusha tukawatuma kwenda Simanjiro. Wamekwenda Simanjiro wamefanya ukaguzi wa jambo hilo hivi tunavyozungumza sasa wako Arusha wanakamilisha hiyo taarifa. Wamekwenda huko tangu tarehe 3 Juni, 2004. Kwa hiyo, nilitaka nimhakikishie kabisa kwamba sikulinyamazia, sikulilazia damu kwa sababu *it was certainly a very serious issue.*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niongezee hapo tu kwamba taarifa hiyo itakapopatikana itatusaidia vile vile kuchukua hatua nyingine zozote tutakazoona zinafaa kwa Watendaji wote ambao watakuwa wamehusika katika ubadhirifu huo na wala hilo hatutalionea aibu. Kwa hiyo nilitaka nimwombe Mheshimiwa Kone atupe nafasi kidogo tuone *what comes from that report* halafu tunamwahidi kabisa kwamba tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba jambo hilo linakwisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wabunge kupatiwa Semina ya Maboresho, tumekubali. Tutai-*organize* na itafanyika kwenye *proper time* ili kila mmoja aweze kuona ni kitu gani kinaendela. Kuhusu uchaguzi wa ngazi za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mbowe, *I respect your views* pamoja na Mheshimiwa Mama Kasella-Bantu, ambayo aliyatoa hapa, lakini naomba niseme kwamba katika jambo hili hatutasita kusema kile ambacho sasa ndiyo maamuzi ya Serikali. Kulikuwa na rai kwamba haiwezekani kufanya uchaguzi huo mpaka kwanza Daftari lile la kudumu litengenezwe. Katika mazingira tuliyonayo tumesema *practically it is not possible* kwa sababu muda wenyewe hauruhusu.

Kwa hiyo, tutatumia taratibu nyingine ambazo tunaamini tutazifanya *in such a way* kwamba ziwe *as fair as can possibly be* na tutaendelea kushirikiana na viongozi wa vyama hivyo vingine kuhakikisha jambo hilo linafanyika na katika kuimarisha jambo hili tulichofanya tumetoa zile Kanuni tukazisambaza nchini kote kwenye magazeti na hivi sasa tumeshaanza kupata maoni mengi tu ambayo tunafikiri yatatusaidia kuboresha hatua hiyo kabla hatua hiyo ya mwisho haijafikiwa. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbowe pamoja na Mheshimiwa Kasella-Bantu kwamba *we are determined in the same way as you are* kufanya kitu ambacho ni kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala bora, ambao Mheshimiwa Losurutia aliusema pamoja na Mheshimiwa Chilolo. Naweza kusema tu kwamba jambo hili linatugusa wote na lina mambo mengi na kama ulivyomsikia Mheshimiwa Losurutia, rai yake kubwa ilikuwa ni Mkuu wa Wilaya kwamba kwa kweli huyu mtu asipotoka basi kufa na kupona. Na sisi tunasema watu wazima hatufanyi hivyo. Watu wazima tunakaa tunazungumza, tunaona *what can be done. (Makofi)*

Tulikuwa na tatizo na *DC* aliyetangulia, muda mchache tu si muda mrefu uliopita. Mhehismiwa alikuja akatuona, akasema *DC* huyu hanifai kabisa, naomba umtoe.

Amechangia katika matatizo mengi. Tukamsikiliza, tukamhamisha yule *DC,* tukamleta huyu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliona kwamba Mmasai kwa Mmasai labda wataelewana vizuri zaidi. Lakini naona matokeo yake sasa imekuwa tatizo lingine tumeli-*create.* Lakini kweli ningependa kusema kwa dhati kabisa kwamba sehemu nyingi, *this thing can be settled among yourselves* na *very rarelly* mnaweza mkaja huku kusema kwamba tunaomba hili tunaomba. Na tukiliona lina uzito tutalifanya tu. Lakini kwa hili nilikuwa nasema Mheshimiwa avute subira tuko pamoja naye. Lakini *we have to find out* sasa *DC* mwingine atakuwa nani, maana inabidi sasa tutafute kwa makini kweli kweli ili tuweze kupata *DC* anayemtaka. Lakini tuko pamoja naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nigusie kidogo ni hili la mfuko wa pembejeo pamoja na barabara zenye maeneo mengi. Lakini Ofisi za Wakuu wa Wilaya, zina matatizo sehemu nyingi tu baada ya kufanya utafiti tulioufanya. Lakini tulitaka tuseme kwamba tutajitahidi kuhakikisha kwamba jambo hili linatekelezwa kwa kadri WaheshimiwaWabunge mlivyoshauri.

Lakini liko jambo moja ambalo Mheshimiwa Janguo alipokuwa anatoa taarifa yake hapa alisema, na tulifikiri na sisi tutalisema kwa nia nzuri tu. Katika taarifa yake alisema Wilaya kwa Bajeti ya mwaka huu 2004 kila Wilaya imetengewa shilingi milioni 2 tena akaweka na neno tu. Milioni mbili tu. Sasa hili sina namna nzuri zaidi ya kulieleza isipokuwa kuomba tu kwamba pengine mkipata muda muda mpitie *Volume III* ya kitabu hiki na mtaona juhudi za Serikali katika eneo hilo.

Kwa kifupi nasema hakuna Wilaya katika Bajeti hii ambayo imepata chini ya milioni 20 kwa mwaka huu. *So, the lowest* itakuwa labda 1.8 milioni hivi kwa kila mwezi ambayo ukii-*total up* unaweza ukafikia hiyo *figure.* Kwa hiyo, inawezekana pengine katika ku-*type* au katika kulisema alitaka kusema pengine kwa kila mwezi. Lakini *certainly* siyo kwa mwaka. Na naomba tu niseme Bagamoyo kwa mfano, wao watakuwa na milioni 28,077,800, Kibaha 29,305,900, Kisarawe 29,607,000., Mafia 28,801,900. Mkuranga 29,000,600 na Rufiji 30,642,000, Kwa hiyo, nilikuwa katika kusahihisha tu nadhani aliteleza kidogo wakati alipokuwa anaielezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa miradi niseme tu kwamba Ofisi yetu inajitahidi sana kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali na hasa barabara. Maofisa wetu Wahandisi wanazunguka, nadhani baadhi ya Wabunge mtakuwa mmeshawaona katika juhudi za kujaribu kuhakiki matumizi ya fedha lakini vile vile na ubora wa barabara. Sasa inawezekana kabisa baadhi ya Mikoa hatujaweza kwa sababu Wahandisi tulionao sio wengi na katika hali kama hiyo tuko radhi kabisa kupokea mawazo kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote ili tuone namna tunavyoweza kusaidiana kupata uhakika wa kazi iliyofanyika katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hili tunalikubali na tuko tayari kusaidiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji Wakuu katika ngazi mbalimbali hususan TAMISEMI hawatembelei maeneo ya nchi na hivyo hawajui matatizo yaliyopo. Mama

Watondoha alilisema hili na nikafikiri pengine niliseme. Nimesema tumeshatembelea Mikoa 16 mpaka sasa mimi na Waziri. Lakini Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu nao wamekwishatembelea Mikoa ya kutosha tu, wamekwenda Mbeya, wamekwenda Shinyanga, wamekwenda Rukwa na maeneo mengine.

Kwa hiyo, kwa kweli wanajitahidi katika mazingira tuliyonayo. Kuhusu Ofisi za Wabunge nilitaka Mheshimiwa Waziri alizungumze hili lakini mimi nasema labda niseme jambo moja au mawili hivi. Hili limezungumzwa sana na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini vile vile Mheshimiwa Ndugai, Mheshimiwa Chiduo na Mheshimiwa Singo wameligusiagusia. Tunaloweza kusema tu ni kwamba eneo hili bado linahitaji kufanyiwa kazi wote ni mashahidi. Ziko juhudi zinafanyika lakini itabidi tuendelee kusaidiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba azma ya Wabunge inafikiwa na pengine katika muda ambao si mrefu sana. Ni suala la fedha lakini ni suala la usimamizi vile vile katika yale yanayotakiwa kufanyika. Kwa hiyo, tutaendelea kulifanyia kazi lakini nadhani Waziri naye atajaribu kulisemea kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za watumishi katika Hospitali za Mikoa. Mheshimiwa Peter Kabisa amelizungumzia sana hili. Na mimi nasema napenda nimhakikishie tu kwamba tutashirikiana kikamilifu na Wizara ya Afya ili tuweze kuona nini tutafanya lakini naomba ni-*caution* tu kwamba katika maswali mengi yanayoulizwa hapa hili limejitokeza na kauli yetu kwa kweli ni ile ile. Ni ile tu kwamba mfa maji haachi kutapatapa, *so we have to keep up momenta m* ili tuone namna gani tunaweza kuifanya hii kazi. Kuhusu mahabusu kujazana magerezani na sehemu nyingine. Hili tumesema tutaliwasilisha kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani na bahati nzuri naona Mheshimiwa Chiligati yuko pale.

Kwa hiyo, tutashirikiana nao kuona hili linafanyika. Kuhusu hali ya chakula Wilaya ya Hai, Mheshimiwa Mbowe alilieleza hili. Tumekubaliana kwamba tutaliwasilisha kwenye Ofisi inayohusika. Lakini tutaomba na Hai vile vile na ninyi muweze kuli-*raise* mapema zaidi kidogo ili msichelewe.

Kuhusu muundo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwamba uangaliwe upya. Ni kweli kabisa juhudi hizo zinafanyika. Na kwa kweli tumeanza muda mrefu kidogo, lakini kama unavyojua mambo haya yana kazi nyingi kidogo, mabishano ya hapa na pale. Lakini zoezi hili tumeshaanza kulifanya. Tumewasiliana na Idara Kuu ya Utumishi ili tuone tutakavyo-*compromize* ili kuweza kuijengea uwezo mkubwa zaidi kuliko pengine ulivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano kati ya TAMISEMI na Wizara ya Tawala za Mikoa Zanzibar. Bahati nzuri, Ofisi hii ya TAMISEMI tayari ilikwishaandikiana na Wizara hiyo ya Zanzibar na watumishi wa Wizara hiyo wameshafika hapa tayari tukakutana tukazungumza. Kwa hiyo, nadhani ni suala tu la kuendeleza hiyo *spirit* kwa kasi kubwa zaidi. Hili la utawala bora Mheshimiwa Halinga alikuwa na hoja moja nzito kidogo kwamba hakuna mwongozo wa Mkuu wa Wilaya kumdhibiti Mkurugenzi. Pengine hoja si kumdhibiti, lugha ya kumdhibiti kidogo ni ngumu. Hizi ni Serikali, tunazitambua zipo.

Kwa hiyo, tunachojaribu kutafuta pale ni kujaribu kutafuta utaratibu utakaoleta mahusiano mazuri *amicable relations* kati ya Wakuu wa Wilaya na hizi *Local Government Authority* ili ziendelee kujiona kwamba ni Serikali lakini zijue kwamba *at the end of the day* yuko kiongozi pale juu ambaye anatakiwa vile vile kusimamia shughuli. Kwa hiyo, tutaendelea kuliangalia hilo ili tuweze kuona ni nini tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Watondoha alikuwa na rai kwamba tunahamisha watumishi wabovu. Kama nilivyosema kwamba Wizara hii ina mambo mengi. Lakini tunajitahidi sana. Si kweli kabisa kwamba tunahamisha wabovu. Wabovu wengi tumewafukuza. Wengi tunadhani mnajua hili. Kwa hiyo, wale ambao bado tunaamini ni watumishi wazuri ndio hawa ambao tunasema basi ukikaa mahali miaka mingi kama mara nyingi mnavyotuambia, basi tunamhamisha kwa sababu itaongeza ufanisi zaidi.

Kwa hiyo, hilo nadhani tutaendelea kulizingatia. Lakini ilikuwepo rai nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kuhusiana na ujenzi wa nyumba ya *DC* ya Mafia. Jambo hili labda nimwambie tu Mama Dr. Gama kwamba tumwombe tu tukaye pamoja, tujaribu kumpa *details* za *what happened stage by stage* ili pengine imsaidie kuweza kuona *what happened.* Lakini ukweli ni kwamba tulijitahidi sana kuzingatia Sheria, Kanuni katika utoaji wa tenda na katika ujenzi na sasa tunaweza tukasema jengo hilo lina a*lmost by 90 percent* hivi katika hali nzuri.

Lakini bado hatusemi kwamba hakuna upungufu au hakuna kasoro. Ndiyo maana nimesema tukikaa tukishampa maelezo haya anaweza pengine akapata nafasi mzuri ya kutuambia, hapana siyo kweli, hili ni uongo fanyeni hivi. Lakini tunachosema ni kwamba tutashirikiana naye tuone kasoro ziko wapi ili tuweze kuhakikisha kwamba zinaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ukarabati wa hospitali, hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Mloka. Tumekubali kwamba tutalitazama hilo jambo kushirikiana na Wizara ya Afya ili tuone nini la kufanya.

Mwisho ni suala ambalo Mama Chilolo alilisema kuhusiana na umuhimu wa kujenga na kuimarisha Sekretarieti za Mkoa. Tumelikubali kabisa kabisa. Na nadhani hata Wakuu wa Mikoa wanajua matatizo tunayoyapata na tumeshaanza kulifanyia kazi na tulidhani katika marekebisho ya Sheria yatakayokuja hapo baadaye, baadhi ya mawazo yatajitokeza humo ili muweze kutusaidia kuona namna ya kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema mwanzoni nilitamani niseme yote lakini si rahisi. Naomba niseme moja tu la mwisho kuhusiana na suala ambalo Mheshimiwa Kaka yangu Nimrodi Mkono alilieleza hapa kwa uchungu sana kuhusiana na ubora wa madarasa na akatoa mfano wa shule moja iliyopo *Oysterbay* kwamba imejengwa na inafanana na boma la ng'ombe. Kidogo ilinishtua nikamweleza Waziri, kwa hiyo mimi nikaenda *Oysterbay,* Jumamosi nimekwenda pale shuleni kuangalia boma hilo la ng'ombe liko wapi. Nimetembelea pale kwa kweli *lets be fair to*

*each other,* MMEM imejitahidi sana. Madarasa yale yapo nane, mimi nasema ni madarasa mazuri, yanatosheleza kabisa mahitaji ambayo katika hali tuliyokuwa nayo tulikuwa tunayahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kweli niseme vile vile kwamba unajua kauli nyingine zinakuwa nzito. Watu wamechangia pale, wananchi wamechangia nguvu zao, wamechangia fedha, ukija kusema *standard* yake ni kama boma la ng'ombe *you know* hata kwa mwananchi aliyechangia anaona shida sana, *can that be true?* Lakini najua Mheshimiwa Nimrod Mkono inawezekana viwango vya majengo yake ni vikubwa zaidi sasa aliona pengine ile *is too low* lakini mimi nasema kwa madhumuni ya mpango huu, *it was not a bad exercise at all. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nimalizie kwa kusema kwamba mimi binafsi narudia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri ambayo imetusaidia na nina hakika itatusaidia sana kukamilisha zoezi hili. Hatukusema yote, yale ambayo tumeyaacha tutayaleta kwautaratibu wa kawaida, tutatoa jedwali ambalo litakuwa linajaribu kueleza tumesema nini. Najua Waheshimiwa Wabunge wengi wamejaribu kusema maneno mazuri juu yangu na mimi nasema nawashukuru lakini *with a caution* kwamba hakuna jambo ambalo nalifanya ambalo sikuagizwa na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mimi ni msaidizi wake, Mmari ni msaidizi wake, *so we have to do the best that we can* kumsaidia Waziri ili aweze ku-*perform* vizuri *as a Minister. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuruni sana na sasa niseme na mimi huo ndio mchango wangu na naunga mkono moja kwa moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge katika kutoa rambirambi zangu za dhati kabisa kwa familia ya marehemu ndugu yetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye amefariki jana usiku na leo hii ndiyo amesafirishwa kwa ajili ya kwenda kuwekwa mahali pake pa mwisho pa kupumzikia. Tunamwomba Mwenyezi Mungu airehemu roho yake na aiweke mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchangia hotuba ya Bajeti ya ofisi yangu, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wametoa hoja kwa kauli na maandishi. Wabunge waliotoa hoja hizo ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, Mbunge wa Kigoma-Ujiji. Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kutoa hoja zao hapa Bungeni na kwa maandishi. Napenda kuwashukuru watoa hoja wote kwa michango yao yenye maelekezo, mapendekezo na ushauri wa namna ya kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kauli hapa Bungeni. Kwanza ni Mheshimiwa Athuman Janguo, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Omar Said Chubi,Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Aaron Chiduo, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi,Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Abdullah Suleiman Lutavi, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, Mheshimiwa Isaac Cheyo na Mheshimiwa Mizengo Pinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Shamim Khan;Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba; Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Semindu Kisange Pawa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Daniel Yona, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa John Singo.

Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Danhi Makanga na Mheshimiwa Emmanuel Kipole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Dr. Zainabu Gama, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Sumri Mohammed, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mheshimiwa Profesa Mbawala, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Damas Nakei; Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Zahor Khamis, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Sijamini Shaame, Mheshimiwa Mloka; Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Balozi Pius Ngw'andu, Mheshimiwa Profesa Dimon Mwaga, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Ramadhan Hashim Khalfan na Mheshimiwa George Francis Mlawa, nawashukuru Waheshimiwa wote hawa waliochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchangia hotuba hii, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala amebainisha mambo makuu yafuatayo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mambo hayo ni pamoja na

ufafanuzi kuhusu ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa, usimamizi wa Mfuko wa Pembejeo; ruzuku kwa Halmashauri ziongezwe na zipelekwe moja kwa moja, hili Mheshimiwa Pinda amelijibu. Uhaba wa wataalam vile vile limejibiwa; mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara uangaliwe. Kiwango cha fedha za matumizi ya kawaida kwa Wakuu wa Wilaya, uboreshaji wa mazingira ya kazi kwa Wakuu wa Wilaya; ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uidhinishaji wa uchapishaji wa sheria ndogo uharakishwe na vigezo vilivyotumika katika mgawanyo wa fedha za *program* za kusaidia Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kambi yaUpinzani msemaji wa Kambi ya Upinzani wakati akichangia hotuba yangu alibainisha yafuatayo: Kukosekana kwa ufanisi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; ukiritimba katika majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kutokuwepo kwa Wizara mahsusi ya Serikali za Mitaa; uhaba wa watumishi katika Serikali za Mitaa; migongano kati ya Madiwani na Watendaji; Ofisi ya Rais, TAMISEMI haina malengo ya muda mfupi na mrefu kuziachia Halmashauri madaraka katika maeneo yao, nafasi za Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tarafa, TAMISEMI haikufafanua kipindi maalum cha kutekeleza majukumu yake, Madiwani kuondolewa katika Bodi za Zabuni, TAMISEMI kuhalalisha maamuzi ya Serikali Kuu na Hazina kutofidia Halmashauri fedha zinazotokana na vyanzo vya mapato vilivyofutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizo pamoja na hoja zingine zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni na kwa maandishi baadhi yake zimekwishatolewa majibu na ufafanuzi na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika hili, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kumwona Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Pinda kwamba kweli ni mchapaka kazi. Mimi pia napenda kukiri kwamba ni Naibu Waziri ambaye amenisaidia sana katika Wizara hii na vile vile napenda kuthibitisha kwamba katika Wizara yetu hii tunafanya kazi kama timu moja. *(Makofi)*

Naomba nitoe maelezo kuhusiana na hoja za Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu ajira za Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Serikali inatambua umuhimu wa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa katika kusimamia shughuli za maendeleo katika ngazi hizo za utawala. Kwa kutambua umuhimu huo, tayari Serikali kwa mwaka huu wa fedha imetenga jumla ya shilingi 5,949,165,600/= kwa ajili ya kulipia mishahara ya Maafisa Watendaji walio katika ajira na ambao wataajiriwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu ambazo zimewekwa na Serikali. Kwa hiyo, tunaamini kwamba utata uliokuwa umejitokeza mwanzoni kuhusiana na sifa na ndiyo maana ilibidi nitoe kauli hapa Bungeni kwamba kwa sasa hivi wale waliopo basi tutawachukua kwa utaratibu wa Mkataba lakini na wao waanze kujishughulisha ili waweze kujiongezea sifa. Sasa hivi Tanzania tunasema elimu haina mwisho na wao wasome, wasiridhike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji wa Kata ilibidi waajiriwe idadi ya karibu 4000 tu kwanza kwa sababu hao ndiyo waliokuwa na barua za ajira. Kiserikali huwezi kuchukua tu kila mtu ukamfanya ni mtumishi. Kwa hiyo, ilibidi tucheki tuone ni nani wana ajira za Halmashauri zao, waliopatikana na ajira ni hawa 3900. Sasa tunaendelea

na utaratibu wa kuajiri hao wengine. Tunajua ni vigumu kupata wenye Elimu ya Kidato cha Nne na sifa zote zilizowekwa. Kwa sasa hivi msisitizo ni kusema kwamba wale watakaoonekana na Vijiji vyao kwamba wanafaa basi tutawachukua lakini kwa Mkataba. Wale ambao wana sifa zinazohitajika watachukuliwa kwa utaratibu wa moja kwa moja kama watumishi wengine wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Pembejeo, mwaka jana imekuwepo hoja ya kuuhamsiha Mfuko wa Pembejeo toka Wizara ya Kilimo na Chakula kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mwaka huu hoja ni kwamba Mfuko huu usimamiwe na TAMISEMI. Kama nilivyoeleza mwaka jana 2003 bado msimamo wa Serikali ni kwamba suala la kuzipa Halmashauri za Wilaya uwezo wa kusimamia Mfuko huu wa Pembejeo kwa madhumuni ya kuwapunguzia wakulima bei ya pembejeo kimsingi ni zuri lakini uzoefu umeonyesha kwamba vyombo ambavyo havina uzoefu wa masuala ya mikopo vimepata matatizo ya kusimamia urejeshaji wa mikopo. *(Makofi)*

Mfano mzuri ni madeni makubwa yaliyolimbikizwa na Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo suala hili linahitaji maandalizi ya kutosha kwa maana ya kuangalia uwezo na taratibu zitakazotumika bila kuziingiza Halmashauri katika madeni kama ilivyokuwa katika Vyama vya Ushirika. Tutawasiliana na Wizara husika ili kuona njia bora zaidi ya kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nieleze kuhusiana na hoja za Msemaji wa Kambi ya Upinzani Dr. Amani Kabourou. Alizungumzia juu ya kukosekana kwa ufanisi katika Wizara ya TAMISEMI. Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika tathmini ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2003/2004 na malengo ya mwaka 2004/2005 ametoa hoja zifuatazo ambazo napenda kuzijibu vilivyo hapa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza madai ya kukosekana ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kisera na kiutendaji ya Wizara ya TAMISEMI. Hoja hii haidhihirishi ukweli wa hali ilivyo kiutendaji katika ofisi yangu. Kama wasemavyo wahenga 'mwenye macho haambiwi aone'. Napenda kumpa changamoto Mheshimiwa Dr. Kabourou arejee tena mafanikio ya wazi ambayo TAMISEMI imepata katika utendaji wake. Naomba kwa ajili ya kuokoa muda nikariri machache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kutekeleza mpango wa MMEM ambao umeiletea nchi hii sifa kubwa inayotokana kwa kiwango kikubwa kabisa na uhamasishaji na usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa mpango huu uliofanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri na katika ngazi za Shule za Msingi. Natambua pia nafasi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuchangia mafanikio hayo. Vile vile Ofisi yangu imehusika na kubuni, kutafsiri na kueneza Sera ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa ambayo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kupeleka madaraka kwa wananchi na kuwapa uwezo zaidi wa kuamua masuala ya maendeleo yao wenyewe. Halmashauri 38 za awamu ya kwanza ya maboresho zimefanikiwa kuweka muundo na mifumo ya uendeshaji ambayo imeleta ufanisi mkubwa katika uzalishaji na utoaji huduma kwa wananchi.

Ushahidi unaonekana kwa wingi wa Halmashauri zilizopata Hati Safi na Hati za Masharti zinazotoka katika kundi la awamu ya kwanza isipokuwa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ambayo imepata Hati Chafu. Ni vizuri tukatambua na kuthamini mafanikio haya kwa njia ya kuwatia moyo viongozi na watendaji katika Halmashauri. Wakati mwaka 2000 ni Halmashauri moja tu iliyopata Hati Safi mwaka 2002 ni Halmashauri 20, haya sio mafanikio madogo ya kubeza. Vile vile utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa Serikali za Mitaa na suala zima la weledi *(awareness creation)* kwa viongozi na wananchi kwa ujumla katika Serikali za Mitaa limefanikiwa. Viongozi ngazi ya Kijiji, Mitaa na Vitongoji wapatao sabini na sita elfu wamekwishapatiwa mafunzo na stadi za uongozi wa utawala bora. Haya ni mafanikio makubwa ambayo wao wenyewe wadau wanakiri kuwa hayajawahi kutolewa toka nchi hii ipate uhuru. Vivyo hivyo kwa Madiwani, Makatibu Tarafa, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wamepatiwa mafunzo na kutunukiwa vyeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uenezaji wa mfumo wa mipango shirikishi jamii katika Halmashauri umetekelezwa, ununuzi wa pikipiki za Makatibu Tarafa wote nchini ni mafanikio makubwa yanayostahili kutambuliwa. Misingi mikubwa ya kupeleka madaraka kwa wananchi ambayo ni kuhamisha madaraka ya kisiasa *(political decentralization),* upelekaji wa raslimali fedha katika ngazi za Halmashauri na Kamati za Shule *(Physical decentralization).* Haya ni mafanikio makubwa ambayo nchi nyingi za Afrika hazijafikia. Vile vile zoezi la kupeleka madaraka ya kusimamia raslimali watu kwenye Halmashauri *(human resources decentralization),* linatekelezwa. Mafanikio mengine mengi kama haya yameonekana katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na madai kwamba majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yanadhihirisha kuwepo kwa ukiritimba unaokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Ni vigumu kukubali kauli hii ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kutokana na kuwepo viashiria vya kutosha kuthibitisha utayari wa Serikali kutekeleza matakwa ya Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuanzia mwaka 1995, Serikali imekuwa ikitekeleza kwa dhati, uadilifu na kwa vitendo zoezi la kubadili Mfumo wa Serikali *(Public Service Rerorm)* ambapo limepunguza majukumu na hivyo muundo wa Serikali kuwa mdogo na wenye ufanisi na tija. Sambamba na hilo, Serikali ilianzisha Mfumo wa Kuboresha Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Program).* Matokeo ya zoezi hili nikupeleka madaraka kwa wananchi kupitia vyombo vya mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, Sheria, kanuni na taratibu za kuhakikisha mazoezi haya yanafanikiwa zimepitishwa na Bunge lako Tukufu kwa mfano Sheria Na. 6 ya mwaka 1999, Sheria Na. 19 ya Mwaka 1997 na Sheria Na. 8 ya Mwaka 2002. Kwa kiwango kikubwa Halmashauri zimeweza kutekeleza majukumu yake chini ya mfumo huo wa uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Kazi ya TAMISEMI Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ni kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake. Huu sio ukiritimba kama Kambi ya Upinzani inavyotaka ieleweke. Napenda kuwasisitizia ndugu zangu wa Kambi ya Upinzani kwamba upelekaji wa madaraka kwa wananchi lazima ujikite katika msingi, nguzo ya dhana ya *subsidiarity* ambayo inatambua kuwepo uhusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na wananchi, *central local relations.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kutokuwepo kwa Wizara mahususi ya Serikali za Mitaa kama ilivyotakiwa na Ibara ya 145 na 146. Hoja hii yenyewe inapingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inampa Rais madaraka ya kuunda Serikali mara baada ya Uchaguzi Mkuu. Katika kutekeleza hilo, Rais anaweza kuunda idadi yoyote ya Wizara ambayo anaona itafanikisha malengo ya utawala wa nchi. Hivyo jukumu la kuunda Wizara ni la Rais mwenyewe na sio Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, itakumbukwa kwamba dhana ya utawala bora imejikita katika misingi ya utawala na sheria ambapo moja ya nguzo zake ni uwajibikaji wa pamoja wa Mawaziri *(Collective Ministerial Responsibility)* katika kutunga, kuamua na kutekeleza sera za Serikali husika. Hivyo basi, madai ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba TAMISEMI imeshabikia Sera za Serikali Kuu badala ya kutetea Serikali za Mitaa sio ya msingi na yanaenda kinyume kabisa na nadharia ya Utawala Bora. Kulikuwa na hoja ya migongano kati ya Madiwani na watendaji wa Halmashauri, hili bahati nzuri, Mheshimiwa Naibu Waziri amelifafanua vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu TAMISEMI haina malengo ya muda mfupi na muda mrefu na kuziachia Halmashauri madaraka katika maeneo yake, kwa hivi sasa Sera na mikakati mbalimbali ya Wizara na Idara zinazojitegemea zinaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 vivyo hivyo Dira ya TAMISEMI inalenga kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo. Kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba TAMISEMI haina kipindi au muda wote tunaongozwa na Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Mojawapo ya Dira ya Taifa ni kutoa madaraka kwa wananchi kwa kuwashirikisha katika kuamua, kupanga na kutekeleza mambo yao wenyewe. Mpango wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa, Sera ya Maendeleo Vijijini na Mpango wa Mkakati wa TAMISEMI vyote vinalenga kutekeleza azma hiyo ya Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya. Kama Naibu Waziri alivyoeleza kwamba hoja zilizotolewa ni nyingi na kuzijibu zote hapa kwa kweli muda uliowekwa hautatosha. Kama tulivyosema, hoja hizi tutaziweka katika jedwali na kutoa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge wote ili tuweze kueleza hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna moja ambalo napenda kuelezea nayo inahusiana na matengenezo ya barabara zilizo chini ya Halmashauri. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii wamezungumzia kwa uchungu hali ya ubovu wa sehemu kubwa wa barabara zilizo chini ya Halmashauri. Ofisi yangu inakubaliana na hoja ya ubovu wa barabara hizo lakini kama ambavyo Ofisi yangu imekuwa ikieleza mara kwa mara katika Bunge lako Tukufu au wakati wa kuwasilisha bajeti ya Wizara kama ninavyofanya hivi sasa wakati wa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge yanayoelekezwa Wizarani kwangu kuhusu ubovu wa barabara nimekuwa nikisisitiza wazi kuwa tatizo la ubovu wa barabara linatokana na uwezo mdogo wa Serikali na mgao wa fedha katika sekta hii ya barabara za Halmashauri. Napenda kutoa takwimu chache zifuatazo. Kwanza ni fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika Halmashauri zinatokana na Fuel Levy ambapo kwa utaratibu uliowekwa na Sheria Na.2 ya mwaka 1998, Halmashauri zinagawiwa asilimia 30 tu ya asilimia 90 siyo ya asilimia 100 ni asilimia 90 ya fedha zote zinazokusanywa chini ya Fuel Levy asilimia 10 inayobaki ya fedha ya Fuel Levy inayokusanywa huelekezwa Wizara ya Ujenzi kugharamia ujenzi wa barabara za mtandao wa Kitaifa na Mikoa. Ofisi yangu haipewi sehemu ya fedha hizi za maendeleo.

Mathalani katika mwaka wa fedha 2002/2003, mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara kwa Halmashauri zilikuwa shilingi bilioni 19.3 ambazo zilitosheleza kutengeneza kilomita 13,727 tu kati ya zaidi ya kilomita 50,000 za mtandao wa barabara za Halmashauri. Hivyo, barabara ambazo hazikupata fedha za matengenezo yoyote katika mtandao huu zilikuwa na urefu wa kilomita 36,000 sawa na asilimia 72.6. Vivyo hivyo, katika mwaka wa fedha 2003/2004, mgao wa Halmashauri ulikuwa shilingi 19.1 ambazo ziliweza kutengeneza kilomita 12,784 kati ya kilomita zaidi ya 50,000 na hivyo kuacha kilomita 37,000 katika hali isiyokuwa ya matengenezo yoyote. Mwaka wa fedha 2004/2005 sasa Halmashauri zimetengewa shilingi 21.8 bilioni kwa ajili ya kutengeneza kilomita 13,868 ambayo ni sawa na asilimia 27 ya mtandao wa barabara zote za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kutokana na takwimu hizo ni kwamba mtandao wa zaidi ya kilomita 38,000 unabaki kila mwaka bila ya fedha za matengenezo na huu ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ndiyo ukweli wa mambo ulivyo. Tatizo la ufinyu wa Bajeti linaathiri ufanisi wa huduma nzuri ya miundo mbinu katika Halmashauri nchini. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge kutegemea kuwa na barabara nzuri katika Majimbo yao kwa kweli wakati mwingine inakuwa vigumu kwa sababu fedha zenyewe zinazotengwa ni kidogo. Tunaweza kutengeneza kiasi tu na sehemu lazima ibaki. Aidha, kwa mujibu wa Sheria Na.2 ya mwaka 1998, fedha zinazokwenda katika Halmashauri kutokana na *Fuel Levy* zina sharti moja kubwa la matumizi kwamba zitumike kwa ajili ya matengenezo *(maintenance)* na sio kwa ajili ya ukarabati wala ujenzi wa barabara mpya, imo katika sheria hiyo. Maombi ya Waheshimiwa Wabunge yameelekezwa kwenye ukarabati wa barabara au ujenzi wa barabara mpya.

Katika mwaka 2004/2005 ofisi yangu imepokea maombi ya fedha za kukarabati na ujenzi wa barabara mpya yenye thamani ya bilioni Sh.15.5 fedha ambazo ofisi yangu haijatengewa katika bajeti hii kama ambavyo mtakuwa mmeona katika bajeti ambayo tunawaomba ipitishwe leo. Hivyo Waheshimiwa Wabunge, bado tatizo la matengenezo la barabara litakuwepo. Nisingependa kuahidi kwamba katika mwaka huu wa fedha sasa barabara zote zitatengenezwa, zitatengenezwa kwa kiwango ambacho fedha zitakuwa zimeidhinishwa katika bajeti tunayoomba.

Kulikuwa na suala la maeneo mapya ya utawala, hoja hii imezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi lakini kwa mujibu wa Ibara ya 2 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, mwenye mamlaka ya kugawa nchi katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengine kwa ajili ya kurahisisha shughuli za utawala na ustawi wa jamii ni Mheshimiwa Rais. Ni kweli maombi mengi ya kugawa maeneo mbalimbali yamekuwa yakipokelewa na kuchambuliwa na ofisi yangu lakini napenda kusema kwamba japokuwa ofisi yangu ingependa kushughulikia maombi yote hayo na kukidhi matakwa ya waombaji lipo tatizo la msingi la kubeba mzigo wa kuanzisha maeneo hayo. Suala la gharama za kuanzisha maeneo mapya nimelieleza katika hotuba yangu, vigezo vya kuanzisha maeneo mapya ni vingi kama vile idadi ya watu, hali ya uchumi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Chiduo kuwa maombi yake ni kweli yalipokelewa na ofisi yangu na ningependa kumhakikishia kwamba pamoja na tafsiri ya hotuba yangu milango ya kushughulikia maombi ya uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala haukufungwa kabisa. Katika hotuba yangu nimeeleza kuwa maeneo mapya ya utawala yataanzishwa pale tu itakapoonekana umuhimu wa kufanya hivyo kwa kuzingatia vigezo nilivyovielezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hoja ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hali hiyo na muda tuliojipangia isingewezekana kujibu hoja zote moja moja hapa Bungeni. Kama nilivyosema tumeandaa jedwali ambalo limeelezea majibu ya hoja zote za Waheshimiwa Wabunge. Lakini la msingi ninalotaka kusema ni kwamba yote yale niliyoyasema kama Naibu Waziri alivyosema hatukukereka, sisi tunaamini mnatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni ukosefu wa mwelekeo kama hatutakubali kwamba haya mliyosema ni ya kweli. Kwa hiyo, jukumu lililopo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba juhudi zinafanywa katika kuyatanzua. Lakini kulingana na uwezo uliopo kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## FUNGU 56 - OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge shughuli za Kamati ndiyo zinaanza tutaanza na kitabu cha pili.

Kif. 1001 - *Administration and General ...* Shs. 2.093,714,500/=

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa dukuduku langu. Kifungu 1001, Kifungu kidogo 250100, Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kwamba Serikali imetoa ahadi ya kuwafidia wananchi wa Kisarawe tangu mwaka 1982, sasa ni miaka ishirini na mbili. Ahadi ile ilikuwa haijatimizwa na kwamba wananchi wale wanahangaika sana aliyekuwa Mbunge marehemu Profesa Kighoma Malima, Mungu amweke mahali pema, amekufa. Aliyekuwa *DC* wakati ule marehemu Seif Bakari, amekufa na Ma-*DC* zaidi ya wanne wamekuja wamepita na hao wote sasa wameondoka wakiwa wameshindwa kupata ufumbuzi wa suala hili. Kwa bahati nzuri waliokuwa Wakuu wa Mikoa ya Pwani wote wanalijua hili suala. Sasa pamekuwa na mawasiliano baina ya mimi, Waziri na Waziri Mkuu na mimi nahesabu kwamba ni agizo kutoka kwa Waziri Mkuu kwa sababu mawasiliano kutoka kwa Waziri Mkuu ni agizo. Namwomba Mheshimiwa Waziri

awahakikishie wananchi wa Kisarawe kupitia Kamati hii hivi sasa na wanasikiliza kwamba deni lile sasa hivi litalipwa katika Bajeti hii, narudia, katika Bajeti hii. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya kujaribu kujibu hoja ya Mheshimiwa Athuman Janguo inayohusiana na fidia ambayo inahitajika wafidiwe wananchi wa Kisarawe. Suala hili ni kweli amewahi kulileta kwangu na agizo lililopo mpaka sasa hivi ni kwamba sisi na Hazina tukae chini tujaribu kuangalia ni jinsi gani litaweza kushughulikiwa ili liweze kufanikiwa. Sasa bado kwa sababu suala hili ndio limejitokeza hivi karibuni wakati tumekwishatengeneza Bajeti itabidi nikae na Hazina ili tuone tutafikia muafaka wa namna gani.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa inaelekea Serikali haijakuwa tayari na mimi nilikuwa nataka niwashawishi wananchi wa Kisarawe wasidai riba. Sasa kama litachukua zaidi ya mwaka huu je, Waziri yupo tayari kuahidi kwamba watalipwa na riba kwa miaka yote hiyo ishirini na mbili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Tutajitahidi lakini nisingeweza kuahidi kuhusiana na riba kwa sababu ni suala linalohusu Wizara ya Fedha na mimi siwezi kuahidi kwa niaba ya Wizara ya Fedha.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tutajitahidi kuhakikisha riba inalipwa au?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kuhakikisha kwamba suala hili linafikiwa muafaka na Wizara ya Fedha ambayo ndiyo ilitakiwa kutoa hizo fedha.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kifungu hicho hicho cha 1001, mshahara wa Waziri. Sina nia ya kutoa shilingi isipokuwa namwomba Waziri atoe ufafanuzi kuhusu mvutano uliopo unaowahusu Wabunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam kutokuingia katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa kuwa kutokuingia kwetu katika Halmashauri ya Jiji kunasababisha tusijue mambo mengi ambayo yanatuhusu sisi tuliochaguliwa na akina mama pale, Wabunge wa Majimbo wanaingia, sisi hatuingii. Hata hivyo nimeona niulizie hapa kwa sababu tayari sisi Wabunge wa Viti Maalum tumeshahangaika sana na mwisho tulimwona yeye Waziri na alituhakikishia kwamba atatumia madaraka aliyokuwa nayo aliyopewa na sheria kumwandikia Mkurugenzi kwamba na sisi tuwe Madiwani katika Halmashauri ya Jiji. Waziri wetu ni mwadilifu sana na ni makini sana. Naamini barua ameandika. Tatizo lipo huko, sasa namwomba Waziri atoe kauli isikike huko kwa yale ambayo aliyaandika kwenye ile barua. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimefurahi sana kwa hawa wawili waliotangulia wametaka ufafanuzi na siyo hotuba. Kwa hiyo, kwa wale wanaoendelea wafuate mfano huu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala la watumishi Waheshimiwa Wabunge katika Halmashauri ya Jiji liliwahi kuletwa. Suala hili lilianzia katika Manispaa na tulitoa maelekezo kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum lazima nao wawe wanaingia katika Halmashauri za Manispaa. Sasa tulikuwa tunaendelea na *process* ya kuwawezesha kuingia katika Halmashauri ya Jiji, bado tunaendelea.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na kwa hiyo naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba alikubaliana nasi na alisema kuwa ameshaandika barua ya kuhakikisha kuwa tunaingia katika vikao hivyo na hata wale wanasiasa waliokuwepo katika Halmashauri ya Jiji wanaona kuwa kuna tatizo, Meya na Madiwani wengine pamoja na Wabunge wenzetu wanaona ni tatizo, sisi inatubidi tuwe tunasoma kwenye magazeti mambo ambayo inabidi tuyajue kupitia kwenye vikao. Kwa hiyo, ile kauli aliyotupa Waziri katika kikao chetu kile tunaomba aizingatie sitaki kusema zaidi ya hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hili hataki jibu anataka ulizingatie.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu hicho hicho cha 1001, mshahara wa Waziri. Mimi napenda kupata ufafanuzi, ni jambo ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi kuhusu posho za Madiwani pamoja na mishahara ya Madiwani.

Ukizingatia kwamba Halmashauri zinaachana, zingine zina mapato makubwa na zingine hazina mapato makubwa. Halafu ukizingatia kwamba Madiwani ndio wanaofanya kazi, lakini Wizara hii haijalitambua vizuri kutokana na posho wanazopata. Sasa napenda hapa leo nipate ufafanuzi kamili kuhusu hao Madiwani, atawaongezea ili kusudi nao wafanye kazi kwa roho moja na kwa ufanisi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala hilo limejitokeza mara nyingi, lakini mara ya mwisho tulipokutana na uongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Serikali za Mitaa*(ALAT)* tulikubaliana kwamba *ALAT* walifanyie kazi na halafu tukae pamoja. Bado wanalifanyia kazi na mara likishakamilika basi litatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu yake mazurim lakini hiyo *ALAT* mimi nitangoja mpaka lini na hao Madiwani watangoja mpaka lini? Sasa hivi tunakwenda kwenye uchaguzi ambao wao ndio wanahusika zaidi. Mimi naomba Serikali itamke vizuri kwamba hiyo *ALAT* itamaliza lini kisha jibu lipatikane kwa hao ndugu zangu Madiwani kote nchini ili nao wafanye kazi zao kwa ufanisi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ushirikiano mzuri sana na *ALAT*. *ALAT* ni Jumuiya ya Serikali za Mitaa zote, ni yao, siyo ya Serikali, wao ndio wamekubali walifanyie uchambuzi, mara watakapotuletea uchambuzi wao tutalifanyia

kazi lakini kwa sasa hivi siwezi nikasema itakuwa baada ya mwezi mmoja kwa sababu siwezi kuwashurutisha.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jana wakati nikichangia nilieleza kwenye barabara zangu kwamba kuna sababu mbili ambazo zimepunguza uwezo wa Wilaya kuzitengeneza na kwa hiyo zimekaa kwa muda mrefu na katika maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri akijibu hilo la mwisho kuhusu uwezo mdogo wa kifedha kutokana na zile tunazozitenga hapa na amefafanua vizuri na nadhani kila mmoja ameelewa. Sasa nilichomweleza jana kwa mujibu wa takwimu alizozitoa kwamba katika Bajeti hii tutatenga bilioni 21.8.

Sasa nilitaka kujua kwa sababu Serikali ni kitu kimoja zile *Euro* milioni 10 ambazo ni zaidi ya bilioni 11 za Mfuko wa *STABEX* ambazo nadhani tukisikilizana vizuri ni zaidi ya nusu ya hizi zilizotengwa kwamba zikipatikana zile zinaweza kusaidia hizi barabara kutengenezwa. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba fedha hizo za *STABEX* zipo kwenye hizi anazosema kwamba zinatengeneza *network* za barabara ambazo zipo chini yake na kama hakubaliani na hilo na wala hazipo kokote je, yupo tayari sasa nimwambie aache kulalamika kwamba tumetenga kidogo, nimweleze zilipo kwa Wizara ya Kilimo ili azidai na Waziri Mkuu atusaidie hapa kwamba hela hizo zije na tuzione kwenye Bajeti ya mwaka huu ili ziweze kutengeneza barabara za kwangu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha shilingi bilioni 21 zinazotajwa katika kitabu hiki haziunganishi na fedha za *STABEX,* siyo sehemu ya fedha hizo. Kwa hiyo, za *STABEX* kama Waziri wa Kilimo alivyoeleza zipo katika fungu lingine na matumizi yake kwa kweli ni tofauti kabisa na haya tunayozungumzia ya matengenezo ya barabara za Serikali za Mitaa.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri na wewe huwa ni mjumbe humu. Fedha hizo za *STABEX* zimetengwa kwa ajili ya *feeder roads* nadhani tunaposema *feeder roads* ni kwa ajili ya barabara hizo tunazozisema ambazo ziko chini ya ofisi yake. Sasa kusema kwamba hazipo kwenye mpango huo mimi sijui ni mpango upi anaousema kwa sababu hizi ni barabara ambazo zipo chini ya TAMISEMI. Sasa mpaka hapo sijui anaweza akasahihisha huo usemi wake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa ameeleza vizuri. Ameeleza zile bilioni 21 zilizotengwa hazitokani na *STABEX,* zile zinatokana na fedha za Mfuko wa Barabara ambazo katika mwaka huu zitakusanywa bilioni 71.45 na bilioni 21 ambazo ni asilimia 30 ya fedha hizo zinakwenda Tawala za Mikoa, zingine zinakwenda Wizara ya Ujenzi na zingine zinakwenda *TANROAD.* Kwa hiyo zile anazozingumzia za *STABEX,* Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alieleza vizuri juzi na alisema atakuja kueleza pia kwenye bajeti yake.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa ajaribu kusubiri ili kusudi apate maelezo mazuri ya fedha zile. Kwa kumbukumbu zangu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alieleza kwamba zile fedha zinatolewa na *European Union* na kabla ya kutumika *European Union* walikubali kuteua *consultant* ambaye atazipitia barabara zote zinazozalisha kahawa ili kusudi yale makubaliano yatakapokuwa yanakamilika zile fedha ndipo zitatolewa Serikalini.

Kwa hiyo, Serikali ingekuwa ya ajabu sana kuanza kupanga fedha ambazo bado haijapewa. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi ni katika kifungu hicho hicho. Suala langu lilikuwa linakaribia kufanana na la Sophia lakini Sophia Simba aka-*specify* kwake kule lakini kulipotokea suala lake ndani ya Bunge tulijitahidi Wabunge wanawake na sisi pamoja na Naibu Waziri tukakubaliana kweli sheria imemwondoa Mbunge wa Viti Maalum katika Kamati ya Fedha. Kwa hiyo, wale ma-*DED* ambao walikuwa wanawaweka walikuwa wanakwenda kinyume cha utaratibu na kweli na ma-*DED* wengine waliposikia hotuba hii tukaondolewa.

Lakini tulizungumza naye kwamba basi tunaomba Serikali ifanye utaratibu hii sheria irudishwe kwa sababu kwa mtindo wetu huu wa kawaida wa Bunge ni mara chache sana Wabunge wanaleta *private motion.* Kwa hiyo, tukamwomba akasema atalifuatilia sasa naomba atuambie amefikia wapi, kwa kweli wanawake Viti Maalum wanawakilisha asilimia hamsini na moja ya wanawake ambao wanahitajika katika maandalizi haya. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge lakini sheria hizo hivi sasa zinafanyiwa mapitio. Kwa hiyo, hiyo hili naamini litarekebishwa.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niko katika kifungu hicho hicho. Naomba nipate maelezo mawili, la kwanza mwaka jana 2003 niliuliza hapa kwamba Mji wa Shinyanga sasa hivi ni Manispaa na Manispaa nyingi zipo katika *USRP* na wakaniahidi kwamba wangefanya kazi hiyo mwaka huu, lakini kwenye Bajeti sikuona. Je, barabara hizo zitakuwepo kweli kwenye *USRP?* Walionyesha kwenye kitabu chao cha majibu ya Wabunge kwamba hii kazi itafanyika mwaka huu 2004 lakini nimetafuta mahali sijapaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba mwaka jana niliahidiwa na Wizara kwamba pale Shinyanga kuna barabara tatu zitawekewa lami kilomita 1.8 yaani *Government Road,* barabara ya Mkoani, *Police Road* pamoja na barabara ya Mkuu wa Mkoa. Lakini na bahati nzuri nilipofuatilia pale ofisini kwa TAMISEMI nikaonyeshwa kwamba hela zilikuwa zimetengwa lakini mpaka sasa hivi kazi hiyo haikufanyika, kumekuwa na tatizo gani? Kwa hiyo, naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za barabara kwa ajili ya Manispaa ya Shinyanga, fedha zilizoahidiwa kwa ajili ya maendeleo Mjini hazikutolewa kwa mwaka huo wa fedha wa 2003/2004. Kulingana na mihadi ya *European Union,* fedha hizo sasa zitatolewa mwaka huu wa fedha 2004/2005. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lile lingine la pili ama amekusanya yote. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Derefa unaonaje amekusanya yote au bado hajajibu? Nadhani ameridhika kwa hiyo tunaendelea.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ni hicho hicho kuhusu mshahara wa Waziri. Katika kuchangia hoja ya Waziri huyu nilieza tatizo la kimsingi la kukua kwa Miji na Vijiji vyetu na nikatoa mfano kwamba mwaka huu Vijiji vikubwa 88 vitakuwa Miji Midogo na kwa mtazamo huu ni kwamba mwakani tutakuwa na Vijiji vingi vikubwa ambavyo navyo vitaomba kuwa Miji Midogo.

Nikashauri kwamba ni vizuri basi tuwe na utaratibu wa kuvipanga Vijiji katika ngazi mbalimbali na kila ngazi iwe na sifa na kila mwaka kuwe na ukaguzi wa Vijiji hivi kwa lengo la kuvipandisha kwenye ngazi fulani ili kuepuka utaratibu wa sasa wa kukua kwa Miji yetu kiholela.

Nilidhani pendekezo hilo lilikuwa la kimsingi sana katika kuendeleza nchi yetu na Vijiji vyetu na nikauliza hali yetu ya baadaye itakuwaje. Je, Waziri haoni kwamba ni muhimu kupokea mawazo hayo ili kuzuia hali hivi inavyokwenda sasa? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nakubaliana na Mheshimiwa Jackson Makwetta, suala hili ni kweli amelieleza lakini ni suala la kufanyia uchambuzi na kulifanyia kazi. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 1001,* mshahara wa Waziri. Kwanza nashukuru kwa maelezo ya Naibu Waziri kuhusu zile *cheques* za MMEM zilizo-*bounce* na kwa *back benchers* wenzangu kwa yale tuliyozungumza ametoa maelezo kwamba ukaguzi umefanyika na taarifa inaandaliwa na nadhani ni hatua ya kuridhisha.

Sasa nilitaka kuelewa kama ukaguzi ulikuwa ufanyike tu kwa hizo *cheques* za MMEM au pamoja na fedha zote zilizotumika vibaya kama shilingi milioni 50 za maji, milioni 90 zilikuwa zinunue lori badala yake zikanunuliwa Toyota au ni hizo fedha za MMEM?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo inaelekea hizo *cheque* zilizo-*bounce* kwenye robo ya pili, zitachota fedha kwenye robo ya tatu, Serikali ikidhibitisha hivyo, je, wananchi wa Simanjiro watarudishiwa fedha hizo na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba maelezo, nilivyosoma katika hotuba ya Mheshimiwa Rais kuna maagizo aliyoyatoa, sasa ni miaka miwili, nayo yapo kati ya haya yatakayoshughulikiwa na timu hiyo au haya hayashughulikiwi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, timu iliyokwenda Simanjiro inafanya ukaguzi wa akaunti zote siyo ya MMEM peke yake. Vile vile kuhusiana na fedha kama itabainika kwamba fedha hizo zimeibiwa, mimi naamini kwamba sheria itachukua mkondo wake na Serikali inajua kitu gani kitafanyika katika hali hiyo.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado la tatu lile ambalo Rais ameagiza lishughulikiwe haraka. Mapungufu yaliyoonekana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema tunasubiri taarifa iletwe. Ikiletwa hiyo taarifa tunajua kuna mapungufu gani na wale wote wanaostahili kuchukuliwa hatua watachukuliwa hatua kulingana na taarifa tunayoisubiri hivi sasa.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho. Naomba tu Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa sababu sina raha, nimeshakwenda kwenye Kijiji kimoja wakakataa kufanya mkutano na mimi wakasema mpeni kadi zake za CCM tu huyo bwana aondoke. Nikamwagiwa kadi za CCM kama mia mbili hivi. Tatizo lenyewe ni kwamba mwaka 2001, tuliomba kuandikisha Vijiji, tukapewa namba, tukaelezwa tusubiri Hati.

Mwaka 2003, tukapeleka maombi mengine tukapewa namba, wakatueleza tusubiri Hati. Sasa wanaendelea kusubiri Hati hadi wanachoka mpaka sasa wanasema mpeni kadi zake za CCM ili aondoke na wakaniambia ukienda huko kama hukurudisha vyeti usije. Sasa nilikuwa namwomba Waziri aidha anisaidie kutoa kauli ili nipokelewe kule au anipe hivyo vyeti basi nikawakabidhi, naomba anisaidie japo mojawapo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya Bajeti nilisema masuala yote haya tunatazamia kuyakamilisha kabla ya mwezi Agosti, 2004 ikiwa ni pamoja na tatizo la Vijiji vyake. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashika kifungu hicho hicho cha 1001, mshahara wa Waziri. Wakati nikichangia katika hoja ya Waziri niliomba majibu katika mambo mawili.

La kwanza, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutengeneza barabara ya kwenda milimani kule Same kutoka Makanya-Suji- Malindi na Suji-Gonjanza ambayo Wizara

yake ilituma Wahandisi wakaenda, wakafanya makisio. Sasa muda umepita na kipindi cha Mheshimiwa Rais kinakwisha na ahadi ile haijatekelezwa na hakuna majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kule katika Jimbo langu taarifa za Mheshimiwa Waziri zinasema kwamba ofisi yangu ilipewa fedha za mapazia na *stationary* ambazo si kweli na yenyewe niliomba kupata majibu ni kwa sababu gani? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwamba Mheshimiwa Singo amelikumbusha hili kuhusiana na ahadi ya Rais na nafurahi kwamba anakiri kwamba tumepeleka Wahandisi kwenda kukagua. Sasa kinachogoma hapa ni fedha, tutaangalia katika mwaka huu kati ya fedha hizi tunazoomba katika fungu la barabara ikiwezekana ahadi hii tutaona jinsi gani tutaitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la mapazia katika ofisi yake nitaomba nifuatilie halafu nitampa jibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anataka pia kusaidia majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alitaka pia kusaidia majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongeze tu kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu lile suala la ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kwa sababu lile lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais alipotembelea katika sehemu hiyo ya barabara ya Makanya hadi Isuji na kwa kuzingatia kwamba Serikali ni moja sisi Wizara ya Ujenzi tumetenga shilingi milioni 50. Kwa hiyo, Mheshimiwa John Singo ataziona katika Bajeti yetu hiyo na tumeshirikiana sana na wenzetu wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana pamoja na kwamba hukuniona vyema lakini na mimi nilisimama. Kifungu hicho hicho cha mshahara wa Waziri fungu 1001. Nilikuwa nataka kupata maelezo. Nina tatizo ambalo niliandika kwa maandishi kwa Waziri wa Fedha, niliandika kwa maandishi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na katika Wizara hii nimeandika kwa maandishi lakini bahati mbaya wote hawajawahi kunijibu. Sasa ni vyema kwa sababu mhusika mkuu ni Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa , ajaribu kunisaidia.

Wakati tunaanzisha sheria ya *Local Government* pamoja na *Regional Administration* tulibainisha kwamba zote ni Serikali moja lakini yupo huyu Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali ambao kila Mkoa wapo. Lakini tatizo linalojitokeza haruhusiwi kukagua mali za Halmashauri anaenda kukagua kwenye Halmashauri lakini anaenda kukagua kwa *DAS.* Mimi ninavyofahamu asilimia 70 au 90 ya fedha nyingi zinaenda kwenye Halmashauri siyo Serikalini, Serikalini ni vitu vichache sana vilivyoko. Sasa Mheshimiwa Waziri haoni ni busara au ni wakati muafaka kubadilisha hiyo sheria

ili imfanye huyu Mhakiki Mali Mkuu wa Serikali akague na mali za Halmashauri? Ndiyo ufafanuzi wangu tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kutoa maelezo kidogo kuhusiana na jambo hili. Kwa kifupi hili ni suala tu la kisheria na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anatoa hotuba yake hapa alisema haoni yeye tatizo kwa sababu halipunguzii wala kumwongezea kitu. Kwa hiyo, tumeishawaagiza wenzetu wa sheria hapa wafanye mawasiliano na Hazina kwa kushirikiana na *Attorney General* ili tuone marekebisho yatakayohitajika ili kuweza kuboresha hili ambalo analisema.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge niliwauliza wote mkasimama nikawa nawaorodhesha tulijitahidi sana kuwaangalia kwa makini.

**MBUNGE FULANI:** Bahati mbaya!

**MWENYEKITI:** Sasa kwa hili tunaendelea kuna vifungu vingi huko mbele nitakupa nafasi.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... Shs. 165,498,900/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... .. Shs. 174,019,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge endelee kwa hilo sasa.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 1003 kwa maana ya *Planning* nina hoja mbili. Hoja ya kwanza ni kwamba sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Tarime tumeleta maombi kwa Wizara kwamba sasa Mji wetu wa Tarime tuna watu wapatao 65,000 na kwamba kwa taratibu zote na vigezo tunastahili tuwe Halmashauri ya Mji. Toka tulete maombi sasa imeishapita muda mrefu na hakuna *action* yoyote inayochukuliwa hata kukiri tu kwamba hayo maombi yetu yalikwishapokelewa Wizarani na kwamba tutegemee *action* katika muda gani. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba hayo majibu anategemea kutupa kwa muda gani na anatupa lini. Halafu swali la pili, nataka kuzungumzia kwa maana ya Wizara ya TAMISEMI na kwa maana ya Waziri wa Nchi na kwa maana kwamba Waziri hasa kabisa wa Wizara ni Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais katika kampeni zake mwaka 2000 alipokuwa Tarime aliahidi kwamba kama CCM inashinda atahakikisha kwamba wakati akiwa Rais Mji wetu wa Tarime utapata maji. Sasa huu ni mwaka 2004 tumebakiza miezi tisa mpaka mwaka 2005 na kipindi cha Mheshimiwa Rais kitakuwa kimekwisha na hiyo ahadi haijatekelezeka wala haina dalili za kutekelezeka. Sasa mimi nilikuwa nataka tu kupata maelezo. Kama Mheshimiwa Rais kwa maana kwamba mtu anayewapa Waheshimiwa Mawaziri wote kazi na kwa maana

kwamba wanatumika kufuatilia zile ahadi zake. Sasa ile ahadi aliyotupa ilikuwa ni geresha au kweli ilikuwa ni ahadi ya kwamba Mji wetu utapata maji na sasa kama utapata maji utayapata lini wakati wa uhai wake wa Urais au baada ya uhai wake wa Urais kwisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Tarime kufanywa uwe Mji limetufikia na wataalamu wetu wanaendelea na uchambuzi ni maombi yameletwa kwa hiyo yanafanyiwa kazi. Hili la maji ndiyo kwanza nalisikia kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi. Nimelichukua tutawasiliana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashangaa kwa majibu hayo. Kwa sababu hii ndiyo Wizara yake na aliahidi na kama Rais sasa alishatoa ahadi zake na Mheshimiwa Waziri haelewi kwamba Rais alitoa ahadi zake, Rais akitoa ahadi tumfuate nani ili kusudi tuelewe kwamba hizi ahadi zilitolewa na Rais kama Mheshimiwa Waziri haelewi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ndiyo ni kweli Mheshimiwa Rais anaahidi na anatoa maelekezo. Ahadi hiyo aliitoa akiwa Tarime, ipo Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo inayoshughulika na maji. Nilichosema ni kwamba nitalipeleka suala hili Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo lazima itakuwa na rekodi nalo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ufafanuzi zaidi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana. Nataka niongezee tu kusema kwamba ahadi hizi zinategemeana sana na uwezo wa Serikali. Lakini pia akitoa ahadi Rais ni Rais ametoa ahadi kwa hiyo Rais ni Taasisi. Sasa suala la kwamba Rais ataondoka hili lisimsumbue Mheshimiwa Mbunge, ahadi ya Rais kama imetolewa iko kwenye rekodi na itafuatiliwa na itatekelezwa. Ziko ahadi nyingi sana ambazo zimetolewa labda miaka 10 au 15 iliyopita lakini zinatekelezwa. Kwa hiyo, ahadi zitaendelea kutekelezwa wala tusiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

| | |
|---|---|
| Kif. 2001 - *Regional Coordination Division ... ... ...* | 22,436,155,400/= |
| Kif. 2002 - *Local Government Coordination Division ...* | 8,363,926,600/= |
| Kif. 3001 - *Institutional Development Division ...* | 3,370,693,100/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Kanuni inatutaka kwa Mikoa tunahoji moja kwa moja kwa Mkoa wote.

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha ... .. 17,752,441,300/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 71 - Mkoa wa Pwani ... 14,286,848,700/=

**MHE. ABDULKARIM E. HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi katika fungu hilo lililotamkwa sasa hivi Katibu ukurasa 6 Mkoa wa Pwani nilikuwa nataka nipate maelezo zaidi kuhusu ukarabati wa nyumba ya *DC* Mafia Mkoa wa Pwani. Inawezekana si mtaalamu mzuri wa mambo ya ujenzi. Lakini ukiangalia gharama zilizotumika kwenye nyumba ile ni kubwa mno milioni sitini na kitu kwa kuezeka paa tu la nyumba pamoja na kupaka rangi. Halafu ziombwe tena milioni 15 nasikia nasema kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa umeme katika nyumba hiyo. Sasa ukilinganisha hata ile nyumba iliyokuwa imetolewa picha na *Celtel* ya milioni 60 ni nzuri inapendeza lakini ukienda kuangalia huo ukarabati uliofanyika utalia. Sasa basi nilikuwa naomba nipate maelezo tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni jinsi fedha hizo zilitumika ili pia na wananchi waweze kufahamu kwa sababu sasa tumeishaanza kutukanwa mpaka kwenye magazeti. Halafu la pili, hivi sasa *DC* hakai pale anakaa katika hoteli leo mwaka, fedha zile atakazokuwa analipa kule katika hoteli ni gharama ya nani, ya Serikali au Mkandarasi aliyechelewesha kumalizia kwa haraka iwezekanavyo nyumba ile. Nilikuwa naomba nipate maelezo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kama nilivyosema wakati nachangia hoja hii nimejaribu kuonyesha tu kwamba maelezo tuliyonayo yanaonyesha hatua zilizochukuliwa tangu tuanze ukarabati na mpaka tulipofika. Lakini nikasema inawezekana pengine kuna *details* zingine ambazo hazikutolewa ambazo nilimwomba Dr. Zainab Gama kwamba tukae tujaribu kumpa tuliyonayo, lakini kwa sababu limeulizwa labda niseme wazi wazi hali ikoje. Halafu labda Waheshimiwa Wabunge watajua la kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa nyumba hiyo ya *DC* ulianza mwaka 2002/2003 na zilitengwa fedha kiasi cha shilingi 32,500,000/= . Lakini gharama ya tender ilikuwa ni milioni 30,700,000/=, fedha zilizotumika ilikuwa ni milioni 27,639,829/= na ambazo amelipwa Mkandarasi ilikuwa ni shilingi 1,840,171/= ambazo alilipwa kama msimamizi kwa maana ya consultant na kufanya jumla ya malipo yote kuwa shilingi 29,880,000/=. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 zikatengwa tena kiasi cha shilingi milioni 30.4 kiasi hiki ilikuwa ni kwa ajili ya kumalizia sehemu ambazo zilikuwa zimebakia kwenye nyumba hiyo na ujenzi wa Ofisi ya *DC.* Sasa *tender* imetolewa kwa Mkandarasi kiasi cha shilingi milioni 33 ya zabuni hiyo na hadi mwezi Juni 2004 kiasi cha shilingi milioni 20,163,899/= zimelipwa kwa mkandarasi na kama nilivyosema, tukasema kiasi hicho kimetosheleza karibu asilimia 90. Sasa suala kulipiwa hoteli uongozi wa Mkoa hauna taarifa juu ya jambo hili. Kwa sababu *DC* aliambiwa akae kwenye *floor* moja kwa sababu walikuwa wanatengeza kwa awamu. Sasa kama aliamua yeye mwenyewe kwenda kukaa kwenye hoteli hiyo siyo *business* tena ya Mkoa wala Serikali na wala hatutawajibika kwa ajili ya jambo hilo. Kwa hiyo, naomba tu kusema kwamba maelezo haya ni kwa maana ya kuweka jambo hili wazi. Lakini kwa

hisia zilizopo tutamwomba Mheshimiwa Waziri basi kama hapana budi tuunde timu iende ikajiridhishe na jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdulkarim Shah ndiye alisimama kwa hoja hii. Hapana tafadhali siyo utaratibu na tumejiwekea utaratibu.

**MHE. ABDULKARIM E. HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana sana. Kwa sababu naamini Serikali haina nia mbaya kwa mambo kama hayo, lakini kuna watu ambao ndiyo tuna wasiwasi wanaofanya itukanwe Serikali yetu na viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa mpango huu aliosema mwisho naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri au Wizara itusaidie haraka iwezekanavyo iunde Tume ndogo au Tume iende Mafia haraka ikaangalie hizo milioni 60 maana zinakaribia milioni 60 wakaangalie kazi iliyofanyika sasa hivi kwa sababu madirisha yake ya nyumba ni ya mbao.

Sasa yametengenezwa toka enzi ya Waingereza ya luva walahi wamechukua luva zile ambazo zimebomoka wameenda kuziweka kwa misumari aibu na nyumba inavuja. Hivi ninavyowambia mvua ya juzi nyumba *ceiling* bodi zimeishaharibika. Kwa hiyo, nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutusaidia kwenda kuunda hiyo Tume haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Amesimama tu kukubali hana hoja ya kuunda hiyo Tume. Kwa hiyo tunaendelea.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge narudia tena tunajiwekea utaratibu. Litakapotamkwa fungu kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye anataka kuchangia au kuuliza asimame ili tutunze rekodi. Kwa hiyo, tunaendelea.

Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma ... 20, 877,578,100/=
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa ... ... ... 22,443,246,800/=
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma ... 16,406,051,400/=
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro ... 25,527,256,100/=
Fungu 76 - Mkoa wa Lindi ... ... ... 12,053,469,000/=
Fungu 77 - Mkoa wa Mara ... ... 19,483,766,000/=
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya ... 30,188,821,300/=
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro ... 21,763,718,300/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara ... ...Shs. 16,595,670, 800/=

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka niseme kwa fungu hili nilikuwa nimezungumza wakati wa kutoa mchango wangu kuhusiana na fedha inayotengwa na Wizara hii juu ya ujenzi wa nyumba wa *DC* sikupata maelezo yoyote kuhusiana na jambo hili kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza kwa kirefu sikupata kusikia akilitaja jambo hili. Nazungumza hili na ninaliunganisha na tatizo tulilonalo la Mheshimiwa Mbunge na yeye kupata mahali pa kufanyia kazi. Maana kwa sasa hivi mimi ofisi yangu ni gari langu na briefcase yangu. Sasa nauliza fedha hizi shilingi milioni 73 zilizokuwa zimetengwa kwa hii bajeti ambayo itakwisha baada ya siku nne kutoka leo, zilikuwa zimetengwa kwa maana tujenge ofisi ya *DC* na sasa bajeti hii tunapewa shilingi milioni 110 zingine. Hizi za kwanza shilingi milioni 73 ziko wapi na amekabidhiwa nani na kazi hiyo inafanyika wapi? Sasa kama hizi milioni 73 za mwanzo hazijafanya kazi tunayoiona, hizi milioni 110 tunazopangiwa leo zinataka kuelekezwa wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuahidi kwamba hizo milioni 73 tutazifanyia kazi tujue zimekwenda wapi.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vilevile nipate ufafanuzi. Katika mchango wangu niligusia kuhusu Kituo cha Afya cha Mang'aka ambacho licha ya kwamba majengo yake yapo ya kutosha kwa karibu miaka miwili hivi sasa lakini Kituo hiki cha Afya hakijaanza kufanya kazi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaniambia Kituo hiki kitaanza kufanya kazi lini kama Kituo cha Afya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalifanyia kazi na kuhakikisha kwamba Kituo hicho kinafanya kazi katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza ... 29,377,811,700/=
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma ... 16,797,487,100/=
Fungu83 - Mkoa wa Shinyanga ... 26,912,094,900/=
Fungu 84 - Mkoa wa Singida ... ... .13,600,499,400/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 85 - Mkoa wa Tabora ... 18,877,169,700/=

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Fungu la Mkoa wa Tabora nataka kujua tu sina tatizo la ofisi katika Jimbo langu lakini wenzangu wana matatizo ya Ofisi. Ninachotaka kujua ni juu ya fedha zinazotumwa katika Mkoa wa Tabora za matumizi ya ofisi ya Mbunge zinapitia kwenye fungu gani katika fungu hili au kuna fungu lingine ambapo zinapitia fedha za matumizi ya ofisi ya Mbunge. Kwa sababu kwa uzoefu tulionao Mkoa wa Tabora hazijawahi kutolewa hata

senti tano tangu tumeingia Ubunge mwaka 2000. Je, ni kifungu gani ambacho fedha hizo zinatumwa kwenye Ofisi za Wakuu wetu wa Mikoa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Mheshimiwa Mbunge huwa zinatengwa katika fungu la *RAS* na baada ya hapo zinapelekwa Wilayani. Sasa kama zilikuwa hazijapatikana basi tunaomba tulifanyie kazi suala hilo ili tujue kwa nini kwa muda wote huu kulikuwa hakuna fedha zinazotengwa.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 86 - Mkoa wa Tanga ... 23,224,573,800/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 87 - Mkoa Kagera ... ... 21, 825,683,000/=

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa naomba kuuliza kuhusu fedha hizi zilizotolewa kwa ajili ya matengenezo ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Inaonekana kila Wilaya fedha ilibaki na ninapoangalia shughuli zilizofanyika sijui waliona ni sababu gani ya kubakiza hizo fedha wakati baadhi ya ofisi ninazozijua zina viti vitatu na meza moja. Je, huyu Mheshimiwa Mbunge sasa ni mtu wa watu, watu wanaweza kuja wengi pengine anaweza kuwa na kikao.

Sasa hizo fedha zilizobaki zinarudi au zitaendelea kuwepo ili zitumike au ni vipi. Kwa sababu naona matumizi ni tofauti tofauti Mikoa mingine wamewekewa *computer* hata simu sasa je, kuna vigezo gani vya kutengeneza hizo ofisi za Waheshimiwa Wabunge ili kiwe kigezo kimoja katika Wilaya zote na Mikoa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiutaratibu fedha za Serikali zikibaki zinarudi Hazina. Sasa kwa nini hazikutumika itabidi tutafute imekuwa kuwaje? Lakini vile vile ni kwamba suala hili linashughulikiwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu jinsi gani ofisi za Waheshimiwa Wabunge sasa zitakuwa zinafanyiwa utaratibu. Kwa hiyo, litafanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Fungu hilo la Mkoa wa Kagera Mheshimiwa Elizabeth Batenga bado hajaridhika.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri hakumaliza kabisa kujibu swali langu. Ni vigezo gani au hali ya ofisi inatakiwa ionekaneje yaani *standard* za ofisi za Waheshimiwa Wabunge ili kusionekane kuna tofauti tofauti kati ya Wilaya na Wilaya na Mkoa kwa Mkoa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema suala hili sasa linafanyiwa kazi ili tujue *standard* zinakuwa vipi, likikamilika naamini ndiyo tutakuwa na *standard* kwa wote.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 88-Mkoa wa Dar es Salaam..Shs.24,287,646,600/=

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Fungu hili la 88 Mkoa wa Dar es Salaam mimi ninazungumzia upande wa ofisi ya Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mimi nimekuwa Mbunge nimeikuta ofisi lakini kuna gharama ambazo nilitumia kufanya matengenezo katika ofisi ile yapatayo shilingi 800,000/= nilikwishapeleka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa maana ya RAS ili niweze kurejeshewa fedha zangu toka mwaka 2000 lakini bado hazijarejeshwa. Kwa mwaka jana Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imenunua kiti kimoja cha Mbunge pamoja na kabati la kuweka ma-file. Lakini jana nimeona kwenye karatasi yao ambayo wametutumia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba zimetumika milioni moja na kitu kwa ajili ya ofisi ya Mbunge Jimbo la Temeke.

Lakini lingine ni kuhusu matumizi ya ofisi, sisi kule Temeke hatupati matumizi yoyote bali huwa tunachangia hadi umeme. Kwa hiyo nilikuwa naomba kujua Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini fedha zangu ambazo nilitumia kufanyia matengenezo zitalipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Mheshimiwa Waziri aniambie sasa tutapata wapi hizi fedha za matumizi ya ofisi. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu fedha zake alizotumia. Matumizi ya fedha za Serikali kuna utaratibu, sijui kama alipata idhini na kama alipata idhini sioni sababu gani asirudishiwe fedha hizo. Lakini kwa sababu hili suala limejitokeza sasa hivi tukimaliza hapa tutawasiliana na Dar es salaam halafu tutampatia jibu. Vile vile kuhusiana na suala la matumizi tutapata jibu kutoka kwenye Mkoa wake halafu tutamwasilishia.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa ... 14,022,166,000/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 95 - Mkoa wa Manyara ..... 13,936,846,800/=

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Simanjiro ni Wilaya mpya, nyumba ya Mkuu wa Wilaya imejengwa na kupauliwa na imesimama hivyo kwa karibu miaka 7 sasa. Hiyo nyumba ingemalizika ingekuwa ni nyumba ya kuishi *DC* na ingekuwa *Rest House.* Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia hiyo nyumba kwa sababu inazidi sasa kuchakaa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itafuatilia suala hilo na tutampatia majibu Mheshimiwa Mbunge.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 56 – OFISI YA RAIS, TAMISEMI**

Kif. 2002 - *Local Government Coordination Division ...* 140,795,026,200/=.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilipokuwa nachangia. *I mean vote 2002 PEDP.* Nilisema kwamba MMEM wananchi walihamasika sana nayo mpaka wakajenga sambamba madarasa pamoja na nyumba za Walimu.

Lakini kuna wakati fulani, wakati ambapo Halmashauri zilizotajwa kwamba hazikutumia fedha ya MMEM ambayo imepelekwa wakaja kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu wakaitwa. Mkurugenzi wa Wilaya aliuliza swali hivi hela hiyo uliitumia namna gani. Akasema yeye alitumia hela ndogo ile kwa kujenga madarasa na nyumba za Walimu. Akaambiwa ulipata wapi idhini.

Sasa tangu siku ile akaogopa. Basi mpaka leo Wilaya ya Bariadi kuna maboma 500 ya nyumba za Walimu ambazo bado hazijakamilika. Nikasema asubuhi Serikali ina mpango gani wa kuweza kupeleka ile fedha ili nyumba zile wa Walimu ziweze kukamilishwa na Walimu wetu waweze kukaa mle ndani. Sasa sijapata jibu kutoka hapo.

**MWENYEKITI:** Watapangana wenyewe hiyo mimi namjua mtoa hoja. Kwa hiyo maadamu Mheshimiwa Waziri wa Elimu atajibu basi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hili afadhali nilijibu mimi kwa sababu nilihusika na ule uamuzi wa mwaka wa kwanza. Kwa kutambua kuwa Serikali ilifanya uamuzi wa kufuta ada ili Elimu ya Msingi iwe ya bure. Tulifahamu kwamba watoto wengi waliokuwa wanashindwa kuja shuleni kutokana na mapato hafifu ya wazazi wao sasa watakuja kwa wingi mkubwa. Kwa hiyo tulielekeza kwa maagizo kabisa ya circular kwamba zile fedha za mwaka wa kwanza za MMEM ile *development grant* itumike zaidi kujenga madarasa ili angalau wale watoto wanaokuja wawe na vyumba vya kusomea.

Lakini sasa kwa haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaeleza nafurahi kusema tulipata nafasi ya kuzungumza naye kidogo. Ni kwamba pale pote ambapo yamejengwa maboma na bado hayajaezekwa katika ruzuku inayokuja yaani ile ya awamu ya tatu ambayo itatoka hivi karibuni. Itatoka awamu ya kwanza na ya pili ya tatu itakayotoka hivi karibuni tunaziachia Wilaya zenyewe zipange kwa kulingana na hali halisi. Hata kama wanapoomba kwanza walisema ni kwa ajili ya madarasa, kama wamekamilisha madarasa na sasa shida iko zaidi kwenye nyumba za Walimu wanaweza kwa kutumia vikao vya Halmashauri ya Wilaya wakarekebisha wakapanga zaidi wakafanya kazi ya nyumba za Walimu.

Lakini pale ambapo nguvu kazi yao imekuwa ni kubwa zaidi kwamba hata ile ruzuku itakayokwenda ya awamu ya tatu haitatosha. Tunashauri Wilaya hiyo Mkurugenzi wa Wilaya hiyo na Afisaelimu wafanye maombi maalum kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo. Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Institutional Development Division*... 359,721,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha..... 1,494,820,000/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 71- Mkoa wa Pwani...... 1,639,371,600/=

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 1001, kifungu kidogo 6213.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilikuwa nataka kuinuka hapa nilipomwona mwenzangu amekubaliwa ndiyo maana nilitaka maelekezo yako ili nisiinuke hapa. Lakini umeniweka ndiyo maana nimeinuka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la nyumba ya *DC* Mafia. Nyumba ile Mhandisi wa Wilaya alikadiria shilingi milioni 15 kwa kuitumia J.K.T. Ilipofika kwa Mhandisi wa Majengo Mkoa akaongeza shilingi milioni 15. Walipomweka Mkandarasi kwa hiyo hela nyingi akala contractor ambaye sio J.K.T. ni *Private.* Kilichofanyika lilifuniliwa paa tu. Kule paa ndio uko kuna bedroom za *DC.* Unamwambia *DC* akae *floor* moja *floor* gani? Kwa sababu chini ni sitting room na vyoo vyote vibovu. *DC* akaomba basi niwekwe wapi, hotelini, wanamwambia shauri yako kaa hivyo hivyo. Ni ukatili mkubwa kabisa. Lakini alipokuja mkandarasi alichofanya ni kupaua zile nini?

**MBUNGE FULANI:** Vigae.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Wanaita vigae. Alipaua vigae. Kenchi ziko pale pale na mbao kidogo zilipomalizwa hakumaliza aliondoa na *cealing board* hakufanya lolote shilingi milioni 30 zimekwenda. Akaongezewa shilingi milioni 30.8 alichofanya amepaka rangi na hizo *rovers* ninavyozungumzia na kutengeneza vyoo vitatu vya chini. Sasa hivi inaombewa shilingi milioni 13. Kwa ajili hela zote zinaliwa na *contractor* na *Private* ambapo tungetumia J.K.T. tungetumia milioni 15. *(Makofi)*

Kama Mwenyekiti wa *African Parliamentary Network Against Corruption* hapa rushwa imetokea. Ninaomba Mwenyekiti kwa sababu Waziri amesema ataunda kitume. Kama Mbunge wake amesema naomba isiundwe kitume iundwe Tume. Katika Tume hiyo kwa sababu na *Local Authority Account Committee (AAC)* wanahusika waingizwe. Lakini namwomba Waziri sana kabisa atakuwa anamnyanyasa *DC* wake anayefanya kwa nguvu zote na kwa hali ngumu sana. Kumwambia alipe hela ya hoteli kwa mwaka mzima ambao *contractor* kwamba amepitisha hata muda wenyewe.

Ahsante Mwenyekiti, ninaomba tu Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERILAI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi Tume itaundwa kwenda kuchunguza ukweli wa mambo yote haya. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye na ni mwenzangu. Lakini naomba aniambie kitu kimoja swali la kumnyanyasa *DC* ajilipie mwenyewe naomba hilo atusaidie. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERILAI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba tutaunda Tume kwenda kuchunguza na haya yakibainika *DC* atarejeshewa gharama zozote zile alizoingia. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma .... 1,441,358,500/=

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa ahadi kwamba itajenga Ofisi ya *DC* Mpwapwa. Kama unavyofahamu Ofisi ya *DC* ya Mpwapwa ni Shule ya Chekechea na kulikuwa na ahadi kwamba itajengwa ofisi mpya na tukaambiwa tutafute kiwanja tumekwishatafuta. Sasa katika maelezo hapa kifungu 1001 sioni ujenzi wa boma la Mpwapwa. Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hali ya Ofisi ya *DC* Mpwapwa sio nzuri. Kwa bahati nzuri mimi nilikwenda pale mara ya mwisho lakini tulituma mtaalamu wetu kwenda kufanya tathmini juu ya hali hiyo kwa matarajio kwamba tutaweza sasa kuingiza katika utaratibu wa bajeti. Lakini kama inavyoelekea inawezekana tulichelewa kuingiza jambo hili katika bajeti. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Prof. Mwaga kwamba

tutajaribu kuliangalia tena tuone nini kinaweza kikafanyika kuhusiana na hilo swali. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Fungu 73 - | Mkoa wa Iringa | ... | 1,869,673,800/= |
| Fungu 74 - | Mkoa wa Kigoma | ... | 1,465,671,400/= |
| Fungu 75 - | Mkoa wa Kilimanjaro | … | 1,530,154,900/= |
| Fungu 76 - | Mkoa wa Lindi | ... | 1,637,176,800/= |
| Fungu 77 - | Mkoa wa Mara | ... | 1,578,634,100/= |
| Fungu 78 - | Mkoa wa Mbeya | ... | 2,481,676,400/= |
| Fungu 79 - | Mkoa wa Morogoro | ... | 3,500,449,800/= |

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara … 1,770,103,000/=

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuwa nataka kusema tena kwamba wakati nachangia mchana huu. Kwanza niseme naishukuru Serikali tunafanya ujenzi mwingi sana kule kwetu. Mwaka huu tumepangiwa kutengewa shilingi milioni 100 kwa ujenzi wa hospitali yetu kuitoa kutoka pale ilipo kuifanya District Hospital, tunashukuru sana. Lakini wakati nazungumza asubuhi hii nilikuwa nimezungumza kutaka kupata ufafanuzi au kueleweshwa utaratibu unaotakiwa kutumika wakati mtu anapopata ukandarasi. Kwa utaratibu wa tenda kupita kwenye Halmashauri anapewa kwanza fedha za Halmashauri ile aende akajengee ndipo au yeye anatakiwa ajenge halafu ikipata *certificate* zile zile ndiyo anapata kulipwa. Nilizungumza hivyo nikasema hivi ndivyo ilivyofanyika kwa Tandahimba wakati tunafanya ujenzi wa nyumba ya Mganga wa *District Hospital* hii tunayoijenga. Sasa nalizungumza hili kwa sababu inanitia hofu kama utaratibu utakuwa ni huu huu wa kuendelea kama huu sio utaratibu basi ukiukwaji huu unaweza ukaendelea kwenye fedha hizi shilingi 100 tunayoizungumza sasa hivi. Sasa nataka kujua hapo kuna ukiukwaji au hakuna ukiukwaji. Kama kuna ukiukwaji Serikali hii Wizara hii inasema nini juu ya hawa wanaofanya mambo haya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe maelezo kidogo tu kuhusiana na jambo hili.

Taratibu za kandarasi zimewekwa pale kwa mujibu wa sheria na kanuni mbalimbali. Ni kanuni ambazo zinaeleweka na Wakurugenzi wote. Sasa *more specifically* kwa hili kwa sababu ame-*pause* kwenye *unique problem* kwamba tenda zimetolewa hata kabla jambo hilo halijaanza kufanyika. Labda tupe subira kidogo tuwaombe wenzetu Katibu Mkuu na wenzake walifanyie kazi ili tuweze kupata *exactly what happened.*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Fungu 81 - | Mkoa wa Mwanza | ... | ... | 5,131,523,600/= |
| Fungu 82 - | Mkoa wa Ruvuma | ... | ... | 1,503,792,200/= |
| Fungu 83 - | Mkoa wa Shinyanga | ... | … | 1,907,432,600/= |
| Fungu 84 - | Mkoa wa Singida | .... | ... | 1,353,979,200/= |
| Fungu 85 - | Mkoa wa Tabora | ... | ... | 2,511,919,100/= |
| Fungu 86 - | Mkoa wa Tanga | ... | ... | 3,427,644,200/= |
| Fungu 87 - | Mkoa wa Kagera | ... | ... | 2,463,327,300/= |
| Fungu 88 - | Mkoa wa Dar es Salaam | .... | ... | 642,598,200/= |
| Fungu 89 - | Mkoa wa Rukwa | ... | ... | 1,469,717,200/= |
| Fungu 95 - | Mkoa wa Manyara | ... | ... | 3,809,604,000/= |

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mikoa na Halmashauri zake kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja iliyopo mbele yetu ni kwamba Makisio ya Wizara hii yakubaliwe rasmi na Bunge hili. Sasa nitawahoji.

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 200/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maelekezo naomba niyapate ili niwe naelewa kila jambo. Amefariki Marehemu Mheshimiwa Ngajulage wakati wa Bunge hili, Bunge likaendelea kama kawaida. Lakini amefariki Makamu wa Rais Bunge lilisitishwa. Leo amefariki Mheshimiwa Mbunge, Bunge linaendelea kama kawaida. Ni taratibu, ni kanuni au nini. Naomba nipate maelekezo?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa kanuni ambazo mmenikabidhi nazifanyia kazi hilo halimo. Kwa hiyo litafikishwa kwa uongozi wa Bunge rasmi na vikao vyake halafu litatolewa ufafanuzi maalum. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Ngawaiya alikuwa na hoja yake sasa kufuatana na kanuni yetu namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atoe hoja ya kuahirisha Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liahirishwe dakika 24 kabla ya wakati wake hadi Jumatatu saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

## HOJA BINAFSI

### Taarifa Fupi Kuhusu Kushambuliwa Kwa Mhe. Thomas Ngawaiya na kuokolewa na Jeshi la Polisi Asiuwawe

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na nashukuru vile vile Wabunge kukubali kupata taarifa fupi kuhusu nilivyoshambuliwa na jinsi Polisi Moshi walivyoniokoa kifo tarehe 29 Mei, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imenilazimu kuomba kwako kipindi maalum kwa kutoa maelezo binafsi kulingana na kanuni zetu za Bunge Na. 40 juu ya kushambuliwa na watu wasiojulikana na kuliteka gari langu *VX T876AAF* na kuitelekeza baada ya kuchukua vitu vyote vilivyokuwemo ndani ya gari ikiwa ni pamoja na bendera ya Bunge, *loud speakers,* fedha taslimu shs. 300,000/= simu za mikononi 3 na mabegi mawili mali ya Madiwani niliokuwa nao kwenye gari hilo pamoja na funguo za gari. Sababu kubwa ya kutoa maelezo hayo binafsi ni kwamba kumekuwa na taarifa mbalimbali zingine zikiwa potovu juu ya jambo hili la kinyama nililofanyiwa mimi mwenyewe pamoja na Madiwani wangu watatu wakiwa ni Janesis Kiwelu, Diwani wa Kata ya Msaranga na pia ni Mwenyekiti wa Wilaya *(TLP).* Diwani Consolata Lyimo, ambaye ni Diwani Viti Maalum *(TLP)* na ni Mwenyekiti wa Akinamama *(TLP)* Mkoa wa Kilimanjaro na Lydia Nassoro Diwani Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kabla ya kuingia ndani nichukue nafasi hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi na hasa *OCD* Moshi kwa jinsi walivyochukua muda mfupi kufika kwenye eneo la tukio na kuweza kuniokoa mimi na wenzangu na kutupeleka katika Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi. Nilipelekwa katika Hospitali ya Mawenzi Mkoa kwa matibabu na pia Polisi waliweza kuokoa gari langu lisiibiwe kwani funguo za gari walikuwa nazo hao majambazi. Hapa Bungeni Wabunge mbalimbali wamezungumzia suala hili kwa njia tofauti. Wengine walisema kuwa eti zilikuwa ni hujuma za Serikali na wengine walisema ni chuki za Wapinzani kwa Wapinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukisoma gazeti la tarehe 23 Juni, 2004 Mwananchi lina maelezo yanadai kuwa yaliyokuwa yametolewa na Mwenyekiti wa *(TLP)* Mheshimiwa Augustine Mrema kuwa "Sijapigwa ila ni usanii kwa kuwa nilisaidia Serikali ya CCM kuchukua Kata zangu". Gazeti liliendelea kusema kwamba "jicho langu liliumiaje bila miwani kuvunjika". Na pia lilisema kuwa: "ni vipi gari langu lilindwe na Polisi siku tatu kama sio njama zangu na Serikali kuhujumu Kata hiyo ya Kirima". Na mwisho gazeti lilisema kuwa "ni vipi niumizwe Jumamosi na kesho yake kupelekwa Misri kama sio njama za Serikali niliwezaje kupanda ndege ya kwenda Misri kesho yake". Mheshimiwa Naibu Spika, gazeti lilimalizia kwamba "kama ni kuondoka *(TLP)* niondoke pole pole na kwa ustaarabu bila visingizio kama hivyo". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba mambo mengi hapa ni ya kudhalilishana maana gazeti lilieleza kuwa hayo yote nimefanya ili niweze kuhurumiwa kwani sifanyi lolote katika jimbo langu. Ukweli wa mambo ni kwamba siku ya Jumamosi tarehe 29 Mei, 2004 nikiwa katika harakati za Uchaguzi Mdogo wa Madiwani katika Kata ya Kirima muda wa saa 2.45 usiku nikiwa na Madiwani niliokwishawataja hapo juu na nikiwa nawarudisha Madiwani hao makwao Mjini Moshi nikitokea Kijijini kwangu nilikozaliwa kupitia barabara ya Kirima nilikuta magari matatu yaliyokuwa yameegeshwa kando ya barabara eneo lijulikanalo kwa jina Ngirini. Nilipokaribia magari hayo Basi la CHADEMA liliondoka na kunitangulia mbele na baadaye lilifuata nyuma yangu Basi dogo aina ya *hiace* mali ya *Zahara Tours* likiwa na watu ndani. Basi hilo lilikimbia *speed* na kunipita na kujichomeka kati ya gari langu na gari la CHADEMA. Hivyo tukawa tunaendelea na safari kwani sote tulikuwa tumetoka kwenye kazi moja ya kampeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyuma yangu kulikuwepo na gari lingine aina ya *Landrover* nyeusi ambayo pia ni mali ya *Zahara Tours* ya huko Moshi. Sote tukiwa kwenye msafara wa kuelekea Mjini, kwani ilikuwa umbali wa mwendo kilomita kama 2 hivi kufikia Mjini. Tulipofika karibu na daraja la Mto Karanga ambako barabara ni nyembamba kwa kupishana, gari aina ya *Hiace* ilisimama katikati ya barabara na hivyo kuzuia gari langu lisiweze kupita. Ila lile la CHADEMA liliendelea na safari yake maana lilikuwa mbele yetu. Nilijaribu kupiga honi lakini gari hilo halikuondoka njiani ila walishuka vijana watano kwanza na kuingia porini kama vile wanataka kujisaidia ndipo walipochukua marungu na fimbo walizokuwa wamehifadhi hapo na nilipojaribu kulazimisha gari langu kupita pembeni kulia lile gari la mbele yangu ambalo ni *Hiace* lilinibana zaidi yaani lilizuia zaidi ili nisiweze kupita na kuashiria ugomvi. Nyuma yangu ilikuweko hiyo *Landrover* nyeusi, hivyo sikuweza hata kurudi nyuma. Ndipo walipoteremka watu 16 kutoka kwenye *Hiace* na watu kama 20 kutoka kwenye *Landrover* ambayo ilikuwa ni *Landrover* ya wazi iliyokuwa nyuma yangu na kuanza kunishambulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kujitetea kuwa wachukue kila kitu chochote wanachotaka ila waniache roho yangu. Lakini hawakusikia na waliendelea kunipiga bila huruma na wengine wakichukua vitu kwenye gari vikiwa ni pochi za wale wanawake pamoja na simu zao za mkononi na ma-*speaker* iliyokuwa kwenye gari pamoja na pesa zilizokuwa kwenye begi shilingi 300,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliweza kuchomoka na kukimbia kwenye nyumba ya jirani nikipiga yowe kubwa, nakufa! nakufa. Ndipo nilipojiingiza humo na kufanikiwa kupiga simu kwa *OCD* wa Moshi ambaye alitumia dakika kama 20 na kuwahi kwenye tukio na ndipo alipokuta gari langu likiwa wazi bila mtu ndani na bila funguo baadaye *OCD* alinipigia simu ya mkononi na kunitaka nijitokeze kwani Polisi wamekwishafika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoka kwa kuchechemea na ninawapongeza sana majirani waliojitokeza na wale walionihifadhi kwenye nyumba yao ambapo nilikimbilia chumba cha watoto kwani hali ilikuwa mbaya sana. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Pole!

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Polisi walikagua gari langu na kulikuta zima ila hakukuwa na kitu ndani na hata bendera yangu ya Bunge haikuwepo, ilichukuliwa na vitu vyote vilivyokuwemo. Hata hivyo, tulichukuliwa na gari la Polisi na kutuwahisha katika Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi na kupatiwa matibabu ya awali. Mimi nilifungwa *bandage* kwenye mguu wa kushoto na kuhusu jicho niliandikiwa *transfer form* ya kwenda Hospitali ya Rufaa ya *KCMC* ambako ndiko kwenye Madaktari bingwa wa mambo ya macho. Hivyo, siku ya Jumapili nilionana na Daktari bingwa wa macho na alipiga *x-ray* na kugundua matatizo ambapo nilipewa dawa ya kutumia kila baada ya masaa manne. Hivyo, si kweli kwamba kesho yake nilikwenda Misri kama Gazeti la Mwananchi lilivyoripoti, ila Misri nilikwenda siku ya Alhamisi tarehe 3 Juni, 2004 kikazi nikiwa na Kamati ya Maji ya Bunge pamoja na Waziri mwenyewe na hizo ni siku tano baada ya tukio. Safari yangu ya Misri ilikuwa ni ya kikazi kama Mbunge na siyo *offer* kwa kuisaidia CCM kushinda kama ilivyodaiwa ndani ya gazeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, si kweli kuwa gari langu lililindwa na Polisi kwa siku tatu, ila gari langu ni *automatic* na kwa kuwa sikuwa na funguo za akiba niliagiza funguo za akiba kutoka kwa mke wangu Dar es Salaam na alifika nazo kesho yake siku ya Jumapili mchana na kwenda kuliondoa gari pale lilipokuwa siku hiyo hiyo ya Jumapili. Hivyo, ni uongo kusema kuwa gari langu lililindwa na Polisi kwa siku tatu.

Tatu, gazeti lilizungumzia kuhusu kuumia jicho bila miwani kuvunjika. Ikumbukwe kuwa ilikuwa ni usiku wa saa mbili na miwani yangu ni ya kuzuia mwanga na kusomea, hivyo sikuwa nimeivaa miwani usiku huo. Pia, nasikitika kusikia habari zilizoandikwa kwenye gazeti hilo kwamba sijafanya chochote kwenye Jimbo langu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nikikubaliana na gazeti maana yake nitakuwa naidhalilisha Serikali hii. Kwanza niishukuru sana Serikali hii ya Tanzania kwa kunipa maendeleo mbalimbali bila kunibagua kiitikadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitaja machache tu ambayo nimeyafanya kwa mwaka huu, nimehamasisha na kufanikisha kufungua Sekondari za Kutwa za Kata nane. Mwaka huu zimefunguliwa Sekondari nane katika Jimbo langu, siyo kitu cha mchezo na Kata yangu mwenyewe nilikozaliwa kuna Sekondari za Wananchi tatu. Sasa hiyo

wanayosema kwamba sijafanya kitu kwanza wasikie hayo na taarifa hizi ziwafikie. Kata yangu tu ina Sekondari tatu ina *Kibosho Girls Secondary* ya Wananchi, ina *Msoo Secondary* na *Sungu Secondary.*

**MBUNGE FULANI:** Njoo CCM.

**NAIBU SPIKA:** Soma, soma, soma.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, zaidi ya asilimia 80 ya barabara zote za Moshi Vijijini zimepigwa greda na ni pamoja na kuiwekea lami barabara ya *TPC* ya Jimboni kwangu. Vile vile, mimi naona hayo ni maendeleo ambayo hayajawahi kuwepo tangu enzi na enzi na sasa nashughulikia maji ya kumwagilia mpunga huko Mabogini pamoja na kufuatilia fedha za *STABEX* kwa wakulima wa kahawa na hayo yote ni pamoja na Shule za *Primary,* vyote vimefanyika wakati huu wa Ubunge wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesoma Gazeti la Mtanzania likihoji kuwa kwa nini nimempokea Rais Mkapa na nisiweze kuandamana na wengine? Mwaka 2002 nilimpokea Rais Mkapa pale Moshi kama Rais wangu. Pamoja na kwamba mimi ni mpinzani, lakini siyo kwamba unapinga Serikali iliyokuwa madarakani. Rais alikuwa anakabidhi barabara ya Jimboni kwangu ya kutoka *KCMC* kwenda *Mweka Wildlife College.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unapaswa kusoma ulichoandika. Kanuni ndiyo inasema hivyo.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Kwa hiyo, tulipata barabara na mambo mengine kwa kumpokea Rais katika Jimbo langu. Je, ni kosa kuishukuru Serikali kwa hayo? Je, siyo mimi niliyefuatilia maendeleo haya? *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Weweeeee. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mwisho, pia Halmashauri yangu ilipata cheti namba moja, Halmashauri yangu ya Moshi Vijijini. Kwa hiyo, hayo vile vile ni maendeleo. *(Makofi)*

Mwisho, katika kujibu gazeti kwamba eti nilikuwa naona aibu na ninasingizia kipigo ili Wananchi wanionee huruma si kweli. Nataka nieleze kwamba katika matajiri wa Tanzania, ukihesabu matajiri wa Tanzania mia moja, mimi ni mmojawapo. Hivyo, siko katika Ubunge kama ajira ya kujikimu na maisha, bali ni uamuzi wa kutumikia Wananchi na kutafuta haki zao pamoja na kuhamasisha maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yote yaliyotokea naomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini hao wanaotaka kuharibu amani ya nchi hii kwani watu hao wanafahamika

kuwa walikodiwa kutoka Mjini Moshi sehemu ya Bondeni na magari yanafahamika. Ni vema na akaulizwe hata huyu mmiliki wa magari hayo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudi CCM, karibu CCM. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ngawaiya mwishoni amemalizia kuiomba Serikali pengine ifanye uchunguzi. Sasa sijui kama Serikali ingependa kusema lolote kwa sasa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumpe pole Mheshimiwa Ngawaiya, kwa mkasa uliompata. Vile vile, pongezi alizotoa kwa Jeshi la Polisi kushughulikia haraka na kumwokoa. Salaam hizo tutazipeleka hasa kwa *OCD* wa Moshi na tatu, kwa niaba ya Serikali nataka kuahidi kwamba tutaunda Tume ya kuchunguza tukio hilo ijulikane nini kilichotokea na wale waliofanya tukio hilo wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja iliyotolewa ni ya Kuahirisha Bunge, ambayo ndiyo nitawahoji. Lakini kabla sijawahoji kuhusu hoja iliyotolewa ya Kuahirisha Bunge, ningependa kuwapa tangazo lifuatalo: Tumepokea barua kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni kutoka kwa Katibu Mkuu ambayo inawaalikeni Waheshimiwa Wabunge kesho Jumamosi kwenye Mashindano ya Mavazi ya Taifa. Mwaliko huu umetoka Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Sasa mnaalikwa hilo, naomba niwakumbushe inafanyika kesho Ukumbi wa Kilimani.

**WABUNGE FULANI:** Saa ngapi?

**NAIBU SPIKA**: Saa za kawaida na vitu vya namna hiyo. *(Kicheko)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa )*

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 28 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*